# KUBADILI MTAZAMO Mkataba mpya KUHUSU MUSTAKABALI wa kijamii WETU wa elimu

RIPOTI KUTOKA KWA TUME YA KIMATAIFA YA MUSTAKABALI WA ELIMU

## UNESCO — shirika linaloongoza miradi ya elimu ulimwenguni

Shirika la UNESCO limepatia elimu kipaumbele kwa sababu ni haki ya msingi ya binadamu na msingi wa amani na maendeleo endelevu. UNESCO ni shirika maalumu la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia elimu kwa kutoa uongozi wa kimataifa na kikanda ili kuendeleza maendeleo, kuimarisha uwezo na uthabiti wa mifumo ya kitaifa na kuwahudumia wanafunzi wote. Pia, shirika la UNESCO linaongoza katika juhudi za kukabiliana na changamoto za kisasa kupitia kwa mafunzo kuhusu ujifunzaji wa kuleta mabadiliko yanayozingatia usawa wa kijinsia na maswala yanayohusu Afrika.

## Mradi wa Mustakabali wa Elimu

Tume ya kimataifa ya Mustakabali wa Elimu ilianzishwa na UNESCO mwaka 2019 ili kutoa mwelekeo kuhusu jinsi ambavyo mustakabali wa binadamu na wa Dunia unaweza kubadilishwa kwa kutumia maarifa na ujifunzaji. Mradi huu unajumuisha ushirikiano mpana baina ya umma na wataalamu na unalenga kuhimiza mjadala wa kimataifa kuhusu jinsi elimu inaweza kubadilishwa katika ulimwengu huu wenye viwango vikubwa vya uchangamani, wasiwasi na udhaifu.

unesco
Shirika la Umoja
wa Mataifa la Elimu,
Sayansi na Utamaduni

Ripoti hii ilichaphishwa mwaka 2025 na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris, Ufaransa na Kampuni ya Waridi Publishing Limited, P.O. Box 34607-00100, Nairobi, Kenya.

© UNESCO na Waridi Publishing Limited, 2025

ISBN: 978-92-3-000252-7
DOI: https://doi.org/10.54675/HUAV8642

CC BY SA

Chapisho hili linapatikana katika leseni ya Open Access chini ya Attribution-ShareAlike 3.0 IGO (CC-BY-SA 3.0 IGO) (http://creativecommons.org/licenses/by-sa/3.0/igo/). Kwa kutumia maudhui ya chapisho hili, watumiaji wanakubali kufuata masharti ya matumizi ya Jukwaa la Ufikiaji Huru (Open Access Repository) la (https://www.unesco.org/en/open-access/cc-sa).

Kichwa asili: *Reimagining our futures together: a new social contract for education*
Toleo la kwanza lilichapishwa mwaka 2021 na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni.

Maelezo na maandishi yaliyotumika katika chapisho hili hayakusudii kutoa maoni yoyote kutoka UNESCO kuhusu hali ya kisheria ya nchi, eneo, mji, au mipaka chini ya mamlaka yake.

Wajumbe wa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu wanakubali kuwajibika kwa ajili ya uwasilishaji wa maoni yaliyotolewa humu. Haya si lazima yawe maoni ya UNESCO.

Mhariri wa chapisho la Kiingereza: Mary de Sousa
Tafsiri ya Kiswahili: Msigwa Wema Lwidiko
Mhariri wa chapisho la Kiswahili: Mercyline Magoma Omari

Toleo hili limetayarishwa na kuchapishwa na UNESCO

*Imechapishwa nchini Ufaransa*

Kazi ya Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu kwa ujumla ilifadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Sweden (SIDA), Serikali ya Ufaransa na Banco Santander.

## MUHTASARI MFUPI

# Mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Kuna hatari kubwa inayowakabili binadamu wote na Dunia. Janga la UVIKO-19 limethibitisha udhaifu na kuunganika kwetu. Sasa, hatua ya haraka inahitaji kuchukuliwa na watu wote ili kubadilisha mwelekeo wa mustakabali wetu. Ripoti hii ya Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu inatambua uwezo wa elimu wa kuleta mabadiliko makubwa. Tunakabiliwa na changamoto mbili za kushughulikia ahadi ambazo hazijatimizwa ili kuhakikisha haki ya elimu bora kwa kila mtoto, kijana na mtu mzima na kufanikisha kikamilifu mabadiliko ya elimu yanayotarajiwa ili tufikie mustakabali endelevu wa pamoja.

Ili kufanya hivi, tunahitaji mkataba mpya wa kijamii wa elimu ambao unaweza kurekebisha athari za dhuluma na kubadilisha mustakabali.

Tunahitaji mkataba mpya wa kijamii wa elimu ambao unaweza kurekebisha athari za dhuluma na kubadilisha mustakabali.

Mkataba huu mpya lazima ujikite katika haki za binadamu na uzingatie kanuni za: kupigana dhidi ya ubaguzi, kuimarisha haki za jamii, kuheshimu maisha, heshima ya binadamu na tofauti za kitamaduni. Lazima uundwe na maadili ya kujali, usawa na mshikamano. Unapaswa kuimarisha elimu kama mradi wa umma na rasilimali ya jamii.

Katika miaka miwili ya kuandaa ripoti hii, kulikuwa na mchakato wa kushauriana uliohusisha takribani watu milioni moja, serikali, taasisi, mashirika na raia ulimwenguni kote ili kuandaa mkataba mpya wa kijamii wa elimu ambao utatusaidia kujenga mustakabali wenye amani, haki na unaoleta uendelevu kwa wote.

Dira, kanuni na mapendekezo yaliyowasilishwa humu ni mwanzo tu. Kuyafafanua na kuyatumia katika mazingira tofauti ni jukumu la watu wote. Mambo mengi mazuri tayari yapo. Ripoti hii inajaribu kuyapanga na kuyatumia. Sio maelekezo wala mipango bali ni mwanzo wa mazungumzo muhimu.

UNESCO unesco

*"Kwa kuwa vita huanzia katika akili za wanaume na wanawake, lazima kinga za amani zijengwe katika akili za wanaume na wanawake."*

# KUBADILI MTAZAMO

Mkataba mpya

KUHUSU MUSTAKABALI

wa kijamii

WETU

wa elimu

RIPOTI KUTOKA KWA TUME YA KIMATAIFA YA MUSTAKABALI WA ELIMU

Waridi Publishing Limited

# Dibaji

**Audrey Azoulay**
Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO

Kama kuna jambo ambalo limetuunganisha pamoja katika mwaka mmoja na nusu uliopita, ni hisia zetu kuhusu udhaifu wetu na wasiwasi kuhusu mustakabali. Kuliko wakati mwingine wowote, sasa tunajua kwamba hatua ya haraka inahitajika ili kubadilisha mwelekeo wa binadamu na kuiokoa sayari kutoka kwa uharibifu zaidi. Lakini hatua hiyo lazima iwe ya muda mrefu na iunganishwe na mawazo ya kimkakati.

Elimu inachangia pakubwa katika kutatua changamoto hizo za kutisha. Hata hivyo, kama ambavyo janga la UVIKO-19 limeonyesha, elimu ina udhaifu. Janga hilo lilipofika kilele chake, wanafunzi billioni 1.6 waliathirika kutokana na kufungwa kwa shule ulimwenguni kote.

Kamwe huwezi kuthamini kitu zaidi mpaka wakati umekipoteza. Kwa sababu hiyo, UNESCO inakaribisha ripoti hii mpya, *Kubadili Mtazamo Kuhusu Mustakabali Wetu: Mkataba Mpya wa Kijamii wa Elimu*, iliyotayarishwa na Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Bi. Sahle-Work Zewde, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia.

Tangu kuanzishwa miaka 75 iliyopita, UNESCO imetoa ripoti kadhaa za kimataifa kuhusu kufikiria upya jukumu la elimu katika nyakati hizi muhimu za mabadiliko ya jamii. Ripoti hizi zilianza na ripoti ya Tume ya Faure ya mwaka 1972 ya *Kujifunza Kuwa*: *Ulimwengu wa Elimu Leo na Kesho* na kuendelea na ripoti ya Tume ya Delors ya mwaka 1996, *Kujifunza: Vipaji Tulivyonavyo*. Ripoti hizi mbili zilikuwa na utambuzi na ushawishi; hata hivyo, kimsingi Dunia imebadilika katika miaka ya hivi karibuni.

Kama ripoti zingine zilizoitangulia, ripoti ya Tume ya Sahle-Work imepanua mazungumzo kuhusu falsafa na kanuni zinazohitajika ili kutumia elimu katika kuboresha maisha ya viumbe wote ulimwenguni. Iliandaliwa katika kipindi cha miaka miwili na kujikita katika mashauriano ya kina na watu zaidi ya milioni moja.

Ripoti hii inatufunza jambo moja: Tunastahilihi kuchukua hatua za haraka kwa kubadili mwenendo wetu kwa sababu mustakabali wa binadamu unategemea mustakabali wa sayari. Ripoti inapendekeza mkataba mpya wa kijamii ambao unalenga kujenga mahusiano mapya baina ya binadamu, Dunia na teknolojia.

Mkataba huu mpya wa kijamii ni fursa yetu ya kurekebisha dhuluma za awali na kurekebisha mustakabali. Zaidi ya yote, unazingatia haki ya elimu bora katika hatua zote za maisha, na kusisitiza kuwa ufundishaji na ujifunzaji ni juhudi za jamii nzima; kwa hivyo, ni rasilimali za jamii.

Kufanikisha dira hii ya elimu sio jambo lisilowezekana. Kuna matumaini, hasa miongoni mwa vijana. Hata hivyo, tunahitaji ubunifu ili kuhakikisha kwamba ujumuishaji, usawa, haki za binadamu na amani ni misingi ya mustakabali wetu. Hatimaye, hivo ndivyo ripoti hii inatutaka tufanye. Kwa sababu hiyo ya kipekee, ina mambo muhimu ya kufunza kila mmoja wetu.

**Audrey Azoulay**

Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO

# Dibaji

**MHE. Sahle-Work Zewde**
Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu
Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia

Mustakabali wa Dunia yetu unastahili kuzingatia maeneo na demokrasia. Ni kupitia kwa hatua za pamoja na za kibinafsi, zinazojumuisha utofauti wa watu na tamaduni zao, tunaweza kufanikiwa katika ujenzi mustakabali bora.

Binadamu ana sayari moja tu; hata hivyo, hatugawi rasilimali zake vizuri au kuzitumia kwa namna endelevu. Kuna ukosefu wa usawa usiokubalika katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Bado hatujafanikisha usawa wa jinsia kwa wanawake na wasichana. Licha ya ahadi za uwezo wa teknolojia wa kutuunganisha, bado kuna tofauti kubwa kwa watumiaji wa teknolojia ya dijitali, hususan Afrika. Kuna ukosefu wa usawa katika uwezo wa watu kupata na kujenga maarifa.

Elimu ndiyo mbinu mwafaka ya kushughulikia ukosefu wa usawa ambao umekithiri. Kwa kuanzia katika kile tunachokifahamu, tunahitaji kufanya mabadiliko ya elimu. Madarasa na shule ni muhimu, lakini ujenzi wao katika siku zijazo unastahili kubadilishwa. Elimu lazima ijenge ujuzi unaohitajika kwenye maeneo ya kazi katika karne ya 21 kwa kuzingatia mabadiliko ya kazi na njia tofauti ambazo usalama wa kiuchumi unaweza kuendelezwa. Zaidi ya hayo, ufadhili wa elimu lazima upanuliwe ili kuhakikisha haki ya kupata elimu ya watu wote inalindwa.

Kuheshimu haki za binadamu na kujali elimu kama rasilimali ya umma lazima iwe mihimili mikuu inayounganisha ulimwengu na mustakabali wetu. Kama ripoti hii inavyoeleza, kanuni hizi mbili lazima ziwe msingi wa elimu kila mahali. Haki ya kupata elimu bora kila mahali na ujifunzaji ambao unajenga uwezo wa watu kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote ni msingi wa mafanikio na mustakabali wa aina mbalimbali za elimu. Tukijitolea kulinda haki za binadamu, tutaweza kufaidika kutoka kwa namna tofauti za kujua katika ulimwengu ambao tamaduni za binadamu na jamii zinaleta mafunzo rasmi na yasiyo rasmi na kutoka kwa maarifa tunayoweza kukusanya kupitia kwa ushirikiano.

Ripoti hii ni matokeo ya kazi ya pamoja ya Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu iliyoanzishwa na UNESCO mwaka wa 2019. Kwa kutambua michango iliyotoka kwa wanachama wote kutoka maeneo tofauti ya kijiografia, ningependa kumshukuru António Nóvoa, Balozi wa Ureno UNESCO, ambaye alisimamia kamati ya utafiti na rasimu. Mapendekezo yaliyowasilishwa katika Kubadili Mtazamo Kuhusu Mustakabali Wetu yanatokana na ushirikiano wa kimataifa na mchakato wa ujenzi wa pamoja ambao ulionyesha kwamba kuna viwango vikubwa vya ubunifu, uvumilivu na matumaini katika ulimwengu unaoshuhudia ongezeko la mashaka, utata na ukosefu wa usalama. Mustakabali wa masuala muhimu yafuatayo unahitaji kufikiriwa na kuchunguzwa upya: uendelevu,

maarifa, ujifunzaji, walimu na ufundishaji, kazi, ujuzi na uwezo, uraia, demokrasia na ushirikishwaji wa jamii, elimu ya umma, elimu ya juu, utafiti na uvumbuzi.

Kazi ya Tume katika kipindi cha miaka miwili iliyopita ilikumbwa na janga la UVIKO-19 na wajumbe wa Tume walikuwa na ufahamu mkubwa kuhusu changamoto zinazowakabili watoto, vijana na wanafunzi wa marika yote ambayo yalikabiliwa na tatizo la shule nyingi kufungwa. Ripoti ya *Kubadili Mtazamo Kuhusu Mustakabali Wetu* imewekwa wakfu kwa wanafunzi na walimu ambao maisha yao yalivurugwa na UVIKO-19 na kwa jitihada zao kubwa za kuhakikisha ustawi, ukuaji na kuendelea kujifunza katika hali ngumu.

Matumaini yetu ni kuwa mapendekezo yaliyomo, kuhusu mazungumzo ya umma na wito wa kuchukua hatua za pamoja, yatatumika kama kichocheo cha kuunda mustakabali wa binadamu na ulimwengu ulio na amani, haki na uendelevu.



**MHE. Sahle-Work Zewde**
Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu
Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia

# Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu

**MHE. Sahle-Work Zewde,** Rais, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, na Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu

**António Nóvoa,** Profesa katika Taasisi ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Lisbon, na Mwenyekiti wa kamati ya kuandaa utafiti na ripoti ya Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu

**Masanori Aoyagi**, Profesa Mstaafu, Chuo Kikuu cha Tokyo

**Arjun Appadurai**, Profesa Mstaafu, Media, Utamaduni na Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha New York na Profesa wa Max Weber Global katika Kituo cha Bard Graduate, New York

**Patrick Awuah**, Mwanzilishi na Rais, Chuo Kikuu cha Ashesi, Ghana

**Abdel Basset Ben Hassen**, Rais, Taasisi ya Kiarabu ya Haki za Binadamu, Tunisia

**Cristovam Buarque**, Profesa Mstaafu, Chuo Kikuu cha Brasília

**Elisa Guerra**, Mwalimu na Mwanzilishi, Colegio Valle de Filadelfia, Mexico

**Badr Jafar**, Mkurugenzi Mkuu, Crescent Enterprises, Umoja wa Nchi za Kiarabu

**Doh-Yeon Kim**, Profesa Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Seoul, Aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Jamhuri ya Korea

**Justin Yifu Lin**, Mkuu wa Kitivo, Profesa, Taasisi ya New Structural Economics, Chuo Kikuu cha Peking

**Evgeny Morozov**, Mwandishi

**Karen Mundy**, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya UNESCO ya Mipango ya Elimu (IIEP) & Profesa (aliye likizoni), Chuo Kikuu cha Toronto – Taasisi ya Ontario ya Masomo ya Elimu

**Fernando M. Reimers**, Profesa, Shule ya Uzamili ya Elimu ya Harvard, USA

**Tarcila Rivera Zea,** Rais, Kituo cha CHIRAPAQ cha Utamaduni wa Wenyeji Asili wa Peru

**Serigne Mbaye Thiam**, Waziri wa Maji na Usafi wa Mazingira, Senegal

**Vaira Vike-Freiberga**, Aliyekuwa Rais wa Latvia, kwa sasa ni mwenyekiti mwenza katika Kituo cha Kimataifa cha Nizami Ganjavi, Baku

**Maha Yahya**, Mkurugenzi, Kituo cha Carnegie Mashariki ya Kati, Lebanon

# Shukrani

Ripoti hii haingeweza kuandaliwa bila ya mchango wa watu, jamii na asasi mbalimbali.

Tume ingependa kuwashukuru wale wote waliochangia kupitia kwa ripoti binafsi, makala ya usuli, pamoja na watu binafsi, asasi na jamii walioshiriki katika mashauriano ya ulimwengu kuhusu mustakabali wa elimu (angalia viambatisho kwa ajili ya orodha ya waliochangia na michango yao).

Maoni muhimu sana yalitolewa na Bodi ya Ushauri ya Mustakabali wa Elimu inayowakilisha washirika muhimu wa elimu, utafiti na uvumbuzi (tazama viambatisho ili kupata orodha kamili ya watu binafsi na asasi).

Shukrani za dhati ziende kwa wataalamu wafuatao ambao walifanya kazi kwa karibu na Sekretarieti ya UNESCO katika hatua ya uchanganuzi na uandishi na ambao walipitia matoleo ya awali ya mswada wa ripoti hii: Tracey Burns, Paul Comyn, Peter Ronald DeSouza, Inés Dussel, Keri Facer, Hugh McLean, Ebrima Sall, François Taddei, Malak Zaalouk, na Javier Roglá Puig.

Mwisho, Tume ingependa kutoa shukrani za dhati kwa UNESCO na hususan, Bi. Stefania Giannini, Msaidizi wa Mkurugenzi Mkuu wa Elimu, kwa uongozi wake, pamoja na Sobhi Tawil, Mkurugenzi Timu ya Mustakabali wa Kujifunza na Uvumbuzi na timu yake, kwa msaada waliotoa kwa Tume bila ya kuchoka. Wajumbe wa timu walikuwa Aida Alhabshi, Alejandra Castaneda, Catarina Cerqueira, Anett Domiter, Keith Holmes, Iaroslava Kharkova, Stephanie Magalage, Jack McNeill, Fengchun Miao, Michela Pagano, Maya Prince, Noah W. Sobe, Elena Toukan, na Mark West. Pia, timu ilisaidiwa na wenzao wengi kutoka shirika la UNESCO ambao walichangia kwa namna tofauti kwenye mradi wa Mustakabali wa Elimu.

# Contents

**Dibaji** **v**
**Audrey Azoulay**
Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO **v**

**MHE. Sahle-Work Zewde**
Mwenyekiti wa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu
Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia **vii**

**Shukrani** **x**

**Muhtasari Mkuu** **1**

## UTANGULIZI 7

Uhai wa binadamu, haki za binadamu, na Dunia hatarini 8
Umuhimu wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu 10
Ufafanuzi mpya wa madhumuni ya elimu 11
Mpangilio wa ripoti 14

## SEHEMU I
## AHADI ZA KITAMBO DHIDI YA MUSTAKABALI USIOTABIRIKA 17

### SURA YA 1 MUSTAKABALI WA ELIMU INAYOLETA USAWA 19

Ukosefu wa ukamilifu na usawa katika upanuzi wa elimu 20
Umasikini mkubwa na ongezeko la ukosefu wa usawa 24
Mtandao wa utengwaji 25

### SURA YA 2 VURUGU NA MABADILIKO IBUKA 29

Dunia hatarini 30
Dijitali inayounganisha na kugawanya 34
Kuzorota kwa demokrasia na ongezeko la miwaganyiko 38
Mashaka kuhusu mustakabali wa kazi 40

## SEHEMU YA II
## KUBADILISHA ELIMU 46

**SURA YA 3 UFUNDISHAJI WA USHIRIKIANO NA MSHIKAMANO** 49

Kubadilisha mbinu za ufundishaji 51
Safari za ufundishaji katika kila umri na hatua 55
Kuimarisha dhamira ya elimu ya juu 59
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 60

**SURA YA 4 MITAALA NA MBADILIKOUMBO WA MAARIFA YA JAMII** 61

Kushiriki katika maarifa ya jamii 63
Mchango wa elimu ya juu 71
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 73

**SURA 5 KAZI YA KULETA MABADILIKO WANAYOFANYA WALIMU** 75

Ualimu kama taaluma shirikishi 76
Safari ya maendeleo ya mwalimu inayosokotana na maisha 79
Mshikamano wa umma katika kubadilisha ualimu 82
Mahusiano baina ya vyuo vikuu na walimu 84
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 85

**SURA YA 6 KULINDA NA KUBADILISHA SHULE** 87

Jukumu la shule lisilofidika 88
Mabadiliko ya lazima katika shule 90
Kuvuka daraja linalounganisha shule na elimu ya juu 95
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 96

**SURA YA 7 ELIMU KATIKA NYAKATI NA NAFASI TOFAUTI** 97

Kuimarisha ujumuishaji na uendelevu wa fursa za elimu 99
Kufafanua swali la 'ni wapi' elimu hutokea 104
Kupanua haki ya kupata elimu 106
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 108

## SEHEMU YA III
## KUHARAKISHA MKATABA MPYA WA KIJAMII WA ELIMU 109

**SURA YA 8 WITO WA KUFANYA UTAFITI NA UVUMBUZI** 111

Ajenda mpya ya utafiti wa elimu 113
Kupanua maarifa, data, na ushahidi 115
Kuvumbua mustakabali wa elimu 118
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 121

**SURA YA 9 WITO WA MSHIKAMANO NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** 123

Kukabiliana na utaratibu wa ulimwengu unaozidi kuwa hatari 124
Malengo ya pamoja, kujitolea, kanuni, na viwango 126
Ushirikiano katika uzalishaji wa maarifa na utumiaji wa ushuhuda 128
Kufadhili elimu mahali ambapo imehatarishwa 129
Jukumu la UNESCO 129
Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu 130

## HITIMISHO NA MUENDELEZO 133
## Kushirikiana katika ujenzi wa mustakabali wa elimu 133

**Mapendekezo ya kujenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu** **135**
**Kauli mbiu** **140**
**Mazungumzo na ushirikishwaji** **143**
**Mwaliko wa kuendelea** **144**

## VIAMBATISHO 147

**Marejeleo yaliyochaguliwa** **148**
*Ripoti huru* *148*
*Makala ya Usuli* *150*
*Maoni kutoka kwa mashauriano ya kimataifa* *152*
*Machapisho ya Tume ya Mustakabali wa Elimu* *153*

**Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu** **154**
*Mamlaka* *154*
*Wajumbe* *154*

**Hatua za Mustakabali wa Elimu** **160**

**Waliochangia katika mashauriano ya kimataifa, mashirika, na mitandao** **161**

# Muhtasari Mkuu

Dunia yetu iko kwenye awamu ya mabadiliko. Tayari tunajua kwamba maarifa na ujifunzaji ni misingi ya mabadiliko. Lakini tofauti za kidunia - na haja kubwa ya kufikiria upya kwa nini, vipi, ni nini, wapi, na lini tunapojifunza - zinamaanisha kuwa elimu bado haitekelezi ahadi yake ya kutusaidia kujenga mustakabali wenye amani, haki, na maendeleo endelevu.

Katika harakati za kutafuta maendeleo yetu, sisi binadamu huzidiwa na mazingira yetu ya asili, ambayo huanza kutishia maisha yetu. Leo hii, viwango vya juu vya maisha vinaambatana na ukosefu wa usawa. Watu wengi wanajishughulisha na maisha ya umma, lakini muundo wa asasi za kiraia na demokrasia unayumba katika maeneo mengi ulimwenguni. Mabadiliko ya haraka ya teknolojia yanabadilisha nyanja nyingi za maisha yetu. Hata hivyo, ubunifu huu hautumiwi ipasavyo katika kuimarisha usawa, ujumuishaji, na ushirikishwaji katika demokrasia.

Kila mtu leo ana wajibu mkubwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo - kuhakikisha kwamba Dunia yetu ina rasilimali ya kutosha, na kwamba kila mtu anapata haki sawa za binadamu kwa ukamilifu. Licha ya kukabiliwa na shinikizo la kuchukua hatua haraka na kuishi katika mazingira ya mashaka, **tuna sababu ya kuwa na matumaini makubwa**. Kama spishi, tuko katika awamu ya historia yetu ya pamoja ambapo tuna nafasi kubwa ya kupata maarifa na zana zinazo tuwezesha kushirikiana. Uwezo wa kushirikisha binadamu katika kuunda mustakabali bora kwa pamoja upo na ni wa kutosha.

Ripoti hii ya kimataifa kutoka Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu inafafanua jukumu ambalo elimu inaweza kutimiza katika kuunda ulimwengu ulioshikamana na mustakabali wa pamoja tunapoelekea mwaka 2050 na kuendelea. Mapendekezo yaliyowasilishwa yanatokana na mchakato wa miaka miwili ya ushirikiano wa kimataifa na ujenzi wa pamoja ambao ulionyesha kwamba idadi kubwa ya watu - watoto, vijana na watu wazima - wanafahamu vyema kwamba **tumeunganishwa** katika Dunia hii na kwa hivyo, ni muhimu **tushirikiane.**

Watu wengi tayari wanajishughulisha katika kuleta mabadiliko haya wao wenyewe. Ripoti hii imejumuisha michango yao kwa kila kitu kuanzia jinsi ya kufikiria upya kuhusu nafasi za ujifunzaji hadi kuangalia historia ya ukoloni katika mitaala ya elimu na umuhimu wa kujifunza mambo ya kijamii na hisia, na inaangazia hofu inayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa, majanga kama UVIKO-19, habari za uongo, na tofauti kubwa baina ya watumiaji wa teknolojia za dijitali.

Elimu - jinsi tunavyofanikisha ufundishaji na ujifunzaji katika maisha yote - kwa muda mrefu imekuwa na jukumu la msingi katika mabadiliko ya jamii za binadamu. Inatuunganisha na ulimwengu na kutuunganisha kama binadamu, inatuonyesha fursa ya mawazo mapya na kuimarisha uwezo wetu wa kuwa na mazungumzo na kuchukua hatua bora. **Lakini ili kuunda mustakabali wenye amani, haki, na uendelevu, elimu lazima ibadilishwe**.

## Mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Elimu inaweza kuangaliwa kwa mujibu wa mkataba wa kijamii - kama makubaliano ya wazi miongoni mwa wanajamii kuhusu kushirikiana kwa manufaa yao. Mkataba wa kijamii ni zaidi ya shughuli moja kwani unajumuisha desturi, ahadi na kanuni ambazo zimetungwa rasmi ili kuongoza utamaduni. **Hatua ya kuanzia ni dira ya pamoja ya madhumuni ya umma kwa elimu.** Mkataba huu unajumuisha kanuni za msingi zinazounda mifumo ya elimu na mikakati inayotumika katika kujenga, kutunza, na kuboresha elimu.

Kipindi cha karne ya ishirini, elimu ya umma ililenga kusaidia raia wa nchi na kufanikisha jitihada za maendeleo kupitia mfumo wa elimu ya lazima kwa watoto na vijana. Hata hivyo, leo hii tunapokabiliwa na hatari kubwa kwa mustakabali wa binadamu na Dunia yenyewe, lazima tubadilishe kwa haraka elimu ili itusaidie kushughulikia changamoto zinazotukabili. Hatua hii ya **kubadili mtazamo inamaanisha kushirikiana katika kujenga mustakabali ambao ni wa kushirikiana na kutegemeana**. Mkataba mpya wa kijamii wa elimu lazima utuunganishe katika jitihada za pamoja na utoe maarifa na uvumbuzi unaohitajika ili kujenga mustakabali endelevu unaoleta amani kwa wote na unaozingatia haki za kijamii, kiuchumi na kimazingira. Kama ripoti hii inavyoeleza, ni lazima mkataba huo utetee wajibu wa walimu.

Kuna maswali matatu muhimu ya kuuliza kuhusu elimu tunapoelekea mwaka 2050: **Tunapaswa kuendelea kufanya nini? Tunapaswa kuacha nini? Kitu gani tunahitaji kukifanya upya na kwa ubunifu?**

### Kanuni za msingi

Mkataba wowote mpya wa kijamii lazima utumie kanuni zinazozingatia haki za binadamu - ujumuishaji, usawa, ushirikiano, mshikamano, uwajibikaji wa pamoja, na muunganiko - na kuongozwa na kanuni mbili zifuatazo:

- **Kuhakikisha haki ya kupata elimu bora katika hatua zote za maisha.** Haki ya kupata elimu, kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 26 cha Azimio La Kimataifa la Haki za Binadamu, lazima iendelee kuwa msingi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu na lazima ipanuliwe ili kujumuisha haki ya kupata elimu bora maishani. Pia, ni lazima ijumuishe haki ya kupata habari, utamaduni, na sayansi - pamoja na haki ya kupata na kuchangia maarifa ya kijamii, ambayo ni rasilimali za maarifa ya jamii ambayo yamekusanywa kwa vizazi kadhaa na yanayoendelea kubadilika.
- **Kuimarisha elimu ili iwe rasilimali ya jamii.** Kama rasilimali ya jamii, elimu hujenga malengo ya pamoja na kuwawezesha watu na jamii kufanikiwa kwa pamoja. Mkataba mpya wa kijamii wa elimu unafaa uhakikishe kuwa gharama ya elimu inaenda kwa umma, na jamii yote inahusishwa kwa kiasi kikubwa kwenye majadiliano kuhusu elimu. Msisitizo huu katika ushiriki ndio unaoimarisha elimu kama rasilimali ya jamii - aina ya ustawi wa pamoja ambao umechaguliwa na kufikiwa kwa pamoja.

Kanuni hizi za msingi zimeundwa kutokana na kile ambacho elimu imeruhusu binadamu kufikia na kusaidia kuhakikisha kwamba tunapoelekea mwaka 2050 na kuendelea, elimu inawezesha vizazi vya baadaye kubadili mtazamo kuhusu mustakabali wao na kubadilisha ulimwengu wao.

## Kati ya ahadi za zamani na mustakabali usiotabirika

Ongezeko la ukosefu na usawa wa kijamii na kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa bioanuwai, matumizi ya rasilimali ambayo yanazidi kuathiri mfumo wa Dunia, kuzorota kwa demokrasia, na uharibifu wa teknolojia za mifumo ya kiotomati ni ishara za mahali tulipofikia sasa kihistoria. Migogoro na changamoto hizi nyingi zinazoingiliana huathiri haki zetu za binafsi na za pamoja na kusababisha uharibifu wa maisha mengi ulimwenguni. Ingawa upanuzi wa mifumo ya elimu umeleta fursa kwa wengi, idadi kubwa imebaki kupata elimu yenye ubora wa viwango vya chini.

Mustakabali unaonyesha kuwa hali inayotukabili ni mbaya. Taswira tuliyonayo ni ya Dunia iliyo na nafasi chache za makazi ya binadamu. Kuna uwezekano wa hali kozorota kiasi kwamba wale watakaoweza kupata elimu bora siku zijazo itakuwa matajiri ilhali watu wengi wataishi kwa taabu na kukosa mahitaji ya lazima. Je, tofauti za sasa za elimu zitazidi kuwa mbaya hadi mitaala itakuwa haina umuhimu tena? Je, mabadiliko haya yataathiri vipi msingi wetu wa ubinadamu?

Hakuna mwelekeo usioweza kubadilika. Njia mbadala za mustakabali zinawezekana, na mabadiliko ya kutatiza yanaweza kutambuliwa katika maeneo kadhaa:

- Dunia iko hatarini lakini hatua za kupunguza kaboni na kufanya uchumi kuwa endelevu zinaendelea. Watoto na vijana tayari wanaongoza njia kwa kupigania mabadiliko na kuwalaumu wale wanaokataa kukabiliana kwa uharaka na hali inayotukabili.
- Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, ulimwengu umeshuhudia kuzorota kwa demokrasia na kushamiri kwa hisia zinazo ambatana na utambulisho unaotokana na umaarufu mkubwa. Vile vile, ushirikishwaji wa raia umeshamiri, na vita dhidi ya ubaguzi na udhalimu vimenawiri.
- Teknolojia za dijitali zina uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa, lakini hatujafikiria jinsi ya kutekeleza ahadi hizi nyingi.
- Changamoto ya kubuni kazi za staha zinaelekea kuwa ngumu zaidi kwani Akili Mnemba (AI), teknolojia za otomatiki, na mabadiliko ya kimuundo yanabadilisha taswira ya ajira kote ulimwenguni. Wakati huo huo, watu kutoka jamii mbalimbali wanatambua thamani ya kazi za utunzaji na njia nyingi ambazo zinaweza kufanikisha usalama wa kiuchumi.

Kila mojawapo ya matatizo haya ibuka yanaathiri elimu. Kile tunachofanya kwa pamoja kitachangia matokeo ya elimu.

Kwa sasa namna tunavyopanga elimu ulimwenguni haisadii katika kuhakikisha tuna jamii zenye haki na amani, Dunia yenye mazingira mazuri, na maendeleo ya pamoja ambayo yanawanufaisha wote. Kwa hakika, baadhi ya matatizo yetu yanatokana na jinsi tunavyoelimisha. **Mkataba mpya**

**wa kijamii wa elimu unahitaji kuturuhusu kufikiria tofauti** kuhusu ujifunzaji na uhusiano kati ya wanafunzi, walimu, maarifa, na Dunia.

## Mapendekezo ya kubadilisha elimu

**Ufundishaji unastahili kuandaliwa kulingana na kanuni za ushirikiano, kusaidiana, na mshikamano.** Unapaswa kuwasaidia wanafunzi ili wajikuze kiakili, kijamii, na kimaadili na waweze kufanya kazi pamoja katika kubadilisha ulimwengu kwa hisia na huruma. Pia, wanastahili kujifunza jinsi ya kutupilia mbali upendeleo, chuki, na migawanyiko. Tathmini inapaswa kuonyesha malengo haya ya ufundishaji kwa njia zinazo himiza ukuaji mzuri na ujifunzaji wa wanafunzi wote.

**Mitaala inastahili kutilia mkazo ujifunzaji wa kiikolojia, kitamaduni, na wa taaluma mbalimbali ambazo zinawasaidia wanafunzi kupata na kuzalisha maarifa huku wakikuza uwezo wao wa kuyakosoa na kuyatumia.** Mitaala lazima iambatane na ufahamu wa kiikolojia wa binadamu ambao unasawazisha jinsi tunavyohusiana na Dunia kama sayari yenye viumbe hai na ambayo ni makao yetu. Uenezaji wa habari potofu unapaswa kupingwa kupitia maarifa ya kisayansi, kidijitali, na ya kibinadamu ambayo yanakuza uwezo wa kutofautisha uongo na ukweli. Katika maudhui ya elimu, mbinu, na sera, tunapaswa kuhimiza uraia wa ushirikiano katika shughuli za kijamii na kidemokrasia.

**Ufundishaji unapaswa kuboreshwa ili uwe jitihada za ushirikiano ambapo walimu wanatambulika kwa kazi yao kama watayarishaji wa maarifa na wahusika wakuu katika mageuzi ya kielimu na kijamii.** Ushirikiano na kazi ya pamoja ni vipengele muhimu vinavyostahili kubainisha kazi ya walimu. Tafakari, utafiti, uundaaji wa maarifa, na taratibu mpya za ufundishaji ni muhimu katika ufundishaji. Hii ina maana kwamba lazima uhuru wao wa kujitawala uungwe mkono na lazima washiriki kikamilifu katika mijadala na mazungumzo ya umma kuhusu mustakabali wa elimu.

**Shule zinahitaji kulindwa kama maeneo ya elimu kwa sababu zinaimarisha ujumuishaji, usawa, na ustawi wa kibinafsi na wa pamoja – na pia zinastahili kubadilishwa ili zichangie katika mabadiliko yatakayoleta mustakabali wenye haki, usawa, na uendelevu.** Shule zinahitaji kuwa sehemu zinazokutanisha vikundi tofauti vya watu pamoja na kuwapatanisha na fursa na changamoto ambazo hawawezi kuzipata mahali pengine. Ili kuhamasisha ushirikiano baina ya wanafunzi, lazima mabadiliko yafanywe katika majengo ya shule, nafasi, muda, ratiba, na makundi ya wanafunzi. Teknolojia za dijitali zinapaswa kulenga kukamilisha - na sio kuwa mbadala wa shule. Shule zinapaswa kuwa modeli ya mustakabali bora kwa kulinda haki za binadamu na kuwa vielelezo vya uendelevu kwa kupunguza au kutotoa kaboni.

**Tunapaswa kutumia na kupanua fursa ili elimu iendelezwe katika maisha yote na katika maeneo tofauti ya kitamaduni na kijamii.** Wakati wote wa maisha watu wanapaswa kuwa na fursa za elimu zenye manufaa na ubora. Tunapaswa kuunganisha nafasi za asili za ujifunzaji, zilizo jengwa, na za kidijitali tukizingatia uwezo wa kila mojawapo ya nafasi hizo. Majukumu muhimu yanastahili kufanywa na serikali: uwezo wa kugharamia na kudhibiti elimu ya umma unapaswa

kuimarishwa. Haki ya elimu inahitaji kupanuliwa ili ipatikane katika hatua zote za maisha na ijumuishe haki za kupata habari, utamaduni, sayansi, na kuunganishwa.

## Kuharakisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Mabadiliko makubwa na uvumbuzi ni mambo yanayowezekana. Tutajenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu kupitia kwa mchango wa mamilioni ya watu na utendaji wa pamoja - vitendo vya ujasiri, uongozi, upinzani, ubunifu, na utunzaji. Mkataba mpya wa kijamii unahitaji kukabiliana na ubaguzi, unyimwaji wa fursa, na utengwaji. Tunapaswa kujitolea ili kuhakikisha kuna usawa wa jinsia na haki za wote bila kujali rangi, kabila, dini, ulemavu, ujinsia, umri, au uraia. Kujitolea kwa kiasi kikubwa kunahitajika katika mijadala ya jamii, kufikiri, na shughuli za pamoja.

**Kauli mbiu ya kufanya utafiti na uvumbuzi**. Mkataba mpya wa kijamii unahitaji programu ya utafiti inayoshirikisha wadau ulimwenguni kote na ambayo inazingatia haki ya kupata elimu katika maisha yote. Programu hii lazima izingatie haki ya kupata elimu na ijumuishe aina tofauti za ushahidi na mbinu za kujua kama vile wanafunzi kufunzana na kubadilishana maarifa kutoka nchi mbalimbali. Michango inapaswa kukaribishwa kutoka kwa kila mtu - kutoka kwa walimu hadi wanafunzi, kutoka kwa wasomi na vituo vya utafiti hadi serikali na asasi za kiraia.

**Kauli mbiu ya mshikamano wa ulimwengu na ushirikiano wa kimataifa.** Mkataba mpya wa kijamii wa elimu unahitaji ahadi mpya za ushirikiano wa kimataifa katika kusaidia elimu kama rasilimali ya jamii, yenye msingi wa haki za binadamu na ushirikiano wenye usawa miongoni mwa watendaji wa serikali na wasio wa serikali. Zaidi ya mtiririko wa misaada ya elimu kutoka nchi za Kaskazini kwenda nchi za Kusini, uzalishaji wa maarifa na ushahidi kupitia ushirikiano wa Nchi za Kusini na ushirikiano wa pembetatu lazima uimarishwe. Jumuiya ya kimataifa ina jukumu muhimu la kutimiza katika kusaidia watendaji wa serikali na wasio wa serikali kufanikisha malengo ya pamoja na viwango vinavyohitajika ili kufikia mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Kanuni ya ushirikiano inapaswa kuheshimiwa, na jitihada za maeneo, kitaifa, na kikanda zinapaswa kuhamasishwa. Mahitaji ya elimu ya wanaotafuta hifadhi, wakimbizi, watu wasio na utaifa, na wahamiaji, yanahitaji kufadhiliwa kupitia ushirikiano wa kimataifa na kazi za taasisi za kimataifa.

**Ushirikishwaji wa vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu katika kila kipengele cha kuandaa mkataba mpya wa kijamii wa elimu.** Kuanzia kuunga mkono utafiti na maendeleo ya sayansi hadi kuwa mchangiaji katika taasisi na programu zingine za elimu kwenye jamii zao, vyuo vikuu vyenye ubunifu na uvumbuzi, na ambavyo vimejitolea kuimarisha elimu kama rasilimali ya jamii vina jukumu muhimu la kutimiza katika mustakabali wa elimu.

**Ni muhimu kila mtu aweze kushiriki katika ujenzi wa mustakabali wa elimu** - watoto, vijana, wazazi, walimu, watafiti, wanaharakati, waajiri, viongozi wa mila, na viongozi wa dini. Tuna utajiri wa tamaduni unaoweza kutusaidia katika ujenzi huu. Binadamu wana uwezo mkubwa wa utambuzi wa pamoja, akili, na ubunifu. Na sasa tunakabiliwa na chaguo zito: kuendelea kwa njia isiyo endelevu au kubadilisha mwelekeo wetu.

Ripoti hii inapendekeza majibu kwa maswali matatu muhimu ambayo ni: Tunapaswa kuendelea kufanya nini? Tuache nini? Ni nini kinahitaji kufikiriwa upya na kwa ubunifu? **Lakini mapendekezo haya ni mwanzo tu**. Ripoti hii ni mwaliko wa kubuni na kufikiria zaidi badala ya kupanga tu. Maswali haya yanahitaji kuchukuliwa na kujibiwa katika jamii, nchi, shule, programu za elimu, na mifumo ya aina zote - ulimwenguni kote.

**Kuanzisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu ni hatua muhimu katika kubadilisha mtazamo wetu kuhusu mustakabali wetu wa pamoja.**

# Utangulizi

Tunakabiliwa na uhuru wa kuchagua: kuendelea kwenye njia isiyo endelevu au kubadilisha mwelekeo. Kuendelea katika njia ya sasa ni kukubaliana na ukosefu wa usawa na unyonyaji, kuongezeka kwa aina nyingi za ukatili, kusambaratika kwa mshikamano wa jamii na uhuru wa watu, uharibifu wa mazingira, na janga kubwa la kupotea kwa bioanuwai. Kuendelea katika njia ya sasa ni ushahidi wa kushindwa kufikiria na kushughulikia hatari zinazo ambatana na mabadiliko ya kiteknolojia na kidijitali.

Bila kuchelewa, tunahitaji kufikiria upya kuhusu mustakabali wetu na kuchukua hatua za kuufanikisha. Maarifa na ujifunzaji ni misingi ya mabadiliko mapya. Lakini tofauti za kimataifa - na mahitaji ya haraka ya kufikiria upya kwa nini, ni vipi, ni nini, ni wapi, na ni wakati gani tunajifunza - zinamaanisha kuwa elimu haisaidii katika ujenzi wa mustakabali wenye amani, haki, na uendelevu.

Sisi zote tuna wajibu kwa vizazi vya sasa na vijavyo - kuhakikisha kwamba Dunia yetu ina rasilimali ya kutosha, na kwamba kila mtu anapata haki za binadamu kwa ukamilifu. Licha ya kukabiliwa na shinikizo la kuchukua hatua kwa haraka na kuishi katika mazingira ya mashaka makubwa, tuna sababu ya kuwa na matumaini. Kama spishi, tuko katika awamu ya historia ambapo tuna nafasi kubwa ya kupata maarifa na zana zinazo tuwezesha kushirikiana. Uwezo wa kushirikisha binadamu katika kujenga mustakabali kwa pamoja upo na ni wa kutosha.

Elimu - namna tunavyopanga ufundishaji na ujifunzaji katika maisha yote - imechangia katika mabadiliko ya jamii za wanadamu kwa muda mrefu. Elimu huleta ushirikiano unaowezesha usambazaji wa maarifa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Kando na kutuunganisha na Dunia, elimu hutuunganisha na watu wengine; hutuweka wazi kwa matumaini mapya; na kuimarisha uwezo wetu wa mazungumzo na wa kuchukua hatua zinazostahili. Lakini ili kujenga mustakabali tunaoutaka, elimu lazima ibadilishwe.

Ripoti hii ya kimataifa kutoka kwa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu inaangazia jukumu la elimu katika ujenzi wa Dunia na mustakabali wa pamoja tunapoelekea 2050 na kuendelea. Mapendekezo inayowasilisha yanatokana na mchakato wa miaka miwili na ushirikiano wa kimataifa ambao ulionyesha kwamba idadi kubwa ya watu - watoto, vijana, na watu wazima - wanafahamu vyema kwamba tunategemeana. Tumeunganishwa kwa pamoja kiasi kwamba matatizo ya Dunia yanatuathiri sisi zote. Kuna mwamko mkubwa ulimwenguni kote kuhusu umuhimu wa kufanya kazi pamoja hasa katika kuthamini tofauti za kijamii.

Kutarajia mustakabali ni jambo tunalofanya wakati wote kama wanadamu. Mawazo kuhusu mustakabali yana nafasi muhimu katika fikra za kielimu, será na utendaji. Mawazo hayo huathiri mambo mengi kama vile maamuzi ambayo hufanywa na wanafunzi na familia na mabadiliko ya elimu ambayo hutekelezwa na wizara za elimu.

Ripoti hii inatambua kwamba elimu ina uhusiano wa kina na matukio ya siku za usoni kama mabadiliko makubwa na migogoro mikubwa. Inaeleza kwamba lengo kuu la kufikiria kuhusu mustakabali wa elimu ni kutuwezesha kubadili hali ya sasa, kubainisha mienendo ambayo inaweza kujitokeza, na fursa tutakazo kumbana nazo. Mustakabali unazua maswali mazito kuhusu maadili, usawa, na haki - ni mustakabali gani unaohitajika na kwa ajili ya nani? Na kwa kuwa elimu haiathiriwi tu na mambo ya nje bali ina jukumu muhimu katika kujenga mustakabali unaotakiwa katika pembe zote za Dunia, ni jambo la kawaida na la lazima kufikiria upya mustakabali wetu unaohusisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

> Mustakabali unazua maswali mazito kuhusu maadili, usawa, na haki - ni mustakabali gani unaohitajika na kwa ajili ya nani?

# Uhai wa binadamu, haki za binadamu, na Dunia hatarini

Kuna vitu ambavyo viko hatarini: hadhi ya kibinadamu; haki za msingi za kila mtu; na afya ya mazingira ya Dunia ambayo ni mahali petu pa kuishi. Ili kubadilisha mkondo na kufikiria mustakabali mbadala, tunahitaji kupanga kwa haraka uhusiano baina yetu sisi kama binadamu na uhusiano wetu na ulimwengu wa teknolojia. Lazima tujifunze upya kuhusu kutegemeana kwetu na jukumu letu kama binadamu walio kwenye Dunia iliyo na vitu vingine zaidi ya binadamu.

Tunakabiliwa na migogoro mingi ya kutatanisha. Ongezeko la ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa bioanuwai, matumizi ya rasilimali yanayolemea Dunia, kuzorota kwa demokrasia, vurugu kutoka kwa teknolojia za otomatiki, na ukatili. Migogoro hii ni ishara tosha kuhusu hali ya mambo ilivyo.

Mikondo ya maendeleo ni kama kweli kinzani: ni njia tata zinazo tuongoza kwenda kwa mustakabali usio endelevu. Ijapokuwa viwango vya umaskini ulimwenguni vimepungua, ukosefu wa usawa baina ya mataifa na ndani ya mataifa umeongezeka. Ukosefu wa usawa unashuhudiwa hadi kwa zile nchi zilizo na viwango vya juu zaidi vya maisha. Mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira hutishia uhai wa wanadamu na viumbe wengine wanaoishi kwenye Dunia. Watu wengi wanazidi kujihusisha kikamilifu na maswala ya umma, lakini maeneo mengi ulimwenguni yanakabiliwa na misukosuko ya kidemokrasia na mashirika yao ya kijamii hayako imara. Ingawa teknolojia imetuunganisha, inachangia migawanyiko na mivutano kwenye jamii. Janga la kimataifa la UVIKO-19 limeonyesha udhaifu tulionao. Migogoro na changamoto hizi hukandamiza haki zetu za kibinafsi na za pamoja na kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya chaguzi na matendo ya binadamu. Ukandamizaji huo hutokana na mifumo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi, ambapo faida za haraka hupatiwa kipaumbele kuliko zile zinazohitaji muda mrefu na maslahi ya wachache kupendelewa zaidi ya maslahi ya walio wengi.

Mifumo ya uchumi, hasa ile inayotumia rasilimali kwa njia ziziso endelevu, inachangia pakubwa katika mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira. Matokeo ya miundo ya uchumi inayotoa kipaumbele kwa faida za haraka na ufujaji wa rasilimali ni: ubinafsi uliokithiri, ushindani, na kutokuwa

na uwezo wa kuelewa hisia za wengine. Utajiri wa Dunia haujasambazwa kwa watu wote; kukithiri kwa ukosefu wa usawa wa kiuchumi kunadhoofisha mshikamano wa jamii zetu.

Wakati huu ambapo tunahitaji ushirikiano na mshikamano dhabiti ili kupambana na masuala ambayo hayatambui wala kuheshimu mipaka ya kisiasa, tunakumbwa na changamoto zinazo lemaza demokrasia kama udikteta, utengwaji, na misimamo mikali ya kisiasa. Kwa miongo kadhaa, juhudi zimetekelezwa katika kuunga mkono mashirika yanayoendeleza mikakati ya kupunguza migogoro na kuendeleza amani. Hata hivyo, migawanyiko ya kijamii na kisiasa inazidi kuongeza. Teknolojia mpya zimechangia matamshi ya chuki, usambazaji wa kiholela wa habari gushi, itikadi kali za dini, na uzalendo unaoimarisha ubaguzi. Utaratibu wa Dunia unaozingatia maadili ya kimataifa, yaliyo katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, unadhoofika. Dunia yetu inakabiliwa na tatizo la kudidimia kwa maadili linalothibitishwa na kuongezeka kwa ufisadi, ukatili, ubaguzi, na uhalalishaji wa ukatili.

Udhalilishaji unaotokana na ubaguzi wa aina mbalimbali na stahamala duni huzidishwa na matukio kama utandawazi wa kasi, ongezeko la uhamaji (ukiwemo uhamaji wa kulazimishwa) na kupoteza kwa makazi. Ukatili huu unaodhoofisha hadhi ya ubinadamu hutokana na miundo ya mamlaka iliyoundwa ili kutekeleza malengo ya kutawala wengine badala ya kushirikiana nao na kuwakomboa. Migogoro ya kivita, uvamizi, na ukandamizaji wa kisiasa haiharibu maisha tu bali huhatarisha hadhi ya binadamu. Mara kwa mara, wale wanaopendelewa na kunufaika kutokana na mifumo ya utawala hubagua wengine kwa misingi ya jinsia, rangi, kabila, lugha, dini, au ujinsia, na kukandamiza makundi wanayoyaona kuwa tishio, iwe ni wenyeji asili, wanawake, wakimbizi, wahamiaji, wanaharakati wa masuala ya wanawake, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati wa mazingira, au wapinzani wa kisiasa.

Mabadiliko ya dijitali yanaathiri maisha yetu na ya jamii kwa njia ambazo hazijawahi kushuhudiwa. Kompyuta zinabadilisha namna ambavyo maarifa yanaundwa, yanapatikana, yanasambazwa, yanathibitishwa, na yanatumiwa. Maarifa yanaweza kupatikana kwa urahisi, na njia mpya na bora za kupata elimu zinafunguka. Lakini hatari ni nyingi. Ujifunzaji unaweza kupungua au kuongezeka katika nafasi za kidijitali; teknolojia inatoa ushawishi na udhibiti mpya wa madaraka ambao unaweza kukandamiza na kukomboa; na uvumbuzi wa teknolojia inayoweza kutambua nyuso za watu na Akili Mnemba unamaanisha kuwa haki yetu ya faragha inaweza kupunguzwa kwa njia ambazo hazikufikiriwa muongo mmoja uliopita. Tunahitaji kuwa makini ili kuhakikisha kwamba mabadiliko ya kidijitali yatatuimarisha na hayatahatarisha mustakabali wa mbinu mbalimbali za kujua au uhuru wa kiakili na wa kubuni.

Njia zetu za kuishi haziwiani na sayari na maisha ya viumbe wote wanaotegemeana; kwa hiyo, maisha yetu ya sasa na ya siku za usoni yamo hatarini. Mara nyingi, utumiaji wetu wa teknolojia hututia kwenye hatari kubwa ya kututenganisha na kupunguza mazungumzo ya kuleta uelewano. Utumiaji wa teknolojia usio bora huchangia kusambaratika kwetu kupitia njia mbalimbali: ukosefu wa usawa; kuvunjika kwa matumaini na nia njema; kudhalilisha walio tofauti nasi; na kupunguza moyo wa kushirikiana katika kukabiliana na changamoto zinazotukumba kama binadamu.

Ukiangalia mustakabali, unapata picha ambayo haipendezi. Unaona picha na sayari iliyo dhoofika kiasi kwamba binadamu wengi hawana mahali pa kuishi. Kuna picha ya ulimwengu ambao

masomo bora ni ya matajiri ilhali watu wa kawaida wanashindwa kujikimu kimaisha kiasi kwamba hata kununua mahitaji ya kila siku ni tatizo kubwa. Je, kuna uwezekano kuwa mitaala ya elimu itazidi kupoteza umuhimu wao na ukosefu wa usawa tunaokabiliana nao saa hivi utaongeza? Je, ubinadamu wetu utaharibiwa zaidi?

> Maamuzi tunayofanya sasa ndiyo yataamua mustakabali wetu sisi wote.

Maamuzi tunayofanya sasa ndiyo yataamua mustakabali wetu sisi wote. Maswali tunayopaswa kujiuliza ndiposa tuweze kufikia malengo yetu ni: Maamuzi yetu yatachangia kuishi kwetu au kuangamia kwetu? Tutaishi kwa amani au tutaruhusu maisha yetu yasongwe na vurugu? Mahusiano yetu na Dunia yatakuwa endelevu au yasiyo endelevu?

# Umuhimu wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Mabadiliko katika jamii hutokana na misingi ya elimu. Elimu hutupatia maarifa ambayo hutusaidia kuishi katika ulimwengu ulojawa na mashaka na unaobadilika kwa kasi mno. Elimu ina uwezo wa kuunganisha walimwengu na kuleta fursa nyingi za maendeleo. Elimu huwaleta watu pamoja ili waweze kushughulikia changamoto zinazokumba jamii kwa jumla. Elimu huchangia maarifa ya sayansi na uvumbuzi tunaohitaji ili tuweze kukabiliana na changamoto za kawaida. Elimu hukuza uelewano na kuunda misingi ya mustakabali unao jumuisha watu wote na ulio na haki za kiuchumi na uelendevu wa mazingira.

Familia, jumuiya, na serikali ulimwenguni zinafahamu vyema kuwa ingawa kuna upungufu katika shule nyingi, mifumo ya elimu ina uwezo wa kuchangia katika maendeleo ya kibinafsi na ya jamii zote. Serikali zinakubaliana na mashirika ya kijamii kuwa elimu ni mojawapo ya nguzo zinazochangia pakubwa katika maendeleo, ukuzaji wa ujuzi wa kutenda kazi, na kuchangia vile raia hujishughulisha na mambo ya demokrasia. Elimu ni nguzo kuu katika Miundombinu ya Maendeleo Endelevu (2030) - hii ni dira jumuishi inayolenga kufanikisha haki za binadamu, amani, na mahusiano endelevu na mazingira.

Kufikia sasa, elimu ulimwenguni kote haijaweza kufikia viwango vinavyostahili. Licha ya mikakati ya kusambaza elimu kuongezeka ulimwenguni, kuna mamilioni ya watoto, vijana, na watu wazima ambao hawajaweza kuipata. Ubaguzi kulingana na jinsia, lugha anayozungumza mtu, utamaduni wa mtu, na njia za ufundishaji umekithiri. Tatizo la kupata elimu huongezwa na changamoto za ubora: Aghalabu, masomo hayaambatani na matarajio ya watoto, vijana, na jamii zao. Mafunzo ulimwenguni huzuia ubunifu na uvumbuzi wa wanafunzi. Mbinu za ufundishaji zinazotumiwa haziwapatii wanafunzi motisha wanayohitaji ili kushiriki kikamilifu katika masomo. Vile vile, elimu haiwatayarishi vya kutosha kwa changamoto za maisha.

Isitoshe mifumo ya elimu inachangia na kuendeleza hali zinazotishia mustakabali wetu - hali zinazopunguza uwezo wa kuleta mabadiliko kupitia kwa elimu ni kama ubaguzi, kutojumuishwa, na mienendo ya maisha isiyo endelevu. Changamoto hizi zinasisitiza umuhimu wa kuwa na dira na kanuni mpya ili tuweze kubadilisha elimu na matokeo yake.

Mkataba wowote wa elimu huanza na dira inayojumuisha madhumuni ya jamii. Mkataba wa elimu una kanuni msingi zinazoongoza mifumo ya elimu na vipengele tofauti vinavyohitajika ili kujenga, kutunza, na kuboresha kanuni hizo.

Elimu ya karne ya ishirini ililenga kuboresha uraia na kuleta maendeleo. Ilikuwa ni lazima kila mtoto au kijana aende shuleni. Leo hii, lazima tujenge elimu upya ili tuweze kupata maarifa murua yanayoendana na changamoto tulizonazo. Lazima tuwe na mkataba mpya wa kijamii wa elimu inayoangazia mambo yanayotuhusu sisi wote na kuendeleza maarifa na ubunifu kwa kujenga mustakabali wenye haki za kijamii, kiuchumi, na kimazingira.

Ili kufanikisha mkataba mpya lazima tuchunguze kwa kina jinsi ambavyo mitazamo yetu kuhusu elimu hufunga njia ambazo zitatufikisha kwenye mustakabali tunaoutamani. Kupanuliwa kwa mfumo wa elimu uliopo hakutatusaidia kikamilifu. Matatizo yetu hayatokani na upungufu wa rasilimali tu, yanatokana na miundo msingi ya elimu na mbinu za ufundishaji.

# Ufafanuzi mpya wa madhumuni ya elimu

Mifumo ya elimu imetupotosha kwa vile huwa inapatia kipaumbele faida za haraka badala ya kuangazia uendelevu wa faida tutakazozipata baada ya muda mrefu. Badala ya kusisitiza maadili kama kushikamana, uelewano, kutegemeana kwetu, na umuhimu wa kujaliana na kujali Dunia, mifumo hiyo huhimiza ubinafsi na mashindano ya kiuchumi baina ya nchi.

Elimu inapaswa kutuunganisha na kutuongezea maarifa, sayansi, na ubunifu unaohitajika ili kuunda mustakabali endelevu utakaozingatia haki za kijamii, kiuchumi, na kimazingira. Tunapojitayarisha kwa mabadiliko ya kimazingira, kiteknolojia, na kijamii, elimu inapaswa kuangazia na kurekebisha dhuluma za kitambo.

Mkataba mpya wa kijamii wa elimu unapaswa kujikita katika kanuni mbili za msingi: (1) haki ya kupata elimu na (2) ahadi ya kuibadilisha elimu ili iwe rasilimali ya jamii inayowanufaisha watu wote.

## Kuimarisha haki ya kupata elimu bora katika hatua zote za maisha

Mazungumzo yanastahili kufanywa na hatua zinafaa kuchukuliwa ili tuweze kuunda mkataba mpya wa kijamii wa elimu unaojikita katika ulinzi wa haki za binadamu. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu lililoandikwa mwaka 1948 linaweka wazi zile haki ambazo haziwezi kuondolewa na mtu yeyote. Azimio hilo linatupatia dira bora ya kubadilisha mustakabali wa elimu. Haki ya kupata elimu - ambayo ni muhimu katika kufanikisha haki zingine za kijamii, kiuchumi, na kitamaduni - inastahili kutumiwa kama mwongozo na msingi wa mkataba mpya wa kijamii. Kulingana na mtazamo wa haki za binadamu, watu wote wanapaswa kupata elimu bila kuzuiliwa na kipato, jinsia, kabila, dini, lugha, utamaduni, ujinsia, misimamo ya kisiasa, ulemavu, au sifa zingine ambazo zinaweza kutumika ili kubagua na kutenga.

> Mazungumzo yanastahili kufanywa na hatua zinafaa kuchukuliwa ili tuweze kuunda mkataba mpya wa kijamii wa elimu unaojikita katika ulinzi wa haki za binadamu.

Haki ya kupata elimu inapaswa kupanuliwa ili ijumuishe haki ya kupata elimu iliyo bora katika hatua zote za maisha. Kwa muda mrefu, haki ya kupata elimu iliangazia na kuzingatia masomo ya watoto na vijana pekee, tunaposonga mbele, haki ya kupata elimu lazima iangazie na kulinda watu wa marika yote. Mtazamo huu wa kina unamaanisha kwamba haki ya kupata elimu inahusiana na haki ya kupata na kuchangia kwa maarifa ya kijamii, ambayo huwezesha binadamu kupanua uwezo wao wa kufikiria.

Uvumbuzi wa kisayansi hutokana na mashindano, mazungumzo, na mijadala inayolenga kukuza elimu. Zaidi ya kuwa kipengele muhimu cha elimu, uvumbuzi ni mojawapo ya rasilimali yenye thamani kubwa kwa binadamu. Maarifa ya kijamii huongezeka wakati watu wengi wanayajua na wanayapata kwa urahisi. Kukua kwa lugha, hesabu, na mifumo ya uandishi kumewezesha maarifa kuenea kwa muda mrefu. Kwa hiyo, jamii mbalimbali zimeweza kustawi na kuendelea. Matokeo yanayoweza kutokana na maarifa ya kijamii hayawezi kuhesabika. Maarifa ya kijamii huibua utofauti na uvumbuzi kupitia kwa ukopaji wa maarifa, majaribio yanayolenga nyanja mbalimbali, na uundaji wa maarifa mapya kwa kuyatafsiri upya mambo ya zamani.

Kwa bahati mbaya, kuna vikwazo ambavyo huwazuia wengi ambao wangependa kuchangia na kuyatumia maarifa ya kijamii. Ni muhimu kurekebisha dosari zilizopo katika maarifa ya kijamii. Kwa muda mrefu, mitazamo inayohusiana na mambo, lugha, na maarifa ya asili imekuwa ikipuuzwa. Wanawake, wasichana, walio wachache, na wenye kipato cha chini wana uwakilishi mdogo sana. Vikwazo vingi ni matokeo ya unyonyaji na sheria kali za kulinda umiliki wa uvumbuzi na ukosefu wa kanuni za kulinda mifumo ya kudhibiti maarifa ya kijamii. Tunapaswa kulinda umiliki wa wasanii, waandishi, wanasayansi, na wavumbuzi. Vile vile, lazima tujitolee kutetea fursa za kutumia na kuunda maarifa. Kwa muktadha wa haki za umiliki wa kijamii, maarifa ya jamii za asili na makundi ya walio wachache yanapaswa kulindwa ili yasiibiwe na kutumiwa vibaya bila idhini yao.

Haki ya kupata elimu inayolenga marika yote inaweza kufikiwa wakati ambapo visuizi vyote vimeondolewa ili maarifa ya kijamii yawe rasilimali inayoweza kudumu milele na kutumiwa na mtu yeyote; maarifa hayo yanapaswa kuangazia maudhui yote kuhusu ulimwengu.

## Kuimarisha elimu ili iwe mradi wa umma na rasilimali ya jamii

Wakati elimu ni rasilimali ya jamii, inakuwa rahisi kuwa na madhumuni yanayowaunganisha watu; hii huwezesha watu binafsi na jamii nzima kustawi. Mkataba mpya wa kijamii wa elimu unastahili kuhakikisha kuwa elimu inapata ufadhili wa kutosha, na kila mtu kwenye jamii anachangia kwenye mazungumzo yanayolenga elimu. Mchango wa kila mtu kwenye jamii lazima usisitizwe kwa vile ndio unaimarisha elimu ndiposa iwe rasilimali ya jamii - hii rasilimali lazima ikuzwe na kutafutwa na watu wote.

Vipengele viwili muhimu vinabainisha kuwa elimu ni rasilimali ya jamii. Kwanza, elimu hufanikisha uhusiano baina ya binadamu na baina ya binadamu na Dunia. Watu binafsi na makundi hufanikisha shughuli za elimu katika taasisi za elimu zinazowaleta pamoja wadau kama walimu na wanafunzi. Kupitia kwa elimu, watu huweza kutumia na kuchangia maarifa kuhusu historia ya binadamu. Kwa vile elimu ni shughuli inayojumuisha watu wengi katika ukuzaji wa maarifa, elimu inainua hadhi ya watu binafsi na hadhi ya jamii zao. Vile vile, elimu hutumika katika kuwepo kwa madhumuni yanayounganisha, uwezo wa kushirikiana, na utu wetu. Kwa hiyo, ni muhimu kwa taasisi za elimu kujumuisha wanafunzi walio tofauti ili waweze kufunzana kuhusu tofauti zao.

Pili, elimu ipo chini ya uongozi mmoja. Kwa vile elimu ni mradi wa jamii, kuna wadau wengi wanaohusika katika kufanya maamuzi kuhusu usimamizi wake. Ni sharti mitazamo mbalimbali ijumuishwe katika michakato ya kuunda sera za elimu. Ushirikishwaji wa mashirika yasiyo ya serikali katika uundaji wa sera za elimu, utoaji wa elimu, na ufuatiliaji wa elimu ni ishara tosha kuwa elimu ni rasilimali ya jamii inayohitaji michango ya watu wengi, uwazi, na uwajibikaji mkubwa. Usawa, ubora, na umuhimu wa elimu unaweza kuimarishwa kwa kuhusisha walimu, vyama vya vijana, mashirika ya jamii, wadhamini, mashirika yasiyo ya serikali, makampuni ya biashara, vyama vya kitaaluma, wahisani, taasisi za dini, na mashirika yanayohusika katika harakati za kijamii. Wadau wasio wa kiserikali wametia fora katika kufanikisha haki ya kupata elimu kwa kukabili ubaguzi na kuimarisha usawa na haki.

Sifa za elimu ni zaidi ya utoaji, ufadhili, na usimamizi wake. Elimu ya umma (1) hufanikishwa katika maeneo ya umma (2) huchangia malengo ya umma (3) inahitaji uwajibikaji. Kando na kukabiliana na ubaguzi, shule za aina zote zinapaswa kuelimisha wanafunzi kuhusu haki za binadamu na umuhimu wa utofauti. Tusisahau kuwa elimu ya umma inaelimisha raia. Elimu huimarisha mshikamano unaotokana na sisi wote kuwa binadamu na kuishi kwenye sayari moja ambapo tunathamini utofauti wetu.

Ndiposa elimu iwe rasilimali inayowanufaisha watu wote, lazima usimamizi wake katika ngazi za kitaifa na kimataifa uwe jumuishi na shirikishi. Lazima serikali zizindue sheria zitakazolinda elimu dhidi ya wabepari wanaolenga kupata faida kwa kuiuza. Elimu ni haki ya binadamu ambayo haistahili kuuzwa kwenye masoko kama bidhaa. Elimu inastahili kuwanufaisha watu wote.

Ili tuweze kufanikisha mustakabali ulio endelevu katika maswala ya kijamii, kiuchumi, na kimazingira, lazima mkataba mpya wa kijamii wa elimu uhakikishe kila mtu anapata haki yake ya elimu na ubadili elimu ili iwe rasilimali ya jamii. Kanuni hizi za msingi zitachangia mazungumzo kamilifu

kuhusu vipengele vya elimu vinavyostahili kubadilishwa kuanzia ufundishaji, mitaala, utafiti, na ushirikiano baina ya mataifa.

# Mpangilio wa ripoti

Ripoti hii imepangwa katika sehemu tatu kuu: kila sehemu inajumuisha sura kadhaa zinazotoa mapendekezo kuhusu uundaji wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu; kanuni za kuongoza mazungumzo yanayohusiana na mkataba huo; na hatua zinazostahili kuchukuliwa. Hitimisho la ripoti hii linatoa mapendekezo kuhusu ufanikishaji wa hatua hizo katika miktadha tofauti. Ripoti hii inarejelea ushahidi wa utafiti uliopo kwenye ripoti mbalimbali: baadhi ya ripoti hizo hazijajumuishwa kwenye sehemu ya marejeleo. Makala rasmi yaliyochaguliwa ili kufanikisha ripoti hii yameorodeshwa katika sehemu ya viambatisho.

Sehemu ya kwanza ya ripoti, "Ahadi za kitambo dhidi ya mustakabali usiotabirika," ina sura mbili zinazoangazia changamoto zinazotokana na mambo ya usawa na umuhimu wa elimu. Sura hizi mbili zinatilia mkazo umuhimu wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu kwa sababu ndio tu unaweza kutatua ubaguzi katika mambo ya elimu na kuhakikisha kuwa mustakabali wetu una uendelevu.

Sura ya kwanza inasimulia matukio ambayo yamechangia katika kutotimizwa kwa ahadi zilizo kwenye Kifungu cha 26 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu. Sura ya 2 inafafanua vurugu na matukio ibuka ambayo yamechangia mabadiliko katika sehemu nne kuu: mazingira, teknolojia, uongozi, na msambaratiko wa jamii na mazingira mapya ya kazi. Sura hizi zinaelezea jinsi ambavyo elimu itakuwa imeathirika kufikia mwaka 2050.Pia sura hizi zinatoa mapendekezo kuhusu mabadiliko yanayohitajika ili kushughulikia athari hizo.

Sehemu ya pili ya ripoti, "Kubadilisha elimu," inapendekeza kuwa elimu inafaa kuboreshwa kwa kuangazia vipengele vitano: ufundishaji, mitaala, ualimu, shule, na haki ya kupata elimu katika kila hatua ya maisha na katika nafasi tofauti za kitamaduni na kijamii. Kila kipengele kina sura yake. Katika sura hizo tano, maudhui kuhusu mazungumzo na hatua sahihi yameangaziwa.

Kauli mbiu ya sura ya tatu inahusiana na kufanikisha kwa ufundishaji ulio na misingi ya ushirikiano, uelewano, heshima kwa utofauti, na huruma ndiposa tuweze kubadilisha jinsi ambavyo watu wanaungana ili wajibadilishe wao binafsi na wabadilishe ulimwengu. Sura ya nne inaunga mkono mitaala inayogusia maswala ya ikolojia, tamaduni, na nyanja tofauti kwa vile itawasaidia wakufunzi kupata maarifa mazuri na kuyatumia kwa weledi katika maisha yao. Sura ya tano inasisitiza kuwa walimu ni nguzo inayoleta mabadiliko ya jamii; kwa hivyo, lazima elimu yao iboreshwe na kufanikishwa kwa njia za ushirikiano. Sura ya tano inasisitiza kuwa shule ni maeneo ya umma yanayostahili kulindwa vizuri ili yaweze kukuza elimu, ujumuishaji, usawa, na ustawi wa watu binafsi na jamii nzima. Vile vile, kulinda shule itakuwa njia ya kuleta mustakabali endelevu. Sura ya saba inafafanua kuwa elimu inaweza kufanikishwa wakati wowote na mahali pengine pengi kando na taasisi za elimu.

Sehemu ya tatu ya ripoti, "Kuharakisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu," inatoa maelezo kuhusu misingi inayohitajika katika mkataba huo: utafiti, mshikamano, na ushirikiano wa kimataifa.

Sura ya nane inatoa wito kuhusu utafiti utakaowawezesha watu kupata haki ya elimu katika umri wowote. Kila mtu ana jukumu la kuzalisha maarifa na kuhusika katika mashauriano yatakayoleta mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Sura ya 9 inajadili umuhimu wa kuimarisha ushirikiano, uthabiti, na ujasiri tunapopiga taswira ya mwaka 2050 na miaka itakayofuata.

Hitimisho la ripoti hii linaeleza kwamba kuna uwezekano wa kujumuisha mapendekezo yaliyojadiliwa humu kwenye programu za elimu. Mabadiliko yatatokana na michakato inayohusisha mazungumzo baina ya wadau. Kushirikisha wadau wote kutachangia pakubwa katika utekelezaji wa hatua zilizopendekezwa. Ni jukumu la viongozi katika ngazi mbalimbali za serikali, wasimamizi wa elimu, walimu, wanafunzi, familia, jamii, na asasi za kiraia kuimarisha elimu.

Jukumu linalotukabili sasa hivi ni kuimarisha mazungumzo (ya kimataifa) kuhusu mikakati bunifu itakayotuwezesha kuzidisha ubora wa elimu ulimwenguni kote. Tunalichukulia kama jukumu la kuimarika: kutumia mbinu mpya katika kukabili makali ya shida tulizonazo kama binadamu walio kwenye Dunia yenye viumbe wengine kando na binadamu. Kusema kweli, tunajua fika kwamba tuko katika hali mbaya; ishara kama kuzorota kwa hali ya hewa na mifumo ya ikolojia zinamaanisha tunapaswa kuchukua tahadhari. Kuimarika inamaanisha kwamba tutatumia maarifa, ambayo tuliyapata kwa jasho, katika kuthibiti mifumo ya elimu ndiposa iwe imara. Ili tuweze kufanikiwa lazima tutumie maarifa tuliyonayo katika kubuni maarifa mapya.

Kwa muda mrefu sasa, mkataba mpya wa kijamii wa elimu umekuwa ukiangaziwa. Kinachohitajika sasa ili tuweze kuufanikisha ni mazungumzo zaidi na wadau wote. Ripoti hii ni mwaliko wa kutimiza ajenda ya mazungumzo na hatua za kufikia lengo la mkataba huo.

Ripoti hii ni mwaliko wa kutimiza ajenda ya mazungumzo na hatua za kufikia lengo la mkataba huo.

# SEHEMU I

## Ahadi za kitambo dhidi ya mustakabali usiotabirika

Ili tuweze kutafakari mustakabali wa elimu kwa utimilifu, lazima tuchunguze hali ya elimu ilivyo kwa sasa na mabadiliko na changamoto zitakazo athiri mustakabali huo. Elimu inafanana mambo mengine ya kimaisha kwa vile inaathiriwa na mambo ya kale. Tunahitaji kuzingatia historia wakati tunapotafakari. Tunaweza kuelewa ni kwa nini elimu imevunja matumaini yetu baada ya kuchunguza upungufu wa elimu ya zamani.

Sehemu ya kwanza ya ripoti hii inaweka elimu ya ulimwengu mzima kwenye muktadha wa maswala ya usawa, haki, na uendelevu - vile vile, inachanganua jinsi ambavyo maswala haya yatabadilika katika siku za usoni. Inaonyesha kuwa elimu iko katika njia panda: baina ya ahadi za zamani na mustakabali usiotabirika.

Sura ya kwanza inaelezea maendeleo ya elimu katika kipindi cha miaka 50 iliyopita. Inafafanua vile mambo kama ukuaji wa uchumi, ufukara, na ubaguzi wa jinsia huingiana na kuathiriwa na maendeleo ya elimu. Inasisitiza kuwa yaliyopita hayawezi kupuuzwa; yatakayojiri kwa takribani miaka 30 ijayo, yatategemea maamuzi tunayoyafanya leo.

Sura ya pili inaangazia mabadiliko ibuka yanayoshuhudiwa katika mazingira, teknolojia, siasa, na mustakabali wa kazi. Ingawa haiwezekani kutabiri hali itakavyokuwa mbeleni, mamilioni ya watu wanakubaliana kuwa mabadiliko ibuka hayastahili kupuuzwa.

# Sura ya 1

## Mustakabali wa elimu inayoleta usawa

Mfumo wa elimu yetu unapaswa kuhimiza malengo ya kuishi pamoja kama jamii, na kufanya kazi pamoja ndiposa sisi zote tuweze kunufaika. Elimu inastahili kuwezesha vijana kuchangia katika ukuaji wa jamii yenye haki ambapo kila mtu anapata mgawo anaostahili, na jamii ambayo maendeleo yanapimwa kwa kuangalia ustawi wa kila mtu na sio bidhaa za bei ghali kama nyumba za kifahari, magari, na vitu vingine vinavyoweza kumilikiwa na mtu binafsi au umma. Kwa hiyo, elimu yetu inahitaji msingi wa umoja ndiposa uwasaide wanafunzi kukubali maadili ambayo yatachangia mustakabali bora.

**Julius Nyerere**, *Education for Self-Reliance*, 1967.

Je, katika kipindi cha miaka thelathini hadi miaka hamsini iliyopita, ni matukio gani yametokea kwenye elimu? Taswira ya elimu ni ipi kwa sasa? Elimu inahitaji kubadilishwa vipi tunapojitayarisha kwa mustakabali?

Bado kuna upungufu katika upatikanaji na ushirikishi: upungufu huo ni matokeo ya unyanyasaji na ubaguzi uliotekelezwa siku za nyuma.

Sura hii inatoa mitazamo miwili kuhusu matukio ya elimu kwa kipindi cha nusu karne kilichopita. Kwanza, inaelezea matukio ambayo yanaweza kuthibitishwa kutumia viashirio ambavyo vinalenga maeneo, viwango vya mapato, jinsia, marika, na mambo mengineyo. Pili, inachanganua matukio hayo kwa kutumia viashirio simulizi kama vile usawa, viwango, na jinsi ambavyo elimu imeweza kukabiliana na vurugu zinazotokana na vita na uhamaji.

Takwimu za muda mrefu haziwezi kueleza taswira kamili ya mambo ambayo hayawezi kuelezwa kwa kutumia hesabu. Hata hivyo, takwimu hutoa mwongozo unaoweza kuleta mabadiliko. Ijapokuwa mambo kama fursa za elimu, ushirikishwaji wa watu waliotengwa, kujua kusoma na kuandika, na uundaji wa mifumo ya ujifunzaji, yanaonekana kufanana, yana tofauti kubwa yanapowekwa kwa miktadha ya nchi, maeneo, na viwango vya mapato. Tunaweza kupata taswira ya mustakabali wa elimu kwa kuangalia matukio ya zamani na changamoto za sasa.

Ingawa tumeshuhudia maendeleo ya elimu kwa kipindi cha miaka hamsini iliyopita, bado kuna upungufu katika upatikanaji na ushirikishi: upungufu huo ni matokeo ya unyanyasaji na ubaguzi uliotekelezwa siku za nyuma. Maendeleo ya siku za usoni hayatategemea kurekebishwa kwa upungufu huo tu bali uchunguzi wa dhana na mipangilio iliyochangia upungufu huo. Kwa mfano, lengo la kupata usawa wa jinsia si lengo binafsi; linastahili kuwa msingi wa kujenga mustakabali wa elimu ulio endelevu.

## Ukosefu wa ukamilifu na usawa katika upanuzi wa elimu

Tangu haki ya kupata elimu iidhinishwe kuwa haki ya binadamu, hatua nyingi zimechukuliwa, ulimwenguni kote, ili kurahisisha upatikanaji wake. Wakati Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu lilipitishwa mwaka 1948, idadi ya watu ulimwenguni ilikuwa bilioni 2.4, huku 45% tu ya watu hao wakiwa wameenda shuleni. Leo hii, idadi ya watu ulimwenguni ikiwa bilioni 8, zaidi ya 95% wameenda shuleni. Usajiri wa wanafunzi mwaka 2020 ulipita 90% katika shule za msingi, 85% sekondari ya ngazi ya chini na 65% sekondari ya upeo. Kwa hiyo, katika miaka hamsini iliyopita ulimwengu umeshuhudia kupungua kwa idadi ya watoto na vijana balehe ambao hawaendi shuleni. Linalofurahisha ni kuwa upanuzi wa elimu ulitokea kipindi ambacho kulikuwa na ongezeko kubwa la watu. Zaidi ya mmoja kati ya watoto wanne alikuwa haendi shule ya msingi mwaka 1970, idadi hii ilipungua kwa 10% mwaka 2020. Wasichana ndio wameweza kustawi zaidi ukizingatia kwamba walikuwa theluthi mbili ya watoto waliokuwa hawaendi shuleni mwaka 1990. Usawa wa jinsia katika kupata elimu ya msingi umetimizwa. Katika nchi zote isipokuwa zile zilizo na umasikini

mkubwa na zilizoko Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wasichana hawana tena uwakilishi mkubwa katika idadi ya wasioenda shule.

Tangu mwaka 2000, ushirikishi katika elimu ya chekechea umeimarika ulimwenguni kote, maeneo yote, na nchi zote. Ushirikishi katika elimu ya chekechea uliongezeka kutoka 15% mwaka 1970, hadi 35% mwaka 2000 na hadi ya zaidi ya 60% mwaka 2019. Katika nchi za kipato cha juu na nchi za kipato cha wastani, ushirikishi katika elimu ya chekechea umeongeza zaidi na inakadiriwa kuwa kufikia mwaka 2050, kila mtu katika nchi hizo atakuwa amepata elimu ya chekechea. Ulimwenguni kote usawa wa jinsia umeongeza. Usawa huo umesuhudiwa katika elimu ya chekechea. Hii ni ishara nzuri inayoonyesha kuwa usawa huo utaendelea kushuhudiwa katika shule za msingi; marika yaliyo katika shule za chekechea sasa hivi yatapata nafasi ya kutia fora katika masomo ya msingi.

Kuanzia mwaka 1990 hadi 2020, nchi zote, tajiri na masikini, zimekuwa zikishuhudia ongezeko la idadi ya vijana na watu wazima walio na uwezo wa kusoma na kuandika. Asilimia ya wanaoweza kusoma katika nchi za kipato cha chini na zile za kipato cha wastani inalingana na ile ya nchi za kipato cha juu, na inapita 90. Katika kipindi cha miaka thelathini iliyopita, idadi ya wanawake walio na uwezo wa kusoma na kuandika imeongeza katika nchi zote. Katika nchi za kipato cha juu na zenye kipato cha wastani, kuna usawa wa jinsia kwa wale wanaoweza kusoma na kuandika. Hii ni hali nzuri mno inayoonyesha kuwa watu wazima, ulimwenguni kote, wanazidi kuimarika katika mambo ya elimu.

Katika miaka hamsini iliyopita, ushirikishi katika elimu ya ngazi za juu umeongezeka. Ushirikishi wa vijana na watu wazima, katika ulimwengu wote, uliongeza kutoka 10% mwaka 1970 hadi 40% leo hii. Ongezeko la ushirikishwaji linamaanisha kuwa idadi ya wanawake waliopata elimu ya ngazi za juu imeongeza kwa miaka hasmini iliyopita. Masomo ya ngazi za juu yalikuwa na wanaume wengi kipindi cha miaka ya 1970 na 1980; hata hivyo, usawa wa jinsia ulianza mwaka wa 1990; tangia hapo ushirikishwaji wa wanawake katika masomo ya ngazi za juu umekuwa ukiongezeka. Ongezeko hili limeshuhudiwa katika nchi zote ijapokuwa zile za Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara ambapo 7% ya wanafunzi wa kike na 10% ya wanafunzi wa kiume hujihusisha. Makadirio na matukio yanaonyesha kuwa kufikia mwaka 2050 ushirikishi katika nchi za kipato cha juu utakuwa 100%, ilhali ushirikishi katika nchi za kipato cha wastani utakuwa kati ya 60% na 80%. Ushirikishi katika nchi za kipato cha wstani utakuwa 35% mwaka 2050. Katika nchi maskini kwa zote, ushirikishi utakuwa chini ya 15%.

Ingawa elimu imepanuliwa kwa kiasi kikubwa katika karne kadhaa zilizopita, kuna wengi ambao hawajaweza kuipata. Ni dhahiri kuwa wengi wametengwa. Mmoja kati ya vijana wanne katika nchi cha kipato cha chini hana uwezo wa kusoma wala kuandika. Pia, Programu ya OECD ya Kuthamini Wanafunzi wa Kimataifa inabaini kwamba wanafunzi wengi walio na umri wa miaka 15 hawana uwezo mkubwa wa kuelewa mambo wanayofunzwa ingawa uwezo huo ni muhimu sana ukizingatia wanaishi kipindi ambacho ushirikishi katika mambo ya uchumi na mambo ya umma umekuwa mgumu. Katika nchi zenye kipato kilicho kati ya wastani na chini, asimilia ya watu wazima wenye uwezo wa kusoma na kuandika ni chini ya 75 na asilimia katika nchi maskini zaidi ni takribani 55. Ingawa swala la usawa wa jinsia limeshughulikiwa inavyostahili tangu mwaka 1990, bado linawaathiri watu masikini. Katika nchi za kipato cha chini, zaidi ya wanawake wawili kati ya watano hawana uwezo wa kusoma na kuandika.

Mmoja kati ya watoto watano katika nchi za kipato cha chini na mmoja kati ya watoto kumi ulimwenguni au takribani watoto milioni 250 hawako shuleni. Kando na upungufu katika maswala ya kusoma, hesabu, na sayansi, ambayo yameangaziwa, kuna upungufu ambao umethibitishwa na utafiti uliokamilishwa na Azimio la Kimataifa la Kutathmini Matokeo ya Elimu. Utafiti huu uliangazia umahiri katika mambo ya umma, mambo ya kitaifa, mambo ya hisia, na mambo ya jamii. Aina hizo za ujuzi ni muhimu katika ushirikishi kwenye mambo ya jamii na uchumi.

Hali katika ngazi ya sekondari ni mbaya zaidi. Watatu kati ya vijana watano (na vijana balehe) katika nchi za kipato cha chini hawako shuleni: hii ni licha ya ahadi ya kuhakikisha kuwa elimu za msingi na upili zitakuwa za hali ya juu, za usawa, na zizisokuwa na gharama yoyote kufikia mwaka 2030. Ingawa usajiri wa wanafunzi kwa masomo ya sekondari ya kiwango cha chini ni 98% katika nchi za kipato cha juu, zaidi ya theluthi moja na vijana balehe (40% ikiwa ni wasichana na 34% wavulana) katika nchi za kipato cha chini hawajajisajiri kwa ajili ya masomo ya sekondari ya kiwango cha chini. Tofauti hizi zimekithiri katika masomo ya sekondari ya upeo. Katika nchi za kipato cha chini, chini ya 35% ya wasichana na 45% ya wavulana wamejisajiri ilhali zaidi ya 90% ya wavulana na wasichana katika nchi za kipato cha juu wamejisajiri.

Kando na maswala ya upatikanaji wa elimu na kujisajiri kwa wanafunzi, kuna matukio mengine yanayohusiana na ubora na umuhimu wa elimu. Mwanafunzi mmoja kati ya wanne wa shule za sekondari za ngazi ya chini na zaidi ya mmoja kati wa wanafunzi wawili wa shule za sekondari za upeo hawakamilishi masomo yao. Takribani 60% ya wanafunzi wa shule za upili katika nchi zinazofuata zile nchi za kipato cha wastani na karibu 90% ya wanafunzi wa shule za upili katika nchi za kipato cha chini hawakamilishi masomo yao ya sekondari. Hatufai kuruhusu maisha ya vijana hao kuharibika hivyo. Kuna sababu kadhaa zinazochangia kukosa kukamilisha masomo yao: masomo yasiyo bora, masomo yasiyoangazia mahitaji ya wasichana, umasikini, kutozingatia mambo ya utamaduni kwenye mitaala, upungufu katika ufundishaji, na mbinu za ufundishaji ambazo zinapuuza hali halisi ya maisha ya vijana.

Changamoto hizi zinaweza kuitwa “mgogoro wa masomo” ulimwenguni. Kuacha masomo kwa wanafunzi wengi kunachochewa na hali duni ya mbinu za ufundishaji. Ubora wa elimu hutegemea motisha wanazopewa walimu, matayarisho ya walimu, rasilimali za masomo, uhuru walionao walimu, na nafasi walimu hupatiwa ili wajiendeleze. Ilimradi walimu wanapata msaada wanaohitaji, wanaweza kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata nafasi za masomo zilizo na usawa na zinazojali utamaduni wao.

Ni sharti ualimu uwe na weledi wa hali ya juu kwa vile walimu ndio huwalea wanafunzi na kuwaongoza vyema ile waweze kutoa mchango kwa mambo ya umma na uchumi. Hili linahitaji ufadhili wa kuhakikisha kuwa wale wanaosomea taaluma ya ualimu ni werevu; ufadhili huo utakuwa wa muhimu zaidi katika miaka yao ya kwanza kama walimu. Lazima wawe na fursa za kutosha za kujiendeleza na kazi zao zinastahili kupangwa kwa namna inayoleta ushirikiano. Shule zinastahili kuwa mahala pa ustawi ambapo walimu wanapatiwa motisha wanapofanya kazi nzuri na maoni yao yanajumuishwa katika michakato ya kuimarisha ualimu na elimu. Ufadhili huo unastahili uongozi mzuri. Kuna kanuni zingine huchangia kuzorota kwa taaluma ya ualimu kama vile kutumia walimu kama maajenti wa kisiasa. Ina maana kwamba, siasa inapoingilia kozi za ualimu, lengo kuu la taasisi zinazofunza kozi hizo ni kutengeneza pesa.

Siasa katika ualimu huleta miundo isiyozingatia jinsi walimu wanafunza. Ubora wa taasisi huharibiwa na siasa hizo potovu kiasi kwamba ualimu hauwezi kulinganishwa na taaluma zingine ambazo zinahitaji matayarisho ya kina kabla mtu aanze kazi. Siasa huwadhalilisha walimu hasa pale inapowalazimu kujihusisha na mambo ya kisiasa yanayodunisha hadhi yao katika jamii. Walimu hudhalilishwa pale ambapo wanalizimika kutafuta ufadhili wa wanasiasa na wakati haki zao zinakiukwa. Haki za walimu hukiukwa wakati wanadhulumiwa kimapenzi kazini na wanapolazimishwa kujihusisha na mambo ya kidini na kisiasa.

Ingawa upatikanaji wa elimu umeongeza na idadi ya walimu wanaohitajika imeongeza, kuna wasiwasi inayotokana na upungufu wa walimu wa shule za msingi waliohitimu hasa katika Afrika Kusini mwa Janga la Sahara ambapo viwango vya hati vinavyohitajika kwa wanafunzi wa ualimu vilipungua kutoka 85% mwaka 2000 hadi 65% mwaka 2020. Upungufu huo umeshuhudiwa katika maeneo ambayo yalikuwa na idadi kubwa ya walimu wa shule za msingi waliohitimu kama vile Uarabuni ambapo viwango vilipungua kutoka 98% mwaka 2004 hadi 85% mwaka 2020. Upungufu wa walimu wa shule za sekondari ni mkubwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Takribani nusu ya walimu wa sekondari katika eneo hilo walikuwa na viwango vya hati vinavyohitajika ikilinganishwa na karibu 80% waliokuwa na hati hizo miaka kumi iliyopita.

Kuna wasiwasi inayotokana na upungufu wa walimu wa shule za msingi waliohitimu.

Mafunzo ya kiufundi hayajaimarika katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Hata hivyo, kuna maeneo kama Asia ya Kati, Ulaya ya Kati na Mashiriki, Asia ya Mashariki, na Pasifiki ambayo yameshuhudia ongezeko la takribani 15% ya vijana kati ya miaka 15 na 24 waliojisajiri kwa masomo na kiufundi. Katika nchi masikini kama Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia ya Kusini, viwango vya usajiri wa masomo ya kiufundi ni takribani 1%. Ni muhimu kukumbuka kwamba mtu anaweza kupata ujuzi wa kiufundi mahali pengine pengi kando na shule za kawaida. Vijana wanaweza kupata ujuzi huo kwa kufunzwa na mafundi ambao wana ujuzi tayari. Hata hivyo, takwimu za Shirika la Wafanyikazi ulimwenguni zinaonyesha kuwa zaidi ya kijana mmoja kati ya watano (walio na umri wa kati ya miaka 16 na 24) hawana masomo, ujuzi wa kazi au kazi; theluthi tatu ya hao ni wanawake.

Takwimu hizi zinathibitisha kwamba ahadi ya kuhakikisha kila mtoto, kijana, na mtu mzima amepata elimu haijatimizwa tangu mwaka 1990. Wale ambao wameathirika zaidi kwa sababu wa uvunjaji wa ahadi hiyo ni wasichana wadogo, wanawake, vijana wanoishi na ulemavu, watu masikini, jamii zinazoishi vijijini, jamii za asili, na makundi ya watu walio wachache. Vile vile, makundi hayo huathirika zaidi panapokuwa na vita na misukosuko ya kisiasa. Jamii nyingi, hasa zilizodharauliwa, zinazidi kutengwa kwa sababu za kijamii, kiuchumi, kitamaduni, na kisiasa.

Ikiwa elimu itasaidia katika kubadilisha mustakabali, lazimu ijumuishe wote kwa kurekebisha ukiukaji wa haki uliotekelezwa zamani. Misingi ya ukosefu wa usawa na utengwaji wa watu na makundi mengine lazima ichunguzwe ndiposa iwe rahisi kufadhili na kuinua wanafunzi wanaotoka kwa jamii zilizotengwa na kudharauliwa.

# Umasikini mkubwa na ongezeko la ukosefu wa usawa

Umasikini huchangia pakubwa kwa fursa alizonazo mtu za kupata elimu. Umasikini hupunguza fursa hizo kwa wanafunzi wa kike, wanaoishi na ulemavu, wale walio kwenye mazingira ya vita na migogoro, na waliotengwa kwa sababu ya ukabila, lugha wanayozungumza, na kuishi maeneo ya pembezoni.

Kuanzia 1990 na 2020, uchumi wa kimataifa uliongezeka mara mbili na nusu. Kuongezeka huko kumetokana na ukuaji wa uchumi wa nchi za Asia ya Mashariki na Pasifiki hasa China na ukuaji wa uchumi wa nchi za kipato cha juu na zenye kipato cha wastani. Zile nchi za kipato cha chini na nchi za kipato cha wastani zimechangia 10% ya uzalishaji hata ingawa nusu ya watu ulimwenguni wanaishi katika nchi hizo. Kasi ya ukuaji wa maeneo ni tofauti. Mwaka 1990 michango ya uchumi ya China na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara katika uchumi wa Dunia ilikuwa 2% na 1.5% mtawalia. Miaka thelathini baadaye, uchumi wa China unachangia 16% kwa uzalishaji wa Dunia ilhali Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara inachangia 2%.

Hali za maisha na mapato ya watu yameimarika kwa sababu ya ustawi wa uchumi wa kimataifa na kupungua kwa viwango vya umasikini. Benki ya Dunia ina takwimu zinazoonyesha kuwa mapato ya mtu mmoja ya kila mwaka yaliongezeka kwa 75% kati ya mwaka 1990 na 2020. Ingawa theluthi moja ya watu ilikadiriwa kuwa maskini mwaka 1990, leo hii viwango vya umasikini ulimwenguni ni chini ya 10%. Imekuwa vigumu kupunguza umasikini ulio katika nchi za kipato cha chini kwa sababu uchumi wa nchi hizo haukui kwa haraka. Kumaliza umasikini ni tatizo ambalo limekithiri. Ingawa viwango vya umasikini vimepungua, takribani watu milioni 690 ulimwenguni ni masikini ambao hujikimu na chini ya dola mbili za Marekani kwa siku. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, 25% ya watu ulimwenguni au watu bilioni 1.8 wanajikimu na chini ya dola 3.20 za Marekani kwa siku. Umasikini mkubwa umekithiri Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara hasa maeneo ya pembezoni, na wanawake ndio wameathirika zaidi. Theluthi mbili ya walio masikini ni watoto wadogo na vijana walio chini ya miaka 25.

Tangu miaka ya 1980, ukuaji wa uchumi wa nchi za kipato cha wastani na nchi zinazokua umepunguza ukosefu wa usawa baina ya nchi. Lakini ukosefu wa usawa baina ya wananchi (wa nchi moja) umeongezeka kwa kasi. Ukosefu wa usawa katika mapato umeongeza katika nchi kama China, Marekani, na Russia; huko Ulaya, ongezeko hilo limekuwa la wastani. Kwa upande mwingine, ukosefu wa usawa wa mapato umesalia kuwa juu Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Brazil. Kwa mujibu wa Ripoti ya Ukosefu wa Usawa Ulimwenguni iliyochapishwa mwaka 2018,10% ya wafanyikazi Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Uarabuni ndio hupata nusu ya mapato yote katika nchi hizo. Katika nchi nyingi, rasilimali za uzalishaji zinamilikiwa na waekezaji binafsi. Ingawa uchumi wa nchi nyingi umepanuka, serikali zimezidi kuwa maskini kiasi kwamba fursa za kuleta mgawo wa mapato unaojikita katika haki na kupunguza kwa ukosefu wa usawa zimedidimia.

Elimu kuhusu matokeo ya ukosefu wa usawa ni muhimu mno. Ukosefu wa usawa ndio huchangia kutengwa kwa masikini kiasi kwamba inakuwa ni vigumu watu kushikamana ndiposa waweze kustawi na kuwa na uongozi bora. Ukosefu wa usawa unamaanisha kuwa fursa ya watoto ya kupata

elimu bora itategemea na mazingira waliyozaliwa kuumanisha kuwa shule haziwezi kuleta usawa. Ili mustakabali uwe ni wa usawa, lazima shule zitoe fursa sawa za kupata elimu kwa watoto wote.

Ukosefu wa usawa ni msingi wa shida zilizo katika jamii nyingi. Ukosefu huo huleta ufisadi katika mambo ya masomo; wengi huchukua njia za mkato katika masomo yao na inakuwa vigumu kufuatilia mambo yanayofanywa katika shule. Kulingana na Ripoti ya Ufisadi iliyochapishwa na Transparency International mwaka 2013, ufisadi katika elimu ni wa aina mbalimbali: wizi na ufujaji wa pesa zilizotengwa kwa ajili ya kununua bidhaa za shule; ununuzi wa vyeti na fursa za masomo; upendeleo kwa mambo ya kuajiri na kufadhili; wizi wa maandiko ya watu wengine; na ukiukaji wa mipaka ya utafiti (kwa sababu ya kuingiliwa na wanasiasa na makampuni). Udhaifu wa taasisi za elimu hudhoofisha imani ambayo jamii imeweka kwa elimu na kufanya wengi kuchukulia ufisadi kama maadili tangu miaka ya utotoni.

# Mtandao wa utengwaji

Umasikini na ukosefu wa usawa katika mapato hukingamana na mambo ambayo huleta ubaguzi katika elimu. Kwa mfano, ubaguzi wa kijinsia hukingamana na mambo mengine kama umasikini, kutoka katika jamii za asili, na ulemavu; kukingamana huko huwazuia wasichana wengi kupata elimu. Ingawa makundi na maeneo mengi yamepiga hatua katika kupata usawa kwenye usajiri wa jinsia, nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zimebaki nyuma. Takwimu kutoka taasisi ya UNESCO zinaonyesha kuwa kwa watoto wavulana 100 wanaostahili kuwa katika shule ya msingi Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuna wasichana 123 ambao hawako shuleni. Kutengwa kwa wasichana ni kwa hali ya juu katika elimu ya sekondari. Wavulana fukara katika nchi tisa masikini hukaa shuleni miaka miwili zaidi ya wasichana. Hii tofauti kubwa ya kijinsia katika elimu ya sekondari inaonyesha kiwango cha kazi inayostahili kufanywa kuwasaidia wasichana kukamilisha kipindi chote cha masomo yao. Upatikanaji wa elimu ni mdogo. Jukumu la kuhakikisha kwamba wasichana wanakamilisha masomo yao linahusisha mambo mengi. Jukumu hilo linahusiana na changamoto za kijamii na kiuchumi ambazo wasichana wengi ulimwenguni hukabiliana nazo hasa wakiwa umri wa kubalehe na changamoto zingine kama ndoa na mimba za mapema, kazi za nyumbani, hedhi, na unyanyapaa.

Ulemavu huathiri elimu maeneo yote ambayo hayana miundo msingi ya kuhakikisha ujumuishaji wa walemavu katika elimu. Hali huwa ngumu zaidi kama walemavu hao ni masikini. Watoto wengi walio na ulemavu wanaishi nchi za kipato cha chini. Viwango vya ulemavu wa watoto, wa marika yote, viko chini katika nchi za kipato cha juu. Umasikini ni chanzo na tokeo la ulemavu; mifumo ya elimu ina jukumu la kuhakikisha watoto walemavu wanapata elimu kwa kujenga mazingira yasiyowatenga.

Mizozano katika sehemu mbalimbali ulimwenguni imechangia nusu ya visa vya watoto ambao hawako shuleni. Migogoro inamaanisha kwamba itakuwa vigumu kwa watoto kuenda shule na inaweza kuchangia uhamaji wa jamii kadhaa. Vile vile, taasisi za elimu, wafanyikazi katika taasisi hizo, na wanafunzi wanaweza kutekwa nyara, kunajisiwa, na kulazimishwa kuwa majeshi katika vita.

Watoto kutoka jamii za asili, wale wanaotoka kabila ndogo, na vijana hukabiliana na vizuizi ambavyo huwazuia kupata elimu bora katika viwango vyote vya elimu. Kando na vizuizi vya kiuchumi, kilugha, na upatikanaji, watoto hao hukumbana na elimu isiyohusiana na tamaduni zao; hii inamaanisha kuwa viwango vya kuacha shule ni vikubwa kwa watoto kutoka jamii za asili na vijana. Kwa jumla, elimu inakosa kuzingatia maarifa na masomo ya kiasili na hivyo basi inakosa kuwa ya maana kwa watu asili, walio vijijini, na mitaani hasa wanapokabiliwa na maisha halisi.

Kihistoria elimu imetumika kama chombo ya kukiuka haki za kitamaduni na haki za kidini hasa pale ilipotumika kuwalazimisha watu kutoka jamii za asili kuacha tamaduni zao au pale ambapo ilitumika kufutilia mbali utambulisho wa kidini na utambulisho wa kitamaduni wa watoto hao. Historia ya elimu kutumika kama silaha ya kuwakandamiza watoto kutoka jamii za asili na familia zao inaendelea kupitia kwa utengwaji wa kina ulioko kwenye jamii. Aghalabu watoto wengi wa jamii za asili wanalazimika kuishi mbali na jamii zao, katika mabweni ambapo hawapati usaidizi wa kijamii na kitamaduni.

Utandawazi wa kiuchumi unazidi kuathiri elimu ya wanafunzi. Umebadilisha mambo ya ajira katika karne ya ishirini na moja; watoto na vijana wanapaswa kuelimishwa kuhusu mabadiliko hayo. Elimu ina jukumu la kuwaandaa wanafunzi kwa ajira. Hata hivyo, kuna mapengo katika malengo ya elimu; malengo hayo hayajalainishwa na maisha halisi ya watoto hao na familia zao na fursa walizonazo maishani. Kuna haja ya kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa maarifa yanapatikana na kutumika katika miktadha mbalimbali. Maarifa yanastahili kuwa zaidi ya kusoma na kuandika: yanapaswa kujumuisha ufahamu kuhusu tamaduni zingine ulimwenguni, mambo ya sayansi, na mambo ya kiroho.

> Ndiposa elimu ifanikishe usawa, lazima ijumuishe aina zote ya maarifa na mbinu za kujieleza.

Hii ni ukweli ukizingatia kuwa idadi ya watoto wa jamii za asili, watoto wanaoongea lugha za wachache, na wale wanaotoka kabila mbalimbali, ambao hawako shuleni ni kubwa zaidi. Ndiposa elimu ifanikishe usawa, lazima ijumuishe aina zote za maarifa na mbinu za kujieleza. Mitihani wanayopatiwa watoto shuleni huwa haitathmini uwezo wao wa kutumia lugha za mama; hili linaweza kuwatenga zaidi watoto kutoka jamii asili na kuchangia wao kuacha masomo ya kabla ya kumaliza. Kwa mfano, matokeo ya Programu ya Kimataifa ya Utafiti wa Kusoma na Kuandika (PIRLS) yalionyesha kuwa ikilinganishwa na wanafunzi wengine, ni vigumu wanafunzi wa darasa la nne, wasiozungumza lugha inayotumiwa katika tathmini nyumbani, kupata matokeo yanayoonyesha ujuzi wa chini kabisa. Lazima tuchangie kuwepo kwa Dunia ambayo inajumuisha hali za watu wote badala ya kuwa na dira moja ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kulinda haki za watu wote kunahitaji kila mtu awe na fursa ya kustawi.

Ikiwa ni haki za binadamu zitaongoza mkataba mpya wa kijamii wa elimu, lazima utambulisho wa wanafunzi - wa kitamaduni, wa kiroho, wa kijamii, na wa kiisimu - utambuliwe na usisitizwe hasa wa wale wanaotoka katika jamii za asili, makundi ambayo yametengwa, na wanaotoka kwa dini, tamaduni, na makundi ya ujinsia yaliyo na watu wachache. Kutambuliwa kwa mambo ya utambulisho katika mitaala, ufundishaji, na mbinu zinazotumiwa na taasisi za elimu kutaathiri kubakia shuleni kwa wanafunzi, afya na akili, viwango vya kujithamini, na ustawi wa jamii.

Mbinu nyingi zinahitajika ili tuweze kupata suluhu kwa mambo ambayo hayajatatuliwa. Lakini jitihada zetu zimekwama kwa sababu ya changamoto kama mabadiliko ya tabianchi, majanga ya kimataifa, na ukosefu wa usalama. Mwaka 2020, UVIKO-19 iliathiri watoto na vijana bilioni 1.6 baada ya shule zao kufungwa. Hata baada ya shule kufunguliwa, wengi wa wanafunzi, hasa wale masikini na waliotengwa, hawakurejea. Ukosefu wa usawa kakika elimu umekithiri.

Kuanzisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu ni swala linalostahili kushughulikiwa kwa haraka kwa vile kuna mabadiliko mengi yanayoendelea katika jamii na vurugu nyingi zitakazotukabili siku za mbeleni. Ni sharti mtandao wa ukosefu wa usawa, ambao umechangia katika kutengwa kwa kielimu na kijamii, ushughulikiwe ndiposa tuweze kujenga mustakabali ulio na uendelevu, haki, na ujumuishaji.

# Sura ya 2

## Vurugu na mabadiliko ibuka

Hapa ningependa kusisitiza kuwa mojawapo ya mafunzo nimepata maishani ni kuacha kuamini kuwa mambo ya sasa, kuwepo, na kutabirika kwa mustakabali ni vitu visivyobadilika. Milipuko, ya mambo ambayo hatukuyatarajia, inaweza kutokea ghafla na kututikisa na kutubadilisha kwa kuleta huzuni au furaha katika maisha yetu ya binafsi, maisha yetu kama nchi, na maisha na binadamu wote.

**Edgar Morin**, *Leçons d'un siècle de vie*, 2021.

Tunapopiga hatua kuelekea mwaka 2050, elimu tutakayohitaji itategemea matarajio yetu kuhusu ulimwengu unavyostahili kuwa hasa mabadiliko yatakayotokea kwa familia, jamii, nchi, na maeneo tofauti.

Sura hii inapiga dharubini ya vurugu ambazo zitaathiri sehemu nne kuu: mazingira, uhusiano wetu na teknolojia, mifumo ya utawala, na ajira.

Hata ingawa ni vigumu kutabiri matukio ya kesho kwa uhakika, kujitayarisha kwa ajili ya mabadiliko ni msingi unaoweza kutupatia dira ambayo itatusaidia katika shughuli ya kubadilisha elimu ili iweze kutosheleza mahitaji ya binadamu ya siku zijazo.

# Dunia hatarini

Wanasayansi wamekubaliana kuwa miaka kati ya 2020 na 2030 ni muhimu katika mustakabali wa binadamu na viumbe wengine. Zile hatua tutakazozichukua - au kosa kuchukua - ili kupunguza kaboni kwenye mazingira zitaathiri mustakabali wa miaka kati ya 2030 na 2040. Matokeo ya hatua hizo yatatuathiri kwa mamia, maelfu, au mamilioni ya miaka. Mabadiliko yanayoendelea sasa, hasa ya kiikolojia, hayajawahi kushudiwa. Mabadiliko katika viungo vya angahewa yanakadiriwa kuwa mara kumi zaidi ya yale ambayo yalishuhudiwa enzi zile kulikuwa na mabadiliko makubwa ambayo yalibadili maisha ya mamalia. Dunia sasa ina joto nyingi kuliko ilivyowahi kuwa wakati wowote tangu mwanzo wa Enzi ya Barafu iliyoanza miaka 125,000 iliyopita. Na kwa sababu matokeo ya mabadiliko ya tabianchi yako kwenye mazingira yetu, yatasalia hapo kwa takribani miaka thelathini ijayo. Elimu lazima ibadilishwe ili tuweze kutimiza malengo ya kurekebisha na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kutiwa saini kwa Mkataba wa Hali ya Hewa wa Paris mwaka wa 2015 kuliashiria kujitolea katika dhamira ya kupunguza viwango vya gesi chafu kama dioksidi ya kaboni na methani ambavyo vimekuwa vikiongezeka tangu mwanzo wa Enzi ya Mvuvumko wa Viwanda. Serikali mbalimbali zilitoa ahadi ya kujitolea katika kurudisha joto la Dunia hadi kiwango lililokuwa kabla ya Mvuvumko wa Viwanda. Kiwango hicho ni kati ya nyusi joto 1.5 hadi 2. Licha ya ahadi za kupunguza utumiaji wa nishati ya visukuku, viwango vya kaboni vimezidi kuongezeka. Ripoti ya Jopo la Kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi iliyochapishwa mwaka 2021 inaonyesha kuwa kupanda kwa halijoto ulimwenguni ni zaidi ya kiwango kilichotarajiwa miaka michache iliyopita. Tumeshindwa kidhibiti na kupunguza viwango vya halijoto. Madhara ya utepetevu wetu ni vipindi virefu mno vya ukame, mafuriko, mioto ya mwituni, na kutoweka kwa ikolojia. Licha ya kupatiwa onyo kali, watu wengine hawafahamu athari za uchimbaji madini na utumiaji wa nishati visukuku. Binadamu wamechangia pakubwa katika mabadiliko ya tabianchi ambayo yamefanya matumbawe kadhaa kufa, trilioni za barafu kuyeyuka, na maji ya bahari kuwa na asidi nyingi. Ingawa ilionekana kwamba lengo la kurudisha viwango vya kaboni hadi sufuri lingengoja hadi mwaka 2050 ndiposa tuweze kubadilisha athari za mabadiliko ya tabianchi, utafiti unaonyesha kuwa athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi zitatokea mapema kuliko tulivyotarajia. Matukio ya miaka inayokuja - ambayo inatoshana na sekunde kwa muktadha wa historia ya Dunia - yanaweza kuzua jinamizi kubwa litakalotokana

na mabadiliko ya tabianchi. Kwa upande mwingine, matokeo hayo yaneweza kuleta mabadiliko ambayo hayataathiri maisha ya binadamu.

Watu katika familia, biashara, mahali pa kuabudu, na shule wametambua kuwa hali ya tabianchi ni jambo la dharura. Watoto na vijana wamekuwa mstari wa mbele katika shughuli za kupeana wito wa kuchukua hatua na kuwakosoa wale wasiotambua umuhimu wa jambo hili. Katika mazungumzo yote yaliyofanywa na makundi mbalimbali ya vijana ndiposa hii ripoti inandikwe, ilibainika kuwa vijana wana wasiwasi kuhusu mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira.

## Kupita mipaka ya Dunia

Ongezeko la joto katika angahewa na bahari linaenda sambamba na matumizi mabaya ya rasilimali yanayoilemea Dunia. Kati ya mwaka 1950 na 2020, idadi ya watu ulimwenguni iliongezeka mara tatu; idadi hiyo ilitoka watu bilioni 2.5 hadi bilioni 8 kwa sababu ya kuongezeka kwa viwango cha kuzaa na muda wa kuishi wa binadamu. waka 2020, mtu wa kawaida aliishi kwa miaka mbili maradufu zaidi mtu aliyeishi mwaka 1920 - hili ni fanikio kubwa lililoonyesha kuimarika kwetu katika mambo ya kisayansi na ya kijamii. Ongezeko la watu ulimwenguni limeambatana na ongezeko la rasilimali inayohitajika ili kuwakimu. Idadi ya watu inaendelea kuongezeka pole pole ukilinganisha na karne zilizopita. Makadirio ya sasa hivi yanaonyesha kuwa kufikia mwaka 2050, kutakuwa na watu bilioni 9.7 ulimwenguni; baada ya hapo idadi hiyo itafika bilioni 11 mwaka 2100.

Ongezeko la watu, uzalishaji wa viwanda, na utumiaji wa rasilimali hulemaza Dunia. Tangu 1950, utumiaji wa maji umeongezeka maradufu, uzalishaji wa chakula na utumiaji wake umeongezeka mara 2.5 ilhali utumiaji wa mbao umeongezeka mara tatu. Kufikia mwaka 2050, mahitaji ya chakula, maji, na nishati yataongezeka kwa 35%, kati ya 20% - 30%, na 50% mtawalia.

Leo hii, tumepita viwango kwa jinsi ambavyo tunazalisha bidhaa, kutumia bidhaa, na kuongeza taka katika mazingira. Kulingana na makadirio mengine, binadamu wanahitaji sayari ambayo ina ukubwa unaozidi Dunia kwa mara 1.6 ndiposa mahitaji yetu yatoshelezwe na tuweze kukabiliana na viwango vya taka. Hii ina maana kwamba ikiwa utumiaji wa rasilimali utaendelea kuongeza, itachukua Dunia mwaka mmoja na miezi nane kuzaa kile ambacho kingezaliwa baada ya mwaka mmoja hapo awali. Endapo hakutakuwa na mabadiliko kufikia mwaka 2050, matumizi ya rasilimali yataongezeka mara nne kumaanisha kwamba vizazi vya kesho vitarithi Dunia yenye maliasili yaliyopunguka kwa kiasi kikubwa.

Leo hii, tumepita viwango kwa jinsi ambavyo tunazalisha bidhaa, kutumia bidhaa, na kuongeza taka katika mazingira.

Uchafuzi wa mazingira, ambao unatokana na matumizi yetu na utumiaji wa kupita kiasi wa rasilimali, ndio umechangia katika kuzorota kwa mazingira na vifo vya binadamu. Inakadiriwa kuwa uchafuzi huo ndio chanzo kikuu cha vifo vya mapema vya takribani watu milioni 9. Idadi hii ni kubwa kuliko jumla ya watu wote walioaga kwa sababu ya UKIMWI, malaria, kifua kikuu, na vita. Uchafuzi wa mazingira ni janga kuu ambalo ni kiini cha umelavu na matatizo ya ujifunzaji. Shughuli

ya kwenda na kutoka shuleni inaweza kuhatarisha afya ya mwanafunzi ukizingatia kuwa uchafuzi wa hewa katika mazingira mengi ni wa hali ya juu, na shule nyingi hazina vichungi vya hewa, mahali pa kusafisha maji taka, na maji masafi. Taasisi zingine zimejengwa katika mazingira ambayo yana kemikali zenye sumu.

Hata kama tungefanikiwa kuwa na mifumo ya nishati safi kwa 100%, bado tungekabiliwa na athari za kimazingira zinazotokana na uharibifu wa misitu, uvuvi kupita kiasi, ukulima wa viwango vya juu, uchimbaji madini, na taka. Tayari, athari hizo zimeanza kuonekana. Sehemu ya Dunia ambayo ni muhimu kwa uhai wa viumbe (biosfera) inaweza kustahimili kwa kiwango fulani - kadiri tunavyozidi kulemaza mifumo ya ikolojia ambayo ni muhimu kwa uhai wetu ndivyo tunazidi kusonga karibu na ncha hatari ambayo itakuwa ni ngumu kubadilisha.

Binadamu wote wanachangia haya - japo kwa njia na viwango tofauti. Mabwenyenye binafsi na nchi za kipato cha juu ulimwenguni ndio hutumia rasilimali kupita kiasi; kwa hivyo, mchango wao wa kaboni ni wa juu. Tunaposhughulika na kubadilisha mwelekeo, ni sharti wale ambao wamechangia katika kulemazwa kwa Dunia walipie hiyo gharama.

## Athari ya mabadiliko ya tabianchi kwa elimu

Hivi sasa, elimu imeathirika kwa njia za moja kwa moja na ziziso za moja kwa moja zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mifumo ya ikolojia. Hali mbaya ya anga na misiba ya asili huweza kufanya watu wengine kukosa elimu. Watoto, vijana, na wanafunzi (walio watu wazima) wanaweza kulazimika kuhamia mahali ambapo ni mbali na taasisi za elimu. Vile vile, majengo ya shule yanaweza kuharibiwa au kubadilishwa kuwa makazi ya wale walioathirika na majanga ya asili. Hata mahali ambapo shule na vyuo vikuu ni wazi, kuna uwezekano wa kuwa na changamoto ya ukosefu wa walimu.

Ongezeko la joto lina athari spesiali kwa elimu. Utafiti mwingi unaonyesha kuwa joto jingi huathiri uelewaji wa wanafunzi. Shule nyingi na makazi mengi ya familia hayana vifaa vya kukabiliana na joto hilo. Kuna nchi ambazo zina misimu ya joto ya hali ya juu. Takwimu za karibuni zinakadiria kuwa pasipokuwa na mabadiliko yanayofaa katika mambo ya gesi chafu, theluthi tatu ya walimwengu, kufikia mwaka 2070, watakosa mahali pa kuishi. Tayari wanafunzi ulimwenguni kote wamezoea hali ya kukatazwa kwenda shule kwa sababu ya ongezeko la joto na mabadiliko mengine ya anga ambayo yatazidi kuongezeka kwa ukubwa na viwango vya kujikurudia.

Kando na athari za moja kwa moja za mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira, kuna zile ambazo si za moja kwa moja ambazo huathiri riziki na ustawi. Uwezekano wa kukosa chakula, kuenea kwa magonjwa, na kuwa na matatizo ya kifedha huchangia katika tatizo la haki ya kupata elimu. Tunavyojua, hali hizi huwaathiri watu kwa njia tofauti.

Imedhihirika kuwa mabadiliko ya tabianchi huzidisha ukosefu wa usawa baina ya jinsia hasa katika jamii masikini zinazopata riziki kutoka kwa ukulima wa kiwango kidogo. Wakati rasilimali ni kidogo, ugavi wake hukosa usawa. Wakati wasichana na wanawake wanapoteza makazi yao kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, inakuwa rahisi kwao kuingia katika mtego wa umasikini. Uwezekano wa wao wa kurejesha maisha yao, pamoja na elimu, huwa mdogo kuliko ule wa wavulana na wanaume.

Mabadiliko ya tabianchi huwafanya wanaume wengi kuhama na kuwaacha wanawake na jukumu la kulinda jamii. Katika maeneo mengine, wasichana wanaozwa mapema kama njia ya kupata riziki ya jamii zao na hivyo wanalazimika kuacha masomo yao. Vile vile, wanawake ni viongozi katika mambo ya kupigania tabianchi - kama mama, walimu, wafanyikazi, wafanya-uamuzi, wanajamii, na viongozi - wanawake wako katika mstari wa mbele kwa mambo ya kubadili tabianchi.

Wanawake wa asili wana ujuzi ambao ni muhimu katika kupigana na mabadiliko ya tabianchi: kukuza misitu, kulinda maji, bioanuwai, mimea, na mbegu. Hata hivyo, michango ya wanawake inapuuzwa.

Mara nyingi mno, waathiriwa wa mabadiliko ya tabianchi ulimwenguni hawajumuishwi vya kutosha katika mazungumzo. Zaidi ya hayo, wadau wa elimu kama wanafunzi, walimu, na familia, pia hawahusishwi katika mazungumzo yanayohusu athari za mabadiliko ya tabianchi katika elimu. Ni muhimu hawa waathiriwa na wadau wahusishwe vikamilifu. Mifumo ya uhusishwaji inahitajika katika sekta zingine kama vile utafiti na uzalishaji wa maarifa kuhusu jinsi ambavyo wanadamu wanaweza kubadilisha Dunia na elimu.

Hivi sasa, mafanikio katika elimu yana uhusiano mkubwa na mambo mengine yasiyo endelevu. Watu wa nchi zilizo na viwango vya juu vya mafanikio ya elimu, ndio wanachangia zaidi katika mabadiliko ya tabianchi. Elimu inatarajiwa kuendeleza amani, uadilifu, na haki za binadamu; sasa tumeanza kutoa wito kuhusu utumiaji wa elimu katika kufungua njia na kuunda misingi ya uendelevu. Kazi hii inafaa kuimarishwa. Kama kuwa na elimu inamaanisha kuishi kwa njia ziziso endelevu, lazima tubadili mitazamo yetu kuhusu malengo ya elimu na maana ya kuwa msomi.

## Sababu ya kuwa na matumaini

Kwa muda mrefu sana, elimu imekuwa ikizingatia dhana ya ukuzaji wa uchumi. Lakini kuna dalili tumeanza kukubali dhana ya elimu inayozingatia ikolojia; dhana hii inatuhimiza kuelewa kutegemeana baina ya mifumo tofauti na mipaka ya mifumo hiyo. Sherehe za Siku ya Dunia zinazoadhimishwa mwezi wa Aprili kila mwaka, ni kati ya sherehe kubwa katika historia ya binadamu. Harakati za tabianchi zimechangia uhusishwaji wa watoto katika utekelezaji wa dira ya mustakabali wao. Hatua wanazozichukua ni matayarisho ya mustakabali mpya. Zaidi ya hayo, ustawi endelevu umezidi kuwa kanuni ya kuongoza elimu na mitaala.

Hatuwezi kukataa uwezo wa kuwa na mustakabali wa 2050 ambapo ufahamu wa binadamu kuhusu mazingira utakuwa umetokea, na njia zetu za kuishi kwa amani na Dunia iliyo hai zitakuwa sambamba.

Ingawa umuhimu wa elimu kuhusu mazingira umetambulika kwa karne kadhaa sasa, na serikali nyingi zimetangaza sera za kuikuza, kuna tofauti kubwa kati ya sera hizo na matokeo yake.

> Tunahitaji mbinu mpya za kuwaongezea wanafunzi maarifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Utafiti kuhusu ufanisi katika elimu kuhusu mazingira umebaini kuwa kwa kiasi kikubwa, elimu hiyo huangazia ufundishaji wa sayansi ambao haukuzi ujuzi wa kutosha kuhusu jinsi wanafunzi

wanaweza kuhamasishwa kuchukua hatua halisi. Tunahitaji mbinu mpya za kuwaongezea wanafunzi maarifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mbinu hizo lazima zijumuishe maarifa waliyonayo kuhusu ujifunzaji wa kina, maarifa ya mambo ya kiraia, na utafiti wa karibuni kuhusu ujuzi wa maisha na kazi.

# Dijitali inayounganisha na kugawanya

Kipindi hiki muhimu kimebainishwa na mabadiliko ya kiteknolojia ambayo yamekuwa yakitukia kwa mwendo wa kasi sana; mabadiliko hayo ni kama mabadiliko ya dijitali na uvumbuzi wa bioteknolojia na sayansi ya neva. Uvumbuzi wa teknolojia umebadilisha jinsi tunavyoishi na utaendelea kuleta mabadiliko zaidi.

Teknolojia ya kidijitali, vifaa, na majukwaa mbalimbali ni nguzo za haki za binadamu zinazoongeza uwezo wa kibinadamu na kuwezesha hatua za kuleta amani, haki, na uendelevu. Ni wazi kuwa elimu ya kidijitali ni hitaji la msingi katika karne hii ya ishirini na moja; bila hiyo elimu, inakuwa vigumu kujihusisha katika mambo ya kiraia na kiuchumi. Janga la UVIKO-19 lilitukumbusha ukweli mchungu kuhusu jinsi wanafunzi walio na rasilimali ya dijitali waliweza kuendelea na masomo yao, ilhali wengine walikosa nafasi ya kuendelea na masomo yao baada ya shule kufungwa. Kwa ajili ya mapengo hayo ya dijitali, tofauti za mafanikio ya elimu baina ya nchi tofauti ziliongezeka. Jambo la kwanza linalostahili kufanywa ni kufunga mapengo hayo ndiposa kila mwalimu na mwanafunzi katika karne hii ya ishirini na moja awe na maarifa ya dijitali.

Utumiaji wa teknolojia katika kuongeza uwezo wa kibinadamu wa kujenga ulimwengu ulio na ujumuishi na uendelevu lazima uhamasishwe. Teknolojia ina sifa ya kukandamiza haki za binadamu na kupunguza uwezo wao. Ni vigumu kupata mafanikio baada ya kupokea mavumbuzi mapya na kuyachukulia kama suluhisho kwa kila mojawapo ya matatizo yetu. Matokeo mazuri yanatokana na mabadiliko yanayoboreshwa hatua kwa hatua; utamaduni wa kufanya majaribio kwa teknolojia ili kufichua athari zao; na kukubali kuwa hakuna suluhisho la jumla.

Dijitali - ambayo ni yale yote yamebadilishwa kuwa idadi zinazoweza kusambazwa, kuhifadhiwa, na kuchambuliwa na tarakilishi - inatumikwa kwenye shughuli zote za kibinadamu. Ni miundombinu ambayo hufanya mambo mengi zaidi ya kutuunganisha. Hata hivyo, kuna mgawanyiko wa kidijitali katika swala la upatikanaji wa intaneti na ujuzi unaohitajika ndiposa mtu aweze kuitumia teknolojia hiyo.

Kuna migongano maalumu katika teknolojia za dijitali. Teknolojia za dijitali zina uwezo mwingi; uwezo wa zingine unatarajiwa kuwa mkubwa. Vile vile, teknolojia zingine zina athari. Kwa hivyo, maendeleo ya kidijitali si tofauti na teknolojia zingine zilizoleta mabadiliko makubwa kama mivuvumko ya kilimo na viwanda. Faida za jumla huambatana na ongezeko na ukosefu wa usawa na ugawanywaji wa binadamu. Changamoto kubwa ni kukabiliana na faida na athari za teknolojia hizo ili kuhakikisha kuna haki za binadamu na usawa wa fursa.

Teknolojia inaweza kuwa na upendeleo - inaweza kuchochea hatua na maamuzi ambayo yanawaganya na kubadilisha Dunia pamoja na mitazamo na hatua za binadamu.

Kuna sifa maalumu za teknolojia za kidijitali ambazo zinaweza kuhatarisha utofauti wa maarifa, ujumuishaji wa tamaduni, uwazi, na uhuru wa kiakili. Uwezo wa kuendeleza elimu kama rasilimali ya jamii una changamoto kama aligorithimu, ubeberu katika majukwaa ya kidijitali, na mifumo ya utawala katika miundombinu ya dijitali. Mambo haya hayajapatiwa kipaumbele katika mazungumzo ya elimu hasa kuhusu utumiaji wa teknolojia za kidijitali katika elimu na uwezekano wa kuanzisha masomo ya mfumo wa kidijitali pekee au yale ya mseto.

Kwa miongo mingi, elimu imejipata katika mabadiliko kwa sababu ya uhusiano wake na teknolojia ya kidijitali. Tarakilishi hutumiwa madarasani na katika nyumba nyingi ulimwenguni. Matumizi ya rununu katika elimu yanaongezeka hasa katika mazingira ya umasikini kama Afrika Kusini mwa Jangwa la Saraha ambapo si wanafunzi wengi walio na uwezo wa kupata tarakilishi. Fursa za kusoma kupitia kwa teknolojia za kidijitali zimeongezeka kwa sababu ya intaneti, barua pepe, data ya simu za mkononi, teknolojia ya kusambaza video na sauti, na vifaa vingine vya masomo ya kidijitali.

Maendeleo haya ibuka yameathiri haki ya elimu, na haki za kitamaduni zinazohusiana na lugha, utamaduni, na maazimio. Haki za kupata taarifa, data, na maarifa na haki ya kujumuishwa katika mambo ya kidemokrasia pia zimeathirika. Kanuni msingi za heshima ya kibinadamu pamoja na haki ya faragha na haki ya kuishi kulingana na madhumuni ya mtu binafsi lazima ziangaliwe tunapochanganua mabadiliko yaliyoletwa na teknolojia za kidijitali.

Maendeleo katika teknolojia ya mawasiliano yamebadili mitazamo kuhusu kuthaminiwa kwa elimu, njia za kuelimisha, na mipango ya mifumo ya elimu. Gharama ya kupata taarifa na kuitumia imepungua kwa sababu ya teknolojia hizi. Vile vile, zimerahisisha ujumuishwaji wa watu katika michakato hiyo. Miradi ya sayansi inayowajumuisha watu wengi ni mifano mizuri kuhusu vile teknolojia za dijitali zinatumiwa kupanua wingi wa taarifa zinazosanywa na kuchunguzwa na utofauti wa watu wanaohusika katika kazi hiyo. Uzalishaji, usambazaji, na utumiaji wa data na maarifa kupitia kwa mifumo ya dijitali umebadilisha ukuaji wa sayansi na taaluma zingine. Kusanya data kwa kutumia tarakilishi kumekita mizizi kushinda njia zingine kama ushuhuda wa kibinafsi ambao hauwezi kuelezwa kupitia kwa hesabu.

Tunapojizoesha na mazingira ambayo mtu anaweza kupata taarifa zozote anazohitaji kupitia kwa rununu, ambayo ni maktaba kubwa tumewahi kuwa nao katika hii milenia, elimu inafaa kufanya mambo zaidi ya kusambaza maarifa. Wanafuzi wanastahili kuhamasishwa ili waweze kutumia maarifa hayo kwa njia inayostahili. Changamoto kuu ipo katika kuwapatia watu vifaa vitakavyo wasaidia kupata maana katikati ya bahari za taarifa ambazo zinapatikana kwa urahisi.

## Utengwaji unaotokana na maarifa ya kidijitali

Teknolojia ya dijitali inawasilisha aina ya maarifa yanayohusishwa na yale yalikuwa Ulaya kipindi cha mwamko-sanaa; maarifa hayo yanapuuza maarifa ya asili. Yale maarifa waliyokuwa wanatumia wavuvi, mabaharia, na wasafiri, yanapuuzwa na wanaastronomia, wataalamu wa hali ya hewa, na wanametolojia ambao wanapendelea teknolojia. Vivyo hivyo, maarifa ya wakulima, wawindaji, na wachungaji wa mifugo yametengwa kutoka kwa maarifa ya teknolojia yanayotumiwa na

wataalamu wa kilimo, wataalamu wa misitu, walinda mazingira, makampuni ya madawa, na wataalamu wa lishe. Kwa sababu ya kupuuzwa kwa maarifa ya asili, binadamu wamenyimwa fursa ya kupata maarifa zaidi kuhusu binadamu, mazingira, na kosmolojia. Waelimishaji wanapaswa kutambua na kurejesha maarifa haya ambayo ni msingi wa utofauti wa tamaduni za binadamu. Kwa upande mwingine, ufundishaji wa sayansi umekuwa kama mtaalamu ambaye hakubaliki wala kuaminika katika miktadha inayohusiana na maarifa ya asili.

Mojawapo ya maarifa ya thamani kubwa ambayo yamo hatarani kwa sababu ya teknolojia za dijitali ni maarifa ya kijamii. Hata ingawa teknolojia inajivunia mchango wake katika kuimarisha ushirikiano, uunganisho, na mahusiano, maarifa mengi ya kijamii, hasa yale yanayotumika kuleta faida, hutegemea utengwaji wa mtu binafsi - mtumiaji, mnunuzi, au mtazamaji - na hivyo inaweza kuleta upweke, ubinafsi, na kujipenda.

Na kwa vile hakuna usawa katika kugawanywa kwa maarifa ya dijitali, vifaa vya dijitali, majukwaa, na vipimo vya data, wanaotegemea maarifa ya asili, yasiyoweza kuuzwa hupuuzwa.

Kwa kiasi kikubwa, utengwaji wa kidijitali hutokea kwa sababu ya kupuuzwa kwa wale wenye mbinu na maarifa ambayo hayawezi kupimwa, kuhifadhiwa, na kuchanganuliwa kwa njia za kidijitali. Kwa hivyo, haya majukwaa yanaweza kuitwa majukwaa na ubeberu. Suluhu siyo ujumuishaji wa jumla wa kidijitali. Hili ni swala tata ambalo linamaanisha kuwa lazima jamii yote ihusishwe katika utafutaji wa njia za kubadilisha dijitali ili iwe rasilimali ya jamii yote na inayoheshimu hata yale maarifa ambayo si ya kidijitali.

> Hata hivyo, idadi kubwa ziziso na maarifa halisi; uunganisho usio jumuisha tamaduni zote; maarifa yasiyo na uwezeshaji; na teknolojia ya dijitali katika elimu isiyo na madhumuni dhahiri, sio viwango vinavyostahili kutumika au kuchangia katika ustawi wa binadamu.

Lazima tuungane ili tuwe na uwezo wa kukabiliana na athari mbaya za dijitali ambazo zina uwezo wa kuenea kufikia mwaka 2050. Juhudi zetu zinastahili kuangazia utumiaji na umaarufu wa aligorithimu kama suluhu katika kufafanua maana ya maarifa. Kupingana na athari hizi haimanishi kupingana na mabadiliko yote ya dijitali kwa jumla.

Katika kipindi cha UVIKO-19, tulishuhudia kuwa teknolojia za dijitali ni muhimu katika mambo ya afya ya umma na ufundishaji wa umma. Teknolojia hizi zilitumika kuelimisha watu kwa umbali, kufuatilia mambo ya wagonjwa na chanjo, na kueneza habari timilifu kuhusu UVIKO-19. Hata hivyo, idadi kubwa ziziso na maarifa halisi; uunganisho usio jumuisha tamaduni zote; maarifa yasiyo na uwezeshaji; na teknolojia za dijitali katika elimu ziziso na madhumuni dhahiri, sio viwango vinavyostahili kutumika au kuchangia katika ustawi wa binadamu.

Ushangiliaji wa mabadiliko ya dijitali unaweza kuangaliwa kama kushindwa kutumia fursa zinazoletwa na teknolojia hizo zenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa. Teknolojia hizo zinatumika kwa mambo ya kibiashara. Makundi mengi katika majukwaa ya kidijitali hutenga makundi ya chini kama vile wanawake, walemavu, na watu wanaotoka kwa kabila na jamii zilizotengwa. Majukwaa hayo hutumiwa kubagua wengine na kueneza habari za uvumi ambazo zinaashiria ukosefu wa utu

katika baadhi ya watu. Lakini, hii haistahili kuwa hatima ya teknolojia za dijitali zilizopo kwa sasa. Teknolojia hizo zinaweza kutumika katika kuwatia nguvu na kuwaunganisha watu kupitia kwa njia ambazo ni nzuri kushinda zile zinazotumika kwa mambo ya kibiashara.

Kuunda mazingira ya dijitali yanayoweza kunyambulika kunahitaji dijitali iliyotenganishwa na miundomsingi ya kibiashara na uongozi wa kimabavu unaotumika katika kutawala majukwaa hayo kwa njia zinazozuia ustawi na mambo mazuri yanayoweza kupatikana.

## Kushawishi wanafunzi ambao ni binadamu

Maendeleo katika bioteknolojia na sayansi ya neva yana uwezo wa kuzindua ubunifu wa binadamu kwa njia ambazo hazijawahi kushuhudiwa. Utawala wa kutumia maadili na unaohamasisha mazungumzo ya jamii unahitajika ndiposa maendeleo yanayohusiana na jeni na nyurokemia yaweze kuchangia katika mustakabali ulio endelevu, wa haki, na amani.

Vifaa vipya vya nyurosayansi huwawezesha watafiti kubaini jinsi akili za binadamu hufanya kazi kumaanisha kuwa hakuna haja ya kuangalia vitendo vya mtu ndipo uweze kujua kinachoendelea akilini mwake. Lakini vifaa hivyo vya kisasa hutumika katika mazingira ya kipekee mbali ya miktadha ya elimu. Utafiti umeangazia sana zile sehemu za akili ambazo huathirika wakati wa shughuli kama kusoma lugha na kufanya hesabu. Kufikia sasa, utafiti haujabaini maudhui yanayostahili kujumuishwa katika mafunzo ya wanafunzi kuhusu vifaa hivyo kwa vile utafiti zaidi unafaa kufanywa.

Hata hivyo, kuna mafunzo mengi yametokana na utafiti huo kuhusu vile akili husaidia katika ujifunzaji. Umuhimu wa afya ya kiakili unasisitiza uhusiano ulio baina ya ujifunzaji na afya ya binadamu; hii ni pamoja na kuashiria uhusiano baina ya haki ya kupata elimu na haki zingine kama haki ya afya.

> Ingawa miaka ya uchanga ni muhimu sana katika ukuaji wa akili, sasa tunaweza kuelewa ni vipi akili ya mwanadamu inaweza kusaidia katika mambo ya ujifunzaji na kemikali zinazosaidia katika kuimarika kwa ubongo baada ya majeraha.

Ushahidi mwingi umeonyesha kuwa ubongo wa binadamu una uwezo wa kubadilika katika kipindi cha uhai wake. Ingawa miaka ya uchanga ni muhimu sana katika ukuaji wa akili, sasa tunaweza kuelewa ni vipi akili ya mwanadamu inaweza kusaidia katika mambo ya ujifunzaji na kemikali zinazosaidia katika kuimarika kwa ubongo baada ya majeraha. Maarifa haya yana ushawishi mkubwa katika maswala ya elimu na ujifunzaji wa watu wazima.

Uwezo wa ubongo wa kujirekebisha unatoa maarifa kuhusu jinsi ambavyo binadamu hukabiliana na mabadiliko ya mazingira na teknolojia. Ripoti hii inasisitiza kuwa watu wa marika yote watalazimika kujifunza jinsi ya kuishi na sayari iliyoharibika. Kujirekebisha kwa ubongo kunahusiana na vile ambavyo watu ulimwenguni kote wanatumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji. Kuna maswala ambayo yameibuliwa kuhusu uwezekano wa teknolojia hizo kukengeusha fikra, kupunguza umaskini, na kuchangia katika mbinu ya kusoma kwa kupitia haraka. Tunaelewa kuwa ubongo hujirejesha kwa njia ambazo huimarisha uwezo wake wa kufanya shughuli kama kusoma

ambayo si kazi rahisi. Umuhimu wa kibayologia na kitamaduni wa kujirekebisha huko umesisitizwa na watafiti wengi wanaongazia mabadiliko kutoka kwa tamaduni za kuongea kuelekea tamaduni za kuandika. Kwa kiasi kikubwa, sisi wanadamu tumekuwa tukijishawishi kwa muda mrefu sasa. Wengi wanapendekeza kuwa tutaweza kujipatanisha na teknolojia mpya za ujifunzaji. Mustakabali wa elimu haustahili kuwa baina ya masomo ya kidijitali na masomo ya vitabu vilivyochapishwa - mustakabali unastahili kufanikisha aina zote za kusoma na kuandika. Masomo ya dijitali na ya vitabu vilivyochapishwa yanastahili kukamilishana.

Ndiposa tuweze kuendesha maendeleo ibuka katika nyurosayansi na bayoteknolojia kwa njia za ufasaha, lazima tuzingatie takwimu huria, sayansi huria, na upanuzi wa kuelewa swala la haki ya kupata elimu ili iweze kujumuisha haki za kuunganishwa, data, na faragha.

# Kuzorota kwa demokrasia na ongezeko la miwaganyiko

Kufikiria kwa makini, uvumbuzi, na kufanikwa katika madhumuni yoyote ni mambo yanayowezekana katika mazingira ya kidemokrasia ambapo haki za binadamu zinaheshimiwa. Hata hivyo, katika muda wa mwongo mmoja uliopita, ulimwengu umeshuhudia kuzorota kwa demokrasia na ongezeko la dhana za kugawanya watu. Dhana hizo huwashawishi wale ambao wanahisi kuwa wamesalia nyuma katika utangamano mpya wa ulimwengu - utangamano ulioangusha kuta, ukatokomeza mipaka, na kubadilisha usafiri wa watu, bidhaa, na maarifa kwa njia ambazo hazikuwa zimeshuhudiwa katika historia. Utangamano huo umechangiwa na uhamaji na kupoteza kwa makazi baada ya vita na kwa sababu ya shida za kiuchumi na mabadiliko ya tabianchi.

> Kuvunjika kwa mazungumzo kuhusu mambo ya kiraia na ongezeko la ukiukaji wa haki ya kujieleza ni mambo ambayo yanaathiri elimu.

Taasisi zinazofanya utafiti na kufuatilia mambo ya demokrasia zina mitazamo tofauti kuhusu mabadiliko haya. Jarida la *The Economist* linaeleza kuwa ulimwengu umehama kutoka kwa demokrasia *kamili* ukaenda kwa demokrasia *yenye kasoro*. Shirika la Freedom House linaelezea kuwa mifumo ya kisiasa iliyokuwa *huru* ina *uhuru wa kiasi* ilhali taasisi ya V. Dem inalinganisha mabadiliko hayo kama kuhama kutoka kwa d*emokrasia ya uchaguzi* kwenda *udikteta wa uchaguzi*. Tukiweka mambo ya majina kando, ni dhahiri kuwa demokrasia ya leo ni dhaifu kushinda ya kitambo.

Mambo ambayo yamechangia mabadiliko hayo ni umaarufu wa viongozi wanaogawanya watu; ongezeko la siasa ya kupendelea wananchi badala ya wahamiaji inayofanywa kuonekana kama uzalendo; mtandao ulio na uwezo kwa kusambaza habari za uongo kwa haraka; na njama ya kutuma data na ujumbe kwa watu maalumu kwa nia ya kuchochea hisia zao. Kiburi cha mabwenyenye na ongezeko la mashaka kuhusu mustakabali pia ni baadhi ya mambo yanayochangia mabadiliko hayo.

Migawanyiko imekithiri ulimwenguni kote kiasi kwamba taasisi nyingi za demokrasia zimelemewa. Taasisi hizo zimepata lawama kutoka kwa wale wanaohisi kuwa demokrasia haijafanikisha ahadi zake. Dhana za ubabe na ubaguzi ni zenye kuleta hasara kwa mambo ya utambulisho, mazungumzo, na uelewano. Haki za kiraia, kisiasa, na kimazingira zinakiukwa na serikali za kidikteta zinazotawala kwa kuwabagua watu na kuwatia uoga.

Kuvunjika kwa mazungumzo kuhusu mambo ya kiraia na ongezeko la ukiukaji wa haki ya kujieleza ni mambo ambayo yanaathiri elimu yenye misingi ya haki za binadamu, uraia, na ujumuishaji katika mambo ya mitaa, nchi, na kimataifa. Wakati huo huo, wananchi wamekuwa wakihamasishwa kwa miaka mingi sasa. Harakati hizi zinazoshindana zinaashiria uthabiti na uwezekano wa kuwa na siasa na demokrasia yenye ushiriki mkubwa.

Harakati hizo zinalenga maswala ya ikolojia, na mara nyingi huongozwa na vijana na raia ambao wamejitolea kupambana na utawala unaokiuka haki za binadamu hasa za walio wachache. Katika muktadha wa kimataifa, harakati hizo zinapigania maswala ya haki za kidemokrasia na heshima kwa utawala wa sheria. Kuna harakati zingine zinazoangazia swala la ubaguzi wa rangi kama vile *Black Lives Matter*, na zile zinazokabiliana na ubaguzi wa jinsia kama *#metoo*. Harakati zingine zinapigana dhidi ya dhana za kikoloni katika mitaala na taasisi za elimu.

Maswala yanayoangaziwa katika harakati hizi yanastahili kujumuishwa katika mitaala ya kesho. Elimu ina jukumu la kukuza demokrasia, nafasi za majadiliaono, mifumo ya ushirikishi, utunzi, na mustakabali wa kushirikiana.

Matatizo ya kiafya yaliyotokana na UVIKO-19 yalitupatia msukumo wa kujihusisha na kushirikiana katika mambo ya kiraia. Serikali nyingi zimegundua kuwa usaidizi wa raia ni muhimu wakati zinapokabiliana na dharura za kiafya. Raia husaidia kupitia kwa uwajibikaji na kwa kutunzana wao kwa wao.

Kwa wakati huo huo, janga la UVIKO-19 lilichangia pakubwa katika kuzorota kwa demokrasia. Tumeona ongezeko la mamlaka ya viongozi, teknolojia za uchunguzi, vizuizi dhidi ya mikutano ya hadharani, vikwazo dhidi ya uhuru wa kutembea, kutumwa kwa wanajeshi katika maeneo ya raia, kubadilishwa kwa kalenda za kura, na athari zinginezo. Ingawa kulikuwa na sababu zilizotolewa kuhalalisha hatua hizo, lazima ikumbukwe kuwa lolote linalotendeka wakati wa dharura huweka wazi aina ya utawala uliopo.

Athari za mabadiliko ya kisiasa zitabaki kuwa nasi kwa karne nyingi zijazo, na zitaathiri elimu kwa sababu siasa huchangia katika ajenda za elimu hasa maswala ya upatikanaji wa elimu, mitaala, na ufundishaji.

Ulimwengu uko katika awamu ya kukabiliana na upungufu wa subira ya watu; upungufu huo umechangiwa na mambo ya mtandao. Tunapokosa kusikizana, maisha ya jamii huharibika. Ili tuweze kujifunza kutunza na kuheshimu wengine, tunahitaji muda wa kutosha. Elimu inaweza kufundisha mambo ya heshima na utunzaji ambayo yatawasaidia katika ushirikishi wao wa kiraia na kidemokrasia.

# Mashaka kuhusu mustakabali wa kazi

Je, elimu ya kesho itaweza kuwasaidia vipi watu binafsi, makundi, na jamii katika maswala na kikazi na kiuchumi?

Mwaka 2019, Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Kazi ilitoa mapendekezo murua yanayoweza kutusaidia katika ujenzi wa mustakabali wa kazi unaozingatia mahitaji ya binadamu. Kwa mujibu wa ajenda hii, watu na kazi ni kitovu cha sera za kiuchumi na kijamii.

Leo hii, ukosefu wa kazi ni wa kiwango cha juu mno. Mabilioni ya watu wanafanya kazi ngumu katika uchumi usio rasmi. Zaidi ya wafanyikazi milioni 300 wanaolipwa wanaishi katika umaskini. Mamilioni ya wanaume, wanawake, na watoto wamekwama katika mazingira ya utumwa wa kisasa. Hatua za kutosha hazijachukuliwa katika maswala ya usalama na unyanyasaji kazini. Katika maeneo mengi ulimwenguni, kuna tofauti kubwa baina ya malipo ya wanawake na ya wanaume, na tofauti baina ya idadi za wanawake na wanaume zinazoshirikishwa katika kazi.

Tangu mwaka 1990, ushirikishi katika kazi umekuwa ukipungua pole pole katika maeneo yote ulimwenguni na katika viwango vyote vya mapato. Hii ni ukweli ukizingatia kuwa ushirikishi wa vijana wa kati ya miaka 15 na 24 umepungua kwa 55% tangu 1990 hadi chini ya 3% leo hii. Sababu ya kupungua huko inaweza kuwa ni ongezeko la idadi ya vijana waliopata masomo ya sekondari na elimu ya viwango vya juu katika miaka thelathini iliyopita. Hata hivyo, mmoja kati ya vijana watano leo hii hana kazi, elimu, au mafunzo. Mmoja kati ya vijana wanne anafanya kazi ya hali ya chini.

Tofauti za ushirikishi katika kazi na fursa za kazi zimeonekana baina ya jinsia. Ushirikishi wa wanawake katika kazi umekuwa ukiongeza kwa karne kadhaa zilizopita. Japo ongezeko la ushirikishi huo limechangia katika usawa wa jinsia, kuna mapengo mapana bado yamesalia. Mwaka 2019, ushirikishi wa wanawake ulikuwa chini ya 50% ilhali ushirikishi wa wanaume ulikwa karibu 75%. Ushirikishi wa wanawake unaathiriwa na viwango vyao vya usajiri katika masomo. Hali za juu za maisha zinaweza kuwachochea wanawake kuacha kazi zao kwa hiari. Lakini, ushuhuda umeonyesha kuwa fursa za kazi walizonazo wanawake ni za hali ya chini. Wanawake hukumbana na vizuizi katika kazi kama kukosa kulipwa wakati wa likizo ya uzazi.

Kiashirio kikubwa cha tofauti baina ya jinsia ni kudumu kwa ubaguzi wa taaluma ambazo wanawake na wanaume wanaweza kuajiriwa. Kwa jumla, kile kinachotambuliwa kama ‘kazi’ na kile kinachokubaliwa kama ‘uzalishaji’ kinachangia pakubwa katika kiini cha kazi kisichoonekana. Hii inajumuisha kazi ambayo ni muhimu kwa jamii lakini inahusishwa na wanawake kwa sababu inafanyika katika mazingira ya nyumbani. Mifano ya kazi hiyo ni kama kulinda watoto, kulinda wagonjwa, kupika, kufanya usafi, na kuwapatia watu wengine msaada wa kimwili na kihisia. Wakati kazi hizi zinafanywa kuwa rasmi, zinawekwa katika kiwango cha chini chenye mapato duni.

Kuimarisha hali ya kazi, na kupanua uhuru walionao watu wa kutafuta riziki ni changamoto ya kimataifa itakayoendelea kushuhudiwa kwa sababu ya vizuizi vilivyotokana na UVIKO-19. Janga hili la kimataifa lilileta mabadiliko katika kazi kwa njia ambazo zitaendelea kutuathiri kwa muda mrefu. Kufungwa kwa mahali pengi pa kazi na kupunguzwa kwa masaa ya kazi kuliathiri mamilioni ya watu ulimwenguni. Kulingana na Shirika la Kazi Ulimwenguni, takribani kazi milioni 150 zilipotea.

UVIKO-19 ni kizuizi katika hatua za kufunga mapengo baina ya jinsia na kurekebisha athari zinazotokana na ukosefu wa usawa ulimwenguni. Ijapokuwa kulikuwa na matumaini kuwa wanawake watanufaika kwa sababu ya fursa za kufanya kazi wakiwa nyumbani, kinyume cha yaliyotarajiwa kimetokea. Katika maeneo yote, wanawake wanaopata viwango vya mishahara mbalimbali wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa ajira kuliko wanaume.

> UVIKO-19 ni kizuizi katika hatua za kufunga mapengo baina ya jinsia na kurekebisha athari zinazotokana na ukosefu wa usawa ulimwenguni.

Tunapoangalia mustakabali wa kazi, tunapata taswira inayokanganya. Maendeleo ya kiteknolojia kama Akili Mnemba, otomatiki, na roboti yataleta kazi nyingi. Vile vile, teknolojia hizo zitafanya wengi wapoteze kazi zao hasa wale ambao hawatakuwa wamejitayarisha kutumia fursa zitakazotokana na teknolojia hizo.

Mamilioni ya fursa za kazi yatapatikana tutakapojenga uchumi ulio endelevu na kuanza kutumia teknolojia zinazotumia nishati safi. Lakini, kuna kazi zingine ambazo zitapotea hasa wakati nchi zitaanza kupunguza viwango vya kaboni zinazotumia katika uzalishaji wao. Uchumi unaoendelezwa katika majukwaa ya kidijitali utarejesha hali za kazi iliyokuwa katika karne 19 na kuchangia katika kuibuka kwa 'wafanyikazi wa siku za kidijitali.' Ujuzi wa hivi leo unaweza kupitwa na wakati na hivyo hautaweza kutumiwa katika kazi za kesho. Mabadiliko haya yanamaanisha kuwa mifumo ya elimu na ujifunzaji lazima iwiane na mabadiliko ya kazi.

## Elimu, ukuzaji wa ujuzi, na kuanza kazi baada ya masomo

Changamoto za mara kwa mara zimeathiri elimu na mafunzo. Taasisi za elimu zina jukumu la kuwatayarisha wanafunzi ili wawe na uwezo wa kujikimu katika mazingira ya uhuru na adhama. Iwapo itawaletea mafanikio katika uchumi rasmi, au uchumi usio rasmi kwa mfano katika kazi ya nyumbani na ya utunzaji, tunatarajia kuwa elimu itawapatia watu wote fursa sawa katika taaluma zao.

Kwa wakati huo huo, elimu haiwezi kurekebisha udhaifu unaotokana na sekta zingine kama zile zimechangia upungufu katika hali ya kazi na ukosefu wa kazi uliokithiri. Elimu ni sehemu moja katika jumla ya sehemu nyingi zilizo katika uchumi. Hali ya kazi inategemea sera za uchumi, viwanda, na kazi. Wakati mwingine mafanikio ya elimu na ukosefu wa ajira huongezeka kwa pamoja. Ulimwenguni kote, vijana wengi waliohitimu vyuo vikuu wanafanya kazi duni na wengine hawajapata kazi zinazolingana na malengo, ujuzi, na uwezo wao. Ukinzani huu ni kama mlipuko: wanasayansi wa kijamii wamethibitisha kuwa kutoridhika, misukosuko, na cheche za migogoro ya kisiasa na kijamii ni baadhi ya mambo ambayo yanaweza kutokea wakati watu waliosoma hawana fursa za kutumia ujuzi wao.

Wakati wa kuanza kazi, baada ya kumaliza masomo, ukinzani hutokea. Masomo lazima yawe sambamba na kazi. Vijana wanahitaji usaidizi ili waweze kupata kazi baada ya masomo yao na waweze kuchangia katika ustawi wa jamii kulingana na uwezo wao. Viongozi wa viwanda na jamii wanastahili kuhusishwa katika maisha ya wanafunzi walio katika shule za upili na walio katika vyuo

> Elimu inastahili kuwasaidia watu katika kupata maarifa ya kujikuza kijamii na kiuchumi ndiposa kuwe na manufaa kwa wao wenyewe, familia zao, na jamii kwa muda mrefu.

vikuu. Kuhusishwa huku kutawasaidia wanafunzi kupata habari kuhusu kazi wanazoweza kufanya. Taasisi za elimu zinastahili kupeana mawaidha juu ya taaluma na usaidizi kupitia kwa walimu ambao watawaongoza wanafunzi kwa muda mrefu. Mafunzo ya ufundi katika sekondari na elimu ya juu yanastahili kujumuisha mafunzo kuhusu kazi halisi. Mafunzo hayo yanaweza kupatia wanafunzi si uzoefu wa kazi tu, bali yanaweza kuimarisha viwango na umuhimu wa elimu na mafunzo. Ni muhimu elimu iangazie masomo ya taaluma mbalimbali ndiposa yasipunguze fursa za kuongeza maarifa watakayohitaji wanafunzi siku za mbeleni.

Elimu pekee haiwezi kutosheleza mahitaji ya kazi. Pia, haiwezi kusuluhisha shida za ukosefu wa ajira unaotokana na misukosuko ya kiuchumi. Vile vile, mabadiliko ambayo yametekelezwa katika mambo ya uzalishaji na ambayo yameathiri mafunzo ya ufundi kwa miaka ya karibuni, hayawezi kuchangia katika ongezeko la kazi.

Lakini elimu inaweza kuimarisha jinsi ambavyo watu wanavumbua, wanavyotumia maarifa yao, wanavyosuluhisha shida, na kukamilisha kazi ngumu. Katika viwango vya juu, elimu hukuza maarifa mengi na ujuzi wa hali ya juu kwa njia ambazo huongeza matumaini waliyonayo wanafunzi kuhusu nafasi watakazopata ili waweze kutumia maarifa hayo na ujuzi huo. Dhana ya elimu kuwa njia ya kupata kazi au kujenga maarifa ya kibiashara ni potovu. Elimu inastahili kuwasaidia watu katika kupata maarifa ya kujikuza kijamii na kiuchumi ndiposa kuwe na manufaa kwa wao wenyewe, familia zao, na jamii kwa muda mrefu. Mustakabali wa kazi unahitaji tujifunze kuishi na teknolojia.

Njia mojawapo ya kujitayarisha kwa ajili ya uchumi ulio endelevu na wenye kaboni kidogo, ni kuhakikisha kuwa ujuzi endelevu unakuzwa kupitia kwa viwango vya ujuzi, programu, na mitaala. Hatua nyingine muhimu itakuwa kuhakikisha kuwa mazingira ya elimu ni endelevu. Wanafunzi watakuwa tayari kufanya kazi katika uchumi endelevu ikiwa watawezeshwa kuongoza njia katika kuunda mitaala ya elimu inayozingatia uendelevu.

## Mabadiliko katika dhana ya kufuzu

Swala la hati za kufuzu liko kwenye njiapanda: kati ya elimu na kazi. Jukumu la shule, vyuo vikuu, na programu za ufundi ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wana ujuzi, uwezo, na maarifa wanayostahili kuwa nayo. Watu wamezidi kuelewa kuwa kufuzu kwao kuna haki kutambuliwa iwe kufuzu huko kumetokea katika mazingira rasmi ya elimu au yasiyo rasmi.

Kuangazia tu hati ya kufuzu kwa mtu hakutoshi. Na ingawa ni muhimu kufikiria juu ya kufuzu, hatustahili kupuuza ushirikiano ambao ni kiini cha elimu. Hati za kufuzu hazionyeshi kazi zote ambazo mtu anaweza kufanya hasa zile zinazohitaji uaminifu wa kijamii.

Jinsi mabadiliko katika uajiri na taaluma yanavyoendelea kububujika, ndivyo utafiti unastahili kufanywa ili kubaini vile watu wanaweza kabadilisha kazi. Ushirikiano baina ya serikali, walimu,

waajiri, na umma wote kwa jumla utasaidia katika kufafanua taaluma na kazi zitakazoibuka. Mifumo ya kuchunguza na kufuatilia mabadiliko katika kazi na taaluma imezidi kuwa changamani. Mifumo ya elimu na ujifunzaji inastahili kulinganishwa ili iweze kuleta mbinu za kutosha katika ujifunzaji wa kazi. Taasisi lazima ziboreshe jinsi ambavyo zinashughulikia maswala ya kufuzu, mitaala, na programu.

## Mabadiliko makubwa kwenye masoko ya ajira

Kando na mabadiliko ya kiteknolojia na kiuchumi, kumekuwa na mambo ya kiuchumi ambayo yanabadilisha masoko ya ajira. Kazi za wanakandarasi na za wafanyikazi huru zimeongezeka na zinathibitisha umuhimu wa uchumi usio rasmi kwa mamilioni ya watu ulimwenguni. Mbinu hizi za uajiri zitawahamasisha wafanyikazi wengi kuongeza ujuzi wao. Njia za kupata masomo lazima zipanuliwe ndiposa taasisi ziweze kuwa na wanafunzi mbalimbali wanaoweza kupata mafunzo wakati wowote.

Mabadiliko ya demografia yatakuwa na uzito mkubwa ifikapo mwaka 2050. Ukizingatia vile idadi ya vijana inaongeza ulimwenguni, kuna maeneo mengine yatakabiliwa na ukosefu wa ajira na shida za uhamaji. Maeneo mengine yatakuwa na idadi kubwa ya watu wazee ambayo italeta matatizo katika mifumo ya utunzaji katika jamii.

Kwa sasa, jamii ya kimataifa inatumia hesabu za uwiano wa utegemezi kulinganisha idadi ya watu wote na ile ya walio kati ya miaka 15 na 64, ambao wana uwezo wa kufanya kazi ili waweze kuwalinda watoto wachanga na wazee. Kufikia mwaka 2050, viwango vya uwiano wa utegemezi vinakadiriwa kuongezeka sana huko Ulaya na America. Uwiano huo utaongezeka kwa viwango vya wastani huko Asia, Amerika ya Kusini na Uarabuni – hii inamaanisha kuwa idadi ndogo ya walio na kazi itategemewa na idadi kubwa ya wasio na kazi (sana sana waliostaafu). Wakati huo huo, uwiano wa utegemeji wa Afrika unakadiriwa kupungua kwa 50% kwa sababu watu wengi watakuwa chini ya miaka 25.

Mabadiliko haya ya kidemografia, ambayo yanaonyesha ongezeko la idadi za watu wachanga na wazee, yanaathiri mambo ya ajira, elimu, na mafunzo ya ufundi. Hii inajumuisha hatua za kupanua mafunzo ya ufundi na mafunzo ya watu wazima ambayo yanatumiwa kuimarisha mafunzo yanayoendelea katika hatua zote za maisha. Ikiwa watu wazee wataendelea kufanya kazi, jamii itanufaika kutoka kwa maarifa na ujuzi wao. Kuwasaidia watu wachanga ndiposa waweze kupata uwezo mkubwa na fursa za kazi kutawafanya maajenti wa mabadiliko. Hii inamaanisha kuwafadhili watu ndiposa waweze kupata uwezo, ujuzi, na maarifa zaidi katika hatua zote maishani mwao.

Mabadiliko haya yanapoendelea kutokea, matarajio ya elimu yatabadilika. Kutakuwa na haja ya kupanua madarasa ya masomo ya msingi na kuajiri walimu zaidi katika maeneo mengi. Ukiangalia jinsi ambavyo elimu ni swala changamani, kuna mambo mengine, katika elimu hayatakuwa rahisi kubadilisha. Kwa sababu hizo, taasisi za mafunzo zinastahili kushirikiana na jamii ndiposa zijithibitishe kama taasisi za msingi. Kufanya kazi pamoja na taasisi za kijamii kutawezesha shule na taasisi kuelewa jamii na kuipatia elimu inayostahili.

## Ni kazi gani itathaminiwa katika siku za usoni ?

Tunapoelekea mwaka 2050, kuna taswira inayojitokeza na ambayo itachangia katika mabadiliko mapya ya historia ya binadamu. Kuna uwezekano wa viwango vya kazi kupungua licha ya kuwepo kwa wafanyikazi waliona ujuzi wa juu kwa sababu ya mabadiliko ya kiteknolojia. Elimu itakuwa na maana gani katika jamii yenye watu wachache walio na kazi za rasmi? Ni aina gani za elimu ambazo watu watahitaji ili waweze kuishi bila ya kazi za rasmi?

Thamani ambayo jamii za binadamu zimeweka kwa kazi ya kibinadamu imekuwa ikibadilika. Katika milenia moja iliyopita kumekuwa na ndoto ya kuwa na uhuru wa kutofanya kazi ngumu. Lakini leo hii tatizo kubwa ni la kukabiliana na viwango vya juu vya wakati wa kupumzika. Ukosefu wa ajira uliokuwa unatatiza nchi maskini kwa karne kadhaa umefika katika nchi tajiri. Kuna mambo mengi yanayostahili kubadilishwa. Je, misukumo ya uzalishaji na ubunifu waliyonayo binadamu itaweza kutumika aje kwa njia ambazo zitafaidi watu binafsi na jamii zao?

> Ni aina gani ya elimu ambayo watu watahitaji ili waweze kuishi bila ya kazi za rasmi?

Kwa bahati nzuri, baadhi ya mapendekezo mazuri ambayo yametolewa yanaweza kubadilisha elimu na uajiri. Kuna mashaka mengi kuhusu mustakabali wa kazi na Dunia ambayo yanaonyesha kuwa lazima tusisitize umuhimu wa wanafunzi kupata uwezo wa kuelewa mambo.

Kwa kweli, itatulazimu tubadilishe mtazamo kuhusu uzalishaji wa thamani ya vitu. Tunapofikiria kuhusu mustakabali wa ajira na elimu, tunaona chaguo mbili: aidha tuendelee na mazoea kinzani ya kutarajia matokeo makubwa au kidogo kutoka kwa elimu – au tuzingatie mafaniko yanayoweza kutokana na elimu.

Katika siku za usoni, thamani ambayo tutaiweka kwa vitu kama kilimo na viwanda itakuwa tofauti. Usalama wa kiuchumi hautokani na kushughulikia mahitaji ya uchumi wa rasmi tu.

Lazima tuangazie kazi ya utunzaji inayotendeka katika mazingira ya nyumbani, utoaji wa bidhaa za kawaida, na miundombinu ya serikali. Ingawa kuna mbinu nyingi za asili zinazoshughulikia maswala hayo, mbinu zingine za kuelewa mambo yanayochangia usalama wa kiuchumi zitakuwa zinatumika kufikia mwaka 2050.

Elimu inayoangazia uchumi wa aina zote inaweza kuchangia ustawi wa kiuchumi wa muda mrefu. Mkataba mpya wa mustakabali wa elimu unastahili kuwa wenye uwezo wa kubadilika.

# SEHEMU YA II
## Kubadilisha elimu

Mwaka 1921, waelimishaji kutoka sehemu mbalimbali walijumuika Calais, Ufaransa kwa ajili ya kongamano la kwanza la Ushirika Mpya wa Elimu ambalo kazi yake ilienea kwa kipindi cha karne mbili na kusaidia katika kuanzishwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi, na Utamaduni ambalo jukumu lake ni kushughulikia elimu. Katika mkutano wa kwanza, ilitangazwa kuwa 'elimu mpya ya enzi mpya' ilikuwa imeibuka.

Jukumu la ripoti hii sio kutoa wito wa kuanza upya tena. Tunahitaji ufundishaji mpya, mitaala mipya, kujitolea kwa walimu, dira mpya ya shule, na kuthamini kupya kwa nyakati na nafasi za elimu. Lakini, hii haimaanishi kutupilia mbali vitu tulivyonavyo kufikia sasa. Badala yake, lazima tuchunguze mila zetu za ufundishaji na elimu, tubadilishe historia, na tujumuishe vipengele vingine vitakavyoimarisha mustakabali wa binadamu na Dunia.

Katika karne moja iliyopita, jamii na familia nyingi zimeongeza matumaini yao kuhusu uwezo wa elimu ya lazima kuwawezesha watoto wao kupata elimu. Ulimwenguni kote, shule zimepangwa kwa njia zinazofanana. Ingawa mipango hiyo inachukua miundo tofauti katika maeneo na tamaduni mbalimbali, imeenea ulimwenguni kwa njia ambazo zimepunguza tofauti za kielimu zilizo shuhudiwa enzi za kitambo. Mkataba mpya wa ulimu ulioanzishwa katika karne za 19 na 20 ulileta kanuni za kuongoza elimu.  Kwanza, elimu ilitazamwa kama mradi wa ufundishaji ambao msingi wake ni mafunzo yaliyotolewa na walimu katika madarasa kwa lengo la kufanikisha ustawi wa kibinafsi. Pili, elimu iliendelezwa kupitia kwa mitaala iliyojumuisha masomo mengi. Tatu, ujifunzaji ulikusudiwa kuwa utendaji uliotegemea maarifa na mwalimu binafsi kufanikisha ujifunzaji katika somo fulani. Nne, shule zilitumia mpangilio uliokuwa sawa.

Na tano, elimu ilipangwa ili wanafunzi wa rika moja wasome pamoja katika taasisi maalumu ambazo zilikwa mbali ya familia na jamii zao. Mara tu watoto na vijana walionekana kuwa tayari kwa maisha ya utu uzima, elimu yao ilikamilika.

Mkataba mpya wa kijamii wa elimu lazima uimarishe elimu kama mradi wa kijamii, jukumu la kijamii, mojawapo ya haki muhimu za binadamu, na mojawapo ya jukumu la mataifa na wananchi. Jukumu la elimu ni kuelimisha watu jinsi ya kuimarisha haki za binadamu. Hili linahitaji wanafunzi walio na uwezo wa kufanya maamuzi mazuri na yenye maadili. Inaamanisha wanafunzi watakuwa na uwezo wa kushirikiana na wengine katika kukuza uwezo wao wa kujiamulia, uwajibikaji, ubunifu, na uwezo mwingine wa kihisia na kijamii. Njia mpya za ufundishaji zinahitajika ndiposa elimu ilainishwe na dira yake. Elimu ni kitovu cha amani ulimwenguni. Sehemu ya pili ya ripoti hii inatoa mapendekezo kuhusu jinsi ambavyo mkataba mpya utaimarisha haki ya kupata elimu ili iwe rasilimali ya umma na mradi wa pamoja wa kuwawezesha binadamu kutunzana na kushirikiana.

Kanuni za kuongoza mazungumzo na hatua tofauti zimeelezwa katika sura tano za maandiko yaliyotokana na mashauriano yaliyofanywa na Tume katika kipindi cha miaka miwili ambapo michango ya vijana ilipatiwa kipaumbele. Vile vile, kanuni zinatokana na maarifa ya kisayansi ambayo yamejengwa kupitia kwa utafiti na mawazo ya wataalamu.

Uwezekano wa kubadilisha kanuni hizi ili ziwe sera zinazofanya kazi, unategemea wale watakaoisoma ripoti hii. Kila mwanafunzi, mwananchi, mwalimu, na mzazi ana uwezo wa kuchangia katika mabadiliko ya miradi ya elimu na taasisi za elimu. Ushirikiano huu ndio utabadilisha mustakabali. Lengo la Tume katika kutoa ripoti hii ni kupanua mazungumzo kuhusiana na kanuni za mabadiliko. Ripoti hii ilitayarishwa kwa njia ya ushirikiano. Kutimizwa kwa mawazo yaliyo pendekezwa kutahitaji ushirikiano pia.

# Sura ya 3

# Ufundishaji wa ushirikiano na mshikamano

'Elimu halisi lazima ihusishe malengo ya wanaofunzwa. Ili kuwe na huo uhusishwaji, lazima walimu wajenge uhusiano wenye misingi ya utunzaji na uaminifu, na wanafunzi na walimu washirikiane katika kujenga madhumuni ya elimu.'

**Nel Noddings,** *Philosophy of Education.*

**Katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, ufundishaji unastahili kuhimiza ushirikiano na mshikamano ili uwezo wa wanafunzi na walimu wa kubadilisha ulimwengu uongezeke.**

Ili kubadilisha mustakabali, lazima ufundishaji uhimize ushirikiano na mshikamano. Swala la 'tutajifunza aje?' linastahili kutegemea mambo tunayojifunza. Msingi wa kufunza na kuinua haki za binadamu unamaanisha kuwa lazima haki za mwanafunzi ziheshimiwe. Lazima tuwe na fursa za watu kufunzana kuhusu tofauti zao za kijinsia, kidini, kijamii, ujinsia, matabaka ya kijamii, ulemavu, uraia, na kadhalika. Kuheshimu adhama ya watu wengine inaamaanisha kuwafunza jinsi ya kufikiria kwa uhuru na si mambo wanayostahili kufikiria au njia za kufikiria. Inaamaanisha wanafunzi kupatiwa fursa za kujielewa na kuamua maisha wanayotaka. Vile vile, tunapaswa kushirikiana katika kujenga ulimwengu ambao kila mtu anashirikishwa katika kuimarisha ulimwengu.

Ufundishaji wa kushirikiana na kushikamana unastahili kueneza dhana za kutobagua, heshima kwa utofauti, ya haki iliyojikita katika maadili ya utunzaji na kutendeana mazuri. La muhimu ni kuwa ufundishaji unahitaji elimu inayoleta ushirikiano na inayoangazia maarifa ya nyanja tofauti, tamaduni mbalimbali, na maswala yanokabili marika yote. Ufundishaji huo unaweza kupatikana katika maarifa ya jamii na kuendelea kwa muda mrefu na kuleta fursa nyingi za kujielimisha katika viwango tofauti vya elimu.

Ujifunzaji kamilifu unatambua umuhimu wa maarifa ya dhana na maarifa ya utaratibu. Ujifunzaji huo unatambua sababu ya kuhusisha akili na hisia na elimu ndiposa mtu akuze maarifa; apate uwezo kwa kubadilisha maarifa yawe matendo; na apate mwelekeo wa kuongoza matendo yake. Mbinu za ufundishaji zinazozingatia mazoea, kufikiria, na ujifunzaji zinahitaji kubadilishwa kulingana na mahitaji ya sasa na ya kesho. Vishawishi vikubwa vya masomo ni uhalisi (ambao unalenga uhusiano baina ya mambo yanayohitaji kusomwa na ulimwengu tunaoishi) na umuhimu (wa kuelewa uhusiano baina ya mambo tunayosoma na maadili yetu). Ujifunzaji unaozingatia miradi na utafutaji wa suluhu huleta fursa ya kupata masomo halisi na yaliyo muhimu.

Nusu ya sura hii inaelezea mbinu za ufundishaji wenye misingi ya ushirikiano na mshikamano kama vile ufundishaji ulio shirikishi, na unaoangazia taaluma mbalimbali na usuluhishaji wa shida; ufundishaji unaothamini na kulinda utofauti; ufundishaji unaowahimiza wanafunzi watupilie mbali ubaguzi na migawanyiko; ufundishaji unaoponya majeraha ya dhuluma; na ufundishaji unaochanganua mambo vizuri. Mbinu hizi zinaweza kutumika katika mazingira yote, yaliyo rasmi na yasiyo rasmi, kama vile majumba ya makumbusho, maktaba, kambi za majira ya kiangazi, na vituo vya umma. Vile vile, sura hii inachanganua mambo yanayostahili kupatiwa kipaumbele katika elimu ya rasmi: kufadhili elimu ya chekechea, kuangazia mahitaji tofauti ya waliobalehe na vijana, na kubadilisha lengo la elimu ya juu. Sura hii inahitimisha na kanuni za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu zitakazochukuliwa na wakufunzi na mameneja wa taasisi za elimu. Kanuni hizo ni kama kujenga mahusiano ya kina na ulimwengu, kuwezesha ushirikiano, kukuza uwezo wa kuelewa hisia za watu wengine, na kutumia tathmini katika kuendeleza ujifunzaji.

# Kubadilisha mbinu za ufundishaji

Ufundishaji ni hali ya uhusiano. Walimu na wanafunzi habadilika kupitia kwa ufundishaji unaowasaidia kufunzana. Mvutano baina ya mabadiliko ya watu binafsi na mabadiliko ya jumla ya makundi ni kitovu cha mapambano ya ufundishaji. Maisha yetu huathiri mazingira; mazingira hutuathiri pia.

Pembetatu ya ufundishaji ina wanafunzi, walimu, na elimu. Ufundishaji na ujifunzaji huchangia katika maarifa ya jamii. Kupitia kwa mapambano ya ufundishaji, elimu hutuambatanisha na historia ya maarifa ya jumla ya binadamu. Leo hii, pempetatu hiyo inastahili kuwekwa katika muktadha wa ulimwengu mzima. Tunahitaji ufundishaji unaotuwezesha kusoma *ndani ya* na *pamoja na* ulimwengu ilituweze kuuboresha.

Ufundishaji huo unataka tuendelee kujifunza kuhusu adhama ya kila mtu na umuhimu wa kuwa na uhuru wa dhamiri unaoweza kutusaidia kutupilia mbali hisia za ubinafsi za kujihisi kuwa wa maana kuliko watu wengine. Ufundishaji unafaa kuwa nguzo ya kutendeana mazuri, utunzaji, na kukubali utegemeano ulio kati ya watu kibinafsi, makundi, na katika spishi. Ufundishaji huo unastahili kutuhimiza kuelewa jinsi tunavyotegemeana na mambo yanayotuunganisha na Dunia.

Walimu na wanafunzi wanastahili kujenga jumuiya ya wanaotafuta na wanaojenga maarifa ya jamii. Hii inastahili kuangalia vitu tulivyonavyo, vile ambavyo vinaweza kujengwa, na kukubali kwamba kila mtu, walimu na wanafunzi, wana haki ya kuchangia katika ukuzi wa maarifa.

> Walimu na wanafunzi wanastahili kujenga jumuiya ya wanaotafuta na wanaojenga maarifa ya jamii.

Kuna maswali mengi kuhusu maana na malengo ya ufundishaji. Je, walimu wanawafunza nini wanafunzi kuhusu hatua na mwingiliano? Wanafunzi wanapata faida gaini kutoka kwa juhudi zao masomoni?

Ufundishaji unaolenga kuleta mabadiliko huchochea mazungumzo baina ya wanafunzi, marafiki zao, na wanajamii. Usayansi na usanii wa ufundishaji hutumiwa kwa njia tofatuti na walimu ambao hupatia wanafunzi fursa za kutangamana na mambo wanayojua na wasiyojua kwa njia zinazokuza udadisi na usikivu. Sehemu zinazofuata zinaelezea mikatati ya kuunganisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu na mbinu za ufundishaji.

## Elimu inayoangazia taaluma kadhaa, matatizo, na ushirikiano

Wanafunzi watapatana na shida na fursa mpya katika siku zijazo. Mitaala inaweza kujumuisha maswala ya mabadiliko kwa njia ambazo zitaongezea uwezo wa wanafunzi wa kubainisha shida na kuzisuluhisha. Elimu hiyo ya kusuluhisha matatizo inahusisha miradi, uvumbuzi, na ushirikiano. Lazima wanafunzi wawe na malengo ndiposa waweze kukiuka mipaka ya kuvumbua na kupata suluhisho. Kuangazia shida na miradi wakati wa masomo kunaweza kuwasaidia kupanua maarifa

waliyonayo wanafunzi kuhusu kubadilika kwa ulimwengu, kujenga maarifa na weledi, na kuimarisha uwezo wa kuandika, kusoma, na kujieleza.

Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu inatambua umuhimu wa wanafunzi kuelewa mbinu tofauti za kutatua matatizo. Lengo la 4.7 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linaeleza kuwa wanafunzi ni raia wa kimataifa wanaohitaji maarifa na ujuzi wa kujenga mustakabali ulio endelevu kwenye ulimwengu wa kutegemeana. Tukiangalia mwaka 2050 na zaidi, tunaona umuhimu wa kuimarisha uwezo huo. Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatupatia mfumo wa kushughulikia shida kupitia kwa masomo yanayolenga taaluma nyingi kwa njia zinazowawezesha wanafunzi kufikia malengo yote.

Kuangazia matatizo na miradi ya kijamii inamaanisha kupatia masomo, utafiti, na ushirikiano kipaumbele. Maarifa ya kibinafsi hupanuka wakati tunapotangamana na wengine, kumaanisha kuwa elimu ina vipengele vingi vilivyounganishwa. Mbinu zinazozingatia miradi na shida tofauti hazipuuzi umuhimu wa elimu, badala yake, zinasisitiza manufaa ya kuwa na maarifa ya kuishi katika mazingira mbalimbali.

Aina nyingi za elimu zilizo mwafaka hutokea katika mazingira yaliyo na wingi wa maarifa yanayoenda zaidi ya mipaka ya masomo ya kawaida. Badala ya kutii mipaka, ufundishaji unastahili kujumuisha maswala ya taaluma nyingi, shida tofauti, na mafumbo ya ulimwengu. Hata ingawa kuna njia nyingi za kusuluhisha shida, ufundishaji unastahili kukuza maadili ya kutegemeana na mshikamano. Masomo kuhusu utumishi na kujihusisha na mambo ya jamii huvunja kuta baina ya madarasa na jamii, huchochea dhana za wanafunzi, na kuwaunganisha na mifumo mipana iliyo zaidi ya mambo ambayo wameyazoea. Ni sharti wanafunzi wajitolee kwa utumishi na moyo wa unyenyekevu usio na ufidhuli hasa dhidi ya wanyonge. Masomo kuhusu utumishi yanastahili kulenga wanafunzi wote, sio wale waliofanikiwa tu kwa vile kila mwanafunzi ana uwezo wa kutoa mchango katika jamii. Masomo kuhusu utumishi yana uwezo wa kukuza mshikamano katika ufundishaji wa kusuluhisha shida badala ya kutumia mbinu za kunufaisha mtu binafsi.

## Kuthamini na kudumisha utofauti na wingi wetu

Ndiposa tubadilishe mustakabali wetu, lazima tuongozwe na dira ya jamii ambayo inakuza utofauti na wingi wa binadamu. Tunahitaji elimu ya kutusaidia kuenda zaidi ya mipaka na kufikia vile vitu visivyojulikana.

Ufundishaji wa mshikamano lazima uendeleze elimu iliyo jumuishi na inayohusu tamaduni nyingi. Ufundishaji huo lazima uangazie aina zote za ubaguzi: ubaguzi wa walemavu, kijamii, jinsia, matabaka ya kipato, dini, na uraia. Haki ya kujumuishwa kulingana na hali ya mtu, ni haki muhimu kuliko haki zote za binadamu. Ufundishaji lazima uwakaribishe wanafunzi wote katika jamii ya kielimu na uwasaidie kupata maarifa ya ujumuishi na kuheshimu adhama ya wengine. Ufundishaji usio jumuishi hudhoofisha uwezo wa elimu kuwa rasilimali ya jamii na kupunguza uwezekano wa kulinda adhama na haki za binadamu.

Ujifunzaji lazima uthamini utofauti na wingi kwa sababu ndio mwanzo wa kuwasaidia wanafunzi katika harakati za kukabiliana na ubaguzi. Hakuna dhana moja au jamii moja ambayo inaweza

kutoa suluhu kwa matatizo tete yanayokumba ulimwengu. Ufundishaji wa mshikamano lazima utambue na kurekebisha kutengwa na kufutwa kunakotokana na ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa jinsia, ukoloni, na uongozi wa kidikteta. Pasi na kuthamini tamaduni na epistemolojia tofauti na njia mbadala za kuishi na kuona ulimwengu, itakuwa vigumu kujenga ufundishaji wa mshikamano. Ufundishaji wa mshikamano hujumuisha utofauti katika kila hatua.

> Ufundishaji wa mshikamano lazima utambue na kurekebisha kutengwa na kufutwa kunakotokana na ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa jinsia, ukoloni, na uongozi wa kidikteta.

Kuongezeka kwa uhamaji wa binadamu ulimwenguni, ambao unaweza kuwa wa hiari au wa kulazimishwa, umebadilisha hali ya ufundishaji kwa kuleta utofauti wa kijamii na kitamaduni katika mazingira ya elimu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira mapya; wanafunzi wana historia, lugha, na tamaduni tofauti. Ufundishaji, wa heshima, ujumuishaji, kukubali wengine, ukuzaji wa amani, na kubadilisha kwa migogoro, lazima ufanye zaidi ya kukubali na kustahimili tofauti. Lazima ufundishaji huo uwasaidie wanafunzi kukaa na kufanya kazi pamoja. Tutaweza kujitayarisha kwa ajili ya mustakabali usiotabirika kupitia kwa elimu inayowaruhusu vijana kuelewa na kuunganisha historia, hali ya sasa, na mustakabali.

Elimu itatuwezesha kupambana na shida za kutengwa na kupuuzwa. Dunia ina wingi wa tamaduni na kabila; kwa hivyo, inastahili kustawisha uraia wa kitamaduni. Kando na kufunza kuhusu umuhimu wa utofauti, elimu inastahili kukuza uwezo, maadili, na hali zinazohitajika ndiposa kuwe na mazungumzo ya ufasaha baina ya watu walio na utofauti na katika miktadha tofauti. Msingi wa uraia wa kitamaduni, ni kukubali aina nyingi za tamaduni. Kujielewa ndio mwanzo wa kuheshimu watu wengine. Elimu kuhusu tamaduni tofauti haistahili kutumika kama chombo cha kuwalazimisha watu wa asili na wale wa makundi yaliyopuuzwa katika jamii waasi tamaduni zao. Elimu hiyo inafaa kuwa chombo cha kuleta usawa na demokrasia katika mahusiano ya makundi. Tunahitaji ufundishaji unaofanikisha kubadilishana maarifa, mitindo, na suluhu, kwa njia za kukamilishana na heshima.

Kupitia kwa tofauti zetu tutaelimishana, na kupitia kwa ushirikishi tutaweza kubaini maana ya vitu. Ni muhimu kutofautisha 'utofautishaji katika ufundishaji', unaolenga wanafunzi wote, na 'kubinafsisha kwa masomo' kunakotoa wanafunzi katika mazingira ya jumla na kukatiza uhusiano wao na wanafunzi wengine. Tofauti zetu ni za kuunganishwa ili ziongeze maafikiano yetu.

Mara nyingi, ufundishaji hutokea kwa muda au mandhari ibuka, yaliyo tofauti na yaliyo chini ya ujenzi siku zote. Tunaweza kuwa na nakala mbili za kitabu kimoja, lakini hakuna njia mbili sawa za kukisoma. Tunaweza kuwa na mipango ya masomo mawili yanayofanana, lakini hakuna njia mbili sawa za kufunza. Hili jambo linatuhimiza tuwe makini katika mambo ya teknolojia za elimu zinazoendelea kuongezeka katika 'sekta ya elimu ulimwenguni.' Tunahitaji mchango wa kibinadamu katika mitaala otomatiki inayotumia Akili Mnemba na inayoahidi miongozo ya kufunza, kusoma, au kutathmini iliyo tayari. Upungufu wa mifumo hiyo unastahili kubainishwa pale ambapo inatumika hasa uwezekano wa kueneza dhana potovu ambazo zinaweza kuwatenga wanaosoma. Juhudi zetu zinastahili kuelekezwa katika kukuza uwezo wa kuelewa hisia za watu wengine, maadili, mshikamano, ushirikiano katika ujenzi, na haki, ambayo ni maswala yanahitaji

kufunzwa na kusomwa kwa ustahimilivu bila ya kuchukua njia za mkato za kiteknolojia. Hizi ni shughuli za binadamu zinazostahili kufanikishwa na binadamu.

## Kuitupilia mbali hulka ya kutenganisha

Ufundishaji wa ushirikiano na mshikamano unahitaji mengi zaidi ya kukubali na kujitolea kuendeleza utofauti. Ufundishaji huo unahitaji kutupilia mbali ubaguzi na hulka ya kugawanya watu. Kwa hakika, maarifa sio bidhaa ya kusambazwa. Badala ya kuzingatia usambazaji wa elimu, ufundishaji unaweza kutoa mwelekeo kuhusu jinsi elimu imekuwa ikibuniwa katika historia.

> Rasilimali za kijamii ni nguzo katika uhusiano wetu na maarifa

Rasilimali za kijamii ni nguzo katika uhusiano wetu na maarifa. Sera za elimu zimekuwa zikilenga kusuluhisha ukosefu wa usawa wa kijinsia, kijamii, kikabila, kidini, makao, uraia, ulemavu, ujinsia, au tabaka la kijamii. Lakini sera hizo hazijasisitiza maswala ya kunyamazishwa kwa watu, kutengwa kwa kumbukumbu, matarajio, tamaduni, na maarifa ya asili. Lazima tujifunze kutupilia mbali mambo mengine ambayo tulijifunza kitambo.

Inaweza kuwa hatari na vigumu kuja pamoja ili tuchanganue hali zetu na tujishughulishe na maarifa ambayo yamekuwa kwa muda mrefu. Mazingira ya elimu yanastahili kuwa mahali salama ambapo wanafunzi wanaweza kuhamasishwa kufanya majaribio, kuwa na ujasiri, kuanguka, na kujenga vitu. Jukumu la ufundishaji ni kuchochea ubunifu, uhuru wa kiakili ambao unajumuisha haki ya kufanya makosa na kupata mafunzo kutoka kwa makosa hayo. Mazingira yanayochangia haya ni muhimu katika ujenzi wa uwezo wa kuelewa hisia za wengine, mifumo ya maarifa, na kukubali tofauti za kuelewa na tofauti za mitazamo. Wakufunzi wana jukumu la kutengeneza mazingira ya kuwaruhusu wanafunzi kufanya makosa hasa wanapokabiliwa na maarifa mapya bila ya kuogopa kuhukumiwa.

## Kujifunza kuponya vidonda vya dhuluma

Kujua kunashikamana na kuhisi. Weledi wa binadamu umeunganishwa na fahamu na njia za kuonyesha hisia. Kuelewa uhusiano huo ni muhimu katika mambo ya elimu. Tunaweza kukabiliana na aina yoyote ya fikra na maadili kwa kutumia njia nyingi za kujua na kuhisi na aina tofauti za epistemolojia. Kusafisha dhana za kikoloni zilizo katika ufundishaji kunawezekana kwa kuangalia uhusiano baina ya dhana na mitazamo ya kiepistemolojia. Tunatarajia kuwa elimu itatumika katika kuleta mshikamano na haki inayotibu dhuluma. Mshikamano ni nguzo ya kujenga jamii iliyo ungamana, na katika siku za karibuni umekuwa lengo kuu katika ufundishaji wa rasmi na usio rasmi.

Ufundishaji wa mshikamano umesaidia katika kushinda utawala unao kandamiza watu kupitia kwa ujenzi wa ufahamu kuhusu umuhimu wa kuchuka hatua za pamoja. Kazi ya elimu inaweza kupanua mshikamano kwa kufunza huruma na kuelewa hisia za wengine kwa njia zinazoleta uponyaji. Kuelewa hisia za watu wengine na maadili ni viungo muhimu vya haki. Kujifunza kuponya

dhuluma za kitambo ni kiungo muhimu kinachostahili kuwa katika ufundishaji wa kushirikiana na mshikamano.

### Kuimarisha tathmini

Kimsingi, tathmini ni harakati ya kawaida inayotumiwa kujua hatua na changamoto za mwanafunzi katika masomo. Tathmini ya viwango inatumika katika kuwapanga wanafunzi katika viwango tofauti na lazima itumiwe kwa makini. Tathmini zinafanya kazi kulingana na dhana tofauti na lazima ziwe sambaba na mitaala na ufundishaji.

Kwa muktadha wa ufundishaji wa ushirikiano na mshikamano, wakufunzi lazima wabainishe malengo ya ufundishaji ambayo yanaweza kukadiriwa na yale ambayo hayawezi kukadiriwa. Masomo yaliyo ya muhimu mno hayawezi kuhesabiwa wala kupimwa. Kusema kuwa kitu hakiwezi kupimwa sio kusema kuwa maendeleo hayawezi kuonekana. Kwa mfano, lengo la kushirikiana linaweza kuonekana wakati wanafunzi wanajadiliana, wanapofanya majaribio, na wanaposuluhisha tofauti kati yao. Katika shughuli hizo, wanafunzi huongeza uwezo wao wa kusikiza mitazamo tofauti, kukubali wanapokosolewa, na kupatiana fursa ili kila mmoja aweze kuchangia.

Kuna nadharia nyingi kuhusu tathmini, na zitaendelea kujadiliwa katika karne zijazo. Lazima wakufunzi na watungaji wa sera wakumbuke kuwa kila tathmini inaathiri ufundishaji. Shinikizo la kutumia tathmini za viwango vya juu, hasa kwa wanafunzi wachanga, linastahili kupingwa vikali kwa sababu linapunguza chaguo za ufundishaji, linachangia mashindano baina ya wanafunzi, na kupunguza nafasi za kushirikiana baina ya wanafunzi. Ni kweli kuwa ushindani huwapatia wanafunzi motisha ya kufanya vizuri. Lakini lazima walimu wabaini njia za kutumia ushindani katika kufanikisha malengo fulani ya ufundishaji badala kushinikizwa kutumia tathmini ambazo hazistahili kutumiwa.

Tathmini ni muhimu katika kuelewa matokeo ya elimu; hata hivyo, miongozo ya tathmini lazima ifae, iwe ya maana, na ifikiriwe kwa kina. Ongezeko la masomo ya kibinafsi ambayo yanaitwa 'elimu ya ziada,'ni mfano wa mtazamo wa mafanikio ya elimu usio timilifu kwa sababu unazingatia uwezo wa mwanafunzi kukumbuka alichofunzwa baada ya muda mfupi. Elimu hii ya ziada haisaidii katika kuwatayarisha wanafunzi ili wapate kufikia malengo yao na yale ya jamii. Tukiangalia mustakabali, inaonekana kuwa ni lazima tubadilishe ongezeko la mashindo katika elimu na tuangazie mifumo inayotumia tathmini za viwango vya juu.

## Safari za ufundishaji katika kila umri na hatua

Ufundishaji shirikishi ni jambo la maana katika viwango vyote vya elimu na mazingira yote ya elimu, yaliyo rasmi na yasiyo rasmi. Ufundishaji huo hutokea katika kila hatua maishani ingawa fursa za kushirikiana zinaweza kuwa tofauti katika hatua hizo. Ulimwenguni, viwango vya elimu ni vinne: chekechea, shule za msingi, sekondari, na elimu ya juu. Ingawa kuna aina mbalimbali za weledi wa binadamu, utofauti wa matilaba ya binadamu, mbinu nyingi za ujifunzaji, na ukuaji tofauti baina

ya binadamu, kuna mbinu zinazofaa kutumiwa katika mafunzo, kuheshimu tofauti za wanafunzi, na kubinafsisha masomo. Dhana ya kawaida kuhusu elimu kuwa kama safari iliyo na hatua tofauti inadhihirisha safari iliyo na madhumuni ya kuwaongoza watu wote. Sehemu iliyosalia katika sura hii inafafanua mitanziko na nafasi katika kila hatua ya maisha na njia ambazo ufundishaji shirikishi unaweza kutumiwa.

## Kuboresha misingi ya chekechea

Watoto wachanga wanaweza kuwa na uwezo wa kuangalia ulimwengu kwa njia tofauti. Ni watu wachache wanaweza kuona vitu kama watoto. Watu wazima wanaweza kujifunza kutoka kwa udadisi na uangalifu wa watoto wachanga. Azingira yote ya elimu yanastahili kukitilia maanani kipindi cha chekechea.

Kila jamii inahitaji elimu ya chekechea iliyo bora. Ukuaji mkubwa wa kimwili, kiakili, kijamii, na kihisia hutokea katika miaka ya mwanzo ya maisha ya binadamu. Utafiti mwingi umethibitisha kuwa elimu ya chekechea ni msingi wa masomo yote na ustawi.

Ufundishaji unaolenga ushirikiano na utegemeano una uhusiano mkubwa na elimu ya chekechea. Katika kipindi hiki, uwiano wa kibinadamu, uvumbuzi, na michezo ni maswala yanayostahili kusisitizwa. Ni muhimu kukumbuka kuwa viashirio vya ukuaji si lazima vifanane na uwezo na tabia zinazoweza kuibuka baadaye. Mojawapo ya utafiti bora wa kisayansi unaangazia jinsi watato wanavutiwa na wadudu. Michezo ya kuigiza inaweza kuwa msingi imara wa masomo ya watoto yaliyo ya hali ya juu. Tunavyofahamishwa na walimu wa chekechea, kile kinachoonekana kama mchezo wa kipumbavu kinaweza kuwa mwanzo wa watoto kujielewa na kuelewa ulimwengu wao.

Changamoto za tabianchi na mazingira zimeathiri elimu ya chekechea. Mbinu ya ufundishaji inayotumika katika mazingira mengi ya chekechea ni ile inayopatia kipaumbele mahitaji ya kibinafsi ya mtoto. Mbinu hizi zinahitaji mabadiliko yatakayoonyesha kuwa watoto wanaishi katika ulimwengu ulio na viumbe na vitu vingine zaidi ya binadamu. Elimu ya chekechea huchangia pakubwa katika uhusiano baina ya watoto na mahali na uhusiano wao na viumbe wengine. Ili tuweze kuwasaidia watoto waishi vizuri katika siku za mbeleni, lazima tuhamasishe ufundishaji unaolenga kuhakiki, kuuliza maswali, na kutafuta nafasi mpya.

Uhusiano baina ya nyumbani na shule huwa na nguvu katika awamu ya chekechea. Familia zina jukumu la kuchangia ukuaji wa watoto wa kimwili, kijamii, kihisia, na kiakili. Tunajua kuwa mafunzo hutokea tunapoingiliana na mazingira. Mazingira bora ya masomo hupatia watoto fursa ya kuiga lugha wanazotumia nyumbani. Kushiriki katika usomaji wa vitabu na kutumia misamiati katika maingiliano ya kila siku ni muhimu katika kukuza uwezo wa kusoma na kuandika. Vifaa vya kielektroniki kama runinga na kompyuta haviwezi kutosheleza uzoefu wa kijamii unaotokana na kuingiliana na watu. Sera bora za likizo za wazazi zinastahili kuanzishwa na serikali na makampuni. Huduma za umma kama vile vituo vya utunzaji wa watoto, maktaba, majumba ya ukumbusho, maeneo ya umma, na bustani huchangia katika ubora wa elimu ya chekechea. Methali ya 'ulezi wa mtoto unahitaji kijiji kizima' imetumika sana lakini inaeleza kwa ufasaha umuhimu wa kushirikiana katika elimu ya chekechea.

Kwa bahati mbaya, elimu ya chekechea imepuuzwa katika jamii nyingi na haitambuliwi jinsi ambavyo elimu ya msingi inatambuliwa. Shule za chekechea ni chache. Walimu wa chekechea hulipwa mshahara mdogo kana kwamba kitu cha muhimu wanachofanya ni kuwalinda watoto. Kwa sababu hiyo, kuna ukosefu wa usawa katika elimu ya chekechea kwa sababu familia tajiri zina uwezo wa kupatia watoto wao elimu bora ilhali zile maskini zinalazimika kutegemea vituo vya umma ambavyo havina rasilimali ya kutosha na ambavyo vina walimu ambao hawalipwi vizuri na ambao hawajatarishwa vya kutosha kwa ajili ya kazi zao. Lazima serikali zihakikishe kuwa kuna ufadhili wa kutosha ili watoto wote waweze kupata elimu bora ya chekechea ambayo ni nguzo ya kukua kwao.

Ni wazi kuwa kuna ukosefu wa usawa na ubaguzi unaogawanya jamii zetu. Kwa mfano, walimu wa kiume katika shule za chekechea ni chini ya 2%, kumaanisha kuwa wavulana wanaamini kuwa hawastahili kujihusisha na kazi za kulinda watoto wachanga na watu walegevu. Kama lugha zinazotumika katika miaka ya kwanza si za kina, kuna uwezekano wa watoto kupoteza uhusiano wao na familia zao na kukosa kuelewa njia za kitamaduni za kujua na kuwasiliana kwa njia zinazowaunganisha na historia zao. Katika jamii nyingi, shule zimetumiwa kama chombo cha kuwakandamiza na kuwalazimisha watoto wafanane na wengine. Kumekuwa na wito wa kukabiliana na taasisi zinazokandamiza wanafunzi. Lazima hatua zichukuliwe ili elimu ya chekechea isitumiwe kuwabagua na kuwatenga watoto. Ufundishaji wa elimu ya chekechea lazima uzingatie na uimarishe utambulisho wa wanafunzi na kuhamasisha mazungumzo kuhusu tamaduni zingine kama njia ya kuthamini utofauti.

## Elimu shirikishi kwa watoto wote

Licha ya upanuzi mkubwa wa elimu ya msingi uliotokea ulimwenguni kati ya miaka ya 1990 hadi 2020, kuna mengi yanoyostahili kufanywa ili kuongeza ubora wa masomo katika kila kiwango na kuhakikisha utumiaji wa ufundishaji ulio shirikishi.

Kwa bahati mbaya, katika shule na jamii nyingi, watoto wa gredi za juu hukatishwa tamaa wanapojaribu kuwa wadadisi; matokeo yake ni nafasi chache za kusoma, kudadisi, kushirikiana, na kuingiliana na wengine. Kuweza kutumia maarifa na ujuzi mpya ni jambo la maana. Lakini, wakati mwingi ujuzi unatumiwa katika shughuli za kibinafsi ambazo hupunguza nafasi za ushirikiano na kutafuta suluhu.

Hata hivyo, kuna mifano mingi ya ufundishaji shirikishi inayotumika katika shule na taasisi zingine za elimu. Maeneo mengine yana shule za jamii ambazo zinazoshughulikia mambo ya dharura kwa kutumia mabwawa ya tamaduni zao. Kwingineko, kuna programu ambazo si rasmi zinazotumika kufanikisha ushirikishi na kuelewa kwa tamaduni kwa kuwahusisha wazee, viongozi, na wakuzaji wa elimu ya jamii.

## Kukuza uwezo wa vijana na vijana

Vijana ulimwenguni kote wanapambana na changamoto tofauti. Changamoto hizi ni kama shida za kupata elimu, ukosefu wa usalama, ukeketaji, ndoa za mapema, na jukumu la kuchangia katika riziki za familia zao. Wengine wanakabiliwa na kutengwa na jamii, matatizo ya kiakili, na matatizo ya utambulisho na motisha ya maisha. Elimu imechangia katika kusuluhisha baadhi ya matatizo haya kwa kuwasaidia vijana kuwa na mahusiano mema na wengine na kuwapatia motisha ya kuishi na kufanikiwa. Katika maeneo mengine, elimu imezidisha changamoto hizo hasa kupitia kwa shinikizo la kufaulu kimasomo na ongezeko la viwango vya kutengwa na jamii.

Ujana unaweza kufananishwa na kipindi cha chekechea ambapo kuna mabadiliko mengi ya kinyurolojia na kimwili hutokea. Vijana hukua kiakili, lakini matarajio ya kitamaduni na kifilosofia hutofautiana kuhusu matayarisho waliyonayo hao vijana kwa ajili ya majukumu ya utu uzima na ya siku za usoni. Elimu inaweza kutoa fursa hizo mbili kwa pamoja - inaweza kuwahimiza vijana na kuwapatia nafasi za kutangamana na ulimwengu kwa njia mwafaka.

Ni katika kipindi hiki ambapo vijana huelewa mambo yanayowavutia, huanza kutafuta talanta zao, na hujua zile taaluma ambazo zinaweza kuwa ndio wito wao. Ili kuziba mapengo yaliyo kati ya maandishi na kazi kamili, lazima ufundishaji uwahimize wanafunzi na kuwapatia uzoefu unaostahili. Mara nyingi, vijana wengi wanaposukumwa na hamu ya haki, wao hubaini unafiki wa watu wazima. Kwa hivyo, watu wazima wanaweza kusema kuwa vijana ni watu wasumbufu, wakaidi, au hatari; hii hupunguza uwezekano wa kuwa na ushirikiano kati ya marika. Kuna mifumo ya sekondari ambayo inahamasisha vijana na kuongeza uwezo wao.

Sasa hivi, kuna mikakati inayotupatia matumaini kuhusu uwezekano wa kubadilisha mustakabali. Kwa nyongeza kubwa, makundi na mashirika yanayoongozwa na vijana yanakabiliana na matatizo haya kwa njia tofauti. Harakati kama Fridays for The Future na The Sunrise Movement ni baadhi ya matayarisho ya siku za kesho. Katika nchi zingine huko Amerika ya Kusini na Asia ya Kusini, mifumo ya elimu na ufundishaji inayotumia vijana wa vijijini waliotengwa kama msingi - badala ya mifumo inayopendelea miji - inawahimiza vijana wajivunie tamaduni zao. Hii, na mifano mingine, inaeleza uwezo wa elimu kusaidia vijana katika kujenga mustakabali wa ustawi na usawa.

Kwa nyongeza kubwa, makundi na mashirika yanayoongozwa na vijana yanakabiliana na matatizo haya kwa njia tofauti.

# Kuimarisha dhamira ya elimu ya juu

Ingawa elimu ni lengo kuu la vyuo vikuu, imepuuzwa katika maeneo mengine kwa sababu ya jinsi inavyopangwa, kupatiwa vibali, na kufadhiliwa. Katika mazingira mengine maprofesa ambao wana jukumu la kustawisha jamii kupitia kwa mafunzo yao, hutathminiwa kulingana na juhudi za kibinafsi; hii ni ishara kuwa ubora, umuhimu, na matokeo ya hao maprofesa hayapatiwi kipaumbele kama juhudi zao.

Ufundishaji umepuuzwa katika vyuo vikuu vingi. Kuna uwezekano kuwa katika miaka ijayo, kazi ya kufunza katika vyuo vikuu itafanywa na taasisi zingine au na teknolojia zinazotumia Akili ya Mnemba. Vile vile, vyuo vinaweza kubadilisha mafunzo kwa kuangazia elimu ya vizazi vyote ambayo itajikita katika utafiti. Taasisi za kufunza ufundi huzingatia kufunza ujuzi na hupuuza maudhui ya maadili, jamii, na dhana. Mustakabali wetu unahitaji uwezo mkubwa wa uzalishaji. Uwezo huo unastahili kuangaliwa kama uwanja mpana wa ufundishaji unaoweza kukuza ufahamu wa kina, ujuzi wa hali ya juu, na mitazamo inayotokana na kutafakari kwa kina..

Ili tuweze kuimarisha dhamira ya elimu ya juu lazima daraja kati ya elimu ya msingi na ya upili liwe imara, na lazima tujishughulishe na mbinu za ufundishaji kwa njia ambazo ni zaidi ya mbinu za kawaida. Aina za ufundishaji zinazohitajika katika elimu ya juu ni kama ushirikiano baina ya wanafunzi, utafiti, usuluhishaji wa shida, masomo ya kibinafsi, mazungumzo katika warsha, kuandika, utafiti wa utendaji, na miradi ya jamii. Ili ufundishaji uwe mbele, lazima kazi ya maprofesa ya kufunza ithaminiwe na lazima wafadhiliwe katika maendeleo yao ya kitaaluma. Lazima maadili kama heshima, kuelewa hisia za wengine, na mshikamano yajumuishwe katika dhamira za vyuo vikuu.

Lazima elimu ya juu iimarishe maadili na iwahimize wanafunzi ili wawe raia wenye ufahamu mkubwa kuhusu majukumu yao ya kiraia na kimazingira. Malengo ya elimu kuu ni kuhimiza kukubali kwa utofauti, kuimarisha haki za binadamu, na kupigana na aina zote za ubaguzi: ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa jinsia, ubaguzi wa masikini, na ubaguzi wa kikabila na kitamaduni. Elimu ya juu inayoendeleza maadili hayo ni zaidi ya yale yanayotokea katika kumbi za masomo na mazingira ya kidijitali. Maudhui ya elimu hubadilika na yanachangia katika wanafunzi kubadilika, kufuata maadili, na kubadilisha mazingira yao.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii imependekeza kuwa katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, ufundishaji unastahili kuongozwa na kanuni za ushirikiano na mshikamano ndiposa wanafunzi wapate uwezo wa kushirikiana katika kubadilisha ulimwengu. Tunapoelekea 2050, kuna kanuni nne za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu zinazohitajika ili kufanikisha mapendekezo hayo:

- **Nguzo kuu za ufundishaji ziwe uunganisho na utegemeano.** Uhusiano baina ya walimu, wanafunzi, na maarifa unastahili kujumuisha mazingira yao. Wanafunzi wote wana uhusiano na mazingira yao, na ujifunzaji wao unatokea ndani ya mazingira hayo. Wanafunzi wanapaswa kuelewa jinsi matendo ya wengine yanawaathiri na jinsi matendo yao yanaathiri wengine, na kwa sababu hiyo, madarasa na shule ni maeneo ya kuwaleta pamoja wanafunzi walio tofauti.
- **Ushirikiano ufunzwe na uendelezwe katika viwango vyote.** Elimu ndiyo hukuza uwezo wa kushirikiana katika kujibadilisha kama mtu binafsi na uwezo wa kubadilisha ulimwengu. Ushirikiano unaweza kufunzwa katika elimu ya chekechea na katika elimu ya juu.
- **Mbinu za ujifunzaji ziangazie mshikamano, huruma, maadili, na uwezo wa kuelewa hisia za wengine.** Ni sharti tujumuishe rasilimali za kitamaduni katika elimu na tufanye zaidi ya kukubali utofauti kwa kuufadhili na kuukuza. Masomo yanastahili kusaidia katika kutupilia mbali mambo kama ubaguzi na kugawanywa kwa watu. Ufundishaji wa mshikamano unaweza kujengwa kwa kutumia uwezo wa watu wa kuelewa hisia za wengine.
- **Tathmini ziendeleze ukuaji wa wanafunzi.** Mitihani na tathmini zingine ziwe sambamba na dhamira ya elimu. Sehemu kubwa ya ujifunzaji haiwezi kukadiriwa au kupimwa kwa urahisi. Tathmini zinazofaa kupatiwa kipaumbele ni zile zinazoimarisha maarifa ya wanafunzi. Tathmini za viwango vya juu na zinazoleta mashindano lazima zitupiliwe mbali.

Tunapojitayarisha kwa ajili ya 2050, tuna jukumu la kushirikiana katika viwango vya mitaa, nchi, maeneo, na kimataifa ndiposa tuweze kufanikisha ufundishaji wa ushirikiano ulimwenguni.

# Sura ya 4

## Mitaala na mbadilikoumbo wa maarifa ya jamii

Tatizo kubwa walilonalo watu wengi ni kutojua maana ya elimu. Tunatathmini elimu kwa njia sawa na ile inayotumiwa kutathmini bei ya shamba au thamani ya hisa katika masoko ya hisa. Tunataka kupatia watoto elimu itakayo wasaidia kupata mshahara zaidi. Ni vigumu tufikirie juu ya kuimarisha tabia za waliosoma. Tunasema kuwa wasichana hawastahili kupata mshahara; sasa mbona wapate elimu? Mradi hizo dhana zinadumu, hakuna matumaini ya sisi kujua thamani halisi ya elimu.'

**Mahatma Gandhi,** "True National Education," 1907.

**Katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, mizizi ya mitaala inastahili kuwa utajiri wa maarifa ya jamii unaojumuisha maswala ya kiikolojia, kitamaduni, na taaluma nyingi kwa njia zinazowawezesha wanafunzi kupata maarifa; kuchangia katika ujenzi wa maarif; na kuimarisha uwezo wao wa kuchambua na kutumia maarifa hayo.**

Daraja mpya linalounganisha elimu, maarifa, uwezo, na maadili linastahili kujengwa. Daraja hilo litaanza na uchanganuzi wa ujuzi na maarifa yanayowezesha ujenzi wa ulimwengu ulio na amani, haki, na uendelevu; uchanganuzi huo utalenga njia zote za mitaala. Ili tujenge mkataba mpya wa kijamii wa elimu, lazima tuangalie mitaala kama vitu vilivyo zaidi ya jumla ya masomo yanayofunzwa shuleni. Maswala ya mitaala yanastahili kuangazia ukuzaji wa uwezo kupitia kwa njia mbili: kupatikana kwa maarifa ambayo ni sehemu ya historia ya binadamu na kushirikiana katika ujenzi wa maarifa na mazingira mapya.

## Ni nini kinastahili kusomwa ni nini kinastahili kutupiliwa mbali?

Kuna nadharia nyingi zinazojibu maswali kuhusu ni nini na ni vipi ujifunzaji na ufundishaji unastahili kutekelezwa. Mitindo ya ufundishaji inaweza kulenga watoto, maudhui, mwanafunzi, au mwalimu. Maarifa yanaweza kuwa ni ya aina ya kitaaluma au utendaji, kisayansi au kibinadamu, na jumla au maalumu. Ingawa kila aina ya mtindo una mchango, namna mpya zinahitajika ili ziangazie ongezeko la utata kuhusu uhusiano kati ya maarifa na ulimwengu.  Waelimishaji wanastahili kuangalia swala la upatikanaji wa maarifa kwa kuuliza haya maswali kwa pamoja: ni nini kinastahili kusomwa ni nini kinastahili kutupiliwa mbali? Haya ni maswali muhimu katika wakati huu ambapo mambo ya kiikolojia yanastahili kujumuishwa katika ustawi na ukuaji wa kiuchumi.

Sura hii inachunguza maswali haya kwa kuanza na maelezo mafupi kuhusu maarifa ya jamii ambayo lazima yabadilishwe ili yawe urithi wa binadamu wote na yapanue njia za kujua na kuelewa. Hii haimaanishi kuwa maarifa lazima yatawale. Mabadiliko katika utengenezaji, utumiaji, na uchunguzi yanatokea kila mara. Sura hii inatoa wito wa kuongeza ushirikiano wetu ili tuweze kujenga maarifa na kuyatumia katika kusuluhisha maswali magumu na changamoto zinazowakumba binadamu.

Elimu inaweza kujumuisha maarifa ya *ni nini* na *ni vipi*. Si lazima kuwe na mashindano baina ya ustadi katika masomo, utumiaji wa ujuzi, na ukuzaji wa uwezo. Badala yake, maarifa yanaweza kutumiwa katika kukamilisha ujuzi. Kwa karne kadhaa, kumekuwa na mijadala kuhusu maarifa na ujuzi. Tuna fursa nzuri ya kujenga miundo tofauti ya kujumuisha maarifa, miradi, na usuluhishaji wa shida. Kama mfano, miundo hiyo inaweza kutumia changamoto za sasa katika kuandika mitaala itakayokuwa ya maana kwa wanafunzi.

Sura hii inaangalia uhusiano baina ya maarifa ya jamii na mitaala, na inaelezea umuhimu wa kuelewa miunganisho ya maarifa hasa katika uwezo wa kusoma na kuandika, kufanya hesabu, utafiti wa kisayansi, masomo ya kibinadamu, na uraia. Inahitimisha na kanuni za mazungumzo na hatua maalumu za kuongoza walimu na waandishi wa mitaala. Kanuni hizo ni: kuboresha upatikanaji wa maarifa ya jamii, kupatia kipaumbele maswala kama mabadiliko ya tabianchi, utafiti wa kisayansi, na haki za binadamu.

# Kushiriki katika maarifa ya jamii

Mitaala inastahili kufafanua kuwa maarifa ni fanikio kubwa la binadamu linalomilikiwa na kila mtu. Kwa wakati huo huo, mitaala lazima ieleze jinsi ambavyo maarifa ya jamii yanachangia katika ubaguzi na wizi unaostahili kurekebishwa ndiposa kuwe na haki. Maarifa hayawezi kukamilika, na walimu wanapaswa kuwashirikisha wanafunzi katika uumbaji wa maarifa. Badala ya kuwastawisha wanadamu, uenezaji wa maarifa kupitia kwa elimu umetumika kuleta vizuizi na kuzalisha ukosefu wa usawa. Elimu yenye kusisitiza uhusiano, uangalifu, na maarifa husaidia katika kuleta haki.

Lazima tupigane dhidi ya maarifa yanayoleta ubaguzi na dhuluma. Elimu ina uwezo wa kuwasaidia wanadamu wa vizazi tofauti ili waweze kuchangia katika ubadilishaji wa ulimwengu kupitia kwa maarifa ya jamii. Ni sharti mitaala iongeze uwezo wetu wa kuchanganua maarifa. Mambo yanayostahili kupanuliwa kila mahali ni uwezo wa kusoma na kuandika, kufanya hesabu, na kufanya utafiti wa kisayansi kwa vile yanachangia katika binadamu kuelewa na kuchangia katika ulimwengu wao.

Lazima tupinge shinikizo la kuandika mitaala inayoweka mipaka kwa taaluma na ujifunzaji. Badala yake, tunaweza kutumia nguvu zetu katika kufafanua utata ulio ulimwenguni na ubora wa mifumo ya maarifa ambayo imetumika katika historia. Kuangazia wingi na upana wa maarifa katika mitaala kunaweza kuwa msingi imara wa kupata mbinu mpya za kuleta mafanikio.

Katika kazi hii, lazima ikumbukwe kuwa mitaala haina 'maarifa yaliyo kamilika' bali ina maarifa kuhusu vizazi tofauti na maarifa hayo yanaweza kubadilishwa au kuongezwa. Ufahamu huu unamaanisha kuwa ufundishaji wa masomo yote unastahili kuangazia historia kama njia ya kuleta midahalo baina ya vizazi kwa njia ambayo itawezesha wanafunzi kupata maana mpya kutoka kwa masomo yao.

## Vipaumbele katika mitaala ya elimu ya kesho

Lazima tutupilie mbali maoni finyu kuhusu elimu na tuanze kujishughulisha na malengo yanayoweza kuleta ufanisi mkubwa. Kando na kulenga ukuaji wa kijamii na kihisia, mitaala lazima iunganishe utambuzi na uwezo wa kutatua matatizo, ubunifu, na uvumbuzi. Aina za uhusiano baina yetu na mitaala ya elimu zinazoelezwa humu zinalenga kuunganisha na kuleta uhuru. Vipaumbele vinavyofuata vina malengo ya kuchochea ujumuishaji, kuleta usawa wa kijinsia, na kubomoa misingi ya dhuluma.

## Mitaala ya sayari iliyoharibika

Tunawezaje kuishi kwenye sayari ambayo inafadhaika? Ndiposa wanafunzi wawe tayari kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, lazima elimu iangazie mambo hayo. Mitaala inastahili kubadilishwa ili isisitize jukumu la binadamu katika sayari. Katika masomo yote, lazima wanafunzi wapatane na maudhui ya mazingira endelevu - kuishi kulingana na mipaka ya sayari

pasi na kuharibu mifumo ya ikolojia wala kuharibu mustakabali wa vizazi vya kesho. Kila somo linaweza kuelezea jinsi ya kuwajibika tunapoishi katika sayari ambayo imeharibiwa na matendo ya binadamu. Hatuwezi kuendelea kufikiria kuwa wanadamu wana thamana kubwa kuliko Dunia.Hii inamaanisha lazima tukubali kuwa tunaishi na kujifunza kupitia kwa ulimwengu wa asili.

Kubadilisha jinsi ambavyo tunazungumzia Dunia katika mitaala ni mkakati wa kubadilisha uhusiano wetu nayo. Lakini, mitaala yenye kufunza wanafunzi jinsi ya kuwa watunzaji wa ulimwengu asili haitoshi. Mbinu hizo zinaweza kuleta mgawanyiko kati ya binadamu na mazingira yao.

Maudhui ya mabadiliko ya tabianchi lazima yasisitizwe. Masomo kuhusu mabadiliko ya tabianchi yatakuwa ya muhimu na bora ikiwa yatajumuisha maudhui ya jinsia, kiuchumi, na kijamii. Pia, masomo hayo lazima yachangie ubunifu na motisha ya kujihusisha na shughuli za kiraia. Elimu hiyo inatambua kuwa uzalishaji na utumiaji wa bidhaa katika enzi hizi sio endelevu, na nchi tajiri ndizo zimechangia pakubwa katika mabadiliko ya tabianchi, ilhali nchi masikini ndizo huathirika zaidi kwa sababu ya mabadiliko hayo.

Maudhui mengine katika elimu hiyo ni kuwa historia za ukoloni na viwanda zimeharibu uhusiano uliopo kati ya binadamu na Dunia ambayo ina jamii nyingi za asili. Kupitia kwa elimu ya mabadiliko ya tabianchi, wanafunzi wanaweza kuhamasishwa na kupata maarifa kuhusu mbinu endelevu za kubadilisha jamii zao. Ni sharti mitaala ituelimishe upya kuhusu uhusiano wetu na sayari hai ambayo imeharibiwa na itusaidie kutupilia mbali ufidhuli wa kibinadamu ambao ni chanzo cha kupotea kwa bioanuai, uharibifu wa mifumo ikolojia, na mabadiliko ya tabianchi yasiyoweza kurekebishwa. Tunaweza kuamua kutumia sehemu ya Dunia ambapo viumbe hai huishi kama jukwaa la elimu.

> Ni sharti mitaala ituelimishe upya kuhusu uhusiano wetu na sayari hai ambayo imeharibiwa.

Tunaweza kutengeneza mitaala inayolenga kuleta mazungumzo kati ya watu wa vizazi tofauti kuhusu mbinu za kuishi kwenye Dunia; mazungumzo hayo yanaweza kuongozwa na vijana au na jamii. Mitazamo ya watetezi wa haki za wanawake na jamii za asili inaweza kutoa mchango mkubwa tunapotafuta mwelekeo. Mifumo ya elimu ya asili ina uwezo wa kuamsha ufahamu wa wanafunzi hadi wakaanza kujishughulisha na mazingira na kupata ufahamu wa kiroho ambao umekuwa nguzo ya maelewano baina ya Dunia na binadamu kwa muda wa milenia. Kila kiumbe aliye hai ana wajibu wa kutoa mchango katika ujenzi wa mifumoikolojia endelevu. Elimu inaweza kufunza jinsi ya kuishi kwa njia endelevu ambazo hazihatarishi maisha ya viumbe wengine. Kwa mujibu wa watetezi wa haki za wanawake, mitazamo inayochochea uadui ndiyo msingi wa binadamu kudhulumu na kuwa na uhusiano mbaya na mazingira. Mifumo ya kiuchumi inayotetea kuongezeka kwa matumizi na kutawala Dunia ni potovu. Lazima tuwe na viwango vya uchumi vinavyohakikisha kuwa maisha yetu ni endelevu.

Haki ya kijamii haiwezi kutenganishwa na haki ya kiikolojia. Hatuwezi kujifunza kulinda Dunia kabla hatujajifunza kutunzana sisi wenyewe. Utunzaji ni zaidi ya mapenzi na hisia - unahusiana na akili pia. Lazima mitaala ieleze jinsi maarifa yanahusiana na vitendo vinavyoambatana na maisha yetu katika Dunia. Maongezi kuhusu uwezo na upungufu wa vifaa vya mazungumzo na kuhusu miradi

ya kijamii na ya kibinafsi ni nguzo za mitaala ya kuongeza ufahamu wa kijamii na kutoa motisha kwa kutetea viumbe wote katika Dunia.

Maadili ya utunzaji hutuwezesha kujielewa zaidi hasa jinsi ambavyo tumeunganishwa kama jamii ya binadamu yenye uwezo mkubwa na inayoweza kuwa dhaifu. Inatubidi tufikirie jinsi ambavyo tunaathiri wengine na Dunia na jinsi tunavyoathiriwa na binadamu wengine na Dunia. Ni muhimu mitaala ikuze maadili ya utunzaji wa kila jinsia kama njia ya kurekebisha ukosefu wa usawa ulioko katika maisha ya nyumbani na ya umma. Maarifa kuhusu kulea watoto, kulinda wagonjwa na wakogwe, kupanga mambo ya nyumbani, na kushughulikia mahitaji ya kisaikolojia ni muhimu kwa jamii na ni sehemu ya maarifa ya jamii yanayoweza kuchangia katika mikakati na kurekebisha Dunia iliyoharibika na iliyodhaifu. Kwa hivyo, lazima maudhui ya utunzaji yajumuishwe katika mitaala inayokusudia kubadilisha uhusiano wetu katika siku za mbeleni.

## Kuunganisha kujua na kuhisi

Mitaala inastahili kuwachukulia wanafunzi kama binadamu wanaoleta ubunifu na kiu cha elimu katika mazingira ya kielimu. Wanaweza kuleta hisia, shauku, Imani na ari. Mitaala inayotambua kuwa wanafunzi ni binadamu huimarisha uwezo wao wa kuwa na mahusiano ya kihisia na Dunia na uwezekano wa kushirikiana katika kuiimarisha.

Nyurosayansi imebaini kuwa kujua na kuhisi ni baadhi ya shughuli za kiakili zinazoelekeza uhusiano wetu na watu wengine. Kwa karne moja iliyopita, kazi nyingi imefanywa katika kuimarisha masomo ya kijamii na kihisia. Mbinu bora za masomo ya kijamii na kihisia katika mitaala hujumuisha aina zote za utambulisho wa wanafunzi: kijamii, kihisia, kiakili, na kimaadili. Mbinu hizo huwezesha ukuaji ulio na maana kubwa katika maisha yao ya kijamii.Katika jamii zote, hasa zile zinazokabiliwa na ugawanywaji, elimu kuhusu kuelewa kwa hisia za wengine, kushirikiana, kupambana na ubaguzi, na kusuluhisha migogoro ina manufaa.

> Katika jamii zote, hasa zile zinazokabiliwa na ugawanywaji, elimu kuhusu kuelewa kwa hisia za wengine, kushirikiana, kupambana na ubaguzi, na kusuluhisha migogoro ina manufaa.

Mbinu za kufunza mambo ya kijamii na kihisia ni nyingi na ni muhimu zilingane na miktadha yao. Mbinu hizo zinahitaji maudhui yaliyopangwa kwa ufasaha, kushikamana na walimu, uhusiano mzuri baina ya marika, kuelewana baina ya vizazi tofauti, na ushirikishi wa jamii. Uangalifu, huruma, na uchunguzi huboresha elimu ya kijamii na kihisia. Kusoma huko ni kazi nyingi inayohitaji walimu wasaidiwe ili watimize wajibu wao. Tunapokaribia 2050, hatuwezi kupuuza masomo ya kijamii na kihisia - ni nguzo ya ubunifu, maadili, uwezo wa kufanya maamuzi, na hatua za kukabiliana na changamoto za kesho.

Kuwachukulia wanafunzi kama binadamu ni kuzingatia mahitaji na uwezo wa miili yao katika kila hatua ya maisha yao. Mustakabali wenye afya unahitaji elimu ya mazoezi ya mwili inayokuza ujuzi wa mazoezi ya aina yote ya miili, jinsia, na watu kutoka sehemu tofauti. Baadhi ya matokeo ya elimu hiyo ni ongezeko la viwango vya kujiamini, uwezo wa kujidhibiti, ujuzi wa kushirikiana na wengine,

kuelewa mazingira, na ujuzi wa kuwasiliana. Elimu ya mazoezi ya mwili isiangaliwe kama shughuli ya wale walio na milli aina fulani; kupatia mashindano kipaumbele kunaweza kuwafungia wengi nje. Ni sharti ielezwe kuwa kila mwanafunzi anaweza kuishi maisha ya afya na kujenga uhusiano wa heshima kupitia kwa shughuli za michezo.

Vile vile, mbinu ya kufunza kuhusu ujinsia ambayo inazingatia umri, utamaduni, weledi wa kijamii na kihisia, na heshima, husaidia katika kuelewa hatua za ukuaji wa mwili wa binadamu na kukuza uhusiano wa heshima. Hatuwezi kukubali ulimwengu ambao wasichana wako katika hatari ya kudhulimiwa kimwili au kimapenzi kiasi kwamba wanakosa kuendelea na masomo yao. Afya ya mama na mtoto, kifo, na ustawi ni mambo yaliyo na uhusiano wa karibu na elimu ya ujinsia. Elimu inayokuza usawa, heshima, na kujiamini ina uwezo wa kujenga jamii zinazoenzi haki na usawa.

## Kupanua uwezo wa kusoma na kuandika na kujenga mustakabali wa lugha nyingi

Uwezo wetu wa kutumia lugha na uhusiano wetu na lugha ni misingi ya utambulisho wa mwanadamu, maarifa, na kuwepo kwetu katika ulimwengu. Misingi hiyo inatusaidia katika kuwasiliana na kufikia viwango vya juu vya kuelewa. Bila ya lugha, maarifa ya jamii hayawezi kuwa. Kwa karne kadhaa zilizopita, vizazi vingi vimeweza kuongeza uwezo wao wa kusoma na kuandika. Ndiposa tupanue ushirikiano na ujumuishaji, lazima mustakabali wa elimu uangazie zaidi ya kusoma na kuandika kwa kuimarisha uwezo wa kuelewa na kujieleza kwa njia zote - kwa njia ya mdomo, maandishi, na kupitia kwa mbinu za kusambaza habari kama vile hadithi na masomo ya kibinadamu. Kwa hakika, kando na kuandika na kusoma, binadamu wametumia mbinu zingine kurekodi historia zao na kuzisambaza kwa vizazi vipya. Mitaala inastahili kuwa na picha na maarifa ya kimwili. Maarifa yaliyoandikwa na yale yaliyoenezwa kupitia kwa njia ya mdomo ni muhimu sana katika historia ya binadamu kwa vile yaliwezesha kurekodiwa kwa maisha ya binadamu katika mazingira tofauti. Maarifa haya yanastahili kufikia vizazi vya kesho.

Uwezo wa kusoma na kuandika unahusiana na elimu ya kesho na kushiriki katika mambo ya jamii. Uwezo huo sio kama swichi ya kuwasha na kuzima. Uwezo wetu wa kuwasiliana na kuelewana kupitia kwa lugha unaweza kuboreshwa tunavyoendelea kuishi. Uwezo wa kusoma na kuandika unaweza kuimarisha uwezo wa kuwasiliana, kusikizana, kuelewa hisia za wengine, na kuchanganua mambo. Kwa mfano, kuwaongoza wanafunzi ili wawe na uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vigumu katika kila somo ni kama kufungua milango ya uwezekano wao wa kujihusisha na maarifa ya jamii. Elimu ya kusoma na kuandika inaweza kutekelezwa nje ya shule na madarasa; hii inamaanisha elimu hiyo itakuwa azimio la jamii yote.

Kwa mfano, kuna taasisi za habari huko India ambazo zimeleta utumiaji wa maandiko yanayoeleza kile kinachozungumziwa; mbinu hii imeboresha uwezo wa kusoma hasa kwa wale wanaohitaji elimu ya ziada.

Mitaala imeanza kuhama kutoka kwa utumiaji wa lugha moja na kwenda katika utumiaji wa lugha nyingi: lugha za kigeni, lugha za asili, lugha za ishara, na zinginezo. Haya ni mabadiliko yanayohitaji kuhamasishwa zaidi. Ni muhimu kuwa kila mtoto, kijana, na mtu mzima apate elimu kupitia kwa lugha yake ya mama. Kufanya hivyo itakuwa ni kukuza utofauti katika elimu. Katika mazingira mengi,

utumiaji wa lugha nyingi ni muhimu katika kulinda utambulisho wa kitamaduni wa wanafunzi na kuwasaidia katika kuchangia mambo ya jamii. Ulinzi wa lugha hizo utatekelezwa kwa kupatia lugha za walio wachache kipaumbele na kuweka misingi ya kuwasaidia wanafunzi kuwa stadi wa lugha inayotumika na wengi.

Lugha hufanya kazi nyingi zaidi ya mawasiliano; lugha hubeba mitazamo yetu kuhusu ulimwengu na njia tofauti za kuelewa. Utofauti wa lugha ni kiungo muhimu katika maarifa ya jamii; elimu ina jukumu la kuimarisha kiungo hicho. Elimu ya lugha nyingi huleta nafasi za kuchangia katika mazungumzo ya kimataifa, kazi, na tamaduni. Katika ulimwengu unaozidi kuwa na kutegemeana kwingi, kuna manufaa mengi ya kujua lugha zingine, na manufaa hayo ni zaidi ya kuwasiliana. Kujua lugha nyingi kunatufanya zote tuwe wakalimani na tuwe na uhuru wa kutafuta ufahamu.

Kujua lugha nyingi kunatufanya zote tuwe wakalimani na tuwe na uhuru wa kutafuta ufahamu.

## Kuboresha uwezo wa kufanya hesabu

Uwezo wa kufanya hesabu rahisi ni muhimu katika mustakabali wa elimu kwa maana watu wanahitajika kutumia maarifa ya hesabu katika shughuli tofauti. Uwezo wa kufanya hesabu unatokana na uwezo wa binadamu wa kutambua mifumo, kuainisha mikusanyiko, kuipanga mikusanyiko, kuhesabu, kupima, kulinganisha, na kutambua uhusiano kati ya vitu au idadi. Mifumo ya hesabu kama vile desimali ya binari ni msingi katika mawasiliano, shughuli za biashara, shughuli za kompyuta, na hesabu. Kando na kuwa na ujuzi wa kuongeza, kotoa, kuzidisha na kugawa, uwezo wa kufanya hesabu za kawaida hutumika mahali pengine kama vile katika mipango ya kifedha, kiafya, mazao ya ukulima, pembejeo, viwango vya uchafuzi wa mazingira, biashara, na shughuli za benki. Uwezo wa kufanya hesabu hufungua uwezo wa kuelewa mabadiliko na kutabiri vile yatakuwa kesho kwa kutumia mitindo na uhusiano kati yao.

Uwezo wa kufanya hesabu ni kitu kinachomilikiwa na watu wote. Kujenga uwezo unaoangazia tamaduni tofauti kunaweza kuleta madaraja ya kijamii na kihisia katika elimu rasmi. Kwa mfano, mbinu za asili za kusuka zinazotumika na jamii za asili huko Norwei ya Kaskazini zimetumika na wanafunzi kuelewa jinsi ya kuzidisha na kutumia aljebra. Vile vile, huko Kanada, bodi za shule zimeajiri wakufunzi na wasanii kutoka jamii za asili wanaofunza aina za usanii kama utengenezaji wa shanga, vikapu, na mokasia kwa kutumia maarifa ya aljebra na usawa. Kuunganisha maarifa ya hesabu na yale ya kitamaduni husaidia katika kuhusisha mambo ya kijamii na kihisia katika elimu kwa njia inayofanya mazingira ya nyumbani na shuleni yafanane. Kuunganisha huko kunakabiliana na dhana kuwa elimu ya hesabu ni ya 'Magharibi' na kutukumbusha kuwepo kwa hesabu za kijamii kama zile za Wainuiti na Wamaori.

## Kugeukia masomo ya kibinadamu

Maarifa na uchunguzi wa jamii ya binadamu na utamaduni ni muhimu katika kuwasaidia wanafunzi kujua mbinu za kusuluhisha matatizo yanayowakumba. Mila ya kibinadamu imechangia pakubwa katika maarifa ya jamii yanayotumika katika ujenzi wa Dunia. Wakati huo huo, lazima tutambue kuwa yale tunayoyajua hayajakamilika na yanaweza kutupotosha. Kubadilisha maana yake inamaanisha kulainisha uhusiano kati yetu, na ule tulionao na Dunia hai na teknolojia. Masomo ya kibinadamu yanastahili kubadilishwa ili yaweze kutusaidia pia sisi tubadilike.

Historia ikifunzwa kwa ufasaha inaweza kutupatia mitazamo ya maana kuhusu mabadiliko ya jamii na mifumo ya jamii kama vile ubaguzi na upendeleo. Kuelewa historia ni msingi wa kutabiri mustakabali. Lakini, lazima historia ifanye zaidi ya kuelezea kronolojia kwa kuanza mazungumzo kuhusu ushuhuda na vile ambavyo tunaelewa maisha ya binadamu na viumbe wengine. Kupata njia mpya za kuunganisha elimu ya masomo ya kibinadamu ni muhimu kwa mustakabali na demokrasia. Filosofia, historia, fasihi na masomo ya kibinadamu yanaweza kuchangia kwa madhumuni yetu maishani, maadili na ubunifu.

Mbinu za kibinadamu ni muhimu katika kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa kuelewa mustakabali. Kuwa 'wataalamu wa mustakabali' inamaanisha kuweza kutuumia mustakabali kwa ufasaha ndiposa uweze kujitayarisha, kujirekebisha na kufanya uvumbuzi mabadiliko yanapotokea. Hili linaweza kuimarishwa kupitia kwa mifumo inayofunza masomo ya kibinadamu katika majukwaa tofauti kando na yanayotumika katika elimu rasmi. Ni muhimu tuunganishe elimu na masomo ya kibinadamu kwa kuanza na mambo ambayo yanatufananisha kama vile ubinadamu wetu, Dunia yetu, na madhumuni ya kuleta haki.

## Upekuzi wa kisanyansi na ufahamu

Hamu ya kuelewa ulimwengu halisi inaashiria uwezo wa binadamu wa kuchunguza na kufahamu. Utaratibu wa uchunguzi wa kisayansi - kuangalia, kuchanganua, kutabiri, kufanya marajibio, kubuni nadharia, kupinga, na kuimarisha ufahamu - unatokana na roho ya kibinadamu. Mizizi ya sayansi ya kisasa ipo katika historia za kwanza zilizorekodiwa katika tamaduni na jamii mbalimbali. Matunda yake yako katika kila sehemu ya maisha yetu, kwanzia utabibu hadi teknolojia. Ni lazima upekuzi wa kisayansi uwe kiungo cha mitaala mipana iliyo na maadili ya kibinadamu.

Katika historia ya binadamu, sayansi imetumika kuonyesha kuwa ukweli hutokana na taratibu na maafikiano ya pamoja. Sayansi ilikuwa kubwa hadi ikaanza kupuuza maswali ya maadili hasa kuhusu athari za uvumbuzi na majaribio ya kisayansi. Hali hii ilichangia mijadala mingi na kuibua maswali mengi ambayo yanapunguza imani ya watu kwa sayansi. Mitaala inastahili kuangalia uhusiano kati ya mbinu, matokeo, na maadili.

Ongezeko la dhana potovu na uongo ni ishara inayoonyesha kuwa tunahitaji maarifa ya kisayansi. Umuhimu wa maarifa ya kisayansi umemulikwa sana ukizingatia kuenea kwa habari za uongo kuhusu ongezeko la joto kwenye Dunia na janga la UVIKO-19. Kukataa ukweli wa kisayansi na habari za kupotosha ni vyanzo vya mashaka, kutoaminiana, uoga, na chuki. Lazima mitaala ijitolee kulinda ukweli wa kisayansi na ijenge viwango vya utambuzi na uwezo wa kupeleleza ukweli ambao ni changamani.

> Lazima mitaala ijitolee kulinda ukweli wa kisayansi na ijenge viwango vya utambuzi na uwezo wa kupeleleza ukweli ambao ni changamani.

Kila mtu ana haki ya kuchangia katika maarifa ya kijamii, ambayo ni muhimu kwa ustawi wa binadamu wote ulimwenguni. Kanuni hii ni muhimu kwa mitaala kwa sababu ina maudhui na dhana zinazoweza kushawishi akili changa. Kwa mfano, katika maeneo na nchi zenye viwanda vingi vya mafuta na viwango vya juu vya uchimbaji wa madini, serikali hufanya mikakati ya kuhakikisha kuwa athari za viwanda vya mafuta na uchimbaji wa madini hazipatiwi kipaumbele katika mitaala. Lazima tupigane na uongo huo kupitia kwa njia zote za kielimu tulizonazo. Tunahitaji juhudi mpya za kueneza maarifa ya kisayansi ulimwenguni hasa kwa jamii zilizotengwa. Kuna habari nyingi zinazoendelea kusambazwa ulimwenguni. Ujuzi wa sayansi, mbinu, ukamilifu, ujarabati, na maadili ni mambo ya mitaala yaliyo muhimu na ya dharura.

## Ujuzi wa ulimwengu wa kidijitali

Teknolojia zimeleta nafasi nyingi za kushiriki katika shughuli nyingi za maisha, kusoma, na kufanya kazi. Kando na kufanikisha upatikanaji wa teknolojia, elimu inaendelea kuwapatia wanafunzi maarifa ya kuwasaidia wanapotumia teknolojia. Ujuzi huo si wa kuzaliwa nao. Unajengwa na kuimarishwa kupitia kwa elimu rasmi na ujifunzaji wa mtu binafsi.

Ingawa elimu ya kidijitali inalenga ujuzi wa kutumia teknolojia, lazima iangalie 'ustadi wa kidijitali'- jumla ya ufahamu na mitazamo ya kisiasa kuhusu jamii ya kidijitali na uchumi wa kidijitali. Kupitia kwa elimu hii, wanafunzi wanaweza kuchanganua uhusiano kati ya mambo ya kisiasa na teknolojia za kidijitali. Lazima wanafunzi waelewe malengo ya wadau walio katika mifumoikolojia ya kidijitali. Leo hii, teknolojia inaweza kuwaathiri hata watu wasioitumia.

> Mitaala inastahili kuwasaidia walimu na wanafunzi wanaposhirikiana kwa mambo ya teknolojia na wanapotafuta ufahamu kuhusu jinsi teknolojia inaweza kutumika kwa dhamira zingine.

Elimu kuhusu teknolojia inategemea teknolojia. Kuna mabadiliko katika ujuzi na mitazamo inayosaidia katika kufahamu mambo ya teknolojia na kuitumia ipasavyo. Hii inamaanisha kuwa elimu inastahili kuongoza uvumbuzi wa kiteknolojia na kusaidia katika mabadiliko ya kidijitali ya jamii. Mitaala inastahili kuwasaidia walimu na wanafunzi wanaposhirikiana kwa mambo ya teknolojia na wanapotafuta ufahamu kuhusu jinsi teknolojia inaweza kutumika kwa dhamira zingine.

## Kuimarisha ubunifu, uamuzi, na uwezekano kupitia kwa elimu ya kibinadamu

Elimu ya kibinadamu - muziki, michezo ya kuigiza, densi, kuchora, usanifu, fasihi, ushairi - inaweza kupanua uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa mambo magumu na kuchangia katika elimu ya kijamii na kiuchumi katika mitaala. Inaweza kuimarisha uwezo wetu wa kibinadamu na wa kuelewa watu wengine.

Masomo ya kibinadamu huweka wazi ukweli ambao mara nyingine unaweza kujificha na hutupatia njia za kusherehekea mitazamo na ufahamu tofauti kuhusu ulimwengu. Aina nyingi za usanii zina maana fiche. Wanafunzi wanaweza kuelewa kuwa tofauti kidogo zinaweza kuleta matokeo makubwa. Usanii unahitaji kujitolea katika kuchunguza na kueleza yasiyojulikana; wanafunzi wanaweza kusoma kuwa kila kitu hubadilika kulingana na hali na fursa zilizopo. Elimu ya kibinadamu inatusaidia kusema, kuonyesha, na kuhisi kile kinachostahili kusemwa, kuonyeshwa, na kuhisiwa na hivyo tunaweza kupanua maarifa yetu na kuwasiliana vyema.

Mitaala inayoendeleza ubunifu ina uwezo mkubwa wa kuboresha mustakabali. Usanii huleta lugha na njia tofauti za kuelewa ulimwengu, kuchanganua tamaduni, na kuchukua hatua za kisiasa. Mitaala inaweza kukuza uwezo wa kutangamana na tamaduni zingine zinazochangia katika utambulisho wetu wa pamoja.

## Kuelimisha kwa ajili ya haki za binadamu, uraia imara na ushirikishi katika demokrasia

Wakati hali ya elimu na haki za binadamu ni bora, tunaweza kuwa na mabadiliko makubwa ambapo elimu hiyo inakuwa kama lugha ya watu wote na kiingilio cha ulimwengu wa maadili na ustawi wa wote. Kuwa na ujuzi wa kuchanganua ukosefu wa usawa na kukuza ufahamu ni njia ya kuimarisha ushirikiano katika maswala ya elimu na haki za binadamu. Umuhimu wa mifumo ya elimu unaweza kuimarishwa kupitia kwa elimu ya haki za binadamu ambazo ni msingi wa maendeleo endelevu ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Ndiposa elimu kuhusu haki za msingi, adhama ya binadamu, na uhuru iwe ya maana, lazima elimu hiyo itoe ahadi ya kuleta usawa. Elimu kuhusu haki za binadamu na uraia ina uhusiano mkubwa na elimu ya amani. Katika mazingira ambayo ukatili ndiyo lugha inayotumika, watu wote, wakiwemo wanawake na watoto, hudhulumiwa na nafasi zao za kuishi na kustawi huwa finyu. Pamoja na sheria za kulinda watu na mashirika ya ustawi, elimu kuhusu haki za binadamu inaweza kuleta amani katika jamii kwa kusisitiza utumiaji wa mazungumzo na diplomasia katika kusuluhisha migogoro.

Elimu huimarisha uwezo wa kuwa na hatua za kiraia, kijamii na kisiasa kwa kufunza watu jinsi ya kufanya kazi kwa pamoja kutumia mifumo tofauti. Uhusiano bora hutokea wakati mitaala inalenga kukuza miungano, uanaharakati na mshikamano. Wakati elimu inalenga kukuza mazungumzo na uwezo wa kufikiria kwa makini, mabadiliko makubwa yanaweza kujiri. Kando na kuangalia maudhui ya kimaadili kama vile jinsi maisha ya viumbe wengine yanaweza kutunzwa, elimu inastahili kuchochea mijadala kuhusu maana ya kuwa binadamu.

Malengo ya elimu hiyo ni kukuza uwezo na ujuzi wa kufikiria kwa kina kuhusu dhuluma, ukiukaji wa haki za binadamu, mifumo inayochangia ubaguzi kwa misingi ya jinsia, rangi ya ngozi, utambulisho wa asili, lugha, dini, umri, ulemavu, ujinsia na hali ya uraia. Kwa hivyo, mazungumzo baina ya mifumo ya elimu na vuguvugu kwenye jamii ni muhimu.

Mitaala inaweza kusaidia katika mapambano dhidi ya ukosefu wa usawa wa jinsia. Athari za mfumo dume - mfumo unaowapatia wanaume haki nyingi za kijamii na kisiasa - zinaendelea kutawala masomo wanayopatiwa watoto shuleni. Ukandamizaji na ubaguzi ni mambo yasiyomfaidi mtu yeyote katika jamii. Lazima kanuni kuhusu usawa wa jinsia zifunzwe kuanzia umri mdogo. Wavulana wanapaswa kujua umuhimu wa kupigania usawa wa jinsia ndiposa wasianze kujihusisha na matendo yanayoimarisha mifumo ya kuwakandamiza dada zao na marika wao wa kike. Matarajio kuwa wasichana ndio wanapaswa kufanya kazi nyingi za nyumbani yanaonyesha kuwa thamani yao ni ya chini kuliko ya wavulana. Kwa sababu ya kazi hizo, wasichana wanaweza kukosa kufanya vizuri katika masomo yao. Kanuni za usawa wa jinsia zinastahili kutawala mazingira yote kuanzia nyumbani, darasani, shuleni na kwenye jamii. Kila mtu ana wajibu wa kuchangia katika usawa wa jinsia.

Pia, mitaala inastahili kupambana na ubaguzi wa rangi na dhana zinazochangia katika ubaguzi dhidi ya watu wanaotoka katika jamii tofauti na wanaozungumza lugha tofauti kama vile wale wa asili ya Afrika, watu kutoka kwa jamii za asili na wale wa kutoka kwa jamii za walio wachache.

# Mchango wa elimu ya juu

Mkataba mpya wa kijamii wa elimu utaangazia namna mpya ambazo elimu itatumika katika kuendeleza na kupanua maarifa ya jamii. Elimu ya juu imethibitisha mchango wake katika kuimarisha maarifa ya jamii. Sasa hivi, elimu ya juu inakabiliana na hali ya mashaka ambayo imekuwa ikiendelea kwa muda mrefu. Vyuo vikuu vina hazina za maarifa na utafiti. Utafiti na uvumbuzi katika taasisi za elimu ya juu umepiga hatua kwa sababu ya sayansi wazi na maarifa ya dijitali yaliyo wazi.

## Utafiti katika vyuo vikuu kwa ajili ya maarifa ya jamii yaliyo wazi

Maarifa yanapaswa kutambuliwa kama mali ya kudumu yanayostahili kufaidi kila mtu. Zaidi ya kupinga usambazaji wa maarifa usio sawa, lazima tupigane dhidi ya hatua za kufanya maarifa yote yawe sawa. Badala ya kujenga maarifa yanayotawalwa na dhana za kiuchumi, kisiasa na kijamii, utafiti katika vyuo vikuu unastahili kulenga dhamira mpya. Hili litaanza na makubaliano kuwa kuna aina nyingi za maarifa na lugha. Vyuo vikuu vinaweza kutoa mchango mkubwa katika kupanua maarifa ya jamii na kuhakikisha kuwa yana ujumuishi na utofauti.

Ushirikiano baina ya vyuo vikuu na hatua za kuanzisha vyuo vya kimataifa ni mifano mizuri ya uwazi inayoonyesha uwezekano wa kuwa na ustawi wa kimataifa. Kulingana na takwimu, usajiri katika vyuo vikuu utaongeza katika miaka ijayo.

Vyuo vingi vina mila ya kuimarisha elimu ya umma kupitia kwa mikakati inayoleta nafasi za umma za kujifunza mambo ya utawala na mengine yanayohusu jamii kwa jumla. Kwa upande mwingine, visuizi vya gharama na haki za umiliki hutokea katika vyuo vikuu. Kwa hivyo, elimu ya juu ina mifumo ya ubaguzi inayostahili kushughulikiwa.

> Elimu ya juu inastahili kutetea maarifa ya jumla na kisayansi yaliyo wazi na yasiyo na gharama.

Elimu ya juu inastahili kutetea maarifa ya jumla na kisayansi yaliyo wazi na yasiyo na gharama; maarifa hayo yanaweza kupatikana kupitia kwa makala ya kitaalamu, rasilimali za ujifunzaji, programu za kompyuta, na muunganisho wa kidijitali. Uwazi unamaanisha kuwa maarifa hayo yanaweza kupatikana kwa urahisi na watu binafsi wanaweza kuyabadilisha.

## Elimu ya juu ya ufundi na maarifa ya jamii

Kando na kutumiwa kama mahali pa ufundishaji, taasisi za ufundi kama vile vyuo vya jamii na vyuo vya ufundi zinastahili kutumiwa kama kumbi za utafiti. Lazima zizingatie uwezo wetu wa kuishi katika jamii, kufanya kazi na kushirikiana katika mambo ya kijamii na kiuchumi. Vyuo hivyo vinaweza kuchangia katika ustawi wa tamaduni. Uhusiano baina ya jamii, maarifa ya jamii, na vyuo vikuu ni wa kipekee.

## Elimu ya juu : kiguzo cha aina nyingi za maarifa

Mara nyingi, uhusiano kati ya elimu ya juu na utofauti wa kitamaduni na kiepistemolojia huwa tatanishi. Kwa upande mwingine, elimu ya juu inajivunia kuwajulisha wanafunzi kuhusu dhana na mitazamo tofauti. Kwa wakati huo huo, elimu ya juu imeleta njia mpya za kupanga, kukagua na kuidhinisha mbinu za kuzalisha maarifa.

Mbinu hizo zinatumika katika sayansi ya asili pamoja na dhana zinazotumika katika utafiti wa kijamii kama vile 'ukamilifu', 'kutegemeka', na 'uhalali'. Hatua zinazofuatwa kabla ya kuchapisha matokeo ya utafiti haziimarishi utofauti wa epistemolojia. Badala ya kuchukuliwa kama aina ya utafiti, maarifa yamekuwa yakichukuliwa kama kitu tu.

Mifumoikolojia ya maarifa ya tamaduni mbalimbali imezidi kuthaminiwa kwa sababu ya ongezeko la umaarufu wa wingi wa kujua na kufanya vitu. Ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu na jamii lazima uwe wa manufaa kwa wote. Kiini cha uendelevu ni kukubali wingi wa njia za kujua na kufanya vitu; uendelevu unaweza kupunguza ukosefu wa usawa katika elimu ya juu.

Utofauti unaweza kuimarishwa kwa kuanzisha aina nyingi ya taasisi za elimu ya juu. Kama upanuzi wa elimu ya juu utaendelea, tutahitaji aina tofauti wa taasisi. Uwazi wa maarifa ya jamii unahitaji mifumo ya elimu inayoweza kurekebishwa na kuwafikia watu wengi kwa urahisi.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii imependekeza kuwa, katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, mitaala inapaswa kuzingatia masomo ya kiikolojia, kitamaduni, na kitaalumu yanayowezesha wanafunzi kupata, kujenga, kukusoa na kutumia masomo hayo. Tunapokaribia mwaka 2050, kuna kanuni nne kuu zinazoweza kuongoza mazungumzo na hatua muhimu zitakazosaidia mkataba huo:

- **Lazima mitaala iimarishe uwezo wa wanafunzi wa kupata na kuchangia katika maarifa ya jamii.** Uti wa mgongo wa mitaala unastahili kuwa maarifa ya jamii ambayo yamekuwa yakikusanywa na vizazi vilivyopita. Maarifa hayo yanastahili kupatikana na kuchangiwa kwa urahisi. Tunapaswa kufunza wanafunzi, wa umri wote, jinsi ya kutumia maarifa hayo kwa weledi. Elimu inastahili kuwahamasisha watu warekebishe yale mambo yaliyosahaulika katika maarifa ya jamii ndiposa maarifa hayo yawe rasilimali wazi itakayodumu na kusaidia katika ustawi wa njia nyingi za kujua na kuwepo katika ulimwengu.
- **Mgogoro wa kiikolojia unahitaji mitaala inayofafanua jukumu la binadamu katika Dunia.** Elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi ipatiwe kipaumbele. Mitaala isisitize umuhimu wa kuwajibika na kuishi kwa heshima katika sayari ambayo imeharibiwa na vitendo vya binadamu.
- **Maarifa ya kisayansi, kidijitali na kibinadamu yatumiwe katika kukabiliana na ongezeko la habari potofu.** Mitaala inastahili kusisitiza utafiti wa kisayansi na uwezo wa kutofautisha utafiti na uongo. Lazima tukuze ujuzi wa kidijitali unaowezesha wanafunzi kupata maana kutoka kwa teknolojia. Mitaala inastahili kuhakikisha kuwa wanafunzi wana uhuru na uwezo wa kuamua ni vipi na ni wapi watatumia teknolojia.
- **Haki za kibinadamu na kushiriki katika shughuli za kidemokrasia ni misingi muhimu ya kubadilisha watu na ulimwengu.** Lazima tupatie elimu kuhusu haki za binadamu kipaumbele kwa vile inahimiza wanafunzi na kufungua ulimwengu wa maadili ambapo kila mtu anatambuliwa na anaweza kustawi. Mitaala yote inastahili kugusia usawa, haki na zile dhana potufu za kijinsia zinazostahili kuondolewa. Wanafunzi wanastahili kuelewa jinsi ya kupambana na aina zote za ubaguzi.

Kanuni hizi nne zinaweza kuchochea kuwepo kwa mkataba mpya wa kijamii katika mifumo ya elimu.

# Sura 5

# Kazi ya kuleta mabadiliko wanayofanya walimu

Mwalimu si bingwa mwenye kujua ukweli kuhusu mambo yote kila wakati. Kama wanafunzi wake, yuko katika mchakato wa kuwa anachostahili kuwa.

**Wei-ming Tu,** *Humanity and Self-Cultivation*, 1996.

**Lazima walimu wawe kigezo cha mkataba mpya wa kijamii wa elimu; taaluma yao lazima itathminiwe na kuumbwa upya ili iwe mradi wa ushirikiano unaochochea maarifa na kuleta mabadiliko ya kielimu na kijamii.**

Ualimu ni taaluma changamani ambayo huathiri maisha ya umma na ya kibinafsi. Walimu hushirikiana katika utumiaji wa maarifa ya jamii katika mazungumzo yao na vizazi vichanga vitakavyorithi na kujenga mustakabali. Ufundishaji ni kazi ya timu inayotumiwa kusaidia wanafunzi binafsi walio na mahitaji na uwezo tofauti. Kazi ya mwalimu haiwezi kufidika kwa sababu inatawalwa na mivutano na ukweli kinzani.

Ufundishaji unahitaji huruma, ustadi, maarifa na maadili. Watu waliosoma na wenye hekima wameshangiliwa katika tamaduni tofauti ulimwenguni; kutokana na mila hii, 'mwalimu' ni mshiriki maalumu katika mazingira ya shule. Walimu ni wadau muhimu katika mabadiliko. Lazima watambue umuhimu wa wanafunzi kushirikiana na kusoma kupitia kwa ufundishaji. Ndiposa watekeleze jukumu hili changamani, walimu wanastahili kuwa na majumuiya shirikishi ya ujifunzaji yaliyo na uhuru na ufadhili wa kutosha. Kufadhili uhuru, ustawi na ushirikishi wa walimu ni kauli muhimu kuhusu mshikamano wa umma katika swala la mustakabali wa elimu.

Sura hii inaanza na taswira mpya ya ualimu ambapo wataalamu wanashirikiana katika kukuza na kubadilisha elimu ili iweze kufanikisha mahitaji ya wanafunzi walio tofauti. Walimu wanapotambuliwa kama wataalamu wanaoumba maarifa, wao huchangia katika kupanuka kwa maarifa ambayo ni mizizi ya kubadilisha mazingira ya elimu, sera, utafiti, na mazoezi ya ujifunzaji.

Sura hii inaangazia athari za mkataba mpya wa kijamii wa elimu kwa hatua zote za maisha ya mwalimu - kuanzia mwajiriwa mpya, mwalimu limbukeni, hadi mwalimu stadi - kama safari ya kibinafsi inayochukuliwa pamoja na walimu wengine katika nyakati na nafasi tofauti.

Sura hii inahimiza wadau kutoka shule, jamii, familia, wasimamizi, na wanasiasa wawe mstari wa mbele katika kuwaunga walimu mkono kwa kutambua umuhimu wa kazi wanayoifanya na kujenga mazingira yatakayochangia ufanisi wa walimu. Sura hii inahitimisha na kanuni kuu za 2050 zitakazoongoza mazungumzo na hatua muhimu hasa zile zinazolenga walimu, wasimamizi wa shule- na serikali: uungaji mkono ushirikiano wa walimu; uumbaji wa maarifa; uungaji mkono uhuru wa walimu, na ushirikishwaji wao katika mijadala ya umma kuhusu elimu.

# Ualimu kama taaluma shirikishi

Wakati mwingi na mahali pengi, walimu huwa na majukumu mengi ya kijamii. Dhana kuhusu majukumu ya walimu ni tofauti katika tamaduni nyingi. Kwa mfano, wanaweza kuwa wafanyikazi wa umma na wasomi wa umma, wataalamu na wasanii, viongozi katika jamii na wanaoleta mabadiliko na viongozi wa maadili na walinzi wa mustakabali. Watu wengi maarufu katika historia ya binadamu wanatambuliwa kuwa walimu; kuanzia viongozi wa kiroho na wanasayansi hadi wanafalsafa wa kale na wataalamu wa hisabati, wote ambao wametoa mchango katika maarifa ya kurithiwa na kuelimisha wengi.

Katika historia, walimu walihusika katika ujenzi wa mkataba wa elimu ya karne za kumi na tisa na ishirini. Waliweka msingi wa elimu ya lazima kwa watu wote. Mwanzoni, walimu walifanya kazi za ualimu na kuanzisha shule za kwanza za umma. Uanishaji uliotumika mara ya kwanza wa "shule za kawaida" unaonyesha kilichotarajiwa kutoka kwa shule hizo: kuhalalisha miundo ya kawaida ya shule, mitaala, ufundishaji, na utaratibu wa kazi. Kuhalalisha huko kulinuiwa kujenga mila na miongozo ambayo ingetumiwa kama marejeleo na shule zingine. Kazi iliyofanyika katika karne iliyopita inaonekana katika uimarishaji wa vyuo vya walimu kuanzia Marekani hadi Uchina na kuanzia Brazili hadi Uhindi.

Kuongezeka kwa elimu kumefanya walimu kuwa wahusika wakuu katika masharti ya kazi yao, majukumu yao, na sifa za kazi hiyo. Vile vile, ongezeko la mahitaji ya elimu limechangia kuwepo kwa mikondo ya madarasa. Lakini mfumo huo ambao ni kama kreti ya kuwekea mayai iliyopanuliwa, haukuangazia jukumu la mwalimu. Mfumo huo umeongeza mzigo wa walimu.

Talanta na uwezo wa walimu ni mambo yanayostahili kuimarishwa kupitia kwa ushirikiano. Walimu wamekuwa na wanastahili kuendelea kuwa kigezo katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu ya mustakabali wetu sisi wote. Uwezo wao unaathiriwa na viwango vya ushirikiano vilivyo katika mifumo ya kazi ya ualimu.

Talanta na uwezo wa walimu ni mambo yanayostahili kuimarishwa kupitia kwa ushirikiano.

## Walimu katika mazingira shirikishi ya elimu

Ndiposa waweze kuwasadia wanafunzi, walimu lazima washirikiane na wataalamu wengine katika kupatia kila mwanafunzi msaada anaohitaji. Dhana kuwa ualimu ni kazi ya kibinafsi inaleta majukumu mengi ambayo hayawezi kukamilishwa na mtu mmoja na inaweza kuchangia walimu wengi kuacha kazi yao. Wakati huo huo, mahitaji ya kimwili, kijamii na kihisia ni muhimu katika uwezo wao wa kusoma. Wanafunzi wanahitaji kusaidiwa kupitia kwa mfumo unaowawezesha walimu kuwasaidia. Mfumo huo unastahili kuwa na usaidizi unaolenga afya na lishe, huduma za kijamii, afya ya kiakili, na mahitaji maalumu ya elimu. Familia lazima zihusike katika elimu ya watoto wao.

Kuna mipango ya kufana inayoleta matumaini kuhusu uwezekano wa walimu kufanya kazi kama timu. Kwa mfano, kuna shule ambazo huwa na timu za walimu, wataalamu wa kusoma na kuandika na walimu wa elimu ya mahitaji maalumu. Timu hizo zinahakikisha kuwa kila mtu anatoa mchango kuhusu jinsi ambavyo watoto wanaweza kusaidiwa katika masomo yao ya lugha. Katika ufundishaji huo wa kushirikiana, walimu hufanya kazi kwa pamoja ili kuwasadia wanafunzi binafsi na madarasa yote kufikia malengo yao kwa wakati mmoja. Kwa miktadha mingine, mashirika ya utumishi wa umma na yale yasiyo ya serikali hufanya kazi kwa pamoja katika kuwaunganisha wanafunzi na familia zao ili waweze kuimarika kielimu na kiafya. Kuna mifumo mingine zaidi, isiyoweza kuhesabika, inayoweza kutumiwa katika kuwawezesha wanafunzi kupata usaidizi kutoka kwa washauri, wataalamu, na walimu wenza.

Kwa sababu ya nafasi nyingi za ushirikiano zinazoweza kutumiwa, ni muhimu kuelewa jukumu la walimu katika kujenga mandhari mapya ya elimu. Mazingira haya mapya sio matokeo ya bahati; ni matokeo ya kazi ya makusudi iliyopangwa na kutekelezwa kwa kila eneo. Viongozi wa mitaa, wazee, wasimamizi, jamii na familia wana majukumu muhimu. Wafanyakazi wa kijamii, washauri, wataalamu wa elimu ya mahitaji maalumu, wakutubi, na wataalamu wa kusoma na kuandika wanaweza kuimarisha michango ya wanafunzi katika mazingira ya elimu yanayojengwa na walimu.

Mazingira ya elimu katika shule yanastahili kuwa na mitandao ya nafasi maalumu za kusoma. Hakustahili kuwa na tofauti baina ya masomo ya darasani ya yale yanayotokana na shughuli za ziada. Walimu ni muhimu katika ujenzi wa miunganisho inayoimarisha mitandao hii, lakini ili waweze kutenda kazi hii vizuri, lazima kuwe na mabadiliko katika maadili na utambulisho. Kwa vile mifumoikolojia mipya na mitandao ya majukwaa ya ujifunzaji ni muhimu katika kufanikisha jukumu kubwa la kijamii na kitaasisi, walimu ni wahusika wakuu katika ujenzi wa mustakabali wa elimu.

> Ualimu sio kuongoza mwanafunzi kutumia mafunzo ya darasani tu.

Ualimu sio kuongoza mwanafunzi kutumia mafunzo ya darasani tu. Tunapaswa kuangalia elimu kama shughuli inayotokea shuleni kote na kupitia kwa ushirikiano na wakufunzi wengine. Si rahisi kuanza kuangalia elimu kama jambo linalotokea shuleni na sio darasani tu. Vizingiti vinaweza kuzuia ushirikiano baina ya walimu. Wazo la kushirikiana linamaanisha kufanya majukumu ya kibinafsi na kuhusika katika uongozi wa shule. Kulazimisha ushirikiano hakuleti manufaa yoyote. Mabadiliko katika mitaala na ufundishaji yanastahili kuleta ushirikiano usio wa kulazimisha. Ikiwa elimu itakuwa ni walimu kufundisha madarasani tu, ushirikiano utakuwa hauna maana. Lakini ikiwa elimu itaendelezwa kupitia kwa nafasi na nyakati tofauti na kuangazia shida na miradi tofauti, kutakuwa na ushirikiano.

## Kupiga taswira na kutekeleza mitaala na ufundishaji

Mitaala sio lile lililobuniwa na kuagizwa tu, bali ni lile linalotekelezwa. Kupiga taswira na kutekeleza aina mpya za mitaala, yenye misingi ya maarifa yaliyo wazi, inategemea kazi ya walimu kwa kiwango kikubwa. Ingawa teknolojia ya dijitali inaleta nafasi nyingi, uvumbuzi hufanikiwa wakati umepangiwa kutimiza mahitaji maalumu ya wanafunzi katika mazingira maalumu. Walimu wana jukumu la kipekee la kutoa elimu inayowasaidia wanafunzi binafsi kufikia mahitaji yao. Walimu wanahitaji uhuru, matayarisho ya kutosha, rasilimali za kufunza na usaidizi katika kurekebisha, kujenga, na kubuni nafasi bora za kusoma kwa manufaa ya wanafunzi wote. Mitaala ya kesho lazima iwapatie walimu kiwango cha juu cha uhuru kinachokamilishwa na teknolojia; ushirikiano na walimu wenza; na ushirikiano na wataalamu kama maprofesa wa vyuo vikuu na wanasayansi.

Ufundishaji wenye misingi ya ushirikiano hutokea sio kupitia kwa masomo ya darasani tu, bali kupitia kwa ujifunzaji shirikishi baina ya madarasa na majumuiya ya walimu. Baadhi ya changamoto za walimu haziwezi kusuluhishwa na mtu binafsi lakini zinaweza kukabiliwa kupitia kwa mitandao ya shule, ushirikiano na vyuo vikuu na majumuiya ya wataalamu yanayoungwa mkono na taasisi maalumu za elimu.

Kuna njia nyingi walimu wanaweza kutumia katika kuboresha masomo: kushirikiana na makundi ya kusoma, mabaraza ya walimu, timu za ufundishaji, ushauri wa marika, ufundishaji, uchunguzi na kuzuru maeneo tofauti.

Maarifa ya taaluma ya ualimu yamejengwa kutumia nadharia na mazoezi ya ufundishaji. Maarifa hayo yanakuzwa kutumia mkusanyiko wa tafakari kuhusu uzoefu wa kibinafsi na wa jumla. Hakuna miktadha miwili ya ufundishaji iliyo sawa; hii ndiyo maana ile kazi ya uhusiano inayofanywa na walimu haiwezi kufanywa hata na mashine zenye uwezo mkubwa. Ufundishaji ndio unaruhusu kila mwanafunzi awe na uhusiano wa kibinadamu na elimu na aweze kufikia ulimwengu wa weledi, ubunifu na uelewa. Hatuwezi kuwa na mabadiliko katika mitaala na ufundishaji bila ya walimu.

Hatuwezi kuwa na mabadiliko katika mitaala na ufundishaji bila ya walimu.

## Walimu na utafiti wa kielimu

Mojawapo ya vitu muhimu walimu wanastahili kutafakari kuhusu ni uhusiano baina yao na maarifa. Kwa wengine, kitu muhimu zaidi ni ustadi katika kufunza masomo. Kwa wengine, maarifa na ufundishaji ndio muhimu zaidi. Aina ya tatu ya maarifa ni maarifa ya ujifunzaji wa kitaaluma. Katika taaluma yoyote, wataalamu huchangia katika uundaji wa maarifa ya kitaalamu, ambayo mara nyingi ni matokeo ya majaribio yanayofuata utaratibu, tathmini ya uzoefu na mazoezi.

Maarifa yenye msingi wa uzoefu ni muhimu katika kujenga taaluma ambayo walimu wanajitambua kama wataalamu wenye uwezo wa kutafakari. Katika kiwango cha kibinafsi, maarifa ya ujifunzaji wa kitaaluma yana vipengele vyenye umaizi, vitendo, na uhusiano. Ufundishaji shirikishi hujumuisha kipengele cha kutafakari na kushirikiana na wanafunzi wenza. Kwa kiwango kikubwa, mwalimu anaweza kubadilisha utafiti huu uwe maandiko. Taaluma haistahili kurekodi historia, uzoefu na vitendo vyake tu; inastahili kutafuta nafasi za udadisi na uvumbuzi, ifafanue maswala ya utafiti na itafute majibu yake. Wakati walimu wanatambuliwa kama wataalamu wanaotafakari na wazalishaji maarifa, wao huchangia katika mikusanyiko ya maarifa inayohitajika kubadilisha mazingira ya elimu, sera utafiti, na uzoefu ndani na nje ya taaluma yao.

# Safari ya maendeleo ya mwalimu inayosokotana na maisha

Walimu wanajitayarisha kwa ajili ya majukumu yao kupitia kwa mifumo na taasisi tofauti. Jambo linalostahili kutambuliwa ni kuwa licha ya vyeti au uzoefu, walimu 'hawamaliziki' au 'kukamilika' katika utambulisho wao wa kitaaluma, uwezo wao au kuendelea kwa kitaaluma. Maendeleo ya mwalimu ni mchanganyiko wa ujifunzaji na uzoefu unaotokea kipindi chote cha maisha yake; mchanganyiko huo umesokotana na maisha.

Vipengele vya kibinafsi na kijamii vya walimu lazima vitambuliwe na kuthaminiwa. Kuwa mwalimu inahitaji upanuzi wa uzoefu wa mwalimu binafsi na mwingiliano na ulimwengu wa maarifa na dhana. Walimu wasiopenda kusoma hawawezi kuwapatia wanafunzi wao motisha ya kusoma. Vile vile, ni vigumu kufunza sayansi ikiwa hauvutiwi na sayansi. Wanafunzi lazima wasome kutoka kwa vitendo vya walimu wao jinsi ambavyo wanasoma kutoka kwa maneno ya walimu.

Maktaba wa maisha ya kila mwalimu ni muhimu katika kazi yake. Ni kupitia kwa raha ya ujifunzaji na kuimarika kwa kijamii walimu huwa maajenti wa elimu inayosokotana na maisha. Na kupitia kwa uajenti wao wanaweza kuchangia urafiki na mshikamano na watu wengine na sayari iliyo hai.

## Kuajiriwa kwa walimu

Kwa wengine, safari ya kuwa mwalimu huanza mapema. Wengine hupata nafasi hiyo baadaye maishani, labda baada ya kubadilisha taaluma zao au kwa sababu zingine. Ongezeko la elimu katika miaka thelathini iliyopita limechangia kuajiriwa kwa walimu wengi. Hilo limechangia matokeo mazuri kama vile ongezeko la idadi ya wanawake katika taaluma ya ualimu na matokeo mabaya kama vile kupungua kwa idadi ya walimu ambao wametayarishwa kitaaluma ; kupunguzwa kwa mshahara na hadhi; na utumiaji wa mifumo ya misaada kupita kiasi.

Mahali pengi, mahitaji ya walimu yameongezeka ; hii inamaanisha kuwa kuajiriwa kwa walimu waliohitimu kumeathirika. Mara nyingi, shinikizo, athari na shida za ufundishaji huwa nyingi kuliko faida ya ufundishaji ; hili ni jambo linalopunguza idadi ya wanaongia katika taaluma ya ualimu. Wakati huo huo, idadi ya walimu wanaohitajika inaendelea kupanda. Takribani walimu milioni 70 wa shule za msingi na upili watahitaji kuajiriwa ulimwenguni kufikia mwaka 2030 ndiposa tuweze kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (nambari ya 4). Hali iliharibika zaidi wakati wa UVIKO-19 na hivyo walimu wengi watahitajika ili wazibe mapengo ya walioacha taaluma ya ualimu. Bila ya mabadiliko mwafaka, itakuwa vigumu kuvutia idadi kubwa ya walimu wenye motisha. Hili ni swala la dharura katika sera za umma na kwa jamii yote.

Hali, ya upungufu wa walimu, ni tofauti katika nchi na maeneo mbalimbali. Upungufu mkubwa umeshuhudiwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule inaendelea kuongeza kwa kasi. Hatua ya dharura itahitajika ili kuongeza uwezo wa ufundishaji wa walimu. Ingawa kuna wengi walio na vipaji, kuna vizuizi vinavyowazuia wengi kupata vyeti hasa katika zile nchi zilizo na nafasi chache za elimu ya juu. Mbinu bunifu za kuajiri na kuendeleza walimu zinastahili kuongezwa ili kuimarisha uwezo wa jamii.

> Hatua za dharura za kuwahifadhi walimu waliohitimu zinahitajika.

Ukosefu wa walimu waliohitimu unashuhudiwa katika maeneo mengi na unatokana na ukosefu wa usawa. Kabla ya janga la UVIKO-19, mgawanyo wa walimu wenye uzoefu na umahiri haukuwa na usawa hasa kati ya shule za vijijini na za mijini zinazo shughulikia wanafunzi kutoka matabaka mbalimbali. Ni kinaya kuwa mazingira yanayohitaji walimu wenye uzoefu mkubwa yana walimu wasio na uzoefu na walimu wa kujitolea kufunza bila malipo au wale ambao hawajahitimu, wote ambao huacha kazi

hiyo kwa viwango vya juu. Kando na kutekeleza sera za kuvutia vizazi vipya vya walimu, hatua za dharura za kuwahifadhi walimu waliohitimu zinahitajika.

Kuajiri walimu katika jamii zao au katika tamaduni wanazozielewa ni mbinu ya kuimarisha utofauti na ujifunzaji wa wanafunzi. Kwa hakika, walimu hao wana uzoefu na wanaweza kuwa na uhusiano na jamii utakao wawezesha kuelewa mahitaji, matarajio na tamaduni kwa njia ambazo zitasaidia katika ujenzi wa mustakabali wa elimu ulio na haki na usawa.

## Elimu ya walimu

Elimu ya walimu inastahili kubadilishwa ili ikubaliane na vipaumbele vya kielimu na changamoto na matarajio ya kesho. Hatua za dharura zinahitajika katika maeneo mengi ulimwenguni hasa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo viwango vya kufuzu ni vya chini. Hakuna suluhu moja linaloweza kumaliza shida hii. Ushirikiano na wadau katika elimu ya walimu – kwa mfano serikali, watafiti, majumuiya ya walimu, na viongozi wa jamii - unaweza kuleta nafasi nyingi za kujifunza na kufanya uvumbuzi.

Elimu ya walimu haiwezi kupuuza teknolojia ya dijitali kwa sababu inatumika katika uzalishaji na usambazaji wa maarifa. Teknolojia ya dijitali inaweza kutumika katika kufanikisha maendeleo ya kitaaluma ya walimu kama maudhui ya kusomwa. Zaidi ya hayo, utafiti unahitajika katika maswala yanayohusiana na teknolojia ya dijitali : gharama, athari kwa ufundishaji, uwezekano wa kimaarifa na kiepistemolojia na upungufu wake.

Elimu ya walimu inaweza kuwa na ufanisi kama inazingatia mambo yanayochangia walimu kuacha kazi ya ualimu. Hatua ya kuunga mkono taaluma ya ualimu inahitaji zaidi ya kuajiri walimu waliohitimu wa kutosha. Inahitaji kubadilishwa kwa majukumu ya walimu ili waweze kufanya kazi kwa kushirikiana kama timu zilizo na rasilimali ya kuleta maendeleo ya kitaaluma. Kwa mfano, kipindi chote ulimwengu ulikuwa unakabiliana na janga la UVIKO-19 walimu walifadhaika kwa sababu ya ukosefu wa majukwaa ya teknolojia ambayo yalihitajika ili kufanikisha masomo na upungufu wa nafasi za kujiendeleza kitaaluma. Kwa hivyo, wengi wao walilazimika kuacha kazi ya ualimu.

## Walimu malimbukeni

Katika taaluma yoyote, hakuna jambo lililo muhimu zaidi kushinda jinsi ambavyo vizazi vipya vinakaribishwa na kufunzwa. Programu za kuingiza walimu malimbukeni katika taaluma ya ualimu zinastahili kuwasaidia miaka ya kwanza kupitia kwa ushirikiano wakati wa kutayarisha mipango ya masomo na ushauri kutoka kwa walimu wenye uzoefu. Kipindi cha mpito cha kujitayarisha na kuanza kazi ya ualimu ni nguzo ya taaluma ya ualimu lakini mara nyingi huwa kinapuuzwa na sera na taaluma yenyewe, na matokeo yake ni viwango vya juu vya walimu kuacha kazi.

Kama taaluma zingine, ualimu unahusiana na msingi wa maarifa. Maarifa ya kitaaluma ya ualimu yanahitaji michakato inayojumuisha taasisi za kuwafunza walimu, shule, na walimu walio na uzoefu. Uhusiano huu ni muhimu tunapozingatia mabadiliko katika mazingira ya elimu na utofauti wa

wanafunzi katika karne ya ishirini na moja. Matatizo mapya yanahitaji ushirikiano baina ya walimu wa vizazi tofauti. Matatizo haya ya kesho yanaweza kusuluhishwa kwa ufasaha kupitia kwa walimu kusadiana kama jumuiya ya marika wanaoaminiana.

Walimu huongoza uumbaji wa maarifa wanapohusika katika utafiti, usuluhishaji wa shida, miradi, na majaribio yanayotumia mbinu mpya. Michakato hii inastahili kuwa misingi ya programu za kuingiza walimu katika taaluma ya ualimu.

### Maendeleo ya kitaaluma

Walimu wanahitaji nafasi za kujiendeleza kitaaluma, kusoma na kufanya kazi na wanafunzi walio na utofauti wa kikabila, kitamaduni na kilugha na wale walio na mahitaji ya kipekee. Lazima wahakikishe kuwa wanafunzi wanaotoka kwenye jamii zilizotengwa wamesaidiwa vya kutosha. Jambo hili ni la dharura katika maeneo ambayo kuna mabadiliko katika madarasa; mabadiliko hayo yanatokana na mabadiliko ya tabianchi, vurugu za kisiasa na kijamii na vita - ambazo ni hali zinazotarajiwa kuongezeka katika miaka ijayo.

Maendeleo ya kitaaluma yanapaswa kuwa kipengele muhimu katika kila hatua ya maisha ya mwalimu kuanzia elimu yao ya mwanzo, shughuli za kupata uzoefu, kuingizwa kwenye taaluma, kushauriwa na kupata maendeleo ya kitaaluma ya mara kwa mara. Maendelo ya kitaaluma yanastahili kuunganishwa na shughuli za kila siku za walimu.

Mara nyingi, programu za maendeleo ya kitaaluma huzingatia mambo ambayo wanafunzi wanastahili kusoma na hatua walimu wanastahili kuchukua ili kuongoza wanafunzi hao na kutathmini kuendelea kwao. Programu zenye ufanisi mkubwa huendelea kwa muda mrefu na hii huwapatia walimu fursa za kutumia maarifa ambayo wamesoma na katika ujenzi wa maarifa ya ufundishaji na dhana.

## Mshikamano wa umma katika kubadilisha ualimu

Ndiposa walimu wachangie katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, lazima mabadiliko yafanywe katika sera zinazoongoza kuchaguliwa kwa walimu, kutayarishwa kwao, njia za kitaalamu za walimu, na mpangilio wa taaluma ya ualimu. Ushirikiano haumanishi kuwaongezea walimu majukumu mengine. Walimu wanahitaji kufadhiliwa ili waweze kushirikiana na wadau wa elimu hasa familia, jamii, elimu ya juu, na aina zote za mashirika ya kijamii.

## Hali za kazi ya walimu

Licha ya utafiti kubainisha kuwa ubora wa ufundishaji huchangia katika ufanisi wa wanafunzi, walimu hawatambuliwi, hawathaminiwi, hawalipwi na hawasaidiwi vya kutosha. Maswala ya muundo wa taaluma ya ualimu, uongozi wa taaluma, uhamasishaji wa walimu na kuridhika na kazi yamekuwa magumu kushughulikia ulimwenguni kote hasa wakati umma haujahusishwa. Kutegemea walimu ambao hawana ujuzi wa kutosha ni mwanzo wa kudhoofisha taaluma ya ualimu na elimu ya umma.

Walimu wengi huacha kazi ya ualimu kwa sababu ya hali duni za kazi na mshahara mdogo. Athari za jinsia kwa taaluma ya ualimu zinastahili kuzingatiwa katika uchanganuzi wa mivutano na mahitaji ya taaluma ya ualimu. Ongezeko la idadi ya walimu wa kike katika nchi zingine limetumika kama sababu ya kupunguza mshahara au kuongeza upana wa mapengo ya mishahara inayolipwa kwa jinsia tofauti. Ni sharti tuboreshe hali ya kazi ya walimu kupitia kwa sio tu mishahara, bali kwa kupunguza idadi ya wanafunzi katika kila darasa, kuboresha usalama shuleni, kuimarisha kutambuliwa kwa kitaaluma, kuongeza usaidizi wa kitaasisi na kujenga utamaduni wa ushirikiano.

Kwa jumla, kazi za walimu zinahitaji kupangwa upya. Maendeleo yanastahili kuzingatia ustadi, maendeleo ya kitaaluma na kuhusika katika programu za shule kama kuhamasisha walimu wapya; kuwahusisha katika mipango ya ufundishaji; kuwapatia majukumu ya kuongoza masomo na nyakati fulani; na huduma zingine kama vile ushauri, likizo za kufanya utafiti na maendeleo mengine ya kitaaluma. Kwa sababu ya ongezeko la shinikizo, walimu wanaomba uwiano baina ya mahitaji ya kitawala na ufundishaji. Pia, walimu wanaomba kutambuliwa kwa ile kazi ambayo wanafanya na haionekani hasa katika mazingira yanayo walazimu walimu kujihusisha na maswala ya jamii zao.

Vipaumbele vipya vya elimu vinahitaji marekebisho ya kina kwenye sheria za kazi za walimu, kanuni na viwango vya kazi. Zaidi ya hayo, ni muhimu kutambua aina mpya za uthibiti na teknolojia ambazo zinapunguza uhuru wa walimu. Ongezeko la tathmini za viwango vikubwa, kutathminiwa kwa walimu, ukaguzi wa shule na viwango vya ualimu ni mifano ya shinikizo ambazo walimu hukumbana nazo ingawa hawana usaidizi wa kutosha wa kukabiliana nazo.

Mifumo mingine ya elimu imeanza kutumia Akili Mnemba kama mbinu na kuimarisha utawala wa ndani, ufanisi na uwajibikaji. Ingawa teknolojia hiyo imeleta manufaa kwa maarifa na uwazi wa michakato ya elimu, ongezeko la teknolojia za ujifunzaji wa mashine unaongeza athari za kuwaganya michakato ya elimu na kuifanya iwe seti za data; kutegemea meneja wataalamu katika usimamizi wa shule; ufuatiliaji; na kupunguza ustadi wa walimu. Utumiaji wa Akili Mnemba katika kuwafuatilia wanafunzi na walimu ni kinyume na Kifungu cha 26 cha Azimio la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa ambacho kinasisitiza lengo la kutumia elimu katika kuimarisha haki za msingi za binadamu.

Kazi ya walimu ni jukumu kubwa; kwa hivyo, lazima kazi hiyo iwajibike kwa jamii na kwa mustakabali. Lazima walimu wawe na usalama wa kufanya kazi katika mazingira ya uwazi na imani; mazingira hayo yataboresha njia mpya za kufikiria na kuishi katika ulimwengu ambapo viwango vya juu vya usimamizi wa mameneja wa kitaalamu na mashirika makubwa umehatarisha kazi yao.

# Mahusiano baina ya vyuo vikuu na walimu

Kuna uhusiano wa karibu baina ya elimu ya juu na taaluma ya ualimu ; miundo mipya ya taasisi inastahili kujumuisha uhusiano huo. Wazo la kubadilisha mustakabali wetu kwa pamoja linastahili kubadilishwa ili liwe ahadi ya kuleta ushirikiano baina ya shule, walimu na vyuo katika maswala ya elimu ya walimu na maendeleo ya kitaaluma yasiyo na kikomo. Elimu ya juu ina uwezo wa kubadilisha mitazamo na ufundishaji wa kizazi cha walimu kinachokuja. Vile vile, walimu wanaweza kusaidia vyuo ili vijibadilishe na kuelewa jukumu lao katika mifumuikolojia ya elimu.

Jukumu muhimu linalohitaji kutekelezwa ni ujumuishaji wa uhusiano kwenye mbinu zinazotumika kwenye programu za elimu ya walimu hasa katika hatua za mwanzo za kutayarisha walimu.

Jukumu la kutoa elimu ya walimu katika vyuo vikuu lazima liimarishwe. Katika historia, kumekuwa na uhusiano baina elimu ya msingi, elimu ya sekondari na vyuo vikuu. Hata hivyo, katika maeneo mengi, kuna haja ya kuleta mabadiliko katika programu na mikakati ya elimu. Jukumu muhimu linalohitaji kutekelezwa ni ujumuishaji wa uhusiano kwenye mbinu zinazotumika kwenye programu za elimu ya walimu hasa katika hatua za mwanzo za kutayarisha walimu. Jukumu la kuwatayarisha walimu haliwezi kukamilishwa na vyuo vikuu na shule tu. Programu zingine zinaziba pengo hili kwa kuleta fursa za kufanikisha ushirikiano baina ya wadau kama vile viongozi wa umma, majumuiya ya walimu na mashirika yasiyo ya serikali. Programu zingine zinatumia mbinu za utafiti ili kufanikisha masomo. Programu hizo hazistahili kubakia katika vitivo vya elimu; zinaweza kupanuliwa ili ziunganishe masomo ya msingi na ya sekondari na maarifa ya jamii yanayohamasishwa na vyuo vikuu. Kuna vyuo vikuu vimeanzisha 'bustani' za sayansi na viwanda; tunahitaji nafasi zingine za kielimu zitakazo waleta pamoja wadau wa aina mbalimbali ili wapange masomo ya walimu.

Mkakati mwingine ni wa kuimarisha programu za kuwaingiza walimu katika taaluma ya ualimu. Programu zilizo na ufanisi ni zile zinazowapatia walimu wapya nafasi ya kutosha ile waweze kuingia katika hatua ya kufanya kazi ya ualimu na kujiendeleza kwa wakati huo huo. Hii inamaanisha lazima kuwe na ushirikiano mkubwa baina ya vyuo vikuu na vyuo vya walimu. Uhusiano, unaoendelea, baina ya vyuo vikuu na walimu unaweza kuchangia pakubwa katika kuimarisha shule na mikakati ya kubadilisha elimu. Lazima kuwe na uhusiano imara baina ya walimu na vitivo vya elimu; kupitia kwa uhusiano huo, walimu wanaweza kuleta maarifa wanayopata kutoka kwa kazi zao kwa vyuo.

Kwa kumalizia, mabadiliko yanahitajika katika ufundishaji wa elimu ya juu. Walimu wa vyuo na maprofesa wanaweza kufaidika sana wakijitolea kushirikiana katika kazi yao. Ufundishaji wa mshikamano na kushirikiana una umuhimu kwa elimu ya juu. Kwa kweli, dhana hizi zinaweza kuwa za maana sana kwa vizazi vipya vya wataalamu, viongozi na watafiti.

### Walimu katika maamuzi ya kielimu na nyanja za umma

Siku hizi umuhimu wa nyanja za umma ambapo maswala ya elimu yanajadiliwa umeongezeka. Mijadala hiyo inalenga mikakati ya kujumuisha viongozi, wazazi, jamii, taasisi za umma na za kibinafsi, makundi ya vijana, walimu na mashirika ya walimu.

Taaluma ya ualimu inajumuisha mambo ya umma, ya kijamii na ujenzi wa ustawi. Kwa hivyo, ni muhimu walimu kuhusishwa katika sera za umma. Lakini katika maeneo mengi walimu wametengwa na hivyo hawakaribishwi katika mijadala ya sera za kielimu.

Kuwa mwalimu inamaanisha kupata fursa katika taaluma na kutoa mchango kwa maswala ya kielimu na ujenzi wa sera za umma. Ushirikishwaji huu si wa kutetea maslahi ya walimu tu, bali ni wa kutumia sauti na maarifa ya walimu katika maswala ya kisiasa na kijamii.

Tunapoangalia mustakabali, tunagundua kuwa ni muhimu kazi ya mwalimu iende nje ya kuta za darasa. Walimu wana jukumu la kuwezesha shule ziwe mahali pa kusoma ambapo walimu hujenga dira na elimu na kushirikiana na wanafunzi katika ujifunzaji. Kando na kuimarisha mifumo ya elimu, walimu wanaweza kutoa mwongozo wa kujenga utamaduni wa utafiti, uvumbuzi na uchunguzi.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii inapendekeza kuwa katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, ualimu unastahili kuwa shughuli ya ushirikiano ambapo walimu wanatumbuliwa kwa kutekeleza majukumu ya kuzalisha maarifa na kuongoza mabadiliko ya kijamii na kielimu. Tunapoelekea mwaka 2050, kuna kanuni nne za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu zitakazo fanikisha pendekezo hili:

- **Kazi ya walimu inastahili kuwa na ushirikiano.** Tunapaswa kuwaunga walimu mkono ili washirikiane katika ujenzi wa mazingira ya elimu. Ualimu bora unatokana na mazingira mazuri yanayohakikisha kuwa wanafunzi wanapata mahitaji ya kimwili, kijamii na kihisia.
- **Misingi ya ualimu inastahili kuwa uzalishaji wa maarifa, kutafakari na utafiti.** Walimu wanastahili kutambuliwa kama wanafunzi wanaotambua maswala yanayohitaji utafiti na uvumbuzi, kufafanua maswali ya utafiti na kuanzisha mbinu mpya za ufundishaji.
- **Uhuru wa walimu lazima uungwe mkono.** Walimu wanahitaji utambulisho wa kitaaluma ulio imara. Utambulisho huo unajumuisha programu za kuingizwa katika taaluma na fursa za kujiendeleza kitaaluma ili waimarishe uwezo wao wa kuongoza masomo ya wanafunzi.
- **Walimu wanastahili kushiriki katika mazungumzo na mijadala ya umma kuhusu mustakabali wa elimu.** Lazima walimu washirikishwe katika mazungumzo ya kijamii na maamuzi ya kubadilisha elimu.

Tunapojenga mustakabali mpya, tunapaswa kuhamasishwa na kanuni hizi zinazohusiana ya kazi ya kuleta mabadiliko wanayofanya walimu. Mazungumzo ya pamoja kuhusu ualimu na walimu ni muhimu katika ubadilishaji wa elimu.

# Sura ya 6

## Kulinda na kubadilisha shule

Nyumbani kulikuwa mahali nililazimishwa kuwa mtu ambaye sikutaka kuwa. Shuleni kulikuwa mahali ningejisahau na, kupitia kwa mawazo, nikajibadilisha . . . Darasa, licha ya upungufu wake, ni mahali pa uwezekano. Katika uwanja huo wa uwezekano, tuna fursa ya kupigania uhuru, kuomba kwa niaba yetu na wanafunzi wenza, uwazi wa akili na moyo unaotuwezesha kukabiliana na hali zetu tanapofikiria jinsi ya kuikaidi mipaka - kuikiuka.

**bell hooks**, *Teaching to transgress: Education as the practice of freedom,* 1994.

**Shule zinastahili kulindwa kama maeneo ya elimu yanayoendeleza ujumuishaji, usawa na ustawi wa binafsi na wa jumla wa wanafunzi. Vile vile, shule zinastahili kubadilishwa ili ziwezeshe ulimwengu kuwa na mustakabali wa haki, usawa na uendelevu.**

Ili kuwe na ufundishaji wenye ushirikiano, mshikamano na uhusiano imara na maarifa ya jamii, lazima kuwe na nyakati na nafasi zilizotengwa kwa ajili ya malengo haya. Shule, pamoja na uwezo na upungufu wao, ni mojawapo ya maeneo muhimu ya elimu. Shule zinaashiria kujitolea kwa jamii katika kufanya elimu iwe shughuli ya kibinadamu na ya umma. Hata hivyo, mipangilio ya shule sio adilifu na inaashiria dhana kuhusu ujifunzaji, kufaulu na uhusiano.

Majengo na utaratibu unaotumika katika shule huonyesha kinachowezekana, kisichokubaliwa, anayekaribishwa na asiyekaribishwa. Walimu, ambao ni waratibu wakuu wa mambo ya elimu, wanastahili kutenga muda wa kutosha ili kushughulikia maswala haya yanayoathiri ujifunzaji. Je, mazingira ya shule yataleta ushirikiano, uchunguzi na majaribio? Mazingira hayo yatakuwa ya ubaguzi au yatahamasisha ujifunzaji na kutafakari baada ya majaribio na kufanya makosa? Mazingira hayo yatachangia katika kupatana na vitu vingi katika kila hatua ya maisha? Na ni aina gani za ushauri, urafiki na mitamazo zitajengwa na kupatana huko? Je, mazingira ya elimu yatazingatia ufanisi wa kibinafsi zaidi ya jambo lingine lolote au yatazingatia ustawi wa kibinafsi na wa marika unaotokana na ushirikiano?

Sura hii inaanza na maelezo mafupi kuhusu kuibuka kwa shule kama taasisi za kijamii zilizo muhimu katika tamaduni zote. Shule si nafasi za elimu ya msingi na upili tu, bali zimekuwa maeneo ya kijamii yanayoleta aina nyingi ya huduma za kijamii zinazosaidia katika ustawi wa watu binafsi, familia na jamii. Walakini, shule zimebanwa katika ufanisi wao kwa sababu ya ufafanuzi mdogo wa nafasi na nyakati za kusoma. Sura hii inafafanua mabadiliko yanayowezekena: kupanua ujifunzaji ili uende nje ya darasa; kubadilisha masaa ya kila somo ili kufanikisha masomo ya kina; na kutafakari juu ya uwezekano wa kutumia teknolojia ili kuimarisha shughuli za shule na mambo yanayostahili kuzingatiwa tunapotumia mkataba mpya wa kijamii wa elimu katika kubadilisha shule.

Ikiwa tunataka elimu itusaidie kujenga mustakabali utakaotuwezesha kukabiliana na majanga na mambo mengine ambayo hatuyajui kwa sasa, lazima tuwe na shule thabiti.

Sura hii inahitimisha na kanuni za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu tunapoelekea mwaka 2050. Kanuni hizo zinalenga wanafunzi, walimu, serikali, na mashirika ya kijamii: kulinda na kubadilisha shule ili ziwe mahali pa ushirikiano; kutumia teknolojia kwa njia nzuri na kuimarisha uendelevu na haki za binadamu.

# Jukumu la shule lisilofidika

> Kama shule haingekua, tungelazimika kuibuni.

Kama shule haingekua, tungelazimika kuibuni. Shule ni nguzo muhimu katika mifumoikolojia ya elimu. Uhai wa shule ni thibitisho la kujitolea kwa jamii katika kukuza elimu kama kitu kinacholeta manufaa kwa wote. Shule huwapatia watoto na vijana mazingira ya kushiriki katika maarifa ya jamii. Ni mahali pa kuthubutu, kukabiliana na changamoto na kufanya majaribio.

Shule huhakikisha kuwa kila mtu anapata uzoefu, uwezo, maarifa na maadili yatakayoimarisha mustakabali. Tukipiga darabuni, tunaona kuwa ifikapo mwaka 2050, shule zitahitaji kuimarisha maadili ya ushirikiano na kutendeana mema.

Kazi nyingi ya elimu hutokea mara nyingi na katika mazingira tofauti, lakini nyakati na nafasi za umma ni za kipekee. Nafasi za shule huimarisha uhusiano wa kijamii. Elimu huchangia miingiliano na mazungumzo; shule zinastahili kujengwa ili kuimarisha shughuli hizi. Shule zingine huwaleta watu, wa umri tofauti, pamoja ili waweze kufunzana. Masomo ya dijitali na ya mbali yanaweza kusaidia kazi ya shule lakini hayawezi kuchukua lile jukumu la kukuza uhusiano baina ya wanafunzi.

Ongezeko la vurugu - kama UVIKO-19 na Ebola, vita, na dharura za tabianchi - limeweka wazi jukumu la kipekee la shule. Visa hivi vimetukumbusha kuwa shule ni muhimu katika elimu na ustawi wa kijamii. Shule ni mojawapo ya taasisi chache zinazostahili kulinda na kuwapatia fursa masikini na waliowadhaifu. Kama maeneo ya kijamii, shule huwawezesha watu kujisimamia na kuwa na uhusiano endelevu na jamii zao na mazingira asili. Kwa mfano, wakati shule nyingi zilifungwa kwa ghafla miaka ya 2020 na 2021, watoto wengi ulimwenguni walikosa fursa ya kufikia shule, wanafunzi wenza na walimu. Kupungua kwa masomo ya moja kwa moja kulileta athari za kijamii na kiakili katika maisha ya mamilioni ya watoto; athari hizo zitawafuata kwa maisha yao yote. Shule zinastahili kuwapatia wanafunzi wa umri tofauti motisha ya kutafuta maarifa.

Wanafunzi wanastahili kupatiwa dhana na uzoefu ambao hawawezi kuupata kwa urahisi wakiwa nyumbani au katika jamii zao. Shughuli za ufundishaji hufanya shule ziwe mahali pasipofidika. Shule, ambazo ni taasisi za kipekee katika mkusanyiko wa taasisi zingine, ni mahali pa ufundishaji na ujifunzaji. Binadamu hujifunza na wana uwezo wa kufundisha na kufunzwa. Hali hii inatuunganisha na maarifa ya jamii, vizazi vingine, njia za kujua, na sisi kama binadamu. Shule haziwezi kuwa bila ya walimu. Walimu huendeleza jukumu la ufundishaji la kuwapatia watu wote maarifa; kujenga dhamira na uwezo wa jamii; na miradi ya kukomboa akili. Vile vile, kazi ya walimu hutegemea afya ya mazingira ya shule.

## Ahadi za kihistoria

Katika tamaduni nyingi, kumekuwa na nyakati na nafasi za kipekee za kukuza maarifa, ujuzi, maadili, na ufahamu. Tamaduni hizo zimekuwa na maarifa changamani ambayo hayawezi kusomwa kupitia kwa kuangalia, kuiga, na hadithi. Kuenda shuleni kuliongezeka baada ya uvumbuzi wa kuandika. Jambo la kupendeza ni kuwa jina 'shule' linalotoka kwa jina *skholè,* ambalo ni jina la Kigiriki linalomaanisha wakati wa mapumziko. Na ingawa Taasisi ya Kigiriki ilitoa modeli ya elimu iliyotumika huko Ulaya, tamaduni nyingi kama vile yeshiva, madrasa, na calmecac, zimejenga taasisi za masomo. Katika karne mbili zilizopita, shule zimeongezeka ulimwenguni na kuwa mojawapo ya miundombinu ya umma inayoongoza mazungumzo baina ya vizazi kuhusu jinsi ya kuishi ulimwenguni, kujenga ulimwengu na kuutunza. Shule hutuwezesha kuelewa historia zetu, kuzijenga, na kuzipanua.

Shule zimekuwa mojawapo ya mbinu za kupanga uhusiano wetu na maarifa ya jamii. Shule zina uwezo wa kuimarisha shughuli za kiepistemolojia kwa kuwapatia wanafunzi mwongozo wa

kufikiria, kusoma, kuchunguza na kufanya utafiti. Shughuli za shuleni zinaweza kukuza maadili, uhusiano na maarifa. Katika historia, jambo ambalo limesisitizwa ni uenezaji wa 'ukweli wa madai' (maelezo kuwa mfumo wa itikadi ni wa kweli). Lakini, mabadiliko ambayo yametokea katika miongo kadhaa iliyopita yamepinga maelekezo ya moja kwa moja yanayotumika katika shule nyingi. Utumiaji wa mbinu za ushirikiano umeimarisha dhamira ya kukuza ufahamu kuhusu 'ukweli wa madai'. Changamoto tunazokabiliana nazo zinaweza kusuluhishwa kwa kutumia aina nyingi za mbinu za epistemolojia na kupitia kwa upanuzi wa uhusiano baina yetu na mifumo tofauti ya maarifa.

Katika mabadiliko hayo ya kueneza maarifa, ni muhimu kuzingatia ushirikishwaji na uchunguzi. Lazima tuwe tayari kutambua kuwa kuna aina nyingi ya ufahamu kuhusu mambo tofauti. Kazi nyingi inastahili kufanywa ili tujenge nafasi na nyakati za kusoma kwa njia zitakazofanikisha masomo ya vizazi tofauti.

# Mabadiliko ya lazima katika shule

Shule zinastahili kuwa mahali ambapo kila mtu anaweza kutimiza malengo ya mabadiliko na ustawi. Zaidi ya yote, shule lazima zitusaidie ili tuweze kufikia uwezekano ambao hatuwezi kuuona kwa sasa. Katika maeneo mengi ulimwenguni, ongezeko la shule limeleta fursa za kubadilisha watu na jamii; fursa hizo zimeongeza ufahamu na ujuzi wao na kuchangia katika maendeleo yao. Hata hivyo, shule za siku hizi zimechangia ukosefu wa usawa na unastahili kurekebishwa.

> Kama shule haingekua, tungelazimika kuibuni.

Mabadiliko makubwa yanaweza kutokea baada ya kutumia kanuni za ujumuishaji na ushirikiano katika kupanga mambo ya shule. Malengo ya ubora, mafanikio, tathmini na maendeleo yanahitaji kutumiwa katika kuleta ujumuishaji badala ya ubaguzi.

Mazingira mapya yanaweza kupangwa kama maktaba makubwa ambayo yana wanafunzi wanaofanya masomo ya binafsi na wengine wanaosoma pamoja na wanafunzi wenza na walimu. Pia, kuna wanafunzi wengine nje ya maktaba hayo wanaosoma kupitia kwa mwingiliano wao na watu wengine na mazingira yaliyo nje ya shule. Maktaba ni nguzo ya aina nyingi za miktadha ya nyakati na nafasi. Ni mazingira mapya ambayo ni tofauti na yale yanayotumiwa shuleni na darasani leo hii. Maktaba haya yanaweza kuchukuliwa kama maktaba ya kawaida au sitiari. Inatukumbusha kuwa nyakati na nafasi za shule lazima zitumike katika kuwaunganisha wanafunzi na maarifa ya jamii.

## Shule kama majukwaa ya ushirikiano, utunzi na mabadiliko

Kuwa mazingira ya ujumuishaji na ushirikiano inamaanisha shule ni sehemu yenye usalama na isiyo na uhasama au uonevu; kwa hivyo, wanafunzi wote wanakaribishwa huko licha ya utofauti wao. Ujifunzaji kwa pamoja na wa kushirikiana haumaanishi kufanana. Mbinu mwafaka za kushirikiana zinazingatia tofauti za uwezo, malengo na vipaji vya wanafunzi na walimu. Kwa upande mmoja,

ujifunzaji ni safari yenye kibinafsi kila mmoja wetu anachukua. Ujifunzaji wa kushirikiana lazima uwe na ujumuishi na usawa bila ya kuhatarisha utofauti wa wanafunzi. Kwa upande mwingine, ujifunzaji ni safari ya watu wengi inayotegemea uhusiano baina yao.

Kujifunza mwenyewe ni muhimu kwa vile malengo ya kibinafsi na ya watu wote yanasukumana na kukamilishana. Ingawa hatuwezi kusoma kwa niaba ya watu wengine, tunaweza kusoma mengi pamoja. Kile tunajua kinategemea kile watu wengine wanajua. Elimu hutoka kwa uhusiano na utegemeano wetu. Ujifunzaji wa kushirikiana unaendelea katika shule nyingi ulimwenguni. Lakini, shule zote ulimwenguni zinastahili kuimarisha uhusiano na utegemeano huo.

Shule na walimu hufanya kazi muhimu katika kuwainua wanafunzi. Watu wengi wanaweza kukumbuka wakati maisha yao yalibadilika na yakawa bora kwa sababu ya mwalimu au shule. Kwa wakati huo huo, shule hubagua wanafunzi na kuchangia katika ongezeko la ukosefu wa usawa. Takribani nusu ya wanafunzi humaliza masomo ya shule ya upili bila ya kufikia viwango vya chini vya ustadi katika ujuzi wa msingi - haya ni matokeo yasiyostahili, na ni ushuhuda wa shule kuwaangusha wanafunzi na jamii zao. Mifano mingi ulimwenguni inaonyesha kuwa kuna uwezekano wa kubadilisha shule ili ziweze kujirekebisha kwa urahisi kulingana na mazingira.

Shule zinaweza kupata manufaa mengi kutoka kwa mabadiliko haya. Watu wengi waliotoa maoni yao kwa mradi wa Mustakabali wa Elimu, wanakubaliana kuwa mipango ya shule - kama majengo, mitaala, mpangilio wa darasa na shughuli za ujifunzaji inahitaji mabadiliko. Kazi ya usanii, inayolenga taswira ya elimu mwaka 2050, inaonyesha mwisho wa safu za meza na madawati. Majopo mengi ya wataalamu wa elimu yameeleza jinsi ambavyo shule zitaimarika tutakapogundua kuwa ujifunzaji hutokea katika nafasi na nyakati nyingi hasa baada ya kukiuka kuta zinazotenga madarasa kutoka kwa ulimwengu wa nje na tunapopanga masomo ili yawe kama safari. Kwa ufupi, shule zitakazotumiwa na vizazi vya kesho zinastahili kuwa jumuishi, zenye kuvutia na bora zaidi.

Shule zinastahili kuwa mahali ambapo wanafunzi wanajifunza jinsi ya kuishi kwa uendelevu ndiposa wapeleke maarifa hayo kwa familia na jamii zao. Kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na shule zenye uendelevu na elimu isiyotoa kaboni.

Ndiposa shule ziweze kutimiza malengo hayo, lazima zitupilie mbali miundo ya mipangilio ambayo imekuwa ikitumika kwa zaidi ya karne mbili. Mabadiliko ni muhimu. Juhudi zilizofanywa katika karne za kumi na tisa na ishirini zilitumika katika ujenzi wa mipangillio ya shule inayotumika sasa na ambayo inatupatia ufahamu kuhusu kesho. Katika kipindi cha miaka mia moja hamsini iliyopita, wataalamu wa ujenzi, afya ya umma, wanafilosofia, wafanyakazi wa umma, wakufunzi, jamii na familia wametumia ufahamu wa historia ya binadamu katika kupanua uwezekano wa elimu. Baada ya muda mrefu, tumeona matokeo yake - kwa mfano kupitia kwa majengo ya shule, madarasa, na taasisi za kijamii za elimu ya umma. Tunahitaji mawazo, jitahada, na ushirikiano kama uliotumika hapo awali ndiposa tujenge shule mpya zitakazo tuletea mustakabali wenye haki na usawa.

## Kutoka kwa madarasa hadi majumuiya ya wanafunzi

Duniani kote, madarasa yamekuwa maeneo msingi ya kielimu ambapo ufundishaji na ujifunzaji hutokea. Tunapofikiria juu ya kumbi mpya za kujumuisha na kushirikiana, kuna uwezekano wa kuacha wazo la 'chumba' nyuma. Lakini wazo la mwanafunzi kuwa katika jumuiya ya wanafunzi wengine halistahili kupuuzwa.

Mipangilio ya kisasa imezingatia kuwapanga wanafunzi kulingana na umri, uwezo, na jinsia. Tofauti na hilo, walimu wanastahili kuwa na uhuru wa kuwapanga wanafunzi. Wanaweza kuwaweka wanafunzi katika makundi madogo au makubwa. Lakini umuhimu wa kuwa katika kundi au jumuiya ya wanafunzi lazima usisitizwe. Inawezekana kuwa katika shule za kesho, wanafunzi hawatazuiliwa na mipaka ya madarasa iliyopo sasa; wataendelea kushirikiana na wanafunzi wengine katika masomo yao.

> Inawezekena kuwa katika shule za kesho, wanafunzi hawatazuiliwa na mipaka ya madarasa iliyopo sasa; wataendelea kushirikiana na wanafunzi wengine katika masomo yao.

Matarajio ya darasani yanastahili kubadilishwa pia. Katika maeneo mengi, kazi ya watoto na vijana ni kukaa na kufunzwa; hawatoi mchango wowote katika ufundishaji wao. Desturi hii imejikita katika ujenzi wa shule, miundo ya samani na vyombo vingine vinavyotumika darasani. Inaaminika kuwa mwanafunzi aliyenyamaza ana umakini na uwezo mkubwa wa kufanikiwa. Mara nyingi, ufundishaji unalinganishwa na kuimarisha utaratibu na kuzuia kelele na mienendo isiyokubaliwa. Hali ya kutosonga inaposisitizwa wakati wa kusoma, shule na madarasa huwa nafasi za kuchosha zizisopendeza. Umakini unaweza kuleta faida kubwa katika masomo. Lakini tunapaswa kuulizia kama mipango ya madarasa na shule inaweza kufanikisha masomo hayo kwa njia zinazostahili.

Ingawa tunapaswa kulinda nafasi za kijamii zilizo katika shule, hakuna haja ya kufungia elimu ndani ya kuta za madarasa. Elimu inastahili kuwa wazi ili itumie rasilimali za kijamii, kitamaduni na kimazingira. Kufungia elimu katika madarasa hupunguza nafasi na uwezekano wa kujifunza mambo mengi.

## Miundo ya kuimarisha ufundishaji mpana

Mabadiliko yanahitajika katika maagizo na ratiba. Maandalio ya masomo ni muhimu katika kuongoza kundi la wanafunzi na kupanga maudhui. Lakini, maandalio yanayotumika leo hii, yana upungufu mkubwa hasa yanapotafsiriwa kumaanisha shughuli za ufundishaji zinarudiwa kila siku na kila wiki.

Masomo lazima yajumuishe ufundishaji unaotumia mbinu nyingi katika kufanikisha ujifunzaji. Kuna mbinu nyingi ambazo walimu wanaweza kutumia katika kuwafunza wanafunzi wa marika tofauti na kufanikisha ufahamu kuhusu tamaduni zingine. Kwa mfano, ukilinganisha mbinu za kawaida, mbinu zinazolenga miradi na matatizo fulani zina viwango vikubwa vya ushirikiano.

Ufundishaji unaojikita katika utafiti unaweza kuwasaidia wanafunzi katika kupata, kujenga na kutumia maarifa kwa wakati mmoja. Ufundishaji unaozingatia mambo ya jamii na huduma kwa jamii huwawezesha wanafunzi kuwa na ufahamu imara kuhusu dhamira yao maishani. Mabadiliko makubwa yanahitajika katika mpangilio wa shule ndiposa ufundishaji huo ukuze ujuzi na uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana katika hatua zote.

## Dijitali inayosaidia shule

Wakati teknolojia za dijitali zinawaunganisha wanafunzi na wenzao walio na malengo na maswali yanayofanana, kazi ya walimu na shule huimarika. Muunganisho wa kidijitali huongeza uwezekano wa walimu na wanafunzi kufikia maarifa, ujumbe na kazi za usanii kutoka maeneo tofauti ulimwenguni. Ni rahisi kufikia maktaba na majumba ya hifadhi yaliyo katika maeneo tofauti. Vifaa vya kidijitali huwawezesha wanafunzi kutengeneza video, maonyesho, michezo na programu za zinazothibitisha ubunifu wao.Kuna uwezekano mkubwa wa kutumia vifaa vya kidijitali katika kufanikisha masomo yenye ubunifu. Vifaa vya dijitali vimeimarisha mawasiliano kati ya wazazi, walimu na wanafunzi; wazazi wanahusika katika masomo ya watoto wao.

Janga la UVIKO-19 limebainisha kuwa masomo hayawezi tukelezwa kupitia kwa nafasi za dijitali tu. Hata katika maeneo ambayo ni rahisi kupata intaneti na vifaa vya dijitali, masomo ya moja kwa moja yanayotokea shuleni ni ya muhimu sana. Madarasa ya dijitali hayawezi kupatia mwanafunzi faida zote za madarasa ya kawaida.

> Janga la UVIKO-19 limebainisha kuwa masomo hayawezi tukelezwa kupitia kwa nafasi za dijitali tu.

Majaribio ya suluhu tofauti wakati wa janga hilo lililovuruga elimu, yamethibitisha ukakamavu wa walimu na wanafunzi. Kwa mfano, baada ya kutambua kuwa mahitaji ya kibinafsi na ya kijamii yalikuwa ya muhimu zaidi, shule nyingi ziliahirisha mitihani na miongozo ya mitaala kuhusu maudhui ili zizingatie ustawi wa kibinafsi na ujifunzaji halisi. Wazazi walielewa kazi ambayo walimu hufanya wakati wa janga la UVIKO-19. Wengi walichunguza viwango vya juu vya maarifa na ufundishaji ambavyo walimu wanahitaji. Wanafunzi wengine walijisikia vyema kwa sababu ya elimu ya dijitali na ya mbali ; hii inatukumbusha kuwa shule za kesho zinastahili kujikita katika mahitaji ya kijamii, kihisia, kiakili na kimaadili ya wanafunzi.

Kuimarisha kipengele cha maswala ya jamii katika elimu inaamanisha kuongeza masomo kuhusu uraia katika ulimwengu uliounganishwa. Ulimwengu huo unahitaji watu watunzane, waheshimu mitazamo ya wengine na wajihusishe na miradi ya kutunza mazingira yetu. Mbinu za kidijitali pekee, haziwezi kufanikisha malengo haya. Ni muhimu kuwe na masomo ya kushirikiana ndani ya na nje ya shule.

Shule zinastahili kuwa maeneo ambayo yanawasaidia wanafunzi kutambua uwezo walionao badala ya kuwakumbusha upungufu wao wa zamani. Kanuni ya usawa inanuia kuwasaidia wanafunzi kutoka miktadha tofauti wanapojikomboa ili wasiwe watumwa wa matarajio ya watu wengine na wanapotafuta mustakabali ulio bora kushinda maisha ya jana.

Tatizo kubwa la ujifunzaji wa mashine ni kuwa unajenga mustakabali kwa kuangalia yaliyopita. Utafiti unaonyesha kuwa majukwaa ya dijitali yameendeleza dhana potofu, ubaguzi wa jinsia na ubaguzi wa rangi kwa sababu mashine hizo zinafunzwa kwa kutumia data zilizo na dhana hizo zinazopatikana kwa jamii leo hii. Bila shaka, mwanafunzi anatathminiwa na matokeo yake ya kitambo kwa kuzingatia maswali ambayo hakuyafanya vizuri na upungufu wake kutokana na kazi alizokamilisha kitambo. Hii inamnyima mwanafunzi fursa ya kujibadilisha, kukuza maadili kibinafsi na uwezo wa kuwa na ufahamu mpana.

Walimu wanaweza kuwa waratibu wa ujifunzaji wa binafsi ambao hauzingatii upungufu wa kitambo bali unazingatia uwezekano wa mwanafunzi kuendelea kufanya vizuri katika masomo. Mbinu za kidijitali zinaweza kutumika katika aina nyingi za ufundishaji na ujifunzaji. Lakini, ni uhusiano, kati ya walimu na wanafunzi, kati ya wanafunzi na kati ya walimu, unaowaunganisha wanafunzi na maarifa mapana ya binadamu na kuwasadia katika ukombozi wa kiakili ambao ni muhimu katika ujenzi wa mustakabali ulio na haki na uendelevu.

Shule ni mahali wanafunzi wanaweza kufundishwa jinsi ya kuona nafasi na mazingira ya dijitali kama vitu dhaifu vilivyoumbwa na mwanadamu. Mifumo mingi ya elimu imeleta masomo ya usimbaji na kufikiria kwa kikompyuta. Kutumia teknolojia ya dijitali tu hakuwapatii wanafunzi fursa za kuchunguza kwa kina uwezekano unaotokana na teknolojia hizo zinazoweza kupangwa kwa njia ambazo zinaathiri uwezo wetu wa kufikiria. Kwa sababu hizi, teknolojia hizi hazistahili kutumiwa kama mbinu za kufikia malengo ya mitaala; zinastahili kuwa maudhui yanayohitaji kuchunguzwa zaidi. Elimu rasmi inastahili kujumuisha maudhui kuhusu haki za kidijitali, ufuatiliaji, umiliki, madaraka, udhibiti na usalama. Inasemekana kuwa tunaishi katika ulimwengu wa kidijitali, na kwa kiwango kikubwa, huu ni ukweli. Katika nchi zingine mtu wa kawaida hutumia zaidi ya masaa kumi kwa siku kwenye mtandao na teknolojia ya kidijitali. Shule zinapaswa kuwaelimisha wanafunzi jinsi ya kuishi katika mazingira hayo na mbinu za kuyatumia katika kukabiliana na changamoto na kujikuza wao wenyewe. Shule zinastahili kuanzisha maadilli ya kuhamasisha wanadamu ili wadhibiti teknolojia.

## Kujenga tamaduni za ushirikiano

Shule zina uwezo wa kuimarisha ushirikiano, uongozi wa pamoja, ujifunzaji wa pamoja na ukuaji utakaotufikisha kwa mustakabali wa haki na usawa. Ndiposa hili liwe lengo kuu la masomo, lazima uwezo wa walimu, wasimamizi na wafanyikazi wa shule uongezwe. Kuwajibika inamaanisha kufanya zaidi ya kutii kanuni ili wanaohusika waongozwe na malengo ya pamoja yanayotathminiwa. Viongozi wa shule wanapaswa kuimarisha ushirikiano wa kitaaluma, uhuru na kusaidiana katika kuongoza na kudhibiti. Shule zinapoimarisha ushirikiano baina ya wanafunzi lazima ziimarishe ushirikiano baina ya walimu pia. Ushirikiano huo unahitaji tamaduni zinazokuza maendeleo ya kitaaluma ya walimu na ya wafanyikazi wengine wa shule. Shule inaweza kujibadilisha ili iwe taasasi ya ujifunzaji kupitia kwa mbinu kama ufundishaji, ushauri, masomo ya kibinafsi na makundi, utafiti wa kusuluhisha matatizo na ushirikiano baina ya shule na vyuo katika kufanya utafiti.

Hatua hizi zimeanza kutekelezwa ulimwenguni kote na mamilioni ya walimu na shule. Kwa mfano, katika mazingira ya asili, shule zinabadilishwa ili ujifunzaji uzingatie maswala ya tamaduni, maarifa

ya kiasili, lugha tofauti na utafiti. Kwingineko, shule zimeanza kujihusisha na utafiti unaolenga mambo ya jamii. Maendeleo katika elimu ya ufundi yameleta uanafunzi mpya, masomo yenye manufaa na mafunzo yenye ufanisi ambayo yameziba pengo lililo kati ya nadharia na mazoezi.

Tunahitaji shule zinazochangia katika mshikamano wa ulimwengu na zilizo tayari kushirikiana na shule zingine ulimwenguni katika dhamira ya kujibadilisha ili ziwe mandhari na umma na ushirikiano. Shule zina jukumu muhimu katika kuimarisha elimu ili iwe ya manufaa kwa watu wote.

# Kuvuka daraja linalounganisha shule na elimu ya juu

Katika historia, vitivo vya elimu katika vyuo havijapatia elimu ya msingi na upili kipaumbele. Lakini, katika miongo ya karibuni, kumekuwa na ongezeko la ufahamu kuhusu uhusiano kati ya mafanikio ya wanafunzi katika vyuo na elimu ya shule za msingi na upili. Miradi imeanzishwa ili kuimarisha uhusiano huo. Miradi hiyo inalenga masomo ya hisabati, sayansi, fasihi, filosofia na mengineyo. Miradi hiyo inalenga makundi ambayo yamewasilishwa kwa viwango vidogo. Vile vile, watafiti wa vyuo wamekuwa maarufu katika mazungumzo ya elimu.

Maoni kuhusu jukumu la elimu ya juu hayawezi kupuuza uhusiano baina ya elimu ya msingi, elimu ya upili, masomo ya watu wazima na masomo yasiyo rasmi. Maadili ya elimu ya viwango vyote lazima yaunganishwe ndiposa yawasaidie wanafunzi kuimarika tunapoelekea mwaka 2050. Ajenda za kesho za sera zinazolenga elimu ya juu zitahitaji kujumuisha viwango vyote vya elimu na kuangazia mbinu mpya za elimu. Kutambua uhusiano baina ya viwango hivyo kunathibitisha umuhimu wa kufuata mpangilio wa masomo yasiyoisha katika ujenzi wa elimu ya juu ya kesho.

Ushirikiano baina ya shule na vyuo unaweza kuchangia katika kuimarishwa kwa elimu. Wanafunzi wa shule za msingi na upili wanaweza kusaidiwa kwa kutumia maktaba ya vyuo na vifaa vya elimu. Maprofesa wanastahili kuwa tayari kufundisha katika shule za mitaa. Ushirikiano huo utaboresha uwezo wa mifumo ya elimu wa kupata majibu na kuyatekeleza. Vyuo vikuu vina fursa ya kutumia malengo matatu makuu: kufanya utafiti, kufundisha na kuhamasisha ili kusaidia umma kwenye harakati za sasa hivi.

Ajenda za kesho za sera zinazolenga elimu ya juu zitahitaji kujumuisha viwango vyote vya elimu na kuangazia mbinu mpya za elimu.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii inapendekeza kuwa katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, shule zinastahili kuwa maeneo ya elimu yanayolindwa kwa sababu zinasaidia katika kuleta ujumuishaji, usawa na ustawi wa kibinafsi na wa pamoja. Vile vile, shule zinahitaji kubadilishwa ili zilete mabadiliko ya haki, usawa, na mustakabali ulio endelevu. Tunapoelekea mwaka 2050, kuna kanuni nne zinazoweza kutoa mwongozo wa mazungumzo na hatua za kufanikisha pendekezo hilo:

- **Shule zinastahili kulindwa kama maeneo ambayo wanafunzi hukumbana na changamoto na fursa ambazo hawawezi kuzipata mahali pengine.** Kama hakungekuwa na shule leo hii, ingetulazimu tuzibuni. Tunapaswa kuhakikisha kuwa shule zinawaleta watu tofauti pamoja ile waweze kufundishana.
- **Ujenzi wa uwezo wa pamoja unastahili kuongoza mabadiliko katika shule.** Majengo ya shule, nafasi, nyakati na makundi ya wanafunzi yanapaswa kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa kufanya kazi pamoja. Tamaduni za ushirikiano zinastahili kutawala uongozi wa shule na uhusiano baina ya shule tofauti.
- **Teknolojia za kidijitali zinastahili kutumika katika kukamilisha masomo, sio kuchukua nafasi ya shule.** Vyombo vya kidijitali vinastahili kutumika katika kuboresha ubunifu na mawasiliano ya wanafunzi. Wakati teknolojia kama Akili Mnemba na aligorithmu za kidijitali zinatumiwa shuleni, tunapaswa kuhakikisha kuwa haziendelezi dhana potofu na mifumo ya ubaguzi.
- **Shule zinastahili kuwa modeli za mustakabali tunaoutamani kwa kutoa mfano mwema katika maswala ya haki za binadamu, uendelevu na kudhibiti viwango vya kaboni.** Wanafunzi wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika miradi ya kuleta uendelevu kwenye sekta ya elimu. Tunastahili kuhakikisha kuwa sera za elimu zinaunga mkono haki za binadamu.

Tunapoendelea kujenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu, kila mtu anastahili kupata motisha kutoka kwa kanuni hizi za kubadilisha shule ambayo ni mojawapo ya taasisi muhimu na yenye nguvu katika maswala ya elimu.

# Sura ya 7

# Elimu katika nyakati na nafasi tofauti

Jiji huelimisha kupitia kwa ujifunzaji, ufundishaji, kujua, kuumba, kuota, na kufikiria kuwa sisi zote – wanaume na wanawake – tunaoishi kwenye nyanja, milima, mabonde, mito, mitaa, chemichemi, nyumba, na majengo, huacha stempu ya mitindo na mielekeo ya enzi fulani . . .
Jiji ni sisi na sisi ndio Jiji.

**Paulo Freire,** *Politics and education,* 1993.

**Katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, lazima tufaidike na tukuze fursa za kielimu zinazostawisha. Fursa hizo hutokea katika hatua zote za maisha na katika nafasi tofauti za kitamaduni na kijamii.**

Watu wengi wanafikiria kuwa elimu ni ya watoto na vijana na kuwa lengo la elimu ni kuwatayarisha kwa maisha ya utu uzima. Katika mazungumzo mengi ya umma, elimu inalinganishwa na taasisi za kipekee zilizo mbali na familia na jamii za wanafunzi. Mazingira ya kipekee yamesaidia katika kulinda nyakati na nafasi za ufundishaji na ujifunzaji wa pamoja. Elimu shuleni imekuwa tukio la nyakati lililo na sifa za kipekee. Kupatia watoto na vijana kipaumbele ni nguzo ya kuendeleza usawa na upatikanaji wa fursa.

Lakini, wakati mazungumzo ya elimu yanalenga taasisi rasmi tu, nafasi nyingi za elimu zilizo katika jamii hufungiwa nje. Kanuni ya msingi ambayo imependekezwa kwenye ripoti hii ni upanuzi wa haki ya elimu. Kanuni hii inatambua kwamba ujifunzaji hauna kikomo; elimu lazima iendelezwe wakati wote na katika nafasi tofauti. Kanuni hii inalenga sehemu zote za maisha ya jamii - miji, vijiji, maadili ya nchi, mifumo ya tamaduni, majumuiya ya maeneo na ya kimataifa. Tuna fursa za ufundishaji na ujifunzaji katika kazi, utunzaji, mapumziko, shughuli za kisanii, tamaduni, michezo, maisha ya jamii, harakati za umma, miundombinu na teknolojia. Mkataba mpya wa kijamii wa elimu lazima uzingatie ujifunzaji unaotokea katika nyakati na nafasi zote.

Mojawapo ya kazi yetu ni kupanua mawazo kuhusu mahali na nyakati elimu inatokea. Changamoto hii ya dharura ilizungumziwa miaka 50 iliyopita kwenye Ripoti ya Tume ya Faure ambayo ilieleza dhamira ya *Cité* éducatif: kubadilisha mifumo ya elimu. Jina jiji limetafsiriwa katika lugha nyingi. Katika lugha ya Kiswahili, jiji linamaanisha 'shirika la ujifunzaji.' Hapa 'jiji' ni sitiari ya nafasi inayojumuisha uwezekano na uwezo kama vitu vilivyounganishwa. Sitiari hii inasisitiza umuhimu wa kuzingatia nafasi na aina zote za shughuli za kijamii zinazoweza kuboresha elimu.

Kwa kawaida, elimu huanzia umri wa miaka tano au sita na kuisha baada ya miaka kumi. Juhudi za miaka ya nyuma zimechangia katika kujumuisha kwa watoto waliochini ya miaka mitano na watu wazima katika elimu. Ingawa elimu ya chekechea ni kiwango huru katika elimu, mara nyingi inaangaliwa kama hatua inayowatayarisha watoto kwa ajili ya masomo ya msingi. Nchi nyingi zimeleta sera za kuimarisha elimu ya watu wazima ili kuwapatia fursa za kuongeza ujuzi wao. Fursa hizo zinaangaliwa kama muendelezo wa shule.

Mifumo ya elimu iliyojikita katika 'muundo wa shule' ilipunguza uwezekano wa kuwa na aina nyingine za elimu. Ni kweli kuwa hatua za kupanua 'muundo wa shule' zimekumbwa na upinzani mkubwa.

Katika elimu ya chekechea upinzani huo unadhihirishwa na mbinu za elimu zinazolenga majaribio, ustawi na maswala ya hisia na uhusiano. Wengi wanaamini kuwa miundo ya elimu ya chekechea inastahili kuwa wazi na yenye kuzingatia nafasi na nyakati zote.

Kuhusu elimu ya watu wazima, kumekuwa na mapendekezo ya kuibadilisha elimu hiyo ili isifuate muundo wa shule rasmi. Mapendekezo hayo yamesisitiza umuhimu wa kuheshimu uhuru na kazi ya watu wazima ndiposa waweza kuendeleza masomo yao nje ya mifumo ya shule rasmi. Haya ni

mapendekezo yanayoweza kuleta ukombozi na kubadilisha uhusiano baina ya watu wazima na elimu kwa kupigana dhidi ya mifumo ya udhalilishaji, ukandamizaji na ukoloni.

Licha ya upinzani huo, hatuwezi kusema kuwa 'muundo wa shule' haujapanua elimu ya chekechea na elimu ya watu wazima hasa kwa kuimarisha ujifunzaji katika hatua zote za maisha. Tunapofikiria juu ya elimu ya mwaka 2050, ni sharti tufahamu umuhimu wa nafasi, nyakati na aina zote za elimu. Lakini hii haimanishi kuwa ulimwengu wote unahitaji kubadilishwa ili uwe darasa moja kubwa. Mabadiliko tunayopaswa kuwa nayo katika kufikiria kwetu yanastahili kulenga fursa za kielimu zilizo katika tamaduni, kazi, mitandao ya kijamii, na ulimwengu wa kidijitali. Kwa miaka 30 inayokuja, dhamira ya mkataba mpya wa kijamii wa elimu itakuwa kuongeza ufahamu kuhusu uhusiano baina ya elimu na maisha. Kwa hivyo, tunapolinda shule kama nafasi na nyakati za kipekee za elimu, lazima tupanue taswira yetu ili ijumuishe nafasi na nyakati zote katika maisha.

Kwa hivyo, tunapolinda shule kama nafasi na nyakati za kipekee za elimu, lazima tupanue taswira yetu ili ijumuishe nafasi na nyakati zote katika maisha.

Sura hii inaanza na maelezo kuhusu aina nyingi za nafasi na fursa za elimu ambazo zinaweza kutumika katika kuimarisha ujumuishaji na uwezo wa kukabiliana na changomoto mpya. Pili, sura hii inafafanua jukumu la serikali la kuimarisha haki ya elimu na umuhimu wa kudhibiti nafasi za dijitali ili teknolojia itumiwe katika kubadilisha elimu kwa njia ambazo zitatufaidi siku zijazo. Biosfera ni nafasi muhimu ya elimu isiyostahili kupuuzwa. Sura hii inahitimisha na kanuni za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu tunapoelekea 2050. Hatua hizi zitakuwa za manufaa kwa serikali na mashirika ya kijamii kwa vile zinaanganzia maswala ya ujumuishaji katika elimu ya watu wazima; kubadilishwa kwa nafasi za ujifunzaji; koberesha ufadhili; na upanuzi wa haki ya elimu.

# Kuimarisha ujumuishaji na uendelevu wa fursa za elimu

Ndiposa utawala wa elimu ufanye kazi bora, lazima utambue kuwa taasisi za elimu, mashirika ya kijamii na mahusiano ya muda mfupi ni vitu vilivyo kila mahali na vinaweza kupanda au kushuka. Wadau wote wanaweza kujitolea katika miradi ya ujumuishaji na uendelevu ikiwa kuna ushirikiano na ahadi za kuhakikisha kuwa fursa za kielimu, ziwe rasmi au ziziso za rasmi, zinawafikia watu wote.

Maadili ya ujumuishaji yanahitaji kuzingatiwa katika utawala wa elimu. Ujumuishaji unastahili kuanza na wale watu ambao wametengwa na walio kwenye mazingira hatari. Matokeo ya kutozingatia maadili ya ujumuishaji ni mifumoikolojia ya elimu iliyo hafifu. Maswala ya mamlaka, ufanisi, unyonyaji na ukandamizaji yanaweza kuathiri uhusiano wa kielimu. Mara nyingi, miundo ya elimu na taasisi za elimu huchangia kutofaulu na ubagazi dhidi ya makabila, watu wa asili na makundi mengine yaliyotengwa. Wakimbizi na walio na ulemavu hawapati huduma bora. Mtazamo mpana wa elimu unazingatia uhusiano baina ya taasisi, wadau na nafasi; hii inamaanisha kuwa hatuwezi kupuuza kutofaulu kwa elimu.

## Jukumu la serikali

Ulimwenguni kote watu wamekubaliana kwamba elimu ni haki muhimu na mataifa yote yana jukumu la kuhakikisha watoto, vijana na watu wazima wote wanaipata. Kwa hivyo, serikali lazima ziwajibike katika jukumu lao la kuendeleza mifumoikolojia ya elimu.

Haki ya kupata elimu, inayopatikana katika Kifungu cha 26 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu, imejumuishwa katika mikataba mingine inayofunga mataifa kisheria. Mikataba hiyo ni kama Mkataba wa 1960 dhidi ya Ubaguzi katika Elimu (CADE) na Kifungu cha 13 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni wa 1966 (ICESCR). Katika mkataba huo wa pili, mataifa yamekubaliana kuwa elimu itawawezesha watu wote kushiriki katika shughuli za jamii na itaimarisha uelewano, stahamala na urafiki kati ya mataifa.

Kulingana na sheria za kimataifa, mataifa yana jukumu la kupatiana elimu ya shule ya msingi ya bure na ya lazima. Aina zote za elimu ya shule ya upili zinastahili kupatikana kwa urahisi na watu wote. Elimu ya juu inastahili kupatikana na watu wote kulingana na uwezo wao. Mataifa yana majukumu matatu yaliyo na uhusiano na haki ya kupata elimu: kutimiza, kuheshimu na kulinda. Jukumu la *kutimiza* linajumuisha kuwezesha na kupatiana elimu. Jukumu la *kuheshimu* linalenga kulinda haki hiyo dhidi ya vitu vinavyoweza kuchangia kudhoofika kwake. Mwisho, mataifa yana jukumu la kulinda haki hiyo ili isiingiliwe na watu wasio na nia nzuri.

Haki ya kupata elimu inahusiana na haki zingine za binadamu. Kama wadhamini wa haki za binadamu, mataifa yana jukumu la kufanya juhudi katika kujenga mazingira yatakayoimarisha ujifunzaji wa watoto na vijana. Hii inamaanisha kuhakikisha wanapata haki za msingi kama haki ya kupata maji na huduma za usafi, chakula na lishe bora, ulinzi wa kijamii, kuishi katika mazingira ya kifamilia na ya kijamii yanayoleta ustawi wa kihisia na kimiwili na haki ya kuishi bila ya aina zote za ukatili.

Tangu mwaka wa 2000, waandishi maalumu wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki ya Elimu wamekuwa wakiita elimu rasilimali ya umma inayolinda maslahi ya jamii. Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa linatambua kuwa elimu ni rasilimali ya umma katika maazimio yake ya 2005 na 2015 kuhusu haki ya kupata elimu. Mwaka 2015, wawakilishi kutoka zaidi ya mataifa 160 walihudhuria Kongamano la Uchumi wa Dunia ambako waliidhinisha *Elimu ya 2030: Azimio la Icheon na Mfumo wa Utekelezaji*. Ripoti hiyo inathibitisha kuwa elimu ni haki muhimu kwa binadamu wote na ni dhamana ya haki zingine. Inasisitiza kuwa 'elimu ni rasilimali ya umma, na kila serikali ina wajibu wa kupatiana hiyo rasilimali'; serikali ni muhimu katika ujenzi na utekelezaji wa viwango na kanuni.

Serikali zina jukumu la kuhakikisha kuwa elimu ni rasilimali ya umma katika mifumoikolojia yote ya elimu. Kama tulivyoeleza hapo awali, tunahitaji mbinu inayojumuisha kila mtu. Shughuli ya kubadilisha elimu ili iwe rasilimali ya umma inalenga walimu wote, shule zote na programu zote za elimu. Na inastahili kukumbukwa kuwa mara nyingi wadau wa serikali na wasio wa serikali hushirikiana katika kuimarisha elimu ya umma.

Serikali zina jukumu la kuhakikisha kuwa mifumo yote ya elimu inapata ufadhili wa kutosha na inaweza kutosheleza mahitaji ya wananchi wanaoitegemea. Lazima zitafute ufadhili wa kutosha

kwa kutumia sera za ushuru zinazowalenga mabwenyenye wanaoficha mali yao katika paradiso za kodi.

Serikali zina jukumu muhimu la kuhakikisha kuwa wale wadau wanaopatiana elimu wanaheshimu haki za binadamu na shughuli zao za kielimu ni bora na hazihatarishi maisha ya wanafunzi.

Mwisho, lazima serikali zihakikishe kuwa elimu inashughulikia mahitaji ya wananchi na wale wanaoishi katika mipaka ya nchi hasa wale ambao wamekuwa wakitengwa kwa muda mrefu. Utawala mzuri wa elimu unahitaji wananchi na wadau wengine wahusishwe katika maamuzi na mazungumzo; hii inamaanisha lazima viwango vya uwazi na uwajibikaji viwe vya juu.

Kuhusu watu wa asili, kuna masharti zaidi. Azimio la Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Watu wa Asili linaeleza kuwa zaidi ya kuhakikisha kuwa watu wa asili wanapata haki ya elimu katika viwango vyote, watu wa asili wana 'haki ya kuanzisha na kudhibiti mifumo ya elimu na taasisi zinazopatiana elimu kwa kutumia lugha zao na kwa njia ambazo ni sambamba na tamaduni zao za ufundishaji na ujifunzaji.'

Idadi ya watu wanaolazimishwa kuhama imeongeza ulimwenguni kwa sababu kama athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Lazima wakimbizi wasiopata msaada kutoka kwa serikali washughulikiwe. Haki ya elimu katika hali hizo inaweza kulindwa kupitia kwa ushirikiano wa kimataifa na ufadhili kutoka kwa mashirika ya kimataifa.

## Kutawala nafasi za ujifunzaji za kidijitali

Ikitumika inavyostahili, teknolojia inaweza kusaidia katika upatikanaji, ujumuishaji na malengo mengine ya kawaida ya elimu. Ingawa kuna teknolojia zingine zenye uwezo za kuleta ukombozi, zingine zinaweza kuleta hatari. Kwa hivyo, 'mvuvumko wa dijitali' sio tofauti na mivuvumko ya kilimo au viwanda. Maendeleo ya hapo awali yamechangia katika ongezeko la ukosefu wa usawa na utengwaji wa watu wengine. Changamoto tuliyonayo ni ya kukabiliana na matokeo hayo.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa maamuzi kuhusu utumiaji kwa teknolojia za kidijitali katika elimu yanahusisha umma na yanaongozwa na kanuni ya elimu kuwa rasilimali ya umma. Hii inamaanisha kuangazia ubinafsishaji wa miundombinu ya dijitali na kupambana dhidi ya kudhibitiwa kwa maarifa ya jamii ya kidijitali, hasa yale yanayotumika kwa mifumoikolojia ya elimu, kwa njia ziziso za demomkrasia.

Ingawa majukwaa ya kidijitali yamechangia katika maarifa, elimu na utafiti kwa miongo iliyopita, faida za kijamii zimekuwa kidogo ukilinganisha na zile faida makampuni ya teknolojia yanapata kutoka kwa matangazo ya biashara. Kwa mfano, kampuni ya Google imekuwa mojawapo ya wapatanishi katika ulimwengu wa dijitali na inaendelea kueneza mizizi yake katika maisha ya umma ya kidijitali. Baadhi ya huduma za kielimu ambazo Google hupatiana ni Google Scholar na Google Classroom ambazo hazileti faida kubwa za kifedha kwa Google. Kuna athari nyingi zinazoweza kukumba mifumo ya dijitali ambayo inategemewa na elimu.

Google imeanzisha huduma zingine nyingi kwa sababu mbalimbali; tuna haki ya kuwa na tashwishi kuhusu hali ilivyo kwa sasa. Kufungwa kwa vyuo vikuu miaka ya 2020 na 2021 kwa sababu ya UVIKO-19 kulimaanisha kuwa hata wataalamu kutoka vyuo vikuu bora zaidi ulimwenguni, na vyenye uwezo mkubwa wa kifedha, walitegemea maamuzi ya ndani ya Google ili kupata huduma kama Google Scholar. Tangu kuanzishwa kwake, Google Scholar haijafanyiwa mabadiliko mengi na hakuna kazi mpya zimeongezwa kwake; hii inamaanisha kuwa Google Scholar haijapatiwa kipaumbele katika ajenda ya kampuni. Hili ni onyo kwetu kuhusu udhaifu wa mifumo ya ujifunzaji ya kidijitali inayotawalwa na makampuni ya kibinafsi. Tunapaswa kuuliza kama kuna mifumo mingine ya kidijitali ya kudumu inayoweza kutusaidia katika elimu ya umma ya kesho.

Uwezekano wa kuwa na majukwaa ya dijitali ya bure unategemea uchimbaji, wa viwango vya juu wa data za kibinafsi, ambao umelinganishwa na 'aina mpya ya mafuta.' Mwanzoni, data hiyo ilitumiwa katika shughuli za matangazo ya biashara. Baadaye, iligunduliwa kuwa data hiyo haitumiwi katika kuimarisha bidhaa na shughuli za kibishiara tu, bali katika kushawishi mawazo na mapendeleo kupitia kwa Akili Mnemba na ujifunzaji wa mashine.

Huo ulikuwa mwanzo wa mashindano makubwa baina ya makampuni makubwa ulimwenguni, kila moja ikilenga kuibuka mshindi kwa kuwa na sehemu kubwa ya soko la Akili Mnemba. Kwa sababu hiyo, uchumi wa kidijitali unaongozwa na lengo la uchimbaji wa data, sensa, alighorithimu, mitandao, vifaa vya kusoma vitabu vya dijitali, vivinjari na saa zinazotumia Akili Mnemba. Wazo kuwa tunaishi katika nyakati ambazo tunafuatiliwa wakati wote linaweza kuwa na athari za kisiasa. Wazo hilo huathiri uhuru wa kujieleza na hisia kuhusu uhuru wa kiakili. Wasiwasi unaotokana na kufuatiliwa huzuia shughuli za ubunifu kwa sababu unawafanya watu kuogopa kuwa sifa zao zinaweza kuharibika ikigunduliwa kuwa wanasoma vitabu fulani. Sifa zetu zinategemea matendo yetu katika ulimwengu wa dijitali.

Athari za wasiwasi huo zinaweza kutokea wakati ufuatiliaji na uchimbaji wa data unafanyika katika mifumoikolojia ya elimu. Kufanya ufuatiliaji jambo la kawaida - hasa mifumo ya elimu inapowafanya watoto kukubali ufuatiliaji huo kutoka umri mdogo - unatuelekeza katika njia itakayomalizia katika mmomonyoko wa adhama ya kibinadamu na ukiukaji wa haki za faragha na kujieleza ambazo zinapatikana katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu.

Swala la usalama wa data za wanafunzi na walimu linastahili kuangaziwa katika mazungumzo yote kuhusu jukumu la majukwaa ya kidijitali katika mifumoikolojia ya elimu. Urahisi wa kujumuisha data, kuihifadhi na kufuatilia nafasi za kidijitali unaweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Sheria imara na itifaki zinahitajika ili kulinda wanafunzi na walimu. Maadili ya uwazi yanastahili kuongoza sera za data na chaguo msingi ili kuhakikisha mwenye data hajulikani ndiposa watu binafsi wasihatarishwe.

Sababu moja ambayo imefanya umaarufu wa majukwaa ya kidijitali na mbinu zao za aligorithimu kuenea hadi kwa mifumoikolojia ya elimu ni ukosefu wa suluhu mwafaka kuhusu jinsi ambavyo maarifa ya ulimwengu, yanayoongezeka kwa kasi mno, yanastahili kujumuishwa na kupangwa kwa ufasaha. Kwa sababu hiyo, hata wataalamu wanalazimika kutegemea huduma za majukwaa ya dijitali. Majukwaa hayo huathiri uhuru wa maoni ya wataalamu hao kwa kutumia aligorithimu za kujumuisha na kupanga. Kupata majibu ya kudumu kwa shida kama 'habari za uongo' na janga la

imani katika sayansi na taasisi za umma kunahitaji tuboreshe uhusiano wetu na ukweli, utaalamu na demokrasia katika ujumuishaji na upangaji wa maarifa.

Mifano hii inasisitiza udhaifu wa miundombinu ya elimu ya dijitali. Ingawa vifaa bora zaidi vinaweza na ni lazima vitengenezwe, mbinu mwafaka ya kutumia mabadiliko ya kidijitali katika kuimarisha elimu ili iwe rasilimali yenye kuleta manufaa kwa watu wote ni kuhakikisha kuwa kuna demokrasia katika nyanja za umma. Jamii nyingi za kidijitali na teknolojia za mtandao za kwanza ziliundwa kwa kutumia teknolojia wazi na kupitia kwa ushirikiano. Ndiposa teknolojia ya kidijitali ya elimu iimarishe uendelevu, haki, na ujumuishaji lazima wadau kama serikali, mashirika ya kijamii na umma wajitolee kubadilisha elimu iwe rasilimali ya umma na sio bidhaa ya kuuzwa kwa ajili ya faida. Elimu inastahili kuwa kama uwekezaji utakaopatia umma faida ya mustakabli endelevu, wenye haki na amani.

Mbinu mwafaka ya kutumia mabadiliko ya kidijitali katika kuimarisha elimu ili iwe rasilimali yenye kuleta manufaa kwa watu wote ni kuhakikisha kuwa kuna demokrasia katika nyanja za umma.

## Kujifunza kuishi na sayari iliyo hai

Lazima tupanue mawazo yetu kuhusu mahali ambapo ujifunzaji unaweza kutokea. Kando na taasisi na nafasi zilizo na watu, ujifunzaji unaweza kutokea katika bustani, mitaa ya majiji, njia za vijiji, mashamba, majangwa, misitu, nyika, maziwa, mabwawa, bahari, na maeneo mengine ambayo viumbe wengine huishi.

Binadamu ni sehemu ya Dunia iliyo hai. Tamaduni nyingi za asili zimelenga kukuza uhusiano mwema baina ya binadamu na viumbe wengine. Biosfera ina mafunzo muhimu. Uhakika wa kwamba ardhi ya watu asili, inayosimamiwa na serikali, ina takribani 80% ya bioanuwai ya Dunia unaonyesha kuwa maarifa ya asili yanaweza kufunza watu wote jinsi ya kulinda sayari.

Maarifa ya asili kuhusu ardhi, maji na kosmolojia za Kiafrika na Kiasia zinaeleza kuwa katika uhusiano baina ya binadamu na viumbe wengine; viumbe hao wengine wana haki na ni walimu wenye wanaweza kuelimisha binadamu. Kwa tamaduni zingine, viumbe hao wengine wanaheshimiwa kwa sababu ya umri na busara yao ; inatambuliwa kuwa wana mengi ya kutufunza.

Desturi za elimu ya Magharibi zimeangazia maswala haya kwa muda mrefu. Nyanja za elimu zimejumuisha mazingira na ulimwengu wa asili katika mikakati ya ujifunzaji. Ripoti hii imesisitiza kuwa mazingira ni muhimu kwa ujifunzaji wa wanafunzi. Wanafunzi wanaweza kujifundisha mengi kupitia kwa mazingira. Mara nyingi, kutegemeana baina ya binadamu na mazingira kumepuuzwa. Pia, viumbe wengine hawatambuliwi kama walimu.  Hivi karibuni, aina nyingi za elimu kuhusu mazingira zimetupilia mbali msimamo huo. Sitiari ya elimu iliyo mwitu inayozingatia uhifadhi na urejesho wa mazingira ni thibitisho la uwezekano wa kujenga elimu kwa njia mpya.

Ufundishaji unaoibuka kutoka kwa mazungumzo kati ya miundomsingi ya maarifa na kosmolojia unaleta matumaini kuhusu uwezekano wa kubadilisha uhusiano baina ya elimu na sayari iliyo hai. Binadamu wanapaswa kuelewa kuwa wao sio viumbe wa kijamii tu, bali ni viumbe wa kiikolojia.

Kanuni za utunzaji wa mazingira zinazoeleza kuwa sisi ni 'watunzaji' na 'walinzi' wa ulimwengu wa asili zinatambua tofauti baina ya binadamu na mazingira yao. Mawazo yetu kuhusu ikolojia yanastahili kutuweka ndani ya sayari iliyo hai.

Majanga ya kiikolojia ambayo yamekuwa yakisababishwa na binadamu yanahitaji mabadiliko yanayolenga mwanafunzi ambaye anahitaji elimu itakayosaidia katika malengo ya jamii. Elimu haistahili kulenga mwanafunzi mwenye mtazamo wa kiulimwengu ambaye ametosheka na ulimwengu uliounganishwa - yaani mwanafunzi wa karne ya ishirini na moja ambaye elimu yake ni juu ya maendeleo ya binadamu tu. Ndiposa elimu isaidie katika ujenzi wa mustakabli ulio wa haki na uendelevu, lazima tuhamasishe ufahamu wetu kuhusu sayari. Mwanafunzi anayejihusisha katika ujenzi wa ulimwengu lazima awe kitovu cha elimu. Wazo hili ni muhimu katika uendeshaji wa elimu ya nyanja zote.

Ndiposa tusawasishe uhusiano wetu wa sayari iliyo hai, lazima tujifunze upya kuhusu kutegemeana kwetu na tupate mawazo mapya kuhusu jukumu la binadamu. Tamaduni nyingi zimejua kwa karne kadhaa kuwa binadamu hawawezi kutengwa kutoka kwa sayari. Kwa mfano, dhana ya 'Sumak Kawsay' ya Quenchua inatambua haki za ulimwengu wa asili na kufafanua jinsi ya kuishi kwa njia ambazo haziharibu ikolojia. Kanuni za uhusiano (Mimi nipo kwa sababu tupo) zinazosisitizwa katika filosofia ya Ubuntu ya Wanguni, ambao ni Wabantu inaweza, kuleta faida nyingi kama ile ya Wabudha inayoitwa Karuna (huruma). Hii ni mifano miwili ya rasilimali za kitamaduni zinazoweza kuwanufaisha binadamu wote.

Jamii zingine zinaendelea kujifunza, kupitia kwa uchungu mwingi, kuhusu kutegemeana baina ya binadamu na sayari. Je, kufikia mwaka 2050, tutawezaje kuishi kama viungo vya Dunia kwa kutumia maadili ya maelewano, ustawi na haki? Bado, hatujapata majibu ya swali hili. Elimu inayozingatia jumla ya maisha ni mojawapo ya vyombo vitakavyo tusaidia kutafuta majibu kwa pamoja.

# Kufafanua swali la 'ni wapi' elimu hutokea

Kwa sababu watu wengi wanazidi kuishi maisha marefu na yenye afya zaidi, uhusiano baina ya elimu na maisha utabadilika. Wakati kuna mabadiliko katika viwango vya watu wanaofanya kazi na wazee na viwango vya wanaopata na wasiopata mshahara, mahitaji, vipaumbele na taratibu za elimu hubadilika pia. Kwa hakika, maswala haya yanaonyesha dhana ambazo hutawala mawazo ya jamii kuhusu uzalishaji.

## Elimu na utunzaji katika hatua zote za maisha

Imeendelea kutambuliwa kuwa ustawi na usalama wetu wa kiuchumi hautegemei uchumi rasmi pekee. Kazi ya kulipwa ni sehemu moja tu. Kazi inayofanywa majumbani ya kuwatunza watu ni muhimu pia. Hii inajumuisha kazi ya kuwatunza watoto na wazee, kuzalisha na kutayarisha chakula, kutafuta maji na kujenga makazi katika mazingira yenye changamoto za kiikolojia. Wanawake hubeba mzigo mkubwa wa kuhakikisha kuwa familia na jamii zimetunzwa, kuna chakula cha

kutosha na watu wanapata mahitaji ya kiafya. Licha ya mchango wao, hawatambuliwi wala kupatiwa ufadhili wa kutosha.

Katika miaka 30 ijayo, uhusiano baina ya shughuli hizi za 'utunzaji' utabadilika kwa njia nyingi. Katika maeneo mengine, wazee watafanya kazi kwa muda mrefu kwa sababu ya kuimarika kwa afya na ukosefu wa wafanyikazi. Katika maeneo mengine kutakuwa na changamoto za kuwatunza wazee na watoto wachanga kwa sababu idadi ya wanawake wanaofanya kazi itaongezeka; hali hii imekuwa ikishuhudiwa kwa miongo mitatu iliyopita. Aina mpya za mipangilio ya familia zitaibuka kwa sababu ya jukumu la kuwasaidia watu wa ukoo. Hii inamaanisha kuwa wanafunzi wa vizazi tofauti wanahitaji elimu kuhusu ujenzi wa uhusiano unaodumu na utunzaji wa watu wengine.

Kuna mambo mengi yanayohitaji kufanywa zaidi ya kujifunza juu ya utunzaji na kuhakikisha kuwa elimu ina maudhui ya utunzaji. Tunapoangalia mwaka 2050 na miaka itakayofuata, tunaona ugumu wa swala hili. Lazima tuendeleze elimu inayolenga maswala ya kutayarisha na kukuza chakula na kutunza familia. Huu ni mtazamo mpana unaoboresha ufahamu wetu kuhusu uhusiano baina ya maisha na elimu inayoendelezwa katika nafasi na nyakati tofauti.

## Ujifunzaji na elimu ya watu wazima kama mradi wa ukombozi

Katika miongo ya karibuni, kanuni ya ujifunzaji usiokwisha imekuwa nguzo ya sera za elimu ulimwenguni. Kwa mfano, Lengo la nne la Maendeleo Endelevu linatuagiza 'tuhakikishe kuna elimu bora, jumuishi na yenye usawa, na tuimarishe nafasi za ujifunzaji katika hatua zote za maisha.'

Kupitia kwa ujifunzaji na elimu, watu wazima hukombolewa ; ukombozi huo unadhihirishwa katika kuboreshwa kwa uwezo wao na ushirikishwaji katika maswala ya kiraia. Katika miaka ya karibuni, dhamira hii imefifia kwa sababu juhudi zote zimeenda kwa ujifunzaji wa ufundi na ujuzi. Kwa sababu hiyo, mojawapo ya haki ya watu wazima - hasa wale ambao hawajawahi kupata elimu yoyote maishani mwao - ilibadilika ikawa 'jukumu' la kuwasaidia watu kuongeza uwezekano wao wa kuajiriwa na uwezo wa kufanya kazi. Matokeo yake ni dhamira ya kukuza ujuzi tu.

Ujifunzaji na elimu ya watu wazima unastahili kuwa tofauti. Mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanamaanisha kuwa elimu ya watu wazima inastahili kupanuliwa ili iangazie maswala zaidi ya yale yanayohusiana na malengo ya kikazi. Fursa za kubadilisha taaluma na kuongeza ujuzi zinastahili kuwa sambamba na mabadiliko ya miundomsingi ya kielimu yanayosisitiza ujuzi wa njia nyingi zinazoweza kubadilishwa. Kama elimu katika nyanja zingine, elimu ya watu wazima inastahili kupangwa upya ili ujifunzaji ulete mabadiliko halisi. Tunatarajia mabadiliko makubwa katika elimu ya watu wazima miaka ya mbeleni hasa kuanzia 2050. Wengine wanatabiri kuwa binadamu wataanza kuishi zaidi ya miaka 100.

Elimu ya watu wazima inastahili kupanuliwa ili iangazie maswala zaidi ya yale yanayohusiana na malengo ya kikazi.

Tukiachana na swala la maisha marefu, lazima tuendelee kufikiria upya kuhusu swala la mahali elimu inastahili kutokea. Katika maeneo mengi, kutakuwa na vizazi vinne vinaishi pamoja kwa njia ambazo hatujawahi kushuhudia katika historia. Dhana za kitamaduni kuhusu utu uzima hazitasalia

zilivyo sasa. Kutakuwa na mabadiliko katika njia za kuishi, uhusiano na kazi na burudani. Kama hali ilivyo sasa, mtu anaweza kubadilisha kazi mara kadhaa katika maisha yake. Tunapaswa kutambua kuwa maisha ya kiraia na kisiasa yanaweza kubadilika mara nyingi; mabadiliko haya yataongezeka katika siku za usoni. Ufahamu mpya wa mazingira unaosisitizwa kwenye ripoti hii ni baadhi ya maswala mapya ya kielimu yanayostahili kusomwa na wanafunzi wa marika yote. Karne ya ishirini na moja inapoendelea, sera za kielimu zinastahili kuzingatia hatua zote za maisha na mahitaji ya watu wazima na wazee.

Jambo la pili, ambalo ni kipengele muhimu zaidi katika desturi ya ujifunzaji usiokwisha, ni ushirikishwaji na ujumuishwaji wa watu ambao wamekuwa wakitengwa na kunyimwa fursa za elimu. Ushirikishwaji na ujumuishwaji huenda sambamba na lengo la kukomboa kwa kutumia elimu ya watu wazima; lengo hili linasisitiza masomo yasiyo rasmi - maarifa na uwezo unaopatikana nje ya mazingira ya shule. Sera za elimu ya watu wazima lazima zitambue ujifunzaji katika hatua zote za maisha kama njia ya kuboresha ujumuishwaji na ushirikishwaji.

Mwisho, wanaoshughulikia elimu ya watu wazima wanapaswa kutafuta mbinu za kuimarisha ushirikishwaji kwa kutumia mbinu za kidijitali. Ingawa vizazi vichanga huanza kupata uzoefu wa ulimwengu wa kidijitali mapema katika maisha yao, vizazi vya watu wazee vinahitaji kufunzwa kuhusu teknolojia hizi mpya. Elimu ya watu wazima inastahili kuimarisha upatikanaji na uwazi wa teknolojia za kidijitali. Kuboresha maarifa ya kisayansi na kukabiliana na aina zote za habari potofu ni vipengele muhimu katika mikakati, ya sasa na ya siku za usoni, ya elimu ya watu wazima.

Ujifunzaji wa watu wazima na elimu yao hutimiza malengo mengi. Ujuzi na uwezo wa kukabiliana na shida huimarika kwa sababu ya ujifunzaji na elimu. Vile vile, watu huwajibika kwa swala la mustakabali na kuelewa mabadiliko ya dhana kwa njia ambazo zinachangia katika ujenzi wa ulimwengu ulio wa haki na uendelevu. Elimu ya watu wazima inastahili kuwa elimu ya wakati wote iliyo na uhusiano mkubwa na maisha. Watu wazima wana jukumu la kulinda ulimwengu wanamoishi kwa sasa na kwa manufaa ya mustakabali. Uwajibikaji ni jukumu ambalo haliwezi kuachiwa vizazi vya kesho. Lazima watu wa vizazi vyote washikamane.

# Kupanua haki ya kupata elimu

Kulingana na changamoto zilizo mbele yetu, jambo la dharura linalostahili kushuligikiwa na wataalamu wa elimu, serikali na asasi za kiraia ni kutekeleza mapendekezo ya kuanzisha elimu inayotokea katika nyakati na nafasi tofauti. Kinachopendekezwa hapa sio ndoto bali ni mkakati imara wa kuimairisha kuwepo kwa spishi ya binadamu. Lazima elimu itumike katika kutuunganisha na raha ya kuishi, ambayo inajumuisha ujifunzaji.

Ripoti hii inasisitiza umuhimu wa kuangalia uhusiano baina ya elimu na maisha kwa jumla. Lakini, tunapaswa kuwa na aina zingine za taasisi kando na shule na vyuo vikuu. Elimu ni shughuli ya pamoja inayozingatia ujifunzaji wa vizazi na wa kitamaduni. Kipengele cha kijamii kinasisitiza umuhimu wa kutunza jamii na sayari. Shughuli hizi za pamoja na vipengele vya kijamii ni muhimu kwa shule na vyuo vikuu.

Tunapoelekea mwaka 2050, haki ya kupata elimu haistahili kuzuiliwa na mipaka inayotokana na ufahamu wa kawaida kuhusu nafasi na nyakati elimu hutokea. Haki ya kupata elimu lazima iwe ya kila mtu, sio watoto na vijana tu. Hatua nyingi zitahitajika ili elimu itekelezwe katika nafasi nyingi zaidi ya madarasa na shule.

Utumiaji wa redio na televisheni katika kuendeleza masomo kipindi cha UVIKO-19 unatukumbusha umuhimu wa vyombo vya habari katika elimu, tamaduni na maarifa ya kawaida hasa kwa wanafunzi wasio na vifaa vya kidijitali. Janga la UVIKO-19 limeonyesha umuhimu wa uunganisho wa kidijitali na majukwaa ya mtandaoni, kiasi kwamba ni lazima tuanze kufikiria jinsi upatikanaji wa taarifa ni haki ya msingi ambayo ina uhusiano mkubwa na haki ya kupata elimu kwa njia ambazo hatungezitabiri mwongo mmoja uliopita.

Haki ya kupata elimu inakamilishwa (na inakamilisha) haki ya kupata taarifa na haki ya utamaduni. Uhuru wa kuwa na maoni na kujieleza unaweza kuimarika wakati watu wana uwezo wa kutafuta, kupata na kueleza maarifa na mawazo. Katika ulimwengu wa sasa ulio na vyombo vingi vya habari na viwango vya juu vya habari potofu, elimu ina jukumu la kusaidia watu katika kupata taarifa sahihi na kuzisambaza zilivyo pasi na kuzibadilisha. Elimu husaidia katika haki ya kushiriki kwenye maisha ya kitamaduni kwa kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za kitamaduni zinazojenga utambulisho na kupanua mitazamo yetu. Pia, elimu husaidia katika kuimarisha uwezo wa watu wa kuchangia katika rasilimali za kitamaduni. Mazungumo wazi baina ya tamaduni tofauti ni muhimu katika kukuza wingi wa tamaduni. Elimu inastahili kutumia mazungumzo kama mbinu ya kuimarisha wingi wa tamaduni.

Elimu husaidia katika haki ya kushiriki kwenye maisha ya kitamaduni kwa kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za kitamaduni zinazojenga utambulisho na kupanua mitazamo yetu.

Kupanua ufahamu kuhusu haki ya kupata elimu katika nyakati na nafasi tofauti huimarisha dhana ya elimu kuwa mradi wa watu wote unaojengwa, kutawalwa, na kufanikishwa na sisi zote. Elimu ni rasilimali ya jamii - ustawi wa watu wote unaostahili kuunganishwa na maisha yetu ya kila siku. Watoto na watu wazima hawastahili kuwa wanunuzi au watazamaji wa elimu, wanastahili kuwa wahusika. Kila mtu ana jukumu tofauti katika elimu. Kila mtu ana haki ya kuhusika katika elimu inayoboresha jinsi tunavyofikiria, tunavyofahamu, tunavyohisi, na tunachofanya katika maisha yetu ya kibinafsi na maisha ya jamii.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii imependekeza kuwa katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu, tunastahili kufaidika na kupanua nafasi za kielimu zinazotokea katika hatua zote za maisha na katika nafasi tofauti za kitamaduni na kijamii. Tunapoelekea mwaka 2050, kuna kanuni nne zinazoweza kuongoza mazungumzo na hatua muhimu.

- **Watu wanastahili kuwa na nafasi za kielimu za hali ya juu wakati wote.** Ujifunzaji haustahili kuwa na mwisho, na elimu ya watu wazima inastahili kuzingatiwa. Tunapaswa kutumia kanuni zinazoleta ujumuishaji, na mipango yote inastahili kuanza na mahitaji ya waliotengwa na walio katika mazingira magumu.
- **Mifumoikolojia ya elimu iliyo na afya inaunganisha nafasi zote za ujifunzaji: za asili, zilizojengwa na za kidijitali.** Tunapaswa kuthamini biosfera kama nafasi muhimu ya ujifunzaji. Nafasi za ujifunzaji za kidijitali ni muhimu katika mifumoikolojia ya elimu na zinastahili kuboreshwa ili zisaidie katika kufanikisha malengo ya elimu ya jamii na ujumuishaji. Majukwaa wazi yanayolinda data ya wanafunzi na walimu yanastahili kupatiwa kipaumbele.
- **Uwezo wa serikali wa kufadhili elimu ya umma na kuidhibiti unastahili kuboreshwa.** Tunapaswa kujenga uwezo wa serikali wa kuanzisha na kutekeleza kanuni za elimu zinazoleta usawa na kuimarisha haki za binadamu.
- **Haki ya kupata elimu inastahili kupanuliwa.** Haki ya kupata elimu ni zaidi ya kuenda shule. Kila mtu anapaswa kuwa na haki ya ujifunzaji usio na mwisho. Tunapaswa kupigania haki ya kupata taarifa na haki ya tamaduni kwa sababu zinachangia pakubwa katika haki ya kupata elimu. Haki ya kuunganishwa lazima ikuwe kitu cha kawaida.

Kanuni hizi zinastahili kuzingatiwa katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Wadau katika viwango vya mitaa, nchi, maeneo na kimataifa wanastahili kujitolea kwa mazungumzo na hatua hizi ili watoe mchango wao katika mustakabali wetu.

# SEHEMU YA III

## Kuharakisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Ndiposa tuweze kupata ufanisi katika kukabiliana na migogoro inayohatarisha binadamu na Dunia, lazima tubadilishe mkondo. Kushirikiana katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu - unaohamasishwa na haki za kijamii, kiepestemolojia, kiuchumi na kimazingira - kutabadilisha mustakabali. Mkataba mpya wa kijamii wa elimu unamaanisha mbinu mpya za kulinda maarifa ya jamii na kuboresha elimu ili iwe mradi wa umma na rasilimali ya jamii. Mkataba huo unatambua umuhimu wa ushirikiano baina ya serikali na wadau wengine walio nje ya serikali; lazima washirikiane katika kutimiza ahadi za kitambo na kutumia elimu katika kubadilisha mustakabali. Jukumu la vyuo vikuu na wadau wengine ni kufanya utafiti na uvumbuzi utakaochangia katika kubadilisha elimu ili iwe rasilimali ya jamii. Vile vile, ni muhimu kuzingatia jinsi mashirika ya maendeleo ya elimu ya kikanda na kimataifa yanaweza kuchangia katika ushirikiano na mshikamano wa kimataifa tunaohitaji tunapoelekea mwaka 2050. Baada ya kuifanya elimu rasilimali ya jamii katika ngazi za kikanda na kimataifa, mkataba mpya wa kijamii wa elimu utaendelezwa katika majimbo mbalimbali ulimwenguni. Ripoti hii ni mwaliko wa kuendeleza mazungumzo kuhusu mkataba huo.

# Sura ya 8

# Wito wa kufanya utafiti na uvumbuzi

> Katika mbinu zote za jamii, mchakato - yaani methodolojia na taratibu - ni muhimu sana. Katika miradi mingi, mchakato ni muhimu kuliko matokeo. Michakato inastahili kuwa ya heshima, inayowezesha watu, inayoponya na inayoelimisha. Inastahili kuongoza watu ili wajiamulie.

**Linda Tuhiwai Smith,** *Decolonizing Methodologies,* 1999.

**Ndiposa mkataba mpya uharakishwe, Tume inasisitiza kuwa ni lazima tuwe na ajenda ya utafiti wa pamoja inayojikita katika haki ya kupata elimu katika hatua zote za maisha. Utafiti huo unahitaji mchango kutoka wa mashirika ya mashinani, waelimishaji, taasisi, sekta na tamaduni tofauti.**

Kuendeleza mapendekezo yalitolewa kwenye sura zilizopita kunahitaji jitihada, majaribio, upelelezi na uvumbuzi wa elimu katika miktadha mbalimbali. Sura hii inaangazia utafiti wa kushirikiana na uvumbuzi katika elimu ya kesho. Utafiti na uvumbuzi ni vitu vinavyofanana na elimu kwa sababu vyote ni rasilimali za jamii na michakato iliyo na jukumu la kuharakisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

Ajenda ya utafiti kuhusu mustakabali wa elimu huanzia kwa wanafunzi na walimu. Kwa njia nyingi, vipengele vya mustakabali wa elimu viko kati yetu. Mwanzo wa mfumo wa elimu yoyote ni katafuta mifano mwafaka inayolingana na kanuni zinazosisitizwa kwenye ripoti hii. Msingi wa ripoti hii unaweza kuwa utafiti na uchambuzi wa hali iliyochangia kwa mifano hiyo; msingi huo unaweza kusaidia katika kubadilisha mawazo ili yawe mkakati wa kuongoza kazi. Elimu ina historia ya kutumia aina nyingi za marejeleo, methodolojia na vielelezo. Zana hizi zinastahili kuimarishwa kwa viwango vyote kuanzia wataalamu na mazungumzo ya jamii hadi vyuo vikuu, ushirikiano wa utafiti na majukwaa ya kitaifa na kimataifa kama vile UNESCO.

Utafiti na uvumbuzi unastahili kuboresha uwezo wetu wa kuona mbele na kuimarisha ufahamu wetu kuhusu mustakabali.

Zaidi ya yote, sura hii inasisitiza kuwa utafiti na uvumbuzi hutusaidia kujifunza pamoja - kutafakari, kufanya majaribio na kuathiri jamii kwa pamoja kwa njia ambazo hubadilisha mustakabali wetu. Kwa hivyo, utafiti na uvumbuzi unastahili kuboresha uwezo wetu wa kuona mbele na kuimarisha ufahamu wetu kuhusu mustakabali kwa kuhamasisha mawazo yetu na ufahamu kuhusu jinsi mustakabali unaathiri tunavyoona na tunachofanya katika elimu. Maadili ya ushirikiano, unyenyekevu na utambuzi huenea katika vipengele vyote vya ajenda ya utafiti wa elimu.

Sura hii inasisitiza kuwa washirika katika elimu wanastahili kutumia mapendekezo ya ripoti hii katika kuendeleza maarifa na kufanya utafiti. Vile vile, wito wa kipekee umetolewa kwa vyuo vikuu, taasisi za utafiti na mashirika ya kimataifa; wito huu unasisitiza kuwa maudhui ya ripoti hii yajumuishwe katika elimu. Ili kuendeleza kanuni za mkataba mpya wa kijamii wa elimu, tunapaswa kujiandaa kwa kutafuta vifaa vitakavyosaidia katika utekelezaji wake. Ripoti hii inahitimisha na kanuni za kuongoza mazungumzo na hatua muhimu tunapoelekea 2050. Kanuni hizi zinazowalenga washirika wote wa elimu zinasisitiza kuanzishwa kwa ajenda ya utafiti wa kimataifa inayojumuisha mitazamo, maudhui na nafasi tofauti.

# Ajenda mpya ya utafiti wa elimu

Ripoti hii imependekeza kanuni ambazo Tume inaamini zinastahili kuongoza ajenda mpya ya utafiti kuhusu mustakabali wa elimu. Ajenda hii inalenga ujifunzaji mpana kuhusu mustakabali wetu. Kando na kujumuisha aina nyingi za maarifa na mitazamo, ripoti hii imejikita katika mfumo unaosisitiza kuwa maarifa yanakamilishana badala ya kupingana na kubaguana.

Ripoti hii ina vipaumbele vinavyoimarishana ili kufanikisha ajenda moja ya utafiti iliyo thabiti. Kama inavyoelezwa katika sura ya kwanza, ajenda hii lazima ilenge haki ya kupata elimu kwa kuchunguza vizuizi vya ubora na usawa kwenye upatikanaji wa fursa ya elimu. Utafiti lazima uchunguze uhusiano baina ya vyanzo vya mabadiliko vinavyoelezwa katika sura ya pilli na elimu – vyanzo hivyo ni kama mabadiliko ya tabianchi na mazingira, mabadiliko makubwa ya kiteknolojia, migawanyiko ya kisiasa, na mustakabali wa kazi na mapato usiotabirika. Utafiti unastahili kutimiza malengo mengine zaidi ya kupima na kukusoa ndiposa uweze kuimarisha elimu kulingana na kanuni zilizo katika sehemu ya pili ya ripoti hii: ufundishaji unaojikita katika mshikamano na ushirikiano, uhusiano baina ya mitaala na maarifa ya jamii, kuhamasishwa kwa walimu, kubadilishwa kwa shule, na mtangamano wa ujifunzaji na nyakati na nafasi zote za maisha. Ujifunzaji, maarifa, na uzoefu kutoka kwa ajenda hii ya utafiti ni vitu vitakavyoharakisha mkataba mpya wa kijamii wa elimu yetu sisi zote.

## Utafiti kutoka ndani ya elimu

Kuna desturi muhimu ya utafiti wa elimu ambayo imekuwa tangu mwanzo wa karne ya ishirini; desturi hiyo imetumika katika kujenga nasaba maarufu za mawazo na matendo. Utafiti wa elimu hutusaidia katika kuelewa hali ilivyo shuleni, madarasani na nafasi zingine ambapo elimu hutokea. Vile vile, utafiti hutupatia maarifa kuhusu mabadiliko yanayotokea katika maisha ya watu binafsi na ya jamii.

Aina za utafiti zinazotumika katika elimu ni utafiti wa mtaalamu, utafiti wa kuchunguza na kutatua shida, utafiti wa kumbukumbu, utafiti wa kesi, ethnografia, na zinginezo. Kwa hivyo, elimu inastahili kuangaliwa sio kama uwanja wa majaribio na kusoma tu, bali kama uwanja wa uchunguzi na uchambuzi.

Uthibitisho kuwa shule ni mahali ambapo maarifa huzalishwa na walimu wenye ujuzi unategemea ushirikiano uliopo baina ya vyuo vikuu, taasisi, watafiti, na wahusika katika elimu. Vyuo vikuu husaidia katika kuimarisha utafiti kwa sababu vina wataalamu wa nyanja tofauti wanaosaidia katika kuendeleza maarifa. Siku zote, walimu watakuwa waandishi wakuu wa maarifa kuhusu taaluma ya ualimu, ambayo hutokana na kutafakari kwa pamoja. Walimu wanastahili kufadhiliwa ili wachapishe utafiti na mawazo yao. Wanafunzi ni vyanzo muhimu vya maarifa na ufahamu unaotoka kwa uzoefu, matarajio, mafanikio, na mawazo yao.

> Wanafunzi ni vyanzo muhimu vya maarifa na ufahamu unaotoka kwa uzoefu, matarajio, mafanikio, na mawazo yao.

Usaidizi kutoka kwa vyuo vikuu na watafiti unaweza kupitia kwa mazungumzo na shule, walimu na wanafunzi. Kuna desturi za methodolojia zinazoweza kuboresha ujifunzaji wa wanaofanya utafiti ndani na nje ya elimu: tathmini ya ushiriki, utafiti wa kushirikiana, utafiti unaoongozwa na vijana na uchunguzi wa mtaalamu. Utafiti wa elimu utasaidia katika kufuatilia mabadiliko ambayo yanahitajika kwenye mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

## Kuhamasisha sayansi za ujifunzaji

Mojawapo ya maendeleo ya kisayansi kwa elimu katika miongo ya hivi karibuni yamekuwa kupitia kwa sayansi za nyuro. Sayansi hizi zinajumuisha ufahamu kuhusu uwezo wa nyuro kubadilika katika hatua zote za kukua kwa binadamu; anatomia, miundo na kazi za ubongo na nyuro za binadamu; uwezo wa kumbukumbu, usindikaji wa habari; ujifunzaji wa lugha; na kufikiria kwa hali ya juu. Vile vile, sayansi hizo zinaangazia athari za vichocheo chanya na hasi kwa ujifunzaji; vichocheo hivyo ni kama usingizi, mazoezi ya mwili, hisia, mfadhaiko na dhuluma. Michakato ya utambuzi na ujifunzaji ni muhimu kwa sababu inachangia katika ufahamu wetu kuhusu ujuzi maalumu kama vile uwezo wa kunena, kusoma, kuandika na uwezo wa kufahamu mazingira.

Ingawa wanasanyansi wako kwenye hatua za mwanzoni katika kuelewa uwanja huu wa nyurosayansi na jinsi unaweza kutumiwa katika elimu, uwanja huo unaathiri ufundishaji na ujifunzaji: walimu, watafiti na wanafunzi wanastahili kuelewa athari hizo. Kwa mfano, wanasayansi wanaweza kuchunguza uhusiano baina ya tabia kwa kuangalia na kufuatilia shughuli za kiakili katika maabara; lakini, bado haijabainika ni vipi uhusiano huo unaweza kubadilishwa ili upatanishwe na mazingira magumu ya kujifunza ya kijamii au jinsi uhusiano huo unaweza kubadilika katika miktadha, nyakati, jamii na nafasi tofauti.

Masomo ya sayansi za ujifunzaji ya kesho lazima yajumuishe watafiti wenye asili mbalimbali - za kijinsia, kitamaduni, kijamii, kiuchumi, kiisimu, na umri na kadhalika - ili kuhakikisha kuwa aina nyingi za maswali, dhana, nadharia, na vipaumbele zimewakilishwa. Maendeleo katika sayansi za ujifunzaji yanaweza kufaidi tofauti za kiakili, tofauti za ujifunzaji, masomo ya ulemavu na elimu maalumu.

Ingawa maarifa ya sayansi za ujifunzaji yana nguvu na ni muhimu, maarifa hayo sio jumla ya elimu. Utambuzi sio mbinu pekee ya ujifunzaji; maarifa ya kijamii, maarifa yaliyo katika akili zetu na akili ya kihisia huathiri vitu vinavyoweza kufafanuliwa kupitia kwa nyurosayansi.

Kama ilivyoelezwa katika sura za awali zinazoangazia ufundishaji na mitaala, elimu ni changamani kwa sababu inatokana na vipengele tofauti vya ulimwengu kama vile vipengele vya kijamii, kiuchumi, kimazingira, kimwili na kiroho. Ni hatari kutenganisha akili na mata kwa sababu hii huchangia dhana potofu kuhusu elimu. Ndiposa tuweze kuendeleza mapendekezo ya ripoti hii, nyurosayansi za ujifunzaji zinatahitajika kuweka wazi matokeo ya miktadha tofauti ya elimu ili kuchangia manufaa ya utambuzi na ya kijamii yanayotokana na elimu ya juu.

### Kubadilisha ushirikiano katika utafiti kwa ajili ya elimu

Ushirikiano katika utafiti unaolenga nyanja, sekta na tamaduni tofauti; unaojumuisha miktadha ya taaluma, asasi za kiraia na elimu na unaoimarisha mawasiliano na ujifunzaji wa pamoja unaleta uwezo mkubwa wa kufanikisha mapendekezo ya ripoti hii.

Sio ushirikiano wote wa utafiti ni wa haki na usawa. Washirika wenye rasilimali nyingi au wenye mamlaka makubwa wanaweza kuwa na ushawishi usiofaa kwa matokeo ya utafiti hata wakati hawana hiyo nia. Unyenyekevu wa kiepistemolojia unahitajika ili kukabiliana na dhana kuhusu elimu; nyingi za dhana hizo zimejikita katika ufahamu wetu kuhusu hali asili ya binadamu, jamii na ulimwengu ulio na viumbe wengine zaidi ya binadamu. Lazima tutupilie mbali uainishaji unaofanya mambo magumu kuonekana rahisi kama vile kutumia 'Kusini/Kaskazini' au 'Magharibi/isiyo Magharibi' tunapoelezea ikolojia za elimu zilizo changamani.

Kwenye mkataba mpya wa kijamii wa elimu, ikolojia hizi zitahitaji uzoefu tofauti wa njia nyingi za kujua ambazo hazipunguzwi na ubaguzi, upungufu wa kufikiria, na dhana pungufu za kiepistemolojia. Elimu ni mchakato wa uhusiano - kati ya wanafunzi, walimu, familia na jamii - na hivyo tunapaswa kutafuta maarifa ya uhusiano badala ya yale ya kihierarkia. Hii inaweza kuwa uhamasishaji wa uwezo wa kufanya utafiti katika ngazi za kitaifa na mitaa na ujumuishaji wa watu wanaoweza kuzalisha na kueleza maarifa kwa njia ambazo ni sambamba na miktadha, tamaduni na lugha tofauti.

Zaidi ya hayo, mchango wa jamii za mashinani na makundi ya kijamii ni vyanzo muhimu vya maarifa ambavyo vinastahili kutumiwa katika elimu. Harakati zinazopinga uharibifu wa Dunia na aina zote za ubaguzi ni mifano ya kubadilisha mustakabali wetu wa pamoja. Ushirikiano baina ya jamii na wanaharakati hauwezi kuwa rasmi lakini ni nguzo katika mchakato wa kujifunza jukumu la elimu na uhusiano wa elimu na harakati hizo.

## Kupanua maarifa, data na ushahidi

Uhamasishaji wa ajenda mpya ya utafiti wa mustakabali wa elimu utajikita katika viwango vikubwa vya maarifa, data na ushuhuda wa aina nyingi: wa kiasi na ubora, kanuni na maelezo, unaoweza kuelezwa kwa nambari na wa muda mfupi na wa kinadharia na vitendo.

Maarifa yanastahili kupanuliwa ili yaeleze haki ya sasa na uwezekano mpya wa elimu katika siku zijazo. Katika historia, kuna vyanzo fulani vya maarifa vimekuwa vikipatiwa kipaumbele na vingine vimekuwa vikipuuzwa. Maarifa, ya kawaida na ya elimu, hukingimana na mamlaka. Mbinu za kutawala watu na sayari kwa mabavu lazima zibadilishwe ili tuwe na zile mbinu zinazoleta ujumuishwaji na ushirikiano katika elimu. Ajenda ya utafiti wa kuimarisha elimu ya kesho inastahili kubadilisha dhana kuhusu hali ya maarifa, data, na ushuhuda katika elimu.

## Kuboresha ikolojia changamani za maarifa

Ndiposa tuweze kufikiria juu ya mustakabali wenye viwango vya juu vya utofauti na ulio zaidi ya hali ya sasa, utafiti na uvumbuzi, lazima tujumuishe njia zote ambazo zinatumika na jamii na tamaduni tofauti katika kusoma na kuelewa ulimwengu. Kwa hakika, kanuni kwenye ripoti hii, za pedagojia, maarifa, ushirikishwaji, ushirikiano na mshikamano, zina desturi ya mitazamo tofauti ya kitamaduni. Kukabiliana na dhana za kikoloni kunahitaji kutambuliwa kwa aina tofauti za vyanzo vya maarifa. Hii inamaanisha kuwa epistemolojia za kiasili zinastahili kutumiwa sio kama vitu vya kusomwa tu bali mbinu mwafaka za kuelewa ulimwengu.

Katika nyanja nyingi, kama maendeleo, uchumi na elimu, aina fulani za maarifa hupendelewa zaidi kuliko aina zingine. Mara nyingi, maarifa kutoka Ulimwengu wa Kaskazini huletwa katika Ulimwengu wa Kusini; dhana inayotawala hatua hii ni kuwa Ulimwengu wa Kusini hauna maarifa au maarifa yake yana upungufu. Hata hivyo, maarifa hayo kutoka Ulimwengu wa Kaskazini hushindwa kuleta maendeleo endelevu au huwafaidi wachache kwa gharama ya walio hatarini na mazingira.

> Mbinu nyingi za kujua, zikiwemo za asili, hukabiliana na dhana za modeli na sera za maendeleo ambazo zimefeli katika kufafanua hali yao halisi.

Kuthamini na kutambua njia nyingi za kujua sio kujilinganisha au kutupilia mbali ukweli. Mbinu nyingi za kujua, zikiwemo za asili, hukabiliana na dhana za modeli na sera za maendeleo ambazo zimefeli katika kufafanua hali yao halisi. Kwa mfano, katika desturi za mawazo huko Magharibi, elimu hufikiriwa kama dikotomia: nadharia dhidi ya mazoezi, mtu binafsi dhidi ya mkusanyiko wa watu, sanaa dhidi ya sayansi, binadamu dhidi ya ulimwengu wa asili, kupendelea maendeleo dhidi ya kushikilia ukale, kujua dhidi ya kuhisi, akili dhidi ya mwili, kiroho dhidi ya kimwili na kisasa dhidi ya kijadi. Mchango muhimu wa mitazamo isiyo ya Magharibi ni kukabiliana na misingi ya dikotomia hizi kwa kufafanua jinsi ambavyo mahusiano na mivutano ni vipengele vya ulimwengu.

Wakati wa migogoro, jamii hutumia mabwawa ya uzoefu, maarifa na ubunifu katika kukabiliana na hali hizo za dharura. Maarifa ya asili kuhusu michakato ya kilimo, ushirikiano wa kijamii na mbinu za kuishi na ulimwengu asili ni baadhi ya vyanzo vya maarifa ambavyo binadamu wanahitaji sasa. Lakini, maarifa hayo hayatambuliwi wala kujumuishwa katika elimu.

Utafiti kuhusu mustakabali wa elimu utahitaji ujumuishi wa aina nyingi za maarifa. Kama ilivyoelezwa katika sura za awali, ujumuishaji huo utategemea kushirikishwa katika maarifa ya jamii yaliyojikita katika haki na usawa. Mafanikio katika ushalizaji wa maarifa ya elimu ya kesho yanastahili kuwa: ujumuishi, utofauti wa kijamii na kitamaduni, utofauti wa nyanja na taaluma na unaoimarisha mawasiliano, ushirikiano, umiliki na ujifunzaji wa pamoja.

## Takwimu, viashiria, na uchambuzi

Takwimu zina uwezo wa kutoa taswira kuhusu kiashiria maalumu ; zinapowekwa pamoja na data zingine, zinaweza kutoa maarifa muhimu kuhusu mahusiano, mabadiliko, na hali katika nyakati na nafasi tofauti. Takwimu zinaweza kufafanua mabadiliko ambayo yametokea katika viashiria kwa muda na zinaweza kutumiwa katika kutabiri matokeo kulingana na hali, chaguo, matukio au hatua.

Taasisi ya Takwimu ya UNESCO inatimiza jukumu muhimu katika kukusanya na kuweka wazi takwimu kuhusu viashiria vya elimu. Taasisi hiyo imekuwa ikiimarisha uwezo wake wa kukusanya na kuthibitisha takwimu za kitaifa, kikanda, na kimataifa. Kutofautisha takwimu hizo, kulinganana na jinsia, eneo, kiwango cha mapato na sifa zingine kunaweza kutuongezea maarifa kuhusu swala la usawa. Taasisi imetia juhudi katika kuboresha ufafanuzi na kuhakikisha uadilifu wa takwimu kwa njia ambazo zinaongeza ubora na umuhimu wa takwimu hizo. Kuunga mkono kazi ya taasisi hiyo kutachangia katika maarifa muhimu kuhusu viashiria vya elimu na katika kuhakikisha kuwa kila mtu anaweza kupata data hizi.

Kwa wakati huo huo, mbinu za twakimu zitakazo tumika miongo ijayo zitalazimika kuepuka mbinu za kuelezea maswala changamani kwa kuyagawa katika sehemu ili iwe rahisi kuyaelewa. Uainishaji ni muhimu katika kuchanganua lakini haustahili kuangaliwa kama kitu ambacho hakiwezi kubadilika. Uanishaji ni jambo ambalo ni changamani; upimaji hauwezi kufanya hesabu yote ya uchangamani huo. Kazi ya kukusanya na kuthibitisha takwimu, hasa za idadi kubwa, ni ngumu na yenye gharama kubwa. Ikiwezekana, jitihada za kukusanya data zinastahili kuimarisha vyanzo vya data ya kitaifa ili kupunguza gharama ya kuwa na seti za data zinazofanana.

Vile vile, uangalifu wa makini utahitajika ili kutambua viashiria vya maana kwa njia ambazo zinaendana na vipaumbele vya elimu ya mitaani na malengo ya kimataifa. Mbinu hizi zinastahili kutambua kuwa si vitu vyote vya muhimu vinafaa kupimwa, na si kila kitu ambacho ni muhimu katika elimu kinaweza kupimwa. Unyenyekevu wa wanaokusanya na kutumia takwimu ni muhimu katika kuhakikisha kuwa maarifa kutoka kwa takwimu hizo ni mwanzo wa uchunguzi utakao fanikisha malengo ya elimu. Kazi inayofanywa na idara za UNESCO na watafiti wengine inaweza kufufua takwimu za kielimu ambazo zitatumika katika kufanya makadirio.

## Data kubwa na mabadiliko ya hali ya maarifa

Maendeleo ya kiteknolojia yameleta dhana mpya kuhusu maarifa na uzalishaji wake. Kulingana na matarajio ambayo yameletwa na teknolojia za kisasa, maarifa yatakuwa makubwa (yatatokana na aina nyingi za data), yatapatikana kwa urahisi, yatahifadhiwa kwa urahisi na yatakuwa na uwezo wa kutimiza malengo ya watu binafsi. Sifa hizi zinahitaji uchunguzi wa makini kwa sababu zinachangia katika ujenzi wa dhana kuhusu elimu kama vile malengo na michakato; kwa hivyo, zinachangia katika kufunguliwa na kufungwa kwa nafasi zingine.

Watafiti wamepata uwezo mkubwa wa kupanga, kuchanganua na kuchakatisha seti nyingi za data. Uwezo mkubwa wa mbinu na vyombo vya dijitali, ukusanyaji na uhifadhi wa data na uchakatishaji wa data kutumia aligorithimu umeongeza hamu ya kutaka kujua jinsi ambavyo teknolojia inaweza

kutumiwa katika kuongeza ufahamu na kuimarisha mbinu za elimu. Vyombo ambavyo watafiti hutumia ni kama uchakatishaji wa takwimu, ramani za kijiografia, ramani za mitandao, utafutaji wa ruwaza na ufuatiliaji wa maneno muhimu. Kuna nafasi kubwa ya kufanya utafiti katika vipengele vya elimu ambavyo vimeathiriwa.

Data kubwa imesifiwa katika kumbi za masomo za vyuo vikuu, ofisi za serikali, na makao makuu ya makampuni. Mazoea haya yana athari mbili. Kwanza, ikiwa hakuna data aina nyingi au mkusanyiko mkubwa wa wasifu, vibonyezo, mboni za macho, au ishara za elektroniki, hakuna miundo inayoweza kutambuliwa. Kulingana na mantiki za uchanganuzi wa data, bila miundo hiyo, hakuwezi kuwa na maana. Athari ya pili ni tabia ya hila ya kuona data, hasa inayoweza kukadiriwa, kama aina ya maarifa iliyo na umuhimu wa juu. Tumeshuhudia kuzaliwa kwa sayansi ya data ambayo imeleta mabadiliko ya kipekee katika elimu.

Watafiti wanaweza kufafanua ni nini kinaweza kupatikana kupitia kwa vyombo vya utafiti vya kidijitali. Kulingana na lengo la uchunguzi, si lazima data iwe nyingi ndiposa ikuwe bora. Sisi tunapendekeza ajenda ya utafiti inayozingatia malengo na tamaduni fulani badala ya kuzingatia vyombo vya utafiti. Maarifa ya komputya si sawa na yale ya binadamu. Wakati mwingine, programu za kompyuta huleta matokeo ya kushangaza na yenye kuelimisha kwa sababu ya uwezo wa kuchakatisha data ya viwango vikubwa kwa mwendo wa haraka kushinda binadamu. Wakati mwingine, akili za binadamu huelewa miktadha, maana, maadili na athari kwa njia ambazo haziwezi kufanywa na Akili Mnemba.

Watafiti wanapoendelea kuchunguza umuhimu wa data kubwa na vyombo vya kidijitali katika elimu, hatustahili kuamini kuwa programu za uchanganuzi wa kidijitali hazina upendeleo. Lazima tuendelee kuchanganua upendeleo na upofu wa mbinu za utafiti za kidijitali; kuzingatia haki na usawa katika kufunua yale ambayo yamefichwa na programu. Ikiwa mikondo hii itaendelea, kuna uwezekano kuwa kufikia mwaka 2050, maarifa mengi yatakuwa yamebadilishwa na kuwa ya kupimwa, ya aligorithimu, ya molekuli, ya kuhifadhiwa kwa urahisi na yanayoweza kusambazwa haraka kupitia kwa vyombo vya kidijitali tu. Tunapaswa kuwa na wasiwasi kwa sababu uwanja wa Akili Mnemba ambao umelipuka unanuiwa kuziimarisha sifa hizi ndiposa data isitegemee usimamizi wa binadamu. Athari za kimaadili za malengo hayo zinastahili kufuatiliwa kwa miaka thelathini ijayo.

## Kuvumbua mustakabali wa elimu

Uvumbuzi wa elimu huonyesha uwezo wa kufanya majaribio, kushiriki na kuhamasisha wengine. Uvumbuzi huo unaweza kutokea katika viwango vyote kuanzia ushirikiano kati ya mwalimu na mwanafunzi binafsi au darasa la wanafunzi, hadi viwango vya shule au nchi nzima. Mara nyingi, uvumbuzi huwa matunda ya ushirikiano na uhamasishaji unaotoka kwa uzoefu na ufanisi wa waelimishaji, watunga sera, watafiti na shule katika miktadha tofauti.

## Kuendeleza, kukopa, kubadilisha sera, na kupanga programu

Itakuwa muhimu kupanua uzoefu wa elimu na uvumbuzi ili ufike mazingira mapya; upanuzi huo utahitaji ushirikiano katika mambo ya sera. Msukumo wa ujifunzaji una uwezo wa 'kubadilisha kitu cha kawaida hadi kikawa cha kigeni' kwa kupanua mitazamo na kuchanganua dhana ambazo hazitiliwi maanani. Kubadilisha na kukopa ni aina za ujifunzaji na uvumbuzi. Kulingana na kanuni zilizo kwenye ripoti hii, tunaweza kushangilia na kupata hamasisho kutoka kwa uzoefu wa wengine na kwa kuzingatia tofauti za miktadha, uzoefu na maarifa kwa wakati mmoja.

Wadau katika mifumo ya elimu ni vyanzo muhimu vya mbinu na maarifa ya ubunifu. Uvumbuzi kutoka kwa nyanja zingine una upungufu kwenye maarifa na mapendekezo yake. Maarifa ya kielimu huzalishwa na kuhalalishwa kwa njia nyingi. Wadau - walimu, wanafunzi, walimu wakuu na shule - wanahusika katika uzalishaji wa utafiti na uvumbuzi. Utengenezaji na ubadilishaji wa mitaala unaweza kuimarishwa kupitia kwa michango ya wanaoitumia. Jukumu la serikali ni kusaidia walimu na shule katika mazungumo na urekebishaji wa mifumo na michakato ya elimu.

Swala la kiwango huibuka mara nyingi katika utafiti na uvumbuzi. Uzoefu wa watu wengine unaweza kukopwa. Lakini, 'mazoea bora' huzingatia matokeo badala ya kuelezea michakato iliyotumika. Kuongeza ushirikiano na majumuiya ya ujifunzaji - baina ya walimu, shule, wataalamu wa elimu, na watunga sera - kunaweza kuimarisha utafiti na utumiaji wa mitaala, maarifa ya programu na sera kutoka miktadha tofauti. Maadili ya unyenyekevu yanaweza kutulinda dhidi ya dhana za kihistoria ambazo hazizingatii muktadha na uvumbuzi wa kielimu unaotegemea dhana hizo.

Lengo linalostahili kuongoza vyuo vikuu, taasisi za utafiti na washirika wao ni kufanya utafiti na uvumbuzi utakaobadilisha elimu ili iwe rasilimali ya jamii na kusaidia katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Lazima mazungumzo yahusishe wale ambao tayari wako katika sekta ya elimu – walimu, wanafunzi, shule, familia na jamii. Kama ilivyoelezwa katika sura za awali, lazima vyuo vikuu vijitolee katika kujenga maarifa ya jamii yaliyo wazi na vitayarishe vizazi vipya vya watafiti na wataalamu watakaojitolea kuendeleza elimu kwa manufaa yao wenyewe na ya binadamu wote.

> Mbinu nyingi za kujua, zikiwemo za asili, hukabiliana na dhana za modeli na sera za maendeleo ambazo zimefeli katika kufafanua hali yao halisi.

Mashirika ya kimataifa yana jukumu la kipekee la kuendeleza utafiti na uvumbuzi katika elimu kwa njia zitakazo tupeleka kwa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Kulingana na ripoti hii, UNESCO imehimizwa kuweka pamoja aina zote za uzoefu zitakazo tumiwa katika mazungumzo na mapendekezo yaliyotolewa na ripoti hii. Ripoti hii inastahili kubadilishwa kila wakati ili iangazie na kujumuisha mabadiliko na maarifa mapya yanayoibuka.

## Tathmini, majaribio na ukadiriaji

Kutathmini na kutafakari ni michakato muhimu katika maisha ya programu za sera za elimu. Tathmini huhakikisha kuwa malengo ya programu au sera yanafikiwa. Tathmini hutumika katika kueleza matokeo ya programu. Kwa mfano, ikiwa programu au sera inachangia katika faida zinazopunguza ubora au ikiwa inahamasisha faida ya muda mfupi badala ya zile za muda mrefu, programu hiyo itahitaji marekebisho ya haraka.

Ili kuhamasisha maadili ya ushirikiano ambayo yamesisitizwa kwenye ripoti hii, tathmini inastahili kuzingatia uwezo wa wadau wa elimu - walimu, wanafunzi na shule - ili kutambua changamoto, udhaifu, uwezo wao wa kuvumbua na kupendekeza mabadiliko, marekebisho au vitu vinavyostahili kutupiliwa mbali. La muhimu zaidi ni kuwa na mfumo wa uchambuzi unaoimarisha uhusiano baina ya vipengele vya uvumbuzi: kusudi, tathmini na mapendekezo.

Majaribio yanaweza kuthibitisha dhana, kubadilisha mbinu, kurekebisha makosa ya hesabu na kuongeza ufahamu kuhusu mipaka ya kutabiri kwa kutumia matokeo ya uchunguzi uliopita. Uwezo wa kutenga vigezo katika mifumo changamani unahitaji umakini mkubwa na mbinu zenye ubora wa juu. Tunapoendeleza maadili ya ushirikiano katika kujenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu, hatustahili kufanya majaribio kwa watu. Watu wote - wanafunzi, walimu na familia - wanastahili kutambuliwa kama wahusika wakuu katika ujifunzaji kuhusu elimu na maendeleo yao. Utumiaji wa majaribio 'ya asili' katika kuelewa athari za hatua fulani au mabadiliko katika elimu unaweza kuongeza maarifa katika siku za usoni. Aina hizi za uchambuzi zinaweza kuleta maarifa yatakayosaidia katika kuelewa uthabiti wa elimu na uwezo wake wa kukabiliana na mabadiliko.

Kulinganisha kunaweza kutumiwa katika utafutaji wa mbinu za kuboresha, kuhamasisha na kufadhili elimu. Mara nyingi, kulinganisha hutumiwa kwa njia ambazo zinapunguza ufadhili kwa familia ambazo zinauhitaji. Kulinganisha uzoefu na matarajio ya watu hakusaidii wakati utofauti wa miktadha, rasilimali na mambo ya kihistoria hauzingatiwi.

Itakuwa muhimu kubadilisha mbinu za ukadiriaji zinazotumika katika elimu ya juu. Ni vigumu kulinganisha kwa kuzingatia maadili na bila ya kulazimisha vitu vifanane. Kulinganisha huleta matatizo wakati vyuo vikuu vilivyo kwenye mazingira tofauti hulazimika kushindana katika ngazi za kimataifa licha ya hali zao za kipekee. Modeli zinazotumiwa na vyuo vikubwa huathiri malengo ya vyuo vingine kwa kiasi kikubwa; hii inamaanisha kwamba mahitaji ya wanafunzi na jamii zao hayazingatiwi.

Lakini, si vyuo vikuu vinastahili kulaumiwa kwa kuwepo kwa ukadiriaji na mashindano baina ya vyuo vikuu. Serikali na jamii za sera za kimataifa zinastahili kulenga dhamira zingine kando na utafiti wa kina katika vyuo vikuu. Vyuo ambavyo watu wengi huenda vinastahili kufuatiliwa kwa umakini. Misingi ya kulinganisha inastahili kuwa jinsi ambavyo taasisi zinasaidia wanafunzi katika ujifunzaji wao; mustakabali wa taaluma zao; mustakabali wa jamii; jinsi ambavyo taasisi zinaimarisha mazungumzo ya kiraia na kisiasa; na jinsi ambavyo taasisi zinaimarisha haki za kimazingira, kiuchumi na kijamii. Tathmini katika elimu ya juu inastahili kufanya zaidi ya ukadiriaji unaoleta mashindano; badala yake, tathmini hizo zinastahili kutumika katika kuboresha elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu ndiposa ziweze kutimiza wajibu wao kwa umma.

# Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Tunapoelekea mwaka 2050, kuna mambo manne yanastahili kupatiwa kipaumbele katika utafiti na uvumbuzi kwa ajili ya mustakabli wa elimu:

- **Tume inahimiza ajenda ya utafiti wa kimataifa inayolenga mustakabali wa elimu.** Programu ya utafiti lazima izingatie haki ya upatikanaji wa elimu kwa watu wote, ieleze mabadiliko na misukosuko ya kesho na iendeleze kanuni zinazopendekezwa kwenye sehemu ya pili ya ripoti hii. Kwa mujibu wa ripoti hii, vipaumbele katika programu ya utafiti ni elimu ya siku zijazo na kufikiria kwa kesho.
- **Mbinu tofauti za kujua lazima zijumuishwe katika maarifa, data na uthibitisho wa mustakabali wa elimu.** Mitazamo tofauti inaweza kuimarisha ufahamu wetu. Hii inamaanisha hatutabaguana wala kushindana.
- **Uvumbuzi katika elimu lazima uzingatie aina zote za uwezekano katika miktadha na nafasi tofauti.** Tunaweza kupata hamasisho kutoka kwa kulinganisha na uzoefu tofauti. Lakini lazima tuzingatie hali za kijamii na kihistoria za miktadha tofauti.
- **Utafiti wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu unastahili kujumuisha kila mtu.** Mbegu zimepandwa tayari, hasa miongoni mwa waelimishaji, wanafunzi na shule. Jukumu la kuifadhili ajenda ya utafiti, inayochochea ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu, ni la taasisi za utafiti, serikali na mashirika ya kimataifa.

# Sura ya 9

## Wito wa mshikamano na ushirikiano wa kimataifa

Mkataba mpya wa kijamii utasaidia vijana kuishi na hadhi ya ubinadamu; utahakikisha wanawake wana matarajio na fursa sawa na zile za wanaume; na utalinda wagonjwa, walio hatarini na walio wachache. . . Baada ya kizazi kimoja, watoto wa watu kutoka nchi za kipato cha chini na za kipato cha wastani wataweza kupata elimu bora katika ngazi zote. Kinachohitajika ni sisi kuamua kutenda. . . Kufunga mapengo hayo, tunahitaji Mpango Mpya wa Kimataifa utakaohakikisha usawa katika ugawaji wa utajiri na fursa katika ngazi za kimataifa.

**António Guterres,** Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Nelson Mandela Lecture, 18 July 2020.

**Ndiposa tuharakishe mkataba mpya wa kijamii wa elimu, Tume inatoa wito wa kujitolea katika ushirikiano wa kimataifa unaolenga kuimarisha elimu ili iwe rasilimali ya jamii; mkataba huo unazingatia ushirikiano baina ya serikali na wadau wengine katika ngazi za mitaa, kitaifa na kimataifa.**

Kanuni ya elimu kuwa rasilimali ya jamii ni wajibu wa kimataifa. Miaka ya 2020 na 2021, majumuiya ya kisayansi ulimwenguni kote yalihamasishwa ili yatengeneze chanjo za UVIKO-19; majumuiya hayo yalifadhiliwa na serikali, mashirika ya umma na ya kibinafsi na asasi za kiraia. Mfano huu unaonyesha jinsi mustakabali wa binadamu, unaoweza kuboreshwa kupitia kwa ushirikiano wa kisayansi wa kimataifa, umekumbwa na changamoto ya ukosefu wa usawa katika usambazaji wa chanjo. Licha ya ufahamu kuwa hakuna aliye salama hadi kila mtu awe salama, utaifa wa chanjo umeonyesha mapengo yaliyo katika uwezo wetu wa kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya watu wote.

> Mbinu nyingi za kujua, zikiwemo za asili, hukabiliana na dhana za modeli na sera za maendeleo ambazo zimefeli katika kufafanua hali yao halisi.

Elimu hukuza werevu wa kibinadamu na uwezo wa kushirikiana; hii ni misingi ya kupambana na changamoto za sasa. Leo, kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya binadamu, ujenzi wa ulimwengu wenye ufanisi, haki, uendelevu na amani unahitaji watu wote, bila kujali asili, tamaduni na hali zao kuhusishwa katika elimu bora maishani mwao. Upatikanaji wa elimu rasmi utahitaji kukamilishwa na upatikanaji sawa wa maarifa na taarifa; kila mtu, kila mahali atahitaji kuwa na teknolojia ya dijitali. Kama vile afya ya mtu mmoja huathiri afya ya wengine, mustakabali wetu unategemea kutimizwa kwa mahitaji ya kielimu ya kila mtoto, kijana na mtu mzima ndiposa wahusike katika ujenzi na udhibiti wa mustakabali wa pamoja.

Ufahamu kuhusu elimu kuwa rasilimali ya jamii lazima uwe msingi wa ushirikiano wa kimataifa katika mambo ya elimu na ufadhili wa elimu unaotoka kwa umma, katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, ameeleza kuwa nguzo ya mpango mpya wa ulimwengu ulio na haki na uendelevu ni kuhakikisha kuwa kila mtoto na kijana anapata elimu yenye ubora wa viwango vya juu. Wajibu wa kuheshimu, kulinda na kufanikisha haki ya kupata elimu ni wa kila serikali na jamii ya kimataifa.

## Kukabiliana na utaratibu wa ulimwengu unaozidi kuwa hatari

Ushirikiano wa kimataifa wa elimu unakabiliana na hali hatari inayoonyesha kuwa maarifa ya kimataifa yanayotawala ulimwengu yameharibiwa sana. Majukwaa ya kimataifa, kama vile Umoja wa Mataifa, yaliyo ya jukumu la kupanga na kuendeleza harakati za ushirikiano wa kimataifa yakabiliwa na ukosoaji mkali na vikwazo vya fedha.

Watendaji wasio wa serikali na asasi za kiraia hukumbwa na changamoto wanapopigania haki za binadamu; kuna changamoto katika ujenzi wa miungano ya kudumu katika ulimwengu ulio

sambaratika. Kupungua kwa ufadhili kutoka ngazi za kimataifa kunamaanisha kwamba kazi yao itaathiriwa na hali mbaya ya kiuchumi katika ulimwengu wa baada ya janga la UVIKO-19. Kwa upande mwingine, wahusika wasio wa serikali wameongezeka na wana uwezo mkubwa wa kutumia teknolojia za kidijitali na taarifa kwa njia ambazo haziimarishi maarifa yaliyoorodheshwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Kibinadamu na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Mabadiliko ya kiuchumi katika nusu karne iliyopita ni ya kina kama mabadiliko ya kisiasa. Matokeo ya mabadiliko ya kisayansi na ya kiteknolojia pamoja na utandawazi wa kiuchumi ni ongezeko la ustawi, kupungua kwa umasikini ulimwenguni, na upatikanaji bora wa elimu. Lakini, mabadiliko hayo hayajaleta usawa na uwazi. Ustawi wa kiuchumi umeongeza nguvu za matajiri. Maendeleo ya kiteknolojia yametokea pamoja na ukiritimba wa kiuchumi na habari kwa njia ambazo huhatarisha misingi ya demokrasia. Licha ya matumaini kuhusu uwezekano wa kuimarisha uhusiano baina ya maendeleo ya uchumi na demokrasia, uwezo wa kushirikiana na utawala wa demokrasia katika nchi tofauti umezuiliwa katika miongo ya karibuni iliyokuwa na maendeleo ya kiuchumi.

Licha ya maendeleo ya pole pole katika swala la tabianchi na maswala mengine yanayohitaji ushirikiano wa kimataifa kama vile uhamaji, amani na faragha ya habari, katika miongo ya karibuni kumekuwa na makubaliano madogo (au uwezo mdogo wa kukubaliana) kuhusu rasilimali ya jamii na aina za ushirikiano wa kimataifa zinazohitajika ili kukabiliana na changamoto zinazowaathiri masikini kwa viwango vikubwa.

Mageuzi ya sasa ya Umoja wa Mataifa yanalenga kubuni njia za kukabiliana na changamoto ya ushirikiano baina ya nchi nyingi. Sura hii inapendekeza mbinu tatu: ujumuishaji wa watendaji wasio wa serikali katika utawala wa kimataifa; kutupilia mbali mbinu za kuanzia juu kwenda chini, kuanza kutumia hatua zinazo wahusisha watu wengi na kuanzisha aina mpya za ushirikiano wa kikanda hasa ushirikiano baina ya nchi za Kusini na ushirikiano wa pembetatu.

## Kutoka kwa misaada na kuanzisha ushirikiano

Ushirikiano wa kimataifa lazima ukabiliane na hali hatari zilizo ulimwenguni. Ufanisi katika kupata mpango mpya wa elimu unahitaji taratibu mpya za ushirikiano wa kimataifa. Wakati huo huo, taasisi za elimu zinastahili kuweka msingi wa ufahamu mpana kuhusu changamoto za sasa zinazohitaji ushirikiano hasa baina ya vijana.

Historia inathibitisha kwamba ujenzi wa ushirikiano katika elimu umekuwa ukitegemea ukoloni na malengo ya kiuchumi na kisiasa. Ushirikiano huo umekuwa ukizingatia mtiririko wa fedha na dhana kutoka Kaskazini kuja Kusini. Leo hii, kuna shida katika maendeleo ya elimu katika ngazi za kimataifa na misaada. Sehemu ya msaada rasmi wa maendeleo ya elimu ni kidogo na mara nyingi huenda kwa nchi za kipato cha kati. Msaada wa elimu unaotumwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara umepungua ingawa hili ni bara ambalo litakuwa na idadi kubwa ya vijana ifikapo mwaka 2050; vile vile, bara hili litaathiriwa pakubwa na changamoto za kimazingira na kiuchumi.

Isitoshe, nchi zenye uchumi kubwa hasa zile za Kundi la mataifa saba (G7) hupendelewa katika ufadhili wa msaada rasmi wa maendeleo ya elimu. Msaada mdogo unatumiwa katika kuhakikisha upatikanaji wa elimu ya chekechea na elimu bora ya msingi na sekondari. Mkakati unaostahili

kutumika kimataifa ili kuimarisha ushirikiano ni wa kutokomeza ujinga wa watoto - lengo hili ambalo lilipitishwa na Umoja wa Mataifa katika karne ya ishirini halijafikiwa. Idadi kubwa ya watoto iko nje ya shule, na kuna idadi kubwa ya watoto na vijana inayoenda shule na bado haijifunzi mambo ya kutosha. Mahitaji ya kielimu ya wakimbizi na wahamiaji hayana ufadhili wa kutosha. Ukosefu wa uratibu baina ya wafadhili wa elimu ni changamoto kubwa.

Hili ni ukweli baina ya mashirika kutoka Kaskazini ambayo hutoa mchango mkubwa wa misaada. Zaidi ya miaka ishirini imeisha tangu Azimio la Paris la 2005 Kuhusu Ufanisi wa Misaada kupitishwa lakini bado wafadhili hutoa msaada kwa kutumia mbinu ambazo hazizingatii mahitaji ya kipekee ya nchi. Njia za kuleta maendeleo ya elimu katika viwango vya kimataifa hazijatumika ipasavyo. Nafasi za kuunganisha rasilimali kwa njia zinazoimarisha ubunifu, kuwezesha utumiaji bora wa ushuhuda na kuimarisha uwezo ya kitaifa zimepotezwa.

> Mahitaji ya kielimu ya wakimbizi na wahamiaji hayana ufadhili wa kutosha.

Hata hivyo, kuna matukio mapya yanayoleta matumaini kuhusu uwezekano wa kujenga ushirikiano katika elimu. Ushiriki wa asasi za kiraia katika mambo ya elimu katika viwango vya mitaa, nchi na kimataifa umeongezeka katika miongo ya karibuni, na ushirikiano baina ya serikali na washirika wasio wa serikali umeongezeka. Kumekuwa na ongezeko la ushirikiano kati ya nchi za Kusini na ushirikiano wa pembetatu. Juhudi za hivi karibuni zimechangia katika elimu kupatiwa kipaumbele kwenye ajenda ya kisiasa. Elimu imezidi kuwa katika ajenda ya mashirika ya kisiasa ya kikanda na yale ya kimataifa.

Tunaposonga mbele, aina tatu za rasilimali za umma zitakuwa muhimu katika ujenzi wa mustakabali wa elimu iliyo na usawa, umuhimu na uendelevu. Kwanza, lazima jumuiya ya kimataifa ishirikiane ili isaidie serikali na washirika wasio wa serikali katika kuhakikisha kuwa kuna uwiano baina ya malengo mapya ya pamoja, kanuni, viwango na mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Pili, ni lazima jumuiya ya kimatifa iwekeze katika uhifadhi wa maarifa, utafiti, data na ushuhuda wa elimu na kuhakikisha kuwa waelimishaji katika viwango vyote wanaweza kutumia ushuhuda huo katika kuimarisha mifumo ya elimu. Mwisho, ufadhili wa kimataifa lazima upanuliwe ili usaidie wale watu ambao wana changamoto ya kupata haki ya elimu.

# Malengo ya pamoja, kujitolea, kanuni, na viwango

Kuanzia miaka ya katikati ya karne ya ishirini, tulishuhudia kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa na UNESCO; kupitishwa kwa Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu; na ongezeko la ushirikiano wa kimataifa katika mambo ya elimu ambao umesaidia katika kufikia makubaliano kuhusu malengo ya elimu. Leo hii, inatupasa kujadiliana kuhusu malengo ya elimu ya pamoja.

Ushirikiano wa kimataifa unastahili kupangwa upya kwa kutupilia mbali lengo la kihistoria ambalo lilikuwa kurudia mipango ya taasisi iliyotumiwa katika nchi zilizoendelea. Mazungumzo yanastahili kuzingatia ushirikiano baina ya nchi za Kusini na ushirikiano wa pembetatu. Kuna haja ya

kuimarisha mazungumzo na makubaliano baina ya wadau wa elimu: vyama vya walimu, mashirika ya wanafunzi, mashirika ya vijana, asasi za kiraia, wauzaji na waajiri wa sekta ya kibinafsi, wahisani, serikali na wananchi. Ushirikiano unaolenga mustakabali haustahili kupuuza sauti za watoto na vijana.

Tunapoanza kipindi chenye changamoto za kifedha zilizotokana na UVIKO-19, tunahitaji kupatia malengo yetu ya pamoja kipaumbele na kuhakikisha kuwa kuna fedha za kutosha katika ngazi za nchi na kimataifa. Wahusika wa kimataifa lazima washirikiane katika ajenda za kuchangisha fedha na katika kuratibu michango hiyo ili kusiwe na mashindano kwa ajili ya misaada.

Sekta za tabianchi na afya zinatoa mafunzo muhimu kuhusu jinsi ambavyo sekta ya elimu inaweza kuwa na malengo na mifumo ya pamoja. Wanaohusika katika ushirikiano wa kimataifa wanaweza kuweka malengo maalumu na kutoa ahadi zao. Kanuni ya kutimiliza inastahili kuwa msingi wa ushirikiano wa kimataifa kwa sababu malengo yanapozingatia mahitaji ya mazingira fulani, inakuwa rahisi kuwa na uwajibikaji. Mifumo imara ya ufuatiliaji wa kikanda na kimataifa inaweza kuundwa kwa kutumia ushahidi wa maendeleo ya kila mhusika.

Katika ngazi za kimataifa, sekta ya elimu na mashirika ya kimataifa yamekuwa na shida ya kupatia maswala yanayolenga sekta nyingi kipaumbele na hili limechangia katika kutofaulu kwa baadhi ya malengo ya elimu. Mashirika ya kimataifa hayastahili kufanya kila kitu. Kazi yao ni kuimarisha uwezo wa wengine ili wachuke hatua zinazostahili. Ili kufanya hivyo, lazima yazingatie kuimarisha uwezo wa kimataifa na wa kikanda kwa kuleta makubaliano na uwajibikaji.

Wahusika wa kimataifa hupata ufanisi katika udalali wa maarifa na ushahidi - hili huchangia katika ushirikishwaji wa wadau tofauti kwenye uzalishaji na utumiaji wa maarifa. Wanaweza pia kutimiza jukumu la kuwa wafadhili wa mwisho wakati elimu imekumbana na changamoto hasa katika nchi za kipato cha chini na wakati wa dharura.

Mashirika ya kimataifa hayastahili kufanya kila kitu. Kazi yao ni kuimarisha uwezo wa wengine ili wachuke hatua zinazostahili.

Katika uundaji wa mustakabali wa elimu, taasisi za kimataifa zinaweza kutimiza jukumu la kipekee la kuhakikisha kuwa tunatilia maanani changamoto za muda mrefu. Kwa mfano, malengo ya utafiti na mazungumzo yanastahili kuwa ni kufafanua jukumu la elimu katika kukabiliana na mabadiliko ya kazi ambayo yameletwa na teknolojia za otomatiki; kuelezea njia za kukabiliana na athari za uhamaji na mabadiliko ya tabianchi; na kufafanua mbinu za kutawala huduma za elimu ambazo zinatumia mifumo ya dijitali. Hii inamaanisha kuwa elimu inaweza kusambazwa nje ya mipaka ya nchi. Ajenda ya pamoja inastahili kujengwa kupitia kwa michakato ya ushirikishwaji na maamuzi ya pamoja. Ajenda hiyo lazima ishughulikie mvutano baina malengo ya muda mrefu na dharura ya kurekebisha ukosefu wa usawa na ubaguzi katika elimu.

# Ushirikiano katika uzalishaji wa maarifa na utumiaji wa ushuhuda

Utafiti na ushuhuda ni rasilimali zinazoleta manufaa kwa elimu. Rasilimali hizi husaidia serikali na washirika wake katika kusuluhisha matatizo na katika kufanya uvumbuzi unaoharakisha mabadiliko ya elimu. Vile vile, rasilimali hizi ni muhimu katika kuimarisha uwajibikaji kwa mujibu ahadi zilizotolewa.

Mashirika ya kimataifa kama OECD na Umoja wa Mataifa yamekosolewa vikali kwa sababu ya utumiaji mbaya wa data. Ukosoaji huu ni muhimu, lakini tunahitaji data ya pamoja itawale mifumo ya elimu ndiposa elimu iwe rasilimali ya jamii. Kama ambavyo imethibitishwa katika sekta za afya na tabianchi na uhamasishaji wa hivi karibuni wa elimu katika ngazi za kimataifa, hatua za kutathmini na kufuatilia maendeleo zinaweza kuchangia katika uwajibikaji wa kimataifa unaohitajika ili tufikie malengo ya pamoja na tushirikishe aina zote za wadau wa elimu.

Mpaka leo hii, wahusika wa kimataifa hawajafanikiwa kuanzisha miradi ya kuboresha upatikanaji na matumizi ya utafiti na ushahidi wa kimataifa. Hii ni tofauti na sekta ya afya ya kimataifa ambayo imesaidiwa na mashirika ya kimataifa katika kujumuisha rasilimali za kuzalisha data bora ya ufuatiliaji. Katika sekta ya elimu, mashirika ya Umoja wa Mataifa hayana mpangilio wa kushirikiana katika kuweka viwango vya elimu na kuimarisha uwezo. Wahusika wa kimataifa wanahitaji viwango vikubwa vya uratibu na ufadhili ili shughuli kama ujumuishaji na usambazaji wa ushahidi, utafutaji wa mapengo katika ushahidi na uimarishaji wa uwezo zikamilike vizuri.

Ufadhili wa kuboresha uwezo wa kuzalisha na kutumia maarifa, data na ushahidi lazima uratibiwe vizuri. Mara nyingi, hatua za kimataifa za maarifa na utafiti huonekana kama mazungumzo ya mhusika mmoja. Haistahili kuwa hivyo. Ushirikiano wa kimataifa lazima ufungue nafasi zaidi kwa ajili ya nchi za Ulimwengu wa Kusini ili ziweze kutoa mchango kwa dhana mpya za utafiti zinazofaa kwa hali zao za kipekee. Katika sekta ya afya, hatua zimechukuliwa ili kuunda majukwaa ya uratibu yanayolenga kuimarisha uwezo wa kitaifa na wa mitaa na kusaidia nchi katika shughuli za kufunzana. Modeli mpya za kuimarisha ushirikiano baina ya nchi za Kusini katika kusuluhisha matatizo ya elimu ni muhimu. Kama ilivyoelezwa katika sura ya 8, hii inahitaji epistemolojia tofauti kupatiwa kipaumbele na njia nyingi za kufahamu zinazoimarisha fikra na kuzingatia aina nyingi za uvumbuzi na ubunifu.

Elimu ya kimataifa ina changamoto ya ufadhili wa utafiti, ushuhuda na data. Ingawa 25% wa msaada wa maendelo ya afya (ODA) hutumika katika bidhaa za kimataifa (zinazogharimu bilioni 7 za dola za Marekani), takwimu zimebainisha kuwa ufadhili wa maarifa ya jamii, ushuhuda na data ni chini ya 3% mwaka wa 2015. Mipango mipya ya kuboresha ufadhili wa kimataifa wa utafiti, maarifa, na ushuhuda inastahili kuanzishwa. Kwa mfano, tunaweza kuwa na fedha za pamoja zinazosimamiwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa. Fedha hizo zinaweza kutumiwa kwa miradi ya maarifa ya kielimu na uzalishaji wa ushuhuda.

# Kufadhili elimu mahali ambapo imehatarishwa

Ingawa ni muhimu kufikiria upya kuhusu swala la ushirikiano wa kimataifa wa elimu na kupunguza utegemeaji wa misaada, lazima tuchunguze jukumu la mahusiano mapya baina ya msaada wa kimataifa na elimu.

Msaada hautoshelezi mahitaji ya kitaifa; kwa hivyo, umuhimu wake katika ngazi za kimataifa utapungua. Msaada umeongeza ukosefu wa usawa uliorithiwa kutoka kwa enzi za ukoloni; kwa hivyo, haujaboresha uendelevu wa mifumo ya elimu. Kwa wakati huo huo, ufadhili kwa nchi za kipato cha chini na kipato cha katikati unastahili kuongezwa - hasa huko Afrika ambako kutakuwa na idadi kubwa zaidi ya vijana miongo ijayo. Leo hii, 47% ya misaada huenda kwa elimu ya K-12 ya nchi za kipato cha chini na cha kati. Tunapaswa kuhakikisha kuwa kuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya elimu ya wahamaji, ambao wanazidi kuongeza hali ya mabadiliko ya tabianchi inapozidi kuwa mbaya. Kama ilivyodhihirishwa na janga la UVIKO-19, kuna haja ya kutenga fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji kama kujenga elimu upya baada ya majanga na matukio ya dharura.

Ndiposa tupate ufanisi katika malengo ya 2050, lazima tuimarishe njia za kimataifa ili ziweze kuongeza rasilimali ya kuziba mapengo na kuboresha uhamasishaji wa rasilimali za kitaifa. Uwiano baina ya misaada na uratibu kati ya wafadhili wa miradi ya elimu unasalia kuwa muhimu leo kama ilivyokuwa wakati wafadhili wa kimataifa walipitisha Azimio la Paris la 2005 Kuhusu Ufanisi wa Misaada.

Harakati za kimataifa huleta fursa bora za kuimarisha ufanisi wa misaada na zina uwezo wa kuelekeza misaada hiyo kwa nchi na watu wanaoihitaji sana. Lakini harakati hizo zinastahili kuimarishwa kwa sababu huwafunga wapokeaji wa misaada kwa maarifa wanayoshaliza na hazina sifa nzuri katika kuboresha uwezo wa kitaifa. Katika sekta ya afya ya kimataifa, mapendekezo ya karibuni yanalenga kurekebisha mapengo haya kwa kutenganisha mambo ya kifundi na kifedha katika mashirika yote na kuzingatia uwajibikaji wa pamoja kutoka kwa mashirika ya kimataifa.

# Jukumu la UNESCO

Katika kipindi cha miaka 25 iliyopita, shirika la UNESCO limekumbana na changamoto kadhaa. Kando na kukabiliana na ukosoaji mkali, shirika hilo limekumbana na changamoto katika kutimiza malengo ya kuratibu mazungumzo ya kimataifa kuhusu elimu; kuweka viwango vya elimu; na kuhakikisha mafanikio ya lengo la nne la maendeleo endelevu. Ni muhimu kuongeza kuwa licha ya kushughulikia majukumu ya elimu, sayansi na tamaduni, bajeti ya jumla ya UNESCO ni kidogo kuliko bajeti za vyuo vikuu vya Ulaya. Bajeti ambayo UNESCO imeweka kwa elimu, ni sehemu ya fedha ambazo Benki ya Dunia imependekeza zitumike katika maarifa na shughuli za kujenga uwezo wa elimu.

Ndiposa shirika la UNESCO lifanikiwe katika jukumu la kujenga mustakabali wa elimu ulio endelevu, lazima mbinu za kuendeleza elimu zinazotumika sasa zibadilishwe. Shirika hili linastahili kutambua kuwa jukumu lake ni kuimarisha mifumo na taasisi za kikanda na kitaifa. Pili, shirika hilo lazima

litambue kuwa majukumu yake ni kuwa dalali wa ushuhuda na mtetezi wa data na uwajibikaji katika viwango vyote vya elimu. Shirika hili linapozingatia jukumu lake la kipekee la kuhamasisha mazungumzo ya kimataifa kuhusu mkataba mpya wa kijamii wa elimu, lazima litumie rasilimali zake za fedha na wafanyakazi katika maeneo ambayo haki ya kupata elimu imehatarishwa sana hasa Afrika.

Katika mazingira changamani ambayo yana wahusika wengi wa kikanda na kimataifa wanaohusika katika kuweka viwango vya elimu, kufadhili na kuhamasisha maarifa, shirika la UNESCO litahitaji kuelewa nafasi yake. Shirika hili linastahili kushirikiana na Umoja wa Mataifa katika kutafuta majibu mwafaka yatakayo hakikisha kuwa wahamiaji wanapata haki ya elimu. Shirika la UNESCO linastahili kuwa mtetezi wa usawa wa kupata taarifa za kidijitali, ambayo ni haki ya binadamu. Pia, lazima shirika la UNESCO lihamasishe ushirikishwaji wa raia na asasi za kiraia katika utawala wa elimu ndiposa elimu iweze kukidhi mahitaji yao. Lazima shirika hilo liendelee kuwa mwangaza unaomulika jukumu la elimu la kujenga mustakabali wa pamoja unaozingatia amani, ustawi na uendelevu.

Shirika la UNESCO lina uwezo wa kipekee wa kuhamasisha watu na taasisi ulimwenguni katika ujenzi wa mustakabali wetu wa pamoja wa elimu. Uwezo huo wa UNESCO unahitajika katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu ya elimwengu na mpango wa kutekeleza mkataba huo.

## Kanuni za mazungumzo na hatua muhimu

Sura hii inatoa wito wa ushirikiano mpya wa kimataifa unaolenga kushughulikia mahitaji ya kesho, changamoto na fursa za elimu. Tunapoelekea mwaka 2050, kuna kanuni nne kuu zinazoweza kuboresha ushirikiano wa kimataifa katika swala la mustakabali wa elimu.

- **Tume inatoa wito kwa wadau wote wa elimu ili washirikiane katika ngazi za kikanda na kimataifa ndiposa wajenge malengo mapya ya pamoja na wapate majibu kwa changamoto za elimu.** Kuanzisha mkataba mpya ni hatua muhimu itakayo hakikisha kuna haki na usawa katika mustakabali wa elimu ya watu wote hasa wale ambao wamezuiliwa kupata haki hiyo kwa sababu ya changamoto za kimataifa. Mbinu zinazostahili kutumiwa ni ushirikishwaji wa wahusika wasio wa serikali; kutupilia mbali mbinu za kuanzia juu kuelekea chini; kutumia mbinu zinazojumuisha watu wote; na kuanzisha aina mpya za ushirikiano wa kikanda hasa ushirikiano baina ya nchi za Kusini na ushirikiano wa pembetatu.
- **Kanuni ya auni inastahili kuwa msingi wa ushirikiano wa kimataifa. Msingi huo utasaidia katika kuimarisha uwezo wa kukabiliana na changamoto kupitia kwa juhudi za kitaifa na kikanda.** Uwajibikaji katika ahadi za elimu na uratibu katika miradi ya kuimarisha elimu ni nguzo zitakazosaidia katika kuimarisha ahadi, kanuni, na viwango vipya vya elimu.
- **Dhamira ya ufadhili wa maendeleo ya nchi za kipato cha chini ya kipato cha kati ni muhimu.** Kanuni hii inalenga zile nchi zenye uchumi wa chini na zenye idadi kubwa ya vijana hasa huko Afrika. Elimu ya watu wanaokabiliana na dharura mbalimbali inastahili kufadhiliwa pia.

- **Uwekezaji wa pamoja katika ushuhuda, data, na maarifa ni muhimu katika ushirikiano wa kimataifa.** Hapa juhudi zetu zinastahili kuzingatia kanuni ya ushirikiano na uwezo wa kuzalisha na kutumia maarifa katika ngazi za mitaa, nchi, na kimataifa. Tunapaswa kuimarisha ujifunzaji wa pamoja katika jamii na nje ya mipaka - matokeo yake yatakuwa kumalizika kwa ukosefu wa usawa na umasikini; kuimarishwa kwa huduma za umma; na kuboresha uwezo wa kukabiliana na changamoto za teknolojia za otomatiki na kidijitali, uhamaji na uendelevu wa mazingira. Ili kuwe na maendeleo ya data na maarifa ya ulimwengu, tunahitaji majukwaa na pamoja na vyanzo vipya vya fedha.

Ajenda za mshikamano wa kimataifa na hatua za pamoja lazima ziwe na ukakamavu, ujasiri, na mshikamano. Ajenda hizi lazima zilenge mwaka wa 2050 ya baadaye. Hii inamaanisha kugawanywa kwa uwajibikaji, kuimarishwa kwa jukumu la UNESCO na kuboreshwa kwa uratibu ndani ya Umoja wa Mataifa. Bila ya hatua hizi, itakuwa vigumu kutimiza mapendekezo ya ripoti hii ambayo yanalenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu utakaobadilisha elimu ili iwe rasilimali ya umma ulimwenguni kote. Baada ya kizazi kimoja, tutaweza kubadilisha mifumo ya elimu ili iwe na ujumuishaji na umuhimu mkubwa na ipanue uwezo wetu wa kushughulikia changamoto za kimataifa.

# Hitimisho na Muendelezo

## Kushirikiana katika ujenzi wa mustakabali wa elimu

Lazima tuchukue hatua za haraka katika uundaji wa mkataba mpya unaoweza kukidhi mahitaji ya siku za usoni ya binadamu na sayari. Ripoti hii imependekeza vipaumbele katika ujenzi wa mkataba mpya unaozingatia kanuni mbili: upanuzi wa taswira ya haki ya elimu katika hatua zote za maisha na ubadilishaji wa elimu ili iwe rasilimali ya jamii na umma.

Kitovu cha ripoti hii ni pendekezo la mkataba mpya wa kijamii wa elimu - makubaliano na kanuni zinazohamasisha ushirikiano katika maswala ya elimu. Hitimisho la ripoti hii linalenga kutoa muhtasari wa vipaumbele na mapendekezo ya kubadilisha mustakabali wa pamoja wa elimu.

Mkataba mpya wa kijamii wa elimu haumanishi kutupilia mbali kila kitu ambacho tumekisoma kufikia sasa; mkataba huo sio marekebisho ya njia ambayo imekwisha tengenezwa. Kwa kipindi kirefu, mkataba mpya umekuwa ukiundwa - na waelimishaji, jamii, vijana, watoto na familia. Wadau hawa wametambua upungufu uliopo katika mifumo ya elimu na wamebuni mbinu za kukabiliana na upungufu huo.

Kwa kipindi kirefu, mkataba mpya umekuwa ukiundwa – na waelimishaji, jamii, vijana, watoto na familia. Wadau hawa wametambua upungufu uliopo katika mifumo ya elimu na wamebuni mbinu za kukabiliana na upungufu huo.

Lakini, bila ya ushirikiano na juhudi za pamoja katika kueleza mafunzo tunayopata tunapoendelea na harakati za kubadilisha elimu, juhudi hizo ni za kibinafsi na hazitakuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko makubwa katika taasisi. Kupitia kwa mazungumzo, elimu inaweza kubadilishwa ili iwe ya haki, usawa na uendelevu. Ripoti hii ni mwaliko wa kuchanganua na kuendeleza mazungumzo ya umma. Inakusudiwa kuchochea mazungumzo ulimwenguni kote kuhusu maana ya mkataba mpya wa kijamii wa elimu katika miktadha tofauti. Ripoti hii ni hatua muhimu katika barabara itakayo tufikisha kwa mustakabali. Ni ushahidi ulio hai na unaopendekeza mifumo, kanuni na hatua zinazostahili kuwanufaisha watu ulimwenguni kote. Dhamira kuu ni kuhamasisha mbinu za kujenga sera na kuanzisha hatua zitakazo badilisha elimu ili iboresha ubunifu wa wanafunzi. Dhamira hiyo itachangia katika mabadiliko ya elimu wakati wadau kama walimu, wanafunzi, familia, wafanyikazi wa serikali watatumia mapedekezo kwenye ripoti hii katika maisha yao.

Tume inahimiza shirika la UNESCO kuimarisha nafasi za makubaliano, ushirikishwaji na ujifunzaji kutoka kwa uzoefu wa wengine. Ufanisi wa ripoti hii utategemea uwezo wa kutafakari kwa kina na hatua muhimu zitakazochukuliwa. Kazi ya muhimu 'haitakuwa na mwisho', na mapendekezo kwenye ripoti hii yanazingatia dhana kuwa lazima kazi hiyo iendelee kubadilika. Tunahitaji ushirikiano tunapoendelea kujifunza kuishi kwa amani na watu wengine, aina zingine za viumbe, mifumo kwenye sayari na teknolojia ambazo zinafungua nafasi mpya kwa binadamu na kuleta hatari ambazo hazijawahi kushuhudiwa.

Makubaliano ya kimataifa kuhusu jukumu la elimu katika kubadilisha ulimwengu ni mwanzo muhimu kwetu sisi zote. Makubaliano hayo huimarisha kujitolea kwetu katika kukabiliana na changamoto mpya. Ndiposa vitu viweze kufanywa kwa njia tofauti, lazima tufahamu, tusikize na

tuwaze kwa njia tofauti. Tunahitaji kuchanganua jinsi ambavyo mawazo ya sasa kuhusu elimu, maarifa, na ujifunzaji yanaweza kufungua njia mpya za kubadilisha mustakabali.

# Mapendekezo ya kujenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu

Ripoti hii imefafanua vipengele vitano vinavyostahili kuzingatiwa katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Mapendekezo ya kila kipengele yamejumuishwa katika sehemu ya pili ya ripoti hii; kuna kanuni za kuongoza utekelezaji wa kila kipengele. Baadhi ya vipengele vimefupishwa katika sehemu hii ndiposa viwe mifumo ya utekelezaji inayoweza kutumika katika mazingira tofauti na kutimiza malengo ya mustakabali wa elimu.

## Ufundishaji wa mshikamano na ushirikiano

Ufundishaji unaoimarisha ushirikiano na mshikamano unastahili kuchukua nafasi ya mbinu zinazoleta ubaguzi na mashindano. Ufundishaji unastahili kuimarisha uwezo wa kuelewa hisia za wengine na huruma. Uwezo wa watu binafsi wa kufanya kazi pamoja katika kujibadilisha na kubadilisha ulimwengu wao unastahili kuimarishwa na ufundishaji. Ujifunzaji hutegemea uhusiano baina ya walimu, wanafunzi na maarifa ambayo yanakiuka kuta za madarasa na yanayotokana na mazingira mengine kando na madarasa.

Ujifunzaji huendeleza uhusiano baina ya wanafunzi, maadili na hatua zinazohitajika katika kulinda Dunia. Ufundishaji ni kazi ya kuleta mabadiliko kwa kutegemea kilichopo na kile kinachoweza kuundwa. Tunapoelekea mwaka 2050, lazima tutupilie mbali mbinu za ujifunzaji ambazo huendeleza mashindano. Badala yake, tunapaswa kupatia kanuni zifuatazo kipaumbele:

Kwanza, uunganisho, utegemeano na mshikamano ni nguzo kuu katika ufundishaji unaoleta mabadiliko ya watu binafsi na jamii kwa jumla. Walimu wanapoendelea kujifunza jinsi ya kukuza uhusiano na ufundishaji unaotokea nje ya madarasa, hatua hizi zinastahili kuwa katika shughuli za shule na mifumo ya elimu. Mbinu ambazo zinaweza kuleta ufanisi ni kama uzoefu, mazungumzo, huduma, hatua za maana, utafiti na mawazo, ushirikishwaji katika harakati na maisha za kijamii. Kuta zilizo katika shule na mifumo ya elimu zinastahili kuvunjwa ili iwe rahisi kusikiza familia na jamii kwa njia ambazo zinapanua ufundishaji ili uenee nje ya madarasa.

> Ufundishaji ni kazi ya kuleta mabadiliko kwa kutegemea kilichopo na kile kinachoweza kuundwa.

Pili, ushirikiano unastahili kuwa kitovu cha ufundishaji ambao ni mchakato wa umoja na uhusiano. Ili kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa kukabiliana na changamoto kwa njia za ubunifu, walimu wanaweza kutumia mbinu kadha za ujifunzaji - maoni ya wanafunzi wenza, kuzingatia miradi maalumu katika ujifunzaji, maabara ya wanafunzi, warsha

za kifundi, maonyesho ya kisanii na ushirikiano katika kubuni. Kuna mbinu kadhaa zinazoweza kutumiwa katika kufanikisha ujifunzaji wa kina wa marika tofauti na katika miktadha tofauti.

Tatu, mshikamano, huruma na uwezo wa kuelewa hisia za wengine ni maswala yanayoweza kujumuishwa kwenye ujifunzaji. Ufundishaji huwezesha wanafunzi kuelewa mambo mengi. Mchango wa wazazi na familia ni muhimu katika ujifunzaji wa watoto hasa kuhusu utofauti wa watu na mbinu za kutupilia mbali ubaguzi na hulka ya kutenganisha watu. Wadau kama walimu na shule wanaweza kujenga mazingira yanayoimarisha historia, lugha na tamaduni tofauti hasa zile za jamii za asili na za aina nyingi za harakati za kijamii.

Nne, tathmini ni kipengele cha ufundishaji; kwa hivyo, tathmini lazima zizingatie maswala yote ambayo ni muhimu katika ujifunzaji na ukuaji wa mwanafunzi. Tathmini zinaweza kutumiwa katika kutambua maswala yanayohitaji kupatiwa kipaumbele ndiposa ujifunzaji wa wanafunzi binafsi na wanafunzi wote uboreshwe. Tathmini haistahili kutumika katika kuwatia wanafunzi kwenye makundi ya 'washindi' na 'walioshindwa'. Sera za elimu hazistahili kutegemea ukadiriaji unaotokana na mitihani isiyozingatia mazingira na ambayo huweka shinikizo kubwa na kushawishi mambo yanayotokea katika nyakati na nafasi za shule.

## Mitaala na maarifa ya jamii

Uhusiano mpya lazima ujengwe baina ya elimu na maarifa, uwezo na maadili yanayochochewa na elimu. Mitaala inastahili kuzingatia michakato miwili muhimu ya kuimarisha elimu: upatikanaji wa elimu kama urithi wa binadamu wote na ushirikiano katika ujenzi wa maarifa na mustakabali. Tunapoelekea mwaka 2050, lazima tutambue kuwa mitaala sio mkusanyiko wa masomo. Mitaala inastahili kuangaliwa kama mitazamo ya kitamaduni na ya nyanja tofauti inayowawezesha wanafunzi kujifunza na kuchangia katika maarifa ya jamii. Kanuni zifuatazo zinastahili kupatiwa kipaumbele:

Kwanza, mitaala inastahili kuboresha uwezo wa wanafunzi wa kupata na kuchangia katika maarifa ya jamii ambayo ni urithi wa binadamu unaostahili kupanuliwa kila wakati ili ujumuishe mbinu tofauti za kujua na kuelewa. Miundo ya mitaala inastahili kufanya zaidi ya kueneza taarifa; miundo hiyo inastahili kuboresha ujuzi, maarifa, na hisia za wanafunzi ili wawe na uwezo wa kupata, kuzalisha, kutumia na kuelewa aina tofauti za maarifa.

> Michakato miwili muhimu ya kuimarisha elimu: upatikanaji wa elimu kama urithi wa binadamu wote na ushirikiano katika ujenzi wa maarifa na mustakabali.

Pili, mabadiliko makubwa ya tabianchi na hali za sayari yanahitaji mitaala inayofafanua jukumu la binadamu katika Dunia. Kuna ongezeko la mabadiliko ya sayari, na elimu inastahili kuzingatia uhusiano baina ya ustawi wa kimazingira, kijamii na kiuchumi.Mitaala lazima iwe na aina nyingi za maarifa ambayo yatawasaidia wanafunzi kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa njia zinazozingatia uhusiano baina ya viumbe tofauti wanaoishi kwenye Dunia. Lazima mitaala izungumzie jinsi ambavyo mabadiliko ya tabianchi yameathiri maisha ya waliotengwa kama vile

masikini, walio wachache, wanawake na wasichana. Maarifa ya mitaala yanaweza kutoa mfumo wa hatua muhimu na kuwasaidia watoto na vijana wanaoshughulikia maswala la tabianchi na ulinzi wa mazingira ambayo yataathiri mustakabali wao.

Tatu, ongezeko la habari potofu linaweza kukabiliwa na aina nyingi za elimu - za kidijitali, kisayansi, maandishi, kiikolojia na hisabati - ambazo zitawasaidia watu kupata maarifa ya ukweli. Elimu hizi huchangia katika ushirikishwaji wa kidemokrasia unaozingatia ukweli. Ndiposa elimu iwe na ufanisi, lazima ikuze ufahamu kuhusu ukweli, taarifa na data; elimu hiyo inastahili kuhamasisha michakato ya ushirikiano katika kutafuta, kuthibitisha na kuwasiliana kuhusu matokeo ya utafiti. Mitaala inaweza kutumia mbinu za kihistoria, kitamaduni na kimethodolojia katika kuboresha uwezo wa wanafunzi wa kuelewa, kudumisha usahihi, na kujitolea katika kuendeleza ukweli.

Nne, misingi muhimu ya mitaala na ujifunzaji inayobadilisha watu na ulimwengu ni haki za binadamu na ushirikishwaji wa kidemokrasia. Haki za binadamu ni takatifu na ni mwanzo wa mkataba wa kijamii; haki hizo zinastahili kuwa msingi wa mitaala inayoongoza ujifunzaji. Lazima mitaala isisitize haki za asili, adhama ya watu wote na umuhimu wa kumaliza vurugu na kujenga jamii zenye amani. Mitaala inaweza kushughulikia maswala ya ubaguzi unaolenga jinsia, rangi ya ngozi, utambulisho wa asili, lugha, ujinsia, umri, ulemavu na uraia kwa kutumia maudhui ya harakati za kijamii.

## Walimu na taaluma ya ualimu

Walimu wana jukumu la kipekee katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Wao ni wachukuzi wanaoleta vipengele na mazingira tofauti pamoja hasa wanaposhirikiana katika kuboresha maarifa na uwezo wa wanafunzi. Hakuna teknolojia inayoweza kuchukua nafasi ya walimu wazuri wa kibinadamu. Tunapoelekea mwaka 2050, ni muhimu tuache kuangalia ualimu kama shughuli ya mtu binafsi ya kufanikisha ujifunzaji. Badala yake, taaluma ya ualimu inastahili kuwa taaluma inayotumia ushirikiano katika kufanikisha ujifunzaji. Kanuni zifuatazo zinastahili kupatiwa kipaumbele:

> Michakato miwili muhimu ya kuimarisha elimu: upatikanaji wa elimu kama urithi wa binadamu wote na ushirikiano katika ujenzi wa maarifa na mustakabali.

Kwanza, kazi ya walimu inastahili kuwa na ushirikiano mkubwa. Hata wale walimu wenye vipaji au uwezo mkubwa, hawawezi kukamilisha malengo yote ya elimu. Lazima walimu washirikiane na walimu wenza, wataalamu wa kusoma na kuandika, wakutubi, waelimishaji wa elimu yenye mahitaji ya kipekee, washauri, wafanyikazi wa kijamii na wadau wengine. Umuhimu wa ushirikiano utaongezeka katika miaka ijayo kwa sababu binadamu watakabiliwa na migogoro, na walimu watakuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia watoto, vijana na watu wazima wanapokabiliana na mabadiliko hayo kwa kutumia njia zinazostahili kulingana na umri wao. Wanafunzi wanaposaidiwa katika maswala ya ustawi, mahusiano mema na afya ya akili, walimu wanahitaji kusaidiwa kupitia

kwa mishahara inayoweza kuwakimu; nafasi za kuendelea katika taaluma yao; nafasi za kusoma; na mazingira ya ushirikiano yanayowawezesha kukamilisha kazi zao.

Pili, nguzo za ufundishaji zinastahili kuwa maarifa, kufikiria na utafiti. Mwanzo wa mustakabali wa utafiti na maarifa kuhusu mustakabali wa elimu ni kazi ya walimu, na vipengele vingi vya mkataba mpya wa kijamii wa elimu vimejumuishwa katika ufundishaji ambao unaongoza walimu wengi. Kazi ya walimu ya kuzalisha maarifa na kuongoza ufundishaji inastahili kutambuliwa na kufadhiliwa ili walimu waweze kurekodi na kujadiliana na wenzao kuhusu utafiti wao kupitia njia rasmi na ziziso rasmi. Miundo mipya ya taasisi inaweza kuanzishwa na vyuo vikuu na elimu ya juu ili iimarishe utafiti na uhusiano wa kitaaluma baina ya walimu.

Tatu, uhuru wa kitaaluma wa walimu unastahili kuboreshwa na kulindwa. Taaluma ya ualimu inahitaji aina nyingi za ujuzi wa viwango vya juu na maendeleo ya kitaaluma yasiyoisha. Katika miongo inayokuja, elimu na walimu inahitaji kuboreshwa na kupanuliwa hasa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo idadi ya walimu iliyopo haiwezi kutosheleza mahitaji ya shule zote. Maendeleo ya kitaaluma ya walimu malimbukeni yanaweza kufanikishwa kupitia kwa elimu isiyoisha, ushauri na ufundishaji wa ushirikiano. Lazima kuwe na wakati wa kutosha wa kujitayarisha kwa kila somo, na malipo lazima yawe ya haki na usawa. Kuhakikisha kuwa kuna uhuru wa kitaaluma, heshima kutoka kwa jamii na mishahara inayofaa kutahamasisha walimu wasalie katika taaluma na wengine kuingia katika taaluma hiyo.

Ushirikishwaji katika mazungumzo ya umma kuhusu elimu na sera za elimu unastahili kutambuliwa kama sehemu ya kazi ya walimu. Mara nyingi, maamuzi kuhusu mambo yanayotokea shuleni na kwenye madarasa hufanywa na wale ambao hawahusiki katika mambo hayo kumaanisha kuwa hakuna mazungumzo na maoni ya kutosha. Hali hii inastahili kubadilishwa katika elimu ya kesho. Walimu wanastahili kuhusishwa katika mazungumzo ya umma kuhusu elimu. Maoni ya walimu kuhusu ni nini kinastahili kujumuishwa katika ufahamu wa pamoja ni sehemu kubwa ya jukumu la walimu; lazima wahusike pakubwa katika utekelezaji wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

## Kulinda na kubadilisha shule

> Shule ni nguzo kuu katika mifumoikolojia ya elimu na ubora wao ni ushuhuda wa kujitolea kwa jamii katika kufanikisha dhamira ya kufanya elimu iwe rasilimali ya jamii.

Shule, pamoja na uwezo na upungufu wao, ni mojawapo ya mazingira muhimu ya kielimu. Shule ni nguzo kuu katika mifumoikolojia ya elimu na ubora wao ni ushuhuda wa kujitolea kwa jamii katika kufanikisha dhamira ya kufanya elimu iwe rasilimali ya jamii. Tunapoelekea 2050, ni wazi kuwa hatustahili kuwa na shule zinazotumia modeli moja bila ya kuzingatia mazingira. Badala ya miundo ya sasa ya ujenzi na utaratibu, tunahitaji umma kutia bidii katika kubadilisha nyakati na nafasi za shule kwa njia ambazo zitalinda na kubadilisha shule. Mapendekezo yafuatayo yanastahili kuongoza kazi hii:

Kwanza, lazima shule zilindwe kwa sababu ni nafasi zinazowapatia wanafunzi changamoto na fursa ambazo hawawezi kupata mahali pengine. Shule zitahitaji mazingira yenye ushirikiano na utunzaji ambayo yatawapatia watu tofauti fursa za kuelimishana. Shule huwawezesha walimu na wanafunzi kupatana na dhana mpya, tamaduni tofauti na njia mpya za kuona ulimwengu ambazo huwatayarisha watoto na vijana kukabiliana na mabadiliko ya sasa na changamoto ambazo watakumbana nazo siku za usoni.

Pili, mabadiliko yanahitajika katika majengo ya shule, nafasi, nyakati, ratiba, na makundi ya wanafunzi ili uwezo wa kushirikiana uongezeke. Mazingira yaliyojengwa na miundo ya ujumuishaji huathiri mambo yanayotokea katika nafasi za ujifunzaji. Desturi za ushirikiano zinastahili kuongoza utawala wa shule na uhusiano baina ya shule ndiposa kuwe na mitandao ya ujifunzaji, fikra na uvumbuzi.

Tatu, teknolojia za kidijitali zinastahili kukamilisha shughuli za shuleni. Teknolojia hizo haziwezi kuchukua nafasi za taasisi za elimu. Utumiaji wa vyombo vya dijitali unaweza kuimarisha ubunifu na mawasiliano ya wanafunzi. Katika miongo inayokuja, nafasi za kidijitali zitafungua nafasi mpya za kupata na kushiriki katika maarifa ya pamoja na uzoefu wa binadamu. Hatua za kuleta Akili Mnemba na aligorithimu zinastahili kuchukuliwa kwa umakini ili kuhakikisha hazizalishi wala kuzidisha fikra potofu na ubaguzi.

Nne, shule zinastahili kuwa modeli za mustakabali bora kwa kutoa mfano mwema katika maswala ya haki za binadamu, uendelevu na kupunguza viwango vya kaboni. Wanafunzi wanapaswa kuhusishwa katika kuleta uendelevu kwenye sekta ya elimu. Miundo ya asili inayozingatia mazingira inaweza kutoa mafunzo kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga mustakabali bora unaotuwezesha kuishi na ulimwengu wa asili na mifumo mingine tunayoitegemea. Lazima tuhakikishe kuwa haki za binadamu zinazingatiwa katika elimu na sera za shule.

## Elimu katika nyakati na nafasi tofauti

Mojawapo ya jukumu letu ni kupanua mawazo kuhusu mahali na wakati elimu inastahili kutokea ili nyakati na nafasi ziwe nyingi na elimu iwe katika kila hatua ya maisha. Lazima tufahamu kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuendeleza elimu kwa kutumia fursa zilizo katika jamii na katika hatua zote za maisha. Fursa hizo ni za kitamaduni, kijamii na kiteknolojia. Tunaweza kupata taswira ya jamii za kesho zilizo na nafasi nyingi za ujifunzaji; nafasi hizo zinaweza kupatikana nje ya shule wakati wowote. Tunapojitayarisha kwa ajili ya mwaka 2050, kuna kanuni nne za kuongoza mazungumzo na hatua zinazohitajika ili kufanikisha pendekezo hili.

Tunaweza kupata taswira ya jamii za kesho zilizo na nafasi nyingi za ujifunzaji na nafasi hizo zinaweza kupatikana nje ya shule wakati wowote.

Kwanza, hatua zote za maisha lazima ziwe na fursa za kutosha za elimu. Elimu hutokea katika hatua zote za maisha. Elimu ya watu wazima inastahili kuimarishwa kwa kufanya zaidi ya kuongeza ujuzi; elimu hiyo inastahili kuongeza uwezekeno wa kuleta mabadiliko. Kwenye mipango ya elimu katika hatua zote za maisha, lengo kuu linastahili kuwa kushughulikia waliotengwa na walio

katika mazingira magumu. Wanafunzi wanastahili kupata maarifa, dhana, mitazamo na ujuzi wa kuwasaidia katika kukabiliana na migogoro ya sasa na ya kesho.

Pili, mifumoikolojia ya elimu yenye afya, inastahili kuunganishwa na nafasi za ujifunzaji kama vile nafasi asili, zilizojengwa na za kidijitali. Biosfera - ardhi, maji, uhai, madini, mifumo ya anga, mifumo mingine na miingiliano - ni nafasi muhimu ya ujifunzaji. Biosfera ni mwalimu wetu wa kwanza. Ujifunzaji wa kidijitali unastahili kujumuishwa katika mifumoikolojia ya elimu na ujifunzaji huo unastahili kuimarisha uwazi, ujumuishaji, na malengo ya jumla ya elimu. Majukwaa wazi ya kidijitali yanayolinda data za walimu na wanafunzi yanastahili kupatiwa kipaumbele.

Tatu, ufadhili wa umma na uwezo wa serikali kwa kudhibiti elimu unastahili kuboreshwa. Tunapaswa kujenga uwezo wa serikali wa kuweka na kutekeleza viwango na kanuni za elimu yenye usawa, uwezo wa kubadilika kulingana na mazingira na inayoendeleza haki za kibinadamu. Mazungumzo, kuhusu kanuni za kubadilisha mustakabali wa pamoja, yanayoongozwa na serikali na taasisi za umma yanastahili kufanywa katika ngazi za mitaa, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Nne, haki ya kupata elimu inastahili kupanuliwa; elimu inahusisha mambo mengi zaidi ya kuenda shule. Tunapoangalia mbele, tunapaswa kuboresha haki ya kupata elimu katika hatua zote za maisha; haki hiyo itasaidiwa na haki ya kupata taarifa, haki ya kuunganishwa, na haki ya utamaduni.

# Kauli mbiu

Ripoti hii imetoa kauli mbiu mbili za kuharakisha juhudi za mkataba mpya kwa kijamii wa elimu. Kauli mbiu ya ajenda mpya ya utafiti wa elimu na kauli mbiu ya kuimarisha mshikamano na ushirikiano katika kuibadilisha elimu ndiposa iwe rasilimali ya umma na ya jamii. Kanuni za kuongoza utekelezaji wa kauli mbiu hizi zimejumuishwa humu ili zitusaidie katika kujenga mustakabali mpya wa elimu tunapokabiliana na mabadiliko ya hali.

## Ajenda mpya ya utafiti wa elimu

Vipaumbele vinavyoangaziwa kwenye ripoti hii vinasisitiza umuhimu wa ajenda thabiti ya utafiti. Ujifunzaji, maarifa na uzoefu wa ajenda hiyo ya utafiti utaharakisha ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Tunapoelekea mwaka 2050, kuna kanuni nne za kuongoza utafiti na uvumbuzi utakaonufaisha mustakabali wa elimu.

Kwanza, programu ya utafiti wa kimataifa, unaolenga mustakabali wa elimu, inastahili kuzingatia haki ya kupata elimu katika hatua zote za maisha. Programu hiyo inastahili kutambua uwezekano wa kuwa na vurugu siku za usoni na athari za vurugu hizo. Utafiti huo unastahili kufanya zaidi ya kupima na kuchambua; unastahili kufafanua jinsi elimu inaweza kubadilishwa kwa kutumia kanuni zilizopendekezwa kwenye ripoti hii. Programu ya utafiti inastahili kuzingatia elimu ya mustakabali na fikra kuhusu mustakabali ili ituongoze hadi kwa mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

Pili, mbinu tofauti za kujua zinastahili kujumuishwa katika maarifa, data na ushahidi kuhusu mustakabali wa elimu. Mitazamo tofauti inaweza kuimarisha uelewano badala ya kuleta ubaguzi na mashindano. Dhana za kimethodolojia zinazopigana dhidi ya ukoloni na zinazoendeleza demokrasisa na haki za binadamu zinastahili kupatiwa kipaumbele na watafiti, vyuo vikuu na taasisi za utafiti. Watafiti wanastahili kutambua kuwa shule, walimu, harakati za kijamii, makundi ya vijana na jamii ni vyanzo muhimu vya maarifa na taarifa. Matokeo ya utafiti, wa sayansi za ujifunzaji, nyurosayansi, data kubwa na viashiria vya takwimu, yanaweza kuleta maarifa muhimu.

> Kwanza, programu ya utafiti wa kimataifa, unaolenga mustakabali wa elimu, inastahili kuzingatia haki ya kupata elimu katika hatua zote za maisha.

Tatu, uvumbuzi katika elimu unastahili kuangazia uwezekano ulio kwenye mazingira, nyakati na nafasi tofauti. Watu wanaweza kuhamasishwa kupitia kwa kulinganishwa na uzoefu wakati hali za kijamii na kihistoria zinazingatiwa. Uvumbuzi katika elimu unastahili kukiuka mifumo ya kawaida inayotawala taasisi za elimu. Tathmini na tafakari zinaweza kutumiwa katika kuhakikisha kuwa sera za elimu zinajumuisha mabadiliko.

Nne, utafiti kuhusu mkataba mpya wa kijamii wa elimu unastahili kujumuisha makundi tofauti ya wadau hasa wale ambao hawahusishwi katika mazungumzo ya elimu. Tayari, mbegu za mkataba mpya wa kijamii ziko hai miongoni mwa walimu, wanafunzi na shule. Jukumu la kufadhili na kuharakisha ujenzi wa mkataba huo liko mikononi mwa taasisi za utafiti, serikali na mashirika ya kimataifa. Shirika la UNESCO linaweza kutimiza majukumu ya kuhifadhi maarifa, kujenga taswira ya mustakabali na kuzalisha mawazo kuhusu mustakabali wetu wa pamoja wa elimu.

## Mshikamano na ushirikiano mpya wa kimataifa

Taswira ambayo imeelezwa kwenye ripoti hii haiwezi kufikiwa bila ya mshikamano na ushirikiano katika ngazi zote - kuanzia madarasa na shule hadi ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa. Ripoti hii inahimiza ushirikiano wa kimataifa katika dhamira ya kubadilisha elimu ili iwe rasilimali ya umma. Ushirikiano baina ya wahusika wa serikali na wasio wa serikali unastahili kuwa wa haki na usawa. Tunapokaribia mwaka 2050, tunapaswa kuzingatia kanuni za ushirikiano na mshikamano wa kimataifa katika kubadilisha mustakabali wa elimu.

> Wanafunzi ambao elimu yao iko hatarini kwa sababu za michafuko na mabadiliko ya kimataifa wanastahili kupatiwa kipaumbele.

Kwanza, Tume inawahimiza wadau wote washirikiane katika ngazi za kikanda na kimataifa ndiposa waweze kutafuta suluhisho kwa changamoto za elimu. Wadau wanastahili kutia jitihada katika kujenga mustakabali wa elimu ambao nguzo zake ni haki ya kupata elimu katika hatua zote za maisha na elimu ambayo ni rasilimali ya jamii. Wanafunzi ambao elimu yao iko hatarini kwa sababu za michafuko na mabadiliko ya kimataifa, wanastahili kupatiwa kipaumbele. Katika miongo inayokuja, ushirikiano

wa kimataifa unastahili kushughulikia ukosefu wa usawa na unastahili kujumuisha washirika wasio wa serikali. Ushirikiano huo unastahili kuwajumuisha watu wote na kukaribisha aina mpya za ushirikiano kama vile ushirikiano baina ya nchi za Kusini na ule wa pembetatu.

Pili, ushirikiano wa kimataifa unastahili kuanza na kuimarisha uwezo na jitihada za mitaa, kitaifa na kikanda. Uwajibikaji utahitajika katika kila hatua ili tufanikishe ahadi, viwango na kanuni mpya za elimu. Shirika la UNESCO linastahili kubadilisha jinsi linashughulikia maendeleo ya elimu ili liwe kama mshirika ambaye kazi yake ni kuimarisha taasisi za kikanda na kitaifa. Pia, shirika hili ilinastahili kuwa dalali wa ushahidi, mzalishaji wa maarifa, mtetezi wa data ya mifumo ya elimu na mtetezi wa uwajibikaji.

Tatu, ufadhili wa maendeleo ya kimataifa wa nchi za kipato cha chini na cha kati ni swala muhimu hasa kwa zile nchi zenye uchumi ambao haufanyi vizuri na zenye idadi kubwa za watoto na vijana. Ufadhili wa maendeleo ya kimataifa unastahili kupelekwa kwa maeneo ambayo haki ya kupata elimu imehatarishwa - hasa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo idadi kubwa va vijana itaishi na kusoma ifikiapo mwaka 2050. Vile vile, ufadhili huo unastahili kutumiwa wakati wa dharura ambazo zitazidi kuongeza kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi yanayozidi kuongezeka.

Nne, uwekezaji wa pamoja katika ushuhuda, data na maarifa ni muhimu katika ushirikiano wa kimataifa. Katika miongo inayokuja, tutapaswa kuimarisha ubadilishanaji wa maarifa baina ya jamii - hasa kuhusu jinsi ya kumaliza ukosefu wa usawa katika elimu na umasikini; jinsi ya kuboresha huduma za umma; mbinu za kukabiliana na changamoto za teknolojia za otomatiki na kidijitali na uhamaji; na uendelevu wa mazingira. Shirika la UNESCO ni daraja litakalofanikisha ubadilishanaji baina ya nchi na maeneo.

# Mazungumzo na ushirikishwaji

Kuna sababu ya kuwa na matumaini. Kuna uwezekano wa kupata mabadiliko na uvumbuzi mkubwa kupitia kwa miundo ya mifumo ya elimu, mipangilio ya shule na taasisi zingine za elimu na mbinu za mitaala na ufundishaji. Kwa pamoja, tunaweza kubadilisha elimu ili itusaidie katika ujenzi wa mustakabali wa elimu ulio wa haki, usawa, na uendelevu; ujenzi huo utahitaji utumiaji wa vitu ambavyo vipo na ujenzi wa vile vinavyostahili kujengwa. Tuna desturi za kitamaduni ambazo tunaweza kutumia. Binadamu wana uerevu na ubunifu wa pamoja. Hatua bora zinaweza kuwa za uvumbuzi au zilizo na msingi wa tamaduni. Mazungumzo ambayo yamependekezwa kwenye ripoti hii lazima yawe na ushirikishwaji mpana.

> Tutabadilisha hali kupitia kwa mamilioni ya hatua za ujasiri, uongozi, ubunifu, upingaji na utunzaji.

Elimu ni swala muhimu la karaia katika ngazi za mitaa, kitaifa na kimataifa. Elimu inahusu kila mtu; kwa hivyo, kila mtu anaweza kushiriki katika ujenzi wa mustakabali wa elimu. Ripoti hii imependekeza kuwa kuna majukumu yanayostahili kukamilishwa na walimu, vyuo vikuu, serikali, mashirika ya kimataifa, na vijana ili kufanikisha mazungumzo na hatua muhimu:

- **Walimu.** Walimu ni nguzo muhimu katika mustakabali wa elimu. Vile vile, wamekuwa msingi wa mkataba wa kijamii wa elimu ambao umekuwa tangu karne na kumi na tisa. Walimu watakuwa viongozi imara, wataalamu, na watafiti katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Kwa sababu hizi, ni lazima walimu wapatiwe uhuru, waungwe mkono wanapotafuta maendeleo ya kitaaluma, watambuliwe, na wahusishwe katika sera za umma. Walimu watakuwa wahusika wakuu katika michakato ya mazungumzo na uvumbuzi ambayo itawaleta watu tofauti pamoja.
- **Vyuo vikuu na elimu ya juu.** Kila sura ya ripoti hii imetoa wito wa kipekee kwa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kwa sababu ni muhimu katika mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Leo hii, kuna watu wachache wanaochunguza jukumu ambalo vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu hukamilisha katika uzalishaji na usambazaji wa maarifa. Hali hii ipo katika nyanja zote. Kazi nyingi ambayo inahusiana na mustakabali wa elimu ya msingi inategemea kazi ya vyuo vikuu. Vyuo vikuu vinatarajiwa kutafuta mbinu mpya za kuelimisha watoto na vijana ili wawe na uwezo wa kushiriki katika shughuli za elimu ya watu wazima. Elimu ya juu ni jukwaa la mazungumzo kati ya vizazi ambayo yananuiwa kuleta mabadiliko. Ujenzi wa maktaba mpya wa kijamii wa elimu hautawezekana bila ya ubora, uhuru, uaminifu, na ubunifu katika elimu ya juu.
- **Serikali.** Ripoti hii imesisitiza jukumu la serikali ambalo haliwezi kufanywa na mtu mwingine. Lakini hii haimaanishi mapendekezo ya ripoti hii yanalenga mifumo ya elimu ya kitaifa tu. Badala ya kufuata muundo wa ripoti unaoangazia jukumu la serikali, ripoti hii inahamasisha ushirikishwaji wa wadau wengi kwenye utafiti, maarifa, uvumbuzi, uchanganuzi na hatua muhimu. Hili ni swala la serikali kuchukua hatua katika viwango vingi ili ziimarishe ushirikishwaji mpana na zihamasishe uvumbuzi. Zaidi ya hayo, serikali zinastahili kutunza sifa za elimu ya umma kwa kuidhibiti na kutoa ufadhili wa kutosha.

- **Mashirika ya kimataifa na asasi za kiraia**. Ripoti hii imesisitiza umuhimu wa mashirika ya kimataifa na asasi za kiraia hasa katika kufanya elimu iwe rasilimali ya umma. Kusisitiza huku kunalenga kuonyesha mabadiliko ya mitazamo ambayo yametoa fursa za sauti mpya katika ushirikiano wa elimu baina ya sekta tofauti katika ngazi za mitaa, kitaifa, kikanda na kimataifa. Uhamasishaji wa mashirika ya kimataifa na asasi za kiraia utasaidia katika utekelezaji wa mapendekezo kwenye ripoti hii. Mashirika haya yana uwezo wa kukabiliana na ubaguzi wa jinsia, rangi ya ngozi, kabila, utamaduni, dini na ujinsia.
- **Watoto na vijana**. Mwisho, ni lazima watoto na vijana wahusishwe katika mazungumzo ambayo yamependekezwa. Mustakabali wao unastahili kuwa wenye fursa na sio mzigo kwao. Hili si swala la kuwasikiza tu bali ni la kuwahamasisha na kuwasaidia ili wajenge mustakabali wao. Harakati za vijana na watoto za hivi karibuni hasa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ubaguzi wa rangi, mfumo dume na kanuni za kijinsia zenye vikwazo zinatuonyesha njia za mustakabali. Vijana wanaoongoza harakati hizo hawakuomba idhini lakini walijitolea kupambana na mambo ya dharura ambayo mara nyingi huwashinda watu wazima. Vijana wana wajibu wa kujenga mustakabali. Kipengele muhimu katika kuendeleza ripoti hii ni kushirikisha vijana katika ujenzi wa mkataba mpya wa kijamii wa elimu.

Ulimwenguni kote, hatua za kuanzisha miradi ya elimu ya kuleta mabadiliko zimeanzishwa na walimu, majumuiya, mashirika na serikali. Kuna mifano kadhaa ambayo inaonyesha jinsi ya kushirikiana katika ujenzi na usambazaji wa maarifa. Mifano mingine inaonyesha jinsi elimu inaweza kuleta maana, kuhamasisha na kukomboa. Mifano mingine inaonyesha jinsi ujifunzaji unaweza kupangwa ndiposa uwanufaishe watu wote. Shughuli za sasa zinastahili kuboreshwa ili zisaidie katika kujenga mustakabali ulio na matumaini mengi.

Kazi nzuri inayoendelea ulimwenguni inastahili kujulikana, na Tume inapendekeza shirika la UNESCO liwe kama ghala la hatua muhimu na uvumbuzi utakaofanikisha kanuni zilizo kwenye ripoti hii.

# Mwaliko wa kuendelea

Kimsingi, ripoti hii inalenga kuanzisha mazungumzo ya kijamii kuhusu mustakabali bora na jinsi elimu inaweza kusaidia katika ujenzi wa mustakabali huo. Ripoti inajumuisha matokeo ya mchakato wa mazungumzo ulioendelea kwa kipindi cha miaka miwili. Mapendekezo yanasisitiza umuhimu wa mazungumzo zaidi na ushirikiano tunapojitarisha kwa siku zijazo. Maudhui yenye umuhimu kwenye mazungumzo na ushirikiano ni mustakabali wa elimu - si ripoti yenyewe.

Ingawa ripoti hii inafafanua changamoto na matumani ya kubadilisha elimu na kuelezea hatua za kufikia lengo hili, inasisitiza kuwa mkataba mpya wa kijamii wa elimu hauwezi kujijenga. Ndiposa uwe na maana na umuhimu, mkataba huo unastahili kujumuishwa kwenye programu, rasilimali, mifumo, na michakato ambayo hubadilisha uzoefu na shughuli za wanafunzi na walimu za kila siku.

Elimu huhusisha idadi kubwa ya watu na makundi yaliyo na uhusiano changamani: wanafunzi, walimu, familia, wasimamizi wa elimu, na viongozi katika ngazi tofauti za serikali. Elimu huhusisha

sekta za umma na asasi za kiraia zilizo katika jamii, mikoa, mataifa, maeneo na mataifa mbalimbali. Mabadiliko katika tamaduni za elimu yatatokana na michakato ya ujenzi inayoshirikisha makundi tofauti kwenye mazungumzo. Ushirikiano utakuwa muhimu katika kufanikisha kanuni, mapendekezo, na mbinu ambazo zimeelezwa kwenye ripoti hii. Ni kupitia kwa ushirikiano huo tunaweza kupiga hatua katika dhamira ya kubadilisha elimu.

Kila mmoja wetu anaweza kubadilisha mahali anapoishi. Sisi zote tuna uwezo wa kuendeleza mazungumzo. Huu ni ukweli ukizingatia kuwa tunaishi wakati ambapo teknolojia za mawasiliano zimewapatia watu wa kawaida uwezo wa kuungana na kushirikiana katika malengo yao. Upatikanaji wa teknolojia na intaneti umeimarisha ushirikiano baina ya walimu, taasisi za elimu na jamii. Ushirikiano huo umesaidia jamii kupata fursa nyingi na kutafuta suluhisho kwa changamoto tofauti.

Janga la UVIKO-19 liliathiri mipango ya kutayarisha na kuchapisha ripoti hii. Janga hilo limethibitisha umuhimu wa ushirikiano. Hatujapima hasara ambayo ililetwa na UVIKO-19, lakini tunajua iliharibu maendeleo ambayo yalichukua miongo kadhaa kupatikana. Watu walio tengwa na walio masikini hasa wanaoishi Ulimwengu wa Kusini ndio wameathirika zaidi. Hasara na maafa yaliyotokana na UVIKO-19 pamoja na changamoto za mabadiliko ya tabianchi ni thibitisho kuwa maisha ya binadamu yameunganishwa. Uvumbuzi wa chanjo za UVIKO-19 ambao ulitokea haraka unaonyesha matunda yanayoweza kupatikana kupitia kwa maarifa, sayansi na jitihada za kutafuta suluhu. Ripoti hii inatoa matumaini kuwa ufahamu huu utahamasisha ushirikiano katika ujenzi wa mustakabali mpya wa elimu.

Katika hali hii ya dharura, mapendekezo kwenye ripoti hii yatatusaidia kubadilisha mustakabali wetu na kujenga mkataba mpya wa kijamii wa elimu. Ripoti hii ni mwaliko unaotuhimiza tutafakari na tuchukue hatua za kujenga mustakabali wa elimu tukiwa tumeshirikiana. Ni mwanzo wa mchakato wa mazungumzo na ushirikiano katika ujenzi. Ripoti hii ni kama elimu kwa vile haijakamilika. Ufanisi wa ripoti hii umeanza sasa kupitia kwa jitihada za walimu ulimwenguni kote na wale ambao huwasaidia kwenye kazi yao.

# Viambatisho

# Marejeleo yaliyochaguliwa

## Ripoti huru

Ripoti zifuatazo zilipokelewa baada ya wito wa wazi wa kuandaa semina na vikosikazi ili kusaidia kubainisha changamoto na fursa muhimu na kutoa maoni na mapendekezo kwa Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu. Pia, baadhi ya taasisi zingine 200 zilitoa ripoti kwa ajili ya mradi wa UNESCO wa Mustakabali wa Elimu; washirika hao wameorodheshwa katika sehemu ya Waliotoa Michango katika Mashauriano ya Kimataifa.

Arab Campaign for Education for All. 2020. *Summary report on the Futures of Education in the Arab States: Building the future* (2020-2050). Ramallah, Arab Campaign for Education for All. http://www.teachercc.org/articles/view/379

Asia South Pacific Association for Basic and Adult Education. 2021. *From the margins to the center: Youth informing the futures of education.* Manila, Asia South Pacific Association for Basic and Adult Education. http://www.aspbae.org/userfiles/2021/Futures_of_Education_Report.pdf.

Barber, P., Bertet, M., Choi, J., Czerwitzki, K., Njobati, F. F., Grau I Callizo, I., Hambrock, H., Herveau, J., Kastner, A., Laabs, J., Manalo, A., Mesa, J., Mutabazi, S., Muthigani, A., Richard, P., Scheunpflug, A., Sendler-Koschel, B., White, M., and Wodon, Q. 2020. *Christian schools and the futures of education: a contribution to UNESCO's Futures of Education Commission by the International Office of Catholic Education and the Global Pedagogical Network – Joining in Reformation.* International Office of Catholic Education and Global Pedagogical Network – Joining in Reformation.http://oiecinternational.com/wp-content/uploads/2020/12/OIEC-GPENR-contribution.pdf

Bridge 47. 2020. *The role of education in addressing future challenges.* Bridge 47. https://www.bridge47.org/sites/default/files/2020-12/bridge47_-_report_to_unesco_foe_international_commission_final.pdf

Éducation, Recherches et Actualités. 2021. *L'Éducation du futur - L'enseignement supérieur : défis et paradoxes.* Beirut et Paris, Université Saint Joseph et Université Gustave Eiffel. https://www.periodicos.ufam.edu.br/index.php/larecherche

Emmaüs International. 2020. *Rapport à l'attention de la commission internationale de l'initiative de l'UNESCO : « Les futurs de l'éducation : apprendre à devenir* ». Montreuil, France, Emmaüs International. https:// emmaus-international.org/images/actualites/2020/10/EMMAS_INTERNATIONAL_-_Contribution_ Les_futurs_de_ldducation juillet_2020_003.pdf

Garcés, C. E. 2020. *Aportación para la Comisión Internacional*. Madrid.

International Council for Adult Education (ICAE). 2020. *Adult Learning and Education (ALE) – Because the future cannot wait.* International Council for Adult Education. https://en.unesco.org/futuresofeducation/sites/default/files/2020-10/ICAE%20-%20Futures%20of%20ALE%20FINAL.pdf

International Task Force on Teachers for Education 2030. 2021. *The futures of teaching: Background paper prepared for the Futures of Education Initiative.* Paris, UNESCO https://teachertaskforce.org/knowledge-hub/futures-teaching-background-paper-prepared-futures-education-initiative-0

International Union for Conservation of Nature (IUCN) Commission on Education and Communication (CEC).2021. *Visions and Recommendations for the Futures of Education. Gland, Switzerland, International Union for Conservation of Nature.* https://www.iucn.org/sites/dev/files/content/documents/cec_report_to_unesco_foe_-_6.5.pdf

Mouvement International ATD Quart Monde. 2020. *Contribution du Mouvement International ATD Quart Monde aux Futurs de l'Éducation. Pierrelaye, France, Mouvement ATD Quart Monde – Agir Tous pour la Dignité.* https://nextcloud.atd-quartmonde.org/index.php/s/DzMMci4yqP6dkPA

Red Regional por la Educación Inclusiva de Latinoamérica. 2020. *Los futuros de la educación - Contribuciones de la Red Regional por la Educación Inclusiva de Latinoamérica.* Buenos Aires, Red Regional por

la Educación Inclusiva de Latinoamérica.https://rededucacioninclusiva.org/wp-content/ uploads/2020/09/Los-futuros-de-la-educaci%C3%B3n-Contribuciones-de-la-Red-Regional-por-la - Educaci%C3%B3n-Inclusiva-de-Latinoam%C3%A9rica.pdf

Schulte, D., Cendon, E. and Makoe, M. 2020. *Re-Visioning the Future of Teaching and Learning in Higher Education: Report on Focus Group Discussions for the UNESCO Futures of Education Initiative.* University of the Future Network. https://unifuture.network/wp-content/uploads/sites/2/2020/08/20200722_UFN_UNESCO-report_fin.pdf

SDG-Education 2030 Steering Committee. 2020. *Contribution to the Futures of Education.* Paris, UNESCO. https://sdg4education2030.org/sites/default/files/2020-07/Futures%20of%20Education%20SDG - Ed2030%20SC%20contribution%20July%202020.pdf

Sefton-Green, J., Erstad, O. and Nelligan, P. 2021. *Educational Futures Across Generations*. Centre for Research for Educational Impact (REDI) at Deakin University and Department of Education at the University of Oslo. https://www.deakin.edu.au/ data/assets/pdf_file/0005/2298551/Educational-Futures-Across-Generations.pdf

Seguy, F. 2021. *Penser l'avenir de l'éducation en contexte de pandémie.* Port-au-Prince, UNESCO. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000378392

UNESCO. 2020. *Humanistic Futures of Learning: Perspectives from UNESCO Chairs and UNITWIN Networks*. Paris, UNESCO. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000372577/PDF/372577eng.pdf.multi

UNESCO Institute for Lifelong Learning. 2020. *Embracing a culture of lifelong learning: Contribution to the Futures of Education Initiative.* Hamburg, UNESCO Institute for Lifelong Learning. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374112/PDF/374112eng.pdf.multi

UNESCO International Institute for Higher Education in Latin America and the Caribbean (IESALC). 2021. *Thinking Higher and Beyond: Perspectives on the Futures of Higher Education to 2050.* UNESCO International Institute for Higher Education in Latin America and the Caribbean. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000377530

UNESCO. 2021. *Caribbean Futures of Education – Final Report*. Kingston, UNESCO. https://en.unesco.org/caribbean-futures-of-education

UNESCO's Collective Consultation of NGOs on Education 2030. 2021. *The role of Civil Society Organisations in 2050 and beyond.* Paris, UNESCO's Collective Consultation of NGOs on Education 2030. https://en.unesco.org/system/files/the_role_of_csos_in_2050_and_beyond.pdf

Unescocat and Fòrum Futurs de L'educació. 2020. How to Get to the Future of Education: Lessons Learned from the Escola Nova 21 Alliance in Catalonia. Unescocat-Center for UNESCO of Catalonia. https://catesco.org/wp-content/uploads/2020/10/Unescocat-contribution-to-Futures-of-Education.pdf

Wong, S., Kwok, V., Kwong, T. and Lau, R. 2020. Individuality, Accessibility, and Inclusivity: Applied Education and Lifelong Learning in Revolutionising Education for the 21st Century. Our Hong Kong Foundation. https://ourhkfoundation.org.hk/sites/default/files/media/pdf/UNESCO_submission_13102020.pdf

World Council on Intercultural and Global Competence. 2021. Contribution from the World Council on Intercultural and Global Competence to the UNESCO Futures of Education Initiative. https://iccglobal.org/wp-content/uploads/World-Council-Futures-of-Education-Learning-to-Become -Initiative_.pdf

Yidan Prize Foundation. 2021. Perspectives from the Yidan Prize Foundation Council of Luminaries on the Futures of Education.

# Makala ya Usuli

Makala ya usuli yafuatayo yalitolewa na UNESCO ili kusaidia kuendeleza mazungumzo kuhusu maswala muhimu yanayoshughulikiwa na Tume ya Kimataifa ya Mustakabali wa Elimu.

Assié-Lumumba, N. T. 2020. *Gender, knowledge production, and transformative policy in Africa*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374154

Buchanan J., Allais S., Anderson M., Calvo R. A., Peter S. and Pietsch T. 2020. *The futures of work: what education can and can't do*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374435

Common Worlds Research Collective. 2020. Learning to become with the world: Education for future survival. *Education Research and Foresight Working Paper 28*. Paris, UNESCO

Corson, J. 2020. *Visibly ungoverned: strategies for welcoming diverse forms of knowledge.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/ pf0000374085

Couture, J. C., Grøttvik, R. and Sellar, S. 2020. *A profession learning to become: the promise of collaboration between teacher organizations and academia.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374156

Damus, O. 2020. *Les futurs de l'éducation au carrefour des épistémologies du Nord et du Sud.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/ pf0000374047

Desjardins, R., Torres, C. A. and Wiksten, S. 2020. *Social contract pedagogy: a dialogical and deliberative model for Global Citizenship Education.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374879

D'Souza, E. 2020. *Education for future work and economic security in India.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374880

Facer, K. 2021. *Futures in education: towards an ethical practice*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000375792

Facer, K. 2021. It's not (just) about jobs: education for economic wellbeing. *Education Research and Foresight Working Paper 29*. Paris, UNESCO. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000376150/PDF/376150eng.pdf.multi

Facer, K. and Selwyn, N. 2021. *Digital technology and the futures of education – towards 'non-stupid' optimism.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000377071

Gautam, S. and Shyangtan, S. 2020. *From suffering to surviving, surviving to living: education for harmony with nature and humanity.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374086

Grigera, J. 2020. *Futures of Work in Latin America: between technological innovation and crisis*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374436

Hager, P. and Beckett, D. 2020. *We're all in this together: new principles of co-present group learning.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374089

Haste, H. and Chopra, V. 2020. *The futures of education for participation in 2050: educating for managing uncertainty and ambiguity.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374441

Hoppers, C. 2020. *Knowledge production, access and governance: a song from the south*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/ pf0000374033

Howard, P., Corbett, M., Burke-Saulnier, A. and Young, D. 2020. *Education futures: conservation and change.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374087

Inayatullah, S. 2020. Co-creating educational futures: contradictions between the emerging future and the walled past. *Education Research and Foresight Working Paper 27*. Paris, UNESCO. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000373581/PDF/373581eng.pdf.multi

Labate, H. 2020. *Knowledge access and distribution: the future(s) of what we used to call 'curriculum'.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374153

Lambrechts, W. 2020. *Learning 'for' and 'in' the future: on the role of resilience and empowerment in education.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374088

Mengisteab, K. 2020. *Education and participation in African contexts*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374155

Moore, S.J. and Nesterova, Y. 2020. *Indigenous knowledges and ways of knowing for a sustainable living.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374046

Saeed, T. 2020. *Reimagining education: student movements and the possibility of a Critical Pedagogy and Feminist Praxis.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374157

Schweisfurth, M. 2020. *Future pedagogies: reconciling multifaceted realities and shared visions.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374077

Smart, A., Sinclair, M., Benavot, A., Bernard, J., Chabbott, C., Russell, S. G. and Williams, J. 2020. *Learning for uncertain futures: The role of textbooks, curriculum, and pedagogy.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374078

Sriprakash, A., Nally, D., Myers, K., and Ramos-Pinto, P. 2020. *Learning with the past: racism, education and reparative futures.* Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374045

Stitzlein, S. M. 2020. *Using civic participation and civic reasoning to shape our future and education*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374034

Vasavi, A.R. 2020. *Rethinking mass higher education: towards community integrated learning centres*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374442

Wagner, D., Castillo, N. and Zahra, F. T. 2020. *Global learning equity and education: looking ahead*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000375000

Ydesen, C., Acosta, F., Milner, A.L., Ruan, Y., Aderet-German, T., Gomez Caride, E. and Hansen, I. S. 2020. *Inclusion in testing times: implications for citizenship and participation*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000374084

Alongside this background research, an interactive game was developed for the Futures of Education initiative to think about alternative learning systems and explore their implications with different groups.

Keats, J. and Candy, S. 2020. *Accession: Building an intergenerational library*. Game developed for the Futures of Education initiative.

# Maoni kutoka kwa mashauriano ya kimataifa

Makala yafuatayo yaliagizwa na UNESCO ili kusaidia katika kuchanganua na kuunganisha mawazo kutoka kwa kikundi lengwa, majukwaa ya mtandaoni na utafiti wa mtandaoni ulioandaliwa kwa ajili mradi huu.

Jacobs, R. and French, C. 2021. Women, robots and a sustainable generation: Reading artworks envisioning education in 2050 and beyond. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/search/faad9f2c-4a70-4b7a-8ac7-c3cffecd156c

Melchor, Y. 2021. *Analysis report of the online consultation modality: Your ideas on the futures of education*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000378271/PDF/378271eng.pdf.multi

TakingITGlobal. 2021. Focus group discussion analysis: Perspectives from the UNESCO Associated School Network's community of students, teachers and parents. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000378054/PDF/378054eng.pdf.multi

UNESCO. 2021. *Education in 2050: Analysis of social media polling campaign for UNESCO's Futures of Education report*. Paris, UNESCO.

Moeller, K., Agaba, S., Hook, T., Jiang, S., Otting, J., Sedighi, M. and Wyss, N. 2021. *Focus group discussions analysis: September 2019 - November 2020*. Paper commissioned for the UNESCO Futures of Education report. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000375579/PDF/375579eng.pdf.multi

# Machapisho ya Tume ya Mustakabali wa Elimu

Katika harakati za kutayarisha ripoti hii na kwa madhumuni ya kupata maoni na mapendekezo, Tume ilichapisha ripoti za muda kuhusu kazi iliyokuwa imekamilika. Kwa kuongezea, Tume ilitoa mapendekezo kuhusu kuvurugwa kwa elimu kulikosababishwa na janga la UVIKO-19.

International Commission on the Futures of Education. 2020. *Visioning and Framing the Futures of Education*. UNESCO, Paris. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000373208

International Commission on the Futures of Education. 2020. *Protecting and transforming education for shared futures: joint statement by the International Commission on the Futures of Education*. UNESCO, Paris. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000373380

International Commission on the Futures of Education. 2020. *Education in a Post-COVID World: Nine ideas for public action*. UNESCO, Paris. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000373717

